# MATHAYO
## **Muhtasari wa Masomo**

I. MAELEZO KWA JUMLA

A. Mwalimi: Denny Petrillo; Mtafsiri Chris Mwakabanje.

B. Kozi hii ina masomo 39 katika 13 DVDs.

C. Kila somo ni takribani dakika 38.

II. MAELEKEZO NA LENGO.

A. Haya ni masomo ya mchanganuo wa injili ya Mathayo, kwa mapana pamoja na masomo mengineyo kama yatakavyojitokeza.

B. Masomo haya yanapaswa kumwongoza mtu ili ajitoe wakfu kwa Yesu na kuelewa kwa mapana huduma yake Yesu.

C. Wanafunzi wanatakiwa kuelewa vema na kuyatendea kazi mambo yanayowahusu katika kitabu hiki.

D. Wanafunzi wanapaswa kuelewa sehemu zenye mafundisho za kitabu na kuweza kuwafundisha wengine kitabu hiki.

III. VIFAA VINAVYOTAKIWA.

A. Vinahitajika.

1. Biblia (UV).

2. Masomo ya video 39.

3. Notisi za kozi.

B. Maoni: Tafsiri sahihi yoyote (kuzingatia mafundisho ya awali) katika Mathayo.

IV. MAHITAJI.

A. Soma kitabu kizima cha Mathayo angalau mara moja.

B. Angalia katika video somo lote kikamilifu.

C. Soma notisi za kozi zote kikamilifu (ni vema kusoma notisi wakati huo huo ukiangalia masomo katika video, ukiongeza notisi zako mwenyewe iwapo itabidi.

D. Maliza kazi yako yote ya kudondoa (kama ilivyotajwa hapo chini).

E. Andaa makala yako ya muhula (kama ilivyotajwa hapo chini).

F. Fanya mitihani yako miwili.

G. Ukijumlisha maksi za kufaulu wastani usiopungua 70.

V. KAZI YA KUDONDOA.

A. Mistari ya kudondoa lazima iandikwe (au kuchapwa) kwa kudondoa, kisha kutumwa kwa VBI kwa ajili kusahihisha. Mistari lazima idondolewe kutoka katika UV, kama ulivyoonyesha katika maombi yako ya awali ya VBI.

B. Mistari yote lazima iandikwe au kuchapwa kwa mkao mmoja. Unaweza kujifunza tena na ukaanza upya ikiwa umekosea, lakini lazima uanze upya kuanzia mwanzo na kuandika mistari yote kwa mkao mmoja.

C. Karatasi ya kuandikia mistari itakusanywa pamoja na mtihani, ingawa itasahihishwa tofauti tofauti.

D. Katika *Mathayo*, mistari ifuatayo sharti idondolewe:

| | | |
|---|---|---|
| 6:33 | 11:28-30 | 16:24-26 |
| 7:21-23 | 15:13-14 | 28:18-20 |
| 10:32-33 | | |

E. Dondoa zinahitajika kutumwa pamoja na mtihani wako wa VBI.

F. Dokezo: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari juu ya kadi ili kurahisisha kuzipitia mara kwa mara wakati wa kozi hii nzima.

VI. MITIHANI.

A. Kuna mitihani miwili katika kitabu cha Mathayo. Wa kwanza unachukua sura 1-12, na wa pili unachukua sura 13-28.

B. Unapokaribia sura 12 wasiliana nasi na omba mtihani wa kwanza, kadhalika unapokaribia sura 28 wasiliana nasi na omba mtihani wa pili.

C. Ukisha kupata mtihani unaruhusiwa kuupitia na kujifunza.

D. Walakini, unapofanya mtihani unatakiwa ufanye wote bila kutazamia kutoka notisi, Biblia n.k.

VII. MAKALA YA MUHULA.

A. Andika muhtasari wa kila sura 28 katika Mathayo. Kwa maneno yako mwenyewe, ukielezea kinachotukia katika kila sura. Ujitoe kuandika angalau nusu ya ukurasa kwa kila sura. Juu ya kila fungu (paragraph), onyesha ni sura gani unaijadili ili iwe rahisi kuona unapotoka sura moja kuingia nyingine.

B. Makala ni lazima yasipungue kurasa kumi na nne, iliyochapwa yenye kuruka nafasi mbili mbili (double space). Ikiwa umeandika kwa mkono, makala lazima isipungue kurasa ishirini, pasipo kuruka msitari (single spaced).

C. Makala inatakiwa unapotuma VBI mtihani wako wa pili na kazi ya kudondoa.

VII. TUNZO.

A. Utapewa tunzo, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu kazi yote utakapokuwa umeimaliza kikamilifu, kanda zimerudishwa (iwapo zilianzimwa), na ada zote kwa ajili ya kozi hii zimelipwa zote.

B. Ni sala zetu kwamba masomo haya yatakuwa msaada katika safari yako ya kwenda mbinguni!

**Maelezo ya Kihistoria**
**na**
**Denny Petrillo, Mfasiri: Chris Mwakabanje**

Eusebius - 260-240 A.D. Palestina - Ecclesiastical History. 3.24:3-8.

"Walakini kati ya wote ambao walikuwa pamoja na Bwana, Mathayo na Yohana tu wametuachia maandiko yao, na mapokeo yanaeleza kwamba walimlazimisha kuandika, Mathayo kwanza alihubiri kwa Waebrania, na alipokuwa katika hatua ya kuwaendea watu wengine, aliyaweka katika maandishi kwa lugha yake mwenyewe injili aliyoiandika, na hivyo kuwa msaada wa maandiko yeye binafsi alipokosekana kuwepo mahali alipohitajika, Marko na Luka walikuwa tayari wameandika injili zao, lakini Yohana imeelezwa kuwa alitumia muda wote ujumbe ambao haukuandikwa tayari, na hatimaye akaandika kwa sababu ya wafuasi."

Eusebius anamnukuu Papias - Ecclessiastical History, Kitabu 3 XXXIX.

Tunafahamu kidogo juu ya Mathayo isipokuwa kusema maandishi ya kale tuliyonayo ya Mathayo yanaanza kwa kusema " ."

Neno Injili linatoka katika neno la Kiyunani " ; Mk.1:1 - "mwanzo wa Injili", na Mk.16:15 - "enendeni mkahubiri Injili." Injili ni habari njema kuhusu Mungu alichofanya kwa njia ya Yesu Kristo. Kuna tofauti kati ya (mafundisho) na (uinjilisti wa kuhubiri kuhusu Yesu). Katika kitabu cha Matendo ya Mitume walihubiri Yesu. Mahubiri ya uinjilisti (Matendo 10:34-42, linganisha na Marko - ujumbe unalingana sana) hilo ndilo lilikuwa kusudi kuu la kanisa la awali. Walakini, ni makosa kudai kwamba hakuna mafundisho katika injili. Ilidaiwa mapema kabisa kwamba kulikuwa na injili nne (maandiko yenye injili).

Irenaeus - A.D. 180 Against Heresy 4.11.8 alisema: "Haiwezekani kwamba ama injili zipungue au zizidishwe kuliko zilivyo sasa. Kwa maana kuna pande nne za ulimwengu ambamo tunaishi na vianzo vya upepo vinne, wakati kanisa limetawanyika duniani kote, na nguzo na msingi wa kanisa ni injili iliyo roho ya uzima; inatosha kwamba kanisa lingelikuwa na nguzo nne, zikitia uhai ufu wetu kila upande; zikihuisha wanadam upya."

Yesu alisema juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu.

Kanisa
M M L J
T K K N

Tatian, Mwashuru Mkristo 170 B.K., kwa mara ya kwanza aliziunganisha injili pamoja. Alitumia injili nne tu katika ulinganifu wake. Akaziunga pamoja katika - "kupitia nne" au "zilizoundwa kutokana na nne." Haya yalikuwa makosa makubwa ya utaratibu, kwa maana ikiwa Mungu alitaka sisi tuwe na injili moja kwa nini basi atupatia nne? Kila injili ina kiini chake binafsi kinachoelezwa, kusudi lake tofauti, maana yake maalum yanayofafanuliwa, ambayo hupotea iwapo utaziunganisha zote pamoja kuwa moja. Habari za ulinganifu wa Tatian ulifurahiwa sana Mashariki mwishoni mwa 400 B.K. Theodoret, ambaye alifanyika kuwa Askofu wa Kipro katika nyanda za juu za Ashuru 423 B.K., alizikuta kopi nyingi za diatessaron zikiwa

zikitumika katika dayosisi yake mwenyewe na zikawa mhimili wa utendaji. Tatian baadaye alikengeuka, hivyo Theodoret akawatangazia Wakristo waumini haswa kutotumia kazi yake, akaziharibu kopi zote alizoweza kuziona (mia mbili) na badala yake akarejeza matumizi ya injili nne za awali.

**Kwa kusoma injili nne hatua kwa hatua, wanadamu mara wakagudua tatizo litokanalo na ujumbe uliowakilishwa na wasimulizi mbalimbali** (Synoptic Problem).

Ilikuwa ni matokeo ya kanuni za uchunguzi wa kawaida - kila kitu lazima kithibitike kisayansi la sivyo hakipo. Lazima ziwepo kanuni zilizothibitika kitu kuwepo kwake. Lazima ieleweke kwa kila msomaji wa injili kwamba hizo za kwanza tatu zinafanana sana katika mpangilio, matukio, na hata katika maneno maeneo fulani. Ya nne ni tofauti sana.

Eusebius aliita injili ya Yohana "injili ya kiroho", na injili za Mathayo, Marko, na Luka kuwa "injili za kimwili." Injili tatu za kwanza ndizo zinazojulikana kama "Synoptic gospels" na ndizo zinatazamwa kuwa 'Synoptic Problem'.

J. J. Griesbach (1745-1812) alikuwa mtu wa kwanza kuona injili ya nne kuwa tofauti kabisa, na zingine tatu za awali zinatakiwa zihusishwe pamoja. Alikuwa akifikiri kisayansi. Alifikiri ingelifaa kuviunganisha pamoja kwa kuwa havikupangwa kinyakati, na badala yake aliunda synopsis (kwa sababu za kisayansi) katika hiyo akayaunganisha mafungu yanayofanana pamoja moja baada ya jingine kwa ulinganifu.

**Uchanganuzi wa (Synoptic Problem).**

Jinsi gani tunaelezea ulinganifu uliopo kwa mandhari ya ulimwengu na muundo kati ya hizi injili tatu, na wakati huo huo kuhesabu mara moja tofauti za kimpangilio, katika kusisitiza, na katika maelezo? Maoni mbalimbali yalitolewa kuelezea tatizo hili (synoptic problem). Maoni hayo ni kama yafuatavyo:

I. **Dhana A**. Inawezekana wote watatu walitegemea **injili** ya awali kabisa ya **Kiarami**. (Dhana hii iliungwa mkono na G. E. Dessing na J. G. Eichorn.) Lakini haielezei sababu ya baadhi ya mambo kuachwa na waandishi wengine na kwa nini Mathayo na Luka wanayo mambo yanayofanana ambayo Marko hana.

II. **Dhana B**. **Dhana ya vipande vipande**. F. Schleirmacher - 1825 - mitume waliandika baadhi ya matukio na maneno waliyoshuhudia mbalimbali na hayo yote yakazunguka na kuwa kitu kimoja. Ushahidi huu umetajwa katika utangulizi wa Luka. Maoni haya hayana maandishi ya kuthibitisha na hayaelezei ulinganifu wa kustaajabisha wa misemo (maneno yenye vitenzi vyenye nyakati sawa).

**III. Dhana C. Kupokezana kwa kuhadithiana**.

A. J. K. L. Guesler ndiye mtu wa kwanza kuanzisha maoni haya. Kimsingi mahubiri ya mitume yalisababisha simulizi sawa za kuhadithiana ambazo baadaye ziliunda msingi wa injili kwa njia ya kuhadithiana. Madai haya hudai yalihifadhiwa kwa njia ya kuhadithiana katika Kiarami lakini yakatafsiriwa kwa Kiyunani katika jitihada ya kuwahudumia Mataifa. Mambo hayo mawili ndiyo yaliunda msingi wa injili iliyoandikwa.

B. B. F. Wescoff - <u>Introduction to the Gospel</u>.

1. Maoni haya ya kuhadithiana yamepingwa vikali juu ya uwezo wa watu wa

kale kupokezana simulizi. Kwa mfano, MISHNAH, maandishi ya Waalimu (Rabbis) wa Kiyahudi yaliyoandikwa 200 K.K. - 200 B.K. Hivi ndivyo ilidhihirisha uwezo wao wa kupokezana simulizi.

2. Alitilia mkazo katika maelezo ya Papias, "Mathayo alikusanya mausia kwa Kiebrania na kila mtu aliyatafsiri kwa kadri alivyoweza.

3. Malengo:

   a. Ni vigumu kwa wadadisi wa mambo ya asili kuamini jinsi vitenzi vinavyokubaliana haswa kama inawezekana kuwa ni simulizi za kuhadithiana.

   b. Inashidikana pia kueleza ni kwa nini mpangilio kwa ujumla wa wote watu ni mmoja.

IV. **Dhana ya kutegemeana wenyewe kwa wenyewe**.

A. Augustine DeHippo - mapema miaka ya 400.

1. "Marko alimfuatilia Mathayo kwa karibu na anaonekana kama mwigizaji na mwenye kufupisha habari."

2. Kwa sababu hii, kutanguliza Mathayo kulitawala kwa muda mrefu hata ingawa Eusebius alisema Marko na Luka walikuwa wameviandika tayari.

B. Karl Lachmann - 1835.

1. Ukizingatia mpangilio wa matukio yalivyosimuliwa na kuona jinsi ambapo Mathayo na Luka wanaandika mambo ambayo pia yanapatikana katika Marko hivyo mpangilio wa matukio unaodhihirika, lakini wanapoandika mambo yasiyopatikana katika Marko mpangilio ni tofauti.

2. Kwa hiyo, lazima Marko kilitumiwa kama kiini cha wengine wawili.

C. C. H. Weisse 1801-1866.

1. Marko alitangulia kuandika kwanza, lakini Mathayo na Luka lazima walikuwa na kiini kingine kilichojulikana kama "Q" = Quella = kiini.

MK

MT LK

Q

2. Haya yanaitwa "dhana ya viini viwili."

3. Mwishoni mwa miaka ya 1800, karibu idadi kubwa ilikubaliana kwamba Marko alitangulia kuandika injili kwanza (hili lilitokana na ushawishi wa mafundisho ya Darwin ya kwamba vitu vimetokea tu, na vikabadilika-badilika na kufikia hatua ya ukamilifu).

D. John Chatman, (1865 - 1933) kuhani wa Dominika, alipinga kwamba Marko

ndiye alitangulia kuandika.

E. B. C. Butler - The originality of St. Matthew (1951).

1. Alionyesha makosa ya mpangilio wa Marko kutangulia (kwa nini basi haileti maana).

2. Inawezekana kwamba Marko alivitumia Mathayo na Luka na kuvifupisha, badala ya wao, kumtumia Marko.

F. William R. Farmer (19640 kwa mafanikio makubwa alipinga Marko kuwa cha kwanza.

G. Sir John Hawkins (1900's).

1. Alifanya uchanganuzi wa kina juu ya takwimu na akaunda katika kitabu chake alichojipatia sifa cha Horace Synopticae (mara ngapi waandishi wanakubaliana, asilimia ngapi n.k.).

2. Hilo ndilo lililozaa dhana ya kutengemeana: "Dhana ya nakala nne."

H. B. H. Streeter.

1. Injili nne - Kujifunza asili yake 1924, chenye kurasa 600, kimesimamia juu ya kanuni za kisayansi.

2. Hatimisho lake ni "Dhana ya Nakala Nne."

MK

M MT LK L

Q

3. Kwa ulimwengu wa kisayansi hili lilitatua tatizo (Synoptic Problem). Dhana hii imeshikiliwa na kuheshimiwa siku hizi.

V. Dhana ya historia ya kutungwa (Form Criticism) imekuja kwetu siklu za hivi karibuni.

A. Martin Dibelius - From Tradition to Gospel - 1919.

1. Injili taratibu zilitungwa kupitia mahubiri na mafundisho ya mitume katika kanisa la awali - wakaisambaza kwa njia ya vipande mbalimbali na kwa njia ya simulizi.

2. Aliyagawanya maandishi katika daraja hizi:

a. Riwaya,
b. Hadithi,
c. Methali,
d. Mapokeo, na
e. Ngano.

B. Rudolf Bultmann.

1. Alisisitiza kuwa Kristo wa kuaminiwa si sawa na Yesu wa kihistoria. (Mtu aliyeitwa Yesu, hakufanya miujiza yeyote, wala hakupokea ufunuo kutoka kwa Mungu - wala hakufufuka kabisa, wanafunzi walipata maono ya ufufuo - kufuatia maono hayo wakaanzisha kanisa - hadithi safi hizi zikakua na kuwa kubwa ajabu kwa jinsi zilivyohubiriwa na kufundishwa.

**<u>TATHMINI YA TATIZO (synoptic problem</u>).**

I. **Dhana ya Nakala Nne haijawahi kuthibitika**.

A. Husimamia kuwa Marko ndiye alitangulia kuandika akitumia "Q."

B. Kusema Marko alitangulia kuandika kumepingwa kwa mafanikio.

C. Kuwepo kwa "Q" sio tu ni dhana - inahitaji imani zaidi kuamini kuwepo kwake.

II. **Ushahidi wa nje ya kanisa la awali ni kinyume kudai Marko alitangulia**.

A. Rejea angalau kwa wazee wa kanisa (apostlic fathers) n.k.

B. Hapakuwa na nakala yoyote ya tafsiri ya Marko hadi kufikia karne ya tano.

III. **Mawazo kwamba ufupi wa kitabu ni sawa na kutangulia unatiliwa mashaka**.

A. Haya ni mafundisho ya Darwin.

B. Filosofi ya Hegel zilipelekea kujifunza Agano Jipya.

C. Chanzo cha dhana ya mageuzi kwamba lazima mabadiliko halisi yatokee:

1. Hakuna miujiza - ilianza kidogo kidogo hadi kufikia kuwa kitu kikubwa.

IV. **"Q" ndiyo nguzo ya dhana ya nakala nne lakini haijathibitika kuwepo**.

A. Kuna Injili ya Tomaso kwa Wamisri (maneno ya wasioamini injili), hivyo "Q" lazima ndiyo maandiko haya (ndivyo walivyodhani wanamageuzi hawa).

B. Farrah aliandika akipinga "Q" aliita <u>On Denspensing With "Q"</u> 1955 (Kutibu "Q").

V. Historia ya kutungwa (Form Criticism) inashindwa kutoa majibu ya kuridhisha sababu za kuwepo kwa kanisa.

A. Kwa nini watu walipoteza uhai wao? Je, walikuwa ni watu wajinga tu? Je, hawakuona wao binafsi miujiza iliyofanywa na Yesu na mitume?

B. Haielezi ni muda gani unapita kwa watu kusimuliana hadithi na zikawa thabiti.

1. Wanajaribu kutueleza kwamba mafundisho kamili yalitokea, mahubiri ya mhimili wa injili, kutokana na ngano kwa muda wa miaka hamsini tu.

2. Wanajaribu kutueleza kuwa kitu kilicho na mfumo bora kama kanisa kiliundwa chini ya miaka ishirini tu.

VI. **Dhana hizi zote ni za kidunia**.

A. Zinaeleza kwa msingi wa fikra tu kwamba hakuna miujiza iliyoweza kutendeka, kwa hiyo basi hulazimika kutoa maelezo mbadala juu ya mafundisho na matukio yaliyoandikwa katika injili.

B. Dhana hizi zimetolewa na wanadamu wasioamini uvuvio wa Biblia.

## MPANGILIO WA INJILI

I. Ukweli ni kwamba injili ilihubiriwa kwanza kabla ya kuandikwa kitu chochote!

A. Hotuba katika kitabu cha Matendo zinalingana kabisa na injili - Matendo 2; 10:34-n.k.

B. Walifuata kielelezo kimoja kikuu:

1. Upatizo,
2. Huduma,
3. Kifo cha Yesu,
4. Ufufuo, na
5. Ahadi ya kurudi kwake mara ya pili.

C. Roho Mtakatifu aliwakumbusha yote ambayo Yesu alisema na kutenda, na kuwaeleza maana halisi - Yoh.14:26; 2:22; Lk.24:44,45.

1. Lingeweza kufafanuliwa hili kwa jinsi ya vitenzi vya aina moja vilivyotumika katika baadhi ya misemo.

2. Hakika mahubiri haya yalirudiwa katika mpangilio bora zaidi.

3. Nakala nne zimeitwa "injili" - kwa hiyo ni lazima ziwe na mambo yote yaliyohubiriwa.

II. Kwa uvuvio waandishi wa injili mbalimbali walipangilia na kuyaweka pamoja mahubiri ya mitume (yao binafsi au ya watu wengine) kwa namna ya kipekee kutokana na wapokeaji wa ujumbe tofauti na kwa malengo mbalimbali. Jambo hili ndilo linafafanua tofauti zilizopo, n.k. Injili zimepangiliwa na kuundwa na watu hawa mbalimbali kwa uvuvio kwa malengo yao binafsi tofauti. Na kuufumbia macho ukweli huu ni kukosa ubora wa kila kitabu cha injili. Tunapojaribu kuziunganisha pamoja ili zilingane, tunajaribu kufanya jambo ambalo haliwezekani kabisa kutokana na namna Mungu alivyokusudia.

A. Waandishi wa injili walitumia vyanzo (k.m. Lk.1:1-4), lakini vyanzo vyao vilikuwa habari za wahudumu na mashahidi wa neno (mitume na manabii, n.k.).

1. Haliondoi hili maongozi ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu alifanya kazi jinsi alivyotaka.

a. Kila mmoja alitumia misamiati yake binafsi, lakini kazi ya kuandika na kukusanya, kuchanganua wasikilizaji, na mawazo yao waliyofikiri yaliongozwa, yalisimamiwa, yalilindwa, na kufinyangwa na Roho Mtakatifu wa Mungu ili kuhakiki kilichosemwa kilikuwa kama alivyotaka, kwa namna ile ile Mungu aliyoikusudia.

b. Kwa sababu tu walitumia vyanzo haina maana kwamba Mungu hakuwaongoza katika kweli yote.

c. Katika 1Kor.2:13 Paulo anadai kwamba maneno yake (au ujumbe) yalitoka kwa Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo alivyosema tu. Lakini, je kutokana na hayo tuseme kwamba Roho Mtakatifu alimpatia Paulo misamiati mipya na kumfunulia neno kwa neno kusema?

d. Pengine dhana ya "neno kwa neno" yanafika mbali zaidi. Kile kilichoandikwa katika kurasa zetu ndicho hicho Mungu alitaka kiandikwe!

2. Injili sio taarifa za habari za magazeti, bali ni injili iliyohai.

a. Viliandikwa kwa namna ya kipekee ili kuongoa nafsi, kufundisha ukweli wa Mungu, na kuelezea nia ya Kristo na kielelezo alichotuachia wanadamu.

b. Havikusudii kueleza ukweli tu (ingawa vinafanya hivyo), bali kuelezea mambo kwa mpangilio wenye kuleta mafanikio katika maisha ya watu.

3. Ebr.2:2-4; Gal.1:11,12; 2:2,6-9.

**Mwisho:**

Kuna viini vya ukweli katika kuwakilisha simulizi (Synoptic Problem), lakini zile zisizo za kweli zinaharibu mawazo haya.

## INJILI YA MATHAYO
### Mambo ya Utangulizi

Injili ya kwanza kihistoria alipewa Mathayo Lawi, mtoza ushuru (publican) aliyeitwa na Yesu kuwa mmoja kati ya kumi na wawili - Mt.9:9-13; 10:3. Baada ya orodha ya mitume ya Matendo 1:13, Mathayo haonekani tena katika historia ya Agano Jipya.

IRENAEUS, *AGAINST HERESIES* 331:

"Mathayo pia aliitoa injili iliyoandikwa miongoni mwa Waebrania...wakati huo Petro na Paulo walikuwa wakihubiri Rumi na kuweka msingi wa Kanisa."

## TAREHE YA MATHAYO

Tarehe ya kuandikwa injili ya Mathayo haijulikani. Kutokana na maoni ya walimwengu, tarehe ya kitabu cha Mathayo hutolewa baada ya 70 B.K. kwa kuwa ina habari maalum kuhusu

kuanguka kwa Yerusalem, kulikotokea mwaka huo. Hawatoi ruhusa ya mtu yeyote kuweza kutabiri (hata Yesu) mambo yanayoweza kutokea baadaye.

## INJILI KAMA ILIVYOANDIKWA NA MATHAYO

## UTANGULIZI

**LENGO**: Kuwashawishi Wayahudi kwamba Yesu ndiye Masihi aliyetabiriwa.

**MPANGO**: Kuwakilisha mafundisho ya Yesu kwa mapana zaidi na kuzungumzia kazi ya Yesu (akisisitiza uweza wake) karibu katika kila sehemu ya mahubiri. Hapa kuna baadhi ya mifano ya jinsi Mathayo anavyoelezea kufikia lengo hili.

I. **Ukoo wa Yesu ndio uliotakiwa juu ya Masihi**.

Sura 1 inathibitisha kwamba ukoo wa Yesu unarejea nyuma hadi kwa Daudi. Masihi alitakiwa atoke katika ukoo huo. Mathayo atadhihirisha bayana kuwa Yesu ametoka katika ukoo huo.

II. **Yesu na Yohana Mbatizaji wametimiza mafungu mengi ya unabii wa Agano la Kale**.

Mwishoni mwa sura 1 na sura yote ya pili na ya tatu zinazungumzia kuzaliwa kimuujiza kwa Yesu na mahubiri ya Yohana Mbatizaji. Wanachofanya Yesu na Yohana, Mathayo atasema, “preloo” au “kutimia” yale yaliyotabiriwa katika Agano la Kale.

Neno hili limetokea mara 13 katika Mathayo lenye maana “timia.” Neno hili hasa linajitokeza katika sura za awali kadhaa. Tunaweza kuona umuhimu wa hilo. Yesu ametimiliza yale Agano la Kale liliyanena. Neno hili ni muhimu sana. Tutaona kwamba neno hili lina wazo *linaloyafunga pamoja na kuyakamilisha*. Kadhalika tunaona “pleroo” Mathayo amelitumia karibu akiondoa kama unabii wa kutimia mara mbili. Ulitimilika katika Agano la Kale na kisha kutimia kikamilifu zaidi katika Agano Jipya. Angalia mfano huu:

Ananukuu Hos.11:1 “Nikakwita mwanangu kutoka Misri.” Hosea anatumia fungu hilo maalum kutabiri kwamba Mungu atawaita watu wake watoke “Misri” (hasa Babeli) kurejea tena nchini, wakati wa Koreshi - 536 K.K. Mathayo ananukuu haya akimaanisha Mungu anapowaeleza Mariam na Yusufu kurudi toka Misri walikokimbilia kukwepa ghadhabu ya Herode. Hivyo unabii wa fungu hili, ulitimilika mara ya pili. Mara ya pili unaleta maana kamili zaidi au maana ya msingi, kwa kuwa unamhusu Masihi.

Hili ndilo kusudi la kitabu hiki linalothibitisha *kwamba Yesu ni Masihi aliyetabiriwa*. Ndilo haswa lingeliwavutia Wayahudi zaidi. Basi ukweli wa kwamba Yesu ni utimilifu wa maandiko ya unabii kungewanufaisha zaidi Wayahudi waliokuwa wakiyaona maandiko hayo kama yenye mamlaka kwao kuhusu Masihi.

III. **Asili ya kutokutenda kwake Yesu dhambi kulitoa sifa kuu iliyotakiwa kuhusu Masihi**.

Katika sura 4 Mathayo anajadili asili ya kutotenda dhambi Yesu. Anatoa somo juu ya ibada. Katika Math.4:10 Yesu anamwambia shetani, “Umwabudu yeye peke yake,” ingawa Mathayo anatumia neno lilo hilo la kuabudu na kuonyesha jinsi Yesu alivyoabudiwa. Tunaposoma Mathayo lazima tuhatimishe kuwa Yesu ni Mungu, kwa kuwa wote wawili wanakubali kuabudiwa.

IV. **Yesu mwenyewe alijidhihirisha kuwa ni Mwalimu Mkuu, hiyo ndiyo sifa iliyotarajiwa kutoka kwa Masihi**.

Ling. Math.7:28; 11:1; 13:53; 19:1; 26:1. Mafungu haya yote yanalingana kwa kusema neno "alipomaliza." "Alipomaliza kusema maneno hayo," au yenye namna kama hiyo. Lilikuwa jambo muhimu kwa Wayahudi kuona Masihi kama mwalimu mkuu. Mathayo anadhihirisha hivyo kwa namna <u>tano za hotuba</u>.

A. Math.5-7 - Hotuba ya Mlimani (ikifuatiwa na 7:28 "Alipomaliza kusema maneno hayo" - usemi uliyotumika kuhatimisha kila sehemu ya mahubiri).

B. Math.9:36 - 10:42 (11:1, "Alipokwisha kuwaagiza")

C. Math.13:1 - 52 (13:53, maneno ya ufunguo).

D. Math.17:22 - 18:35 (19:1, maneno ya ufunguo).

E. Math.23:1 - 25:46 (26:1, maneno ya ufunguo).

Tunachopaswa kufanya ni kujadili mazingira ya sehemu hizi tano zifuatazo. Kitu gani, kama kipo, kinachojitokeza katika mafungu haya? Ni kweli kwamba Mathayo ana namna fulani ya uandishi na utaratibu. Ana **lengo** (kuthibisha kuwa Yesu ndiye Masihi aliyetabiriwa) na lengo hili limefanikiwa katika sehemu hizi za hotuba. Katika kuangalia kila sehemu ya hotuba hizi, ni masomo gani makuu ambayo Yesu anayatilia manani na kusisitiza?

1. Yesu anatia mkazo juu ya "ufalme." Tukiangalia katika kila sehemu ya hotuba hizi tutaona sisitizo juu ya ufalme. Neno hili limetokea mara hamsini na sita katika injili ya Mathayo, zaidi katika sehemu za hotuba za Yesu. Kati ya hizo hamsini na sita, mara thelathini ametaja "ufalme wa mbinguni." Wanaounganisha injili pamoja hujumuisha mafungu haya na kuona kwamba Marko na Mathayo wote wanazungumzia jambo hilo. Nini maana ya jambo hili, je linazungumziwa jambo moja? Wayahudi wanatarajia Masihi mwenye nguvu, duniani, na wanatazamia ufalme kuwa Yerusalem. Bali Yesu anazungumzia ukweli kwamba ufalme ni "wa mbinguni." Anajaribu kuwaonyesha kwamba wameshindwa kuelewa maana halisi ya ufalme ule ujao ulivyo. Yesu atasisitiza ufalme huu wa mbinguni na jinsi ulivyo haswa. Wayahudi walitarajia Masihi kuzungumzia jambo hili.

2. Neno la pili ambalo Yesu ametilia mkazo ni neno "Baba." Neno hili limetumika mara sitini na moja katika injili ya Mathayo (na zaidi ya mara tisini katika kitabu cha Yohana) na Yesu analitumia mara hamsini na sita kati ya hizo zote. Yesu amekuja ili kuwatia fikra mpya Wayahudi kuhusu Baba, hata wazo la kuwa yeye ni Baba. Hawamwoni Mungu kwa jinsi alivyo haswa, au namna ambayo wanapaswa kufikiri juu yake. Mara kumi na saba katika Hotuba ya Mlimani, atasema, "Baba yenu aliye mbinguni." Katika sura 11:27 Yesu anasema, "Nimekabidhiwa vyote na Baba yangu...wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana..." Yesu amekuja kumfunua mtu fulani ambaye hatuwezi kumfahamu isipokuwa yeye amemfunua kwetu. Yesu anasisitiza zaidi akiamsha fikra zao juu ya Baba. Jambo hili ni la kufurahisha. Tumelizoea zaidi hili (kumwona Mungu kama Baba) pengine si taabu kwetu, lakini Wayahudi walikuwa na historia ambayo iliwafanya wapoteze dira ya upendo wa asili wa Mungu. Angalia Mal.1:1, 2. "Nimewapenda ninyi, lakini ninyi mnasema, umetupendaje? Kitabu hiki

kinaonyesha mkanganyiko walikuwa nao Wayahudi kwa Mungu. Baadhi ya vitabu - Isaya, Hosea, n.k. vilitoa ahadi kwamba watakoporejea tena katika nchi ya ahadi wangebarikiwa kupita kipimo. Kipindi cha Malaki walikuwa wamekata tamaa na kutokuamini tena kwamba Mungu anawapenda. Kwa karne nne baada ya Malaki, mawazo haya yalizidi kushamiri. Hawakubarikiwa tena kipindi cha kati ya maagano kilikuwa kibaya mno kwa Wayahudi. Wayahudi ni wenye kukanganyika mno ulimwenguni. Yesu anaanza kwa kutokutenda jambo lolote na atajaribu kumtambulisha Baba yao Wayahudi.

Mara sitini na moja katika Mathayo, na katika Yohana zaidi ya mara tisini, Yesu anazungumzia kuhusu Baba na jambo hili ni muhimu sana. Angalia maelezo juu ya "Yesu na Baba" katika Hotuba ya Mlimani. Jambo gani anatufundisha kuhusu Baba katika Hotuba ya Mlimani? Angalia maelezo juu ya "Baba."

V. **Miujiza ya Yesu inathibitisha kwamba alikuwa Masihi**.

Ni kitu gani tunapata kati ya hizi sehemu za mahubiri? Miujiza. Kwa nini? Kwa sababu ilithibitisha kuwa Yesu alikuwa kama alivyodai. Neno analolitumia Mathayo lililothibitisha miujiza ni neno mamlaka.

A. Math.7:28,29 - Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka, na siyo kama waandishi.

B. Math.9:6 - Mwana wa Adamu ana mamlaka.

C. Math.28:18-20 - Yesu alipewa mamlaka katika kufundisha kwake na akathibitisha hivi kwa miujiza aliyoifanya. Alikuwa Mwalimu Mkuu, na hivyo ndivyo Masihi alivyotarajiwa kuwa.

VI. **Masihi angekuwa na wafuasi wengi**.

Ni kitu gani tena tunapata kati ya hizi sehemu za mahubiri? Kuitwa kwa mitume KUFUATA yeye. Hili ni neno lingine la ufunguo katika kitabu cha Mathayo. Neno nifuate linatokea mara ishirini na nne. Neno mwanafunzi limetumika mara sabini na mbili. Ndilo neno lenye maana ya "mfuasi." Jumla ni mara tisini na sita juu ya wazo la ufuasi. Yesu atafundisha nini maana halisi ya kuitwa mfuasi. Watu wanamfuata kimwili, lakini Yesu atawafundisha maana halisi ya kumfuata yeye, pamoja na mitume kumi na mbili kwa kuwa lazima nao wamfuate pia. Wazo lingine tutakaloliona ni "kwenda" kwa Yesu. Neno hili limetokea mara hamsini na mbili katika injili; mara thelathini na nane anatoa Yesu mwenyewe. Tutapata muda wa kulizungumzia hili baadaye. Haya ni masomo muhimu ajabu: wanaomjia kupata maelekezo, wanaomwendea ili waponywe, maadui zake wanamwendea ili wamjaribu...sababu mbalimbali za kumwendea Yesu.

Maneno mengine muhimu ni: ibada - mara kumi na moja, nabii mara thelathini na saba.

**1:1 Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu**.

Anaaza kwa hoja zake (akithibitisha kwamba Yesu ni Masihi) na msitari wa kwanza kabisa. Ikiwa Yesu alikuwa kweli ni Masihi, hivyo basi ingelipasa kutoka katika ukoo sahihi. Basi Mathayo, kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu, atajadili kikwazo kikubwa hiki kwanza muhimu.

**Ukoo** - historia ya alivyozaliwa Yesu Kristo. Alitokeaje? Anachosema ni kwamba ni mwana wa **Daudi**, mwana wa **Ibrahamu**. “Mwana wa” maana yake “uzao wa.” Ni jambo muhimu sana na la msingi kueleza kwamba Yesu ni wa ukoo wa **Daudi**.

Kwa ajili ya ukoo wa Mariamu angalia habari iliyoandikwa na Luka. Hapa ni ukoo wa Yusufu. Wayahudi hasingelijali kamwe ukoo wa mama, ingawa Yusufu hakuwa baba wa Yesu, ilingekuwa jambo muhimu sana kwa Wayahudi hivyo basi Mathayo anaonyesha ukoo huu. Wayunani wangejua kwamba Yesu hakuwa mwana wa Yusufu na wasingejali juu ya ukoo wa Yusufu.

Genesewv - kitabu cha historia ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Kuna mambo mawili ambayo ni muhimu katika fikra za Wayahudi. Na mambo hayo ni uhusiano wa Abrahamu na Daudi. Abrahamu - Mwa.12:1-3; 15:4-20; 17:21; 22:17,18; 26:4; 28:13,14; 35:10,11; 50:24,25. Kimadhubuti katika Vitabu Vitano vya Musa lilikuwepo wazo kwamba katika uzao wa Abrahamu taifa la Israeli lingebarikiwa.

Mwana wa Daudi - (“mwana wa” au “uzao wa”) - pia ni muhimu mno (2Sam.7:12,13). Masihi angekuwa mfalme kwa mfano wa Daudi (Isa.9:6,7). Wayahudi hawakuwahi kufikiri juu ya mfalme wa kiroho wakati wowote ule, hasa kutokana na Dan.2 na Zab.110. Anachofanya Mathayo katika ukoo ni kuanzisha uhusiano thabiti baina ya Yesu na sura mbili kubwa na muhimu sana kama vile Wayahudi walivyotarajia.

**1:2 Ibrahim alimzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Yuda na ndugu zake;**
**1:3 Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari; Peresi akamzaa Esromu; Esromu akamzaa Aramu;**
**1:4 Aramu akamzaa aminadabu; Abinadabu akamzaa Nashoni; Nashoni akamzaa Salmoni;**
**1:5 Salmoni akamzaa Boazi kwa Rahabu; Boazi akamzaa Obedi kwa Ruthu; Obedi akamzaa Yese;**
**1:6 Yese akamzaa Mfalme Daudi. Daudi akamzaa Sulemani kwa yule mke wa Uria;**
**1:7 Sulemani akamzaa Rehoboamu; Rehoboamu akamzaa Abiya; Abiya akamzaa Asa;**
**1:8 Asa akamzaa Yehoshafati; Yehoshafati akamzaa Yoramu; Yoramu akamzaa Uzia;**
**1:9 Uzia akamzaa Yothamu; Yothamu akamzaa Ahazi; Ahazi akamzaa Hezekia;**
**1:10 Hezekia akamzaa Manase; Manase akamzaa Amoni; Amoni akamzaa Yosia;**
**1:11 Yosia akamzaa Yekonia na ndugu zake, wakati wa ule uhamisho wa Babeli.**
**1:12 Na baada ya ule uhamisho wa Babeli, Yekonia akamzaa Shealtieli; Shealtieli akamzaa Zerubabeli;**
**1:13 Zerubabeli akamzaa Abihudi; Abihudi akamzaa Eliakimu; Eliakimu akamzaa Azori;**
**1:14 Azori akamzaa Sadoki; Sadoki akamzaa Akimu; Akimu akamzaa Elihudi;**
**1:15 Elihudi akamzaa Eleazari; Eliazari akamzaa Matani; Matani akamzaa Yakobo;**
**1:16 Yakobo akamzaa Yusufu; Yusufu mumewe Mariamu aliyemzaa Yesu aitwaye Kristo.**

**Akamzaa** = egennhsen = alizaliwa “...kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa” Mwa.21:12.

## MAJINA KATIKA UKOO WA YESU

| | |
|---|---|
| Ibrahamu ... | Mwa.12:1-3; 17:7; Gal.3:16 |
| Isaka | Mwa.21:1-3; 26:4; Ahadi imerudiwa |
| Yakobo | Mwa.25:25,26; 28:13,14 (pia aliitwa Israeli) |

| | |
|---|---|
| Yuda | Mwana wa Lea - Mwa.29:35 |
| Peresi | Mmoja wa mapacha waliozaliwa kwa uharimu baina ya Yuda na Tamari mkwewe - Mwa.38:12-30 |
| Hesroni | Mwana wa Yuda - Mwa.46:12 |
| Ramu | Ruthu 4:18 - mwana wa Hesroni |
| Aminadabu | Ruthu 4:19 |
| Nashoni | Ruthu 4:20 |
| Salmoni | Ruthu 4:20 |
| Boazi | Ruthu 4:21 - Mumewe Ruthu |
| Obedi | Ruthu 4:21 |
| Yese | Ruthu 4:21 - Baba wa Daudi |
| Daudi | Ruthu 4:21 - Mfalme wa Israeli |

**UFALME WA YUDA**

| | |
|---|---|
| Sulemani | Mwana wa kumi wa Daudi, wa pili kwa Bethsheba - 2Sam.12:24 |
| Rehoboamu | 2Nyak.9:31 |
| Abiya | (Abiyamu) mwana wa Rehoboamu - 1Fal.14:31 |
| Asa | 1Fal.15:8 |
| Yehoshafati | 1Fal.15:24 |
| Yoramu | 1Fal.22:30; 2Fal.8:16 |
| Ahazi | 2Fal.8:25 |
| Yoashi | 2Fal.13:1 |
| Amazia | 2Fal.14:21 |
| Azaria | 2Fal.15:1 |
| Yothamu | 2Fal.15;7 |
| Ahazi | 2Fal.10:1 |
| Hezekia | 2Fal.18:1 |
| Manase | 2Fal.21:2 |
| Amoni | 2Fal.21:18,19 |
| Yosia | 2Fal.22:1 |
| Yohoazi | 2Nyak.36:1 |
| Uzia | (Katika Young 1019) anaitwa pia Azaria, 2Fal.15:1 uzao hugawanyika mara tatu toka kwa Yoramu |
| Yekonia | 1Nyak.3:16 |
| Shealtieli | Babaye Zerubabeli - Ezra 3:2 |
| Zerubabeli | Ezra 2:2 - aliyeongoza watu kutoka utumwani |
| Abihudi | Katika Math.1:13 (pengine mjukuu) |
| Eliakimu | Katika Math.1:13 na Lk.3:30 |
| Azori | Katika Math.1:13,14 |
| Sadoki | Math.1:14 |
| Akimu | Math.1:14 |
| Eliudi | Math.1:14 |
| Eliazari | Math.1:15 |
| Matani | Math.1:15 |
| Yakobo | Math.1:15 |
| Yusufu | Math.1:16 |

Aliyemzaa = - ni jinsia ya kike, hapa haihusiani na Yusufu, bali inamhuru Mariam. Katika ukoo ulioandikwa na Luka anatajwa Yesu kupitia Mariamu. Kufuatana na sheria, Yusufu alikuwa kisheria ndiye baba wa Yesu, hivyo basi Mathayo kwa jumla anaelezea kufuatia na ukoo wa Yusufu. Hata hivyo anabainisha zaidi katika mst.16 kwamba Yesu hakuzaliwa na

Yusufu.

**1:17 Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vinne; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli ni Vizazi kumi na vinne; na tangu ule uhamisho wa Babeli hata Kristo ni vizazi kumi na vinne.**

**Vizazi kumi na vinne**. Kwa kujifunza ukoo huu inadhihirika kwamba Mathayo anatueleza kuwa hapakuwa na baba na wana halisi kumi na wanne, bali anaeleza hivyo kwa urahisi wa mtu kukariri, aligawanya katika mafungu yenye kumi na nne tatu tatu. Kwa njia hiyo watu (hasa vijana Wayahudi) wangeliweza kukariri, na wangetambua kwamba wana majina yote kwa kuhesabu kwa kumi na nne. Kwa vizazi vya Kiyahudi, hawakujali hasa jinsi mpangilio ulivyokuwa (mjomba, n.k.)

Mathayo anagawanya kutoka Abrahamu hadi Daudi vizazi 14; kutoka Daudi hadi uhamishoni vizazi 14; na kutoka uhamishoni hadi kuzaliwa kwake Yesu vizazi 14. Yesu alikuwa ni wa mwisho katika kundi la tatu la vizazi 14, ambalo lingelingana na kizazi chao. Anachosema ni kuwa, “aitwaye Kristo,” na tena anamwita Kristo katika mst.17. Kwa mara nyingine tena, Mathayo bado hajathibitisha kwamba Yesu ndiye hakika Kristo, bali anaanza kutoa ushahidi wa kushawishi. Wayahudi walikuwa wakati wote na vipingamizi (kama katika kitabu cha Yohana wanapodai, “Ametokea mahali si penyewe”).

**Kristo** = cristov = “mpakwa mafuta” - kazi au cheo. “Yesu” ni jina la mtu. “Bwana Yesu Kristo” maana yake Yesu wa Nazareti ambaye ni Bwana wa wote wakaao juu ya kiti cha enzi cha Daudi. Baadaye “Kristo” likawa karibu ni jina pekee lililotumika kwa sababu ya Mkristo akimkubali Yesu kuwa ni Kristo. Kwa Wayahudi, majina Yesu na Kristo hayana mausiano kabisa.

**1:18 Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.**

Mathayo angali bado hajathibitisha kwamba Yesu ndiye **Kristo**. Lakini anaendelea kuijenga hoja yake. Kufikia hapa ameonyesha (1) Yesu ametoka katika uzao wa Ibrahamu; (2) Yesu ametoka katika ukoo wa Daudi; (3) Ukoo wa Yesu ni mmoja unaojumuishwa katika makundi matatu ya 14 ya vizazi hivi. Pamoja na kuelezea vizazi, Mathayo anaweza sasa kuendelea kuthibitisha zaidi Umasihi wa Yesu.

Mariamu mama yake, alipokuwa ameposwa na Yusufu, lakini kabla hawajakaribiana, (kabla ya kukutana kimwili) alionekana ana mimba. Basi kwa uhakika mtoto sio wa Yusufu. Alionekana ana mtoto kwa uwezo wa **Roho Mtakatifu**. Mafungu machache sana yanayoonyesha jinsi Wayahudi walivyofikiri kuhusu Roho Mtakatifu, hivyo kufikia hapa wasingeelewa haswa kuwa Roho Mtakatifu ni nani. Hata ingawa wangelifahamu kwamba kulikuwa na nguvu fulani ambayo ilikuwa “Roho wa Mungu” ambayo iliyomtia nguvu Samson na Sauli, n.k.

**1:19 Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alikuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.**

**Asitake kumwaibisha**. Katika Mishnah (Mapokeo ya Kiyahudi kuhusu Sheria za Musa) kuna Sotah (mazungumzo) juu ya “aliyehisiwa kuwa mzinzi.” Katika Sotah hii inatoa kanuni ya dini ya kuifuata kumtambua mwanamke asiyekuwa mwaminifu katika ndoa (kama jaribio la maji machungu katika Hes.5:11-31), ambapo tumbo lingevimba ikiwa alikuwa na hatia. Posa ilikuwa dhamana kubwa. Sheria ya Musa ilimpatia mume haki ya kumpiga mawe. Lakini ambalo angeweza Yusufu kufanya ni kumdhalilisha na kumfedhehesha hadharani. Mtu mwenye haki

kama Yusufu hilo lilikuwa jambo la aibu kwake kuona mwanamke aliyetaka kumwoa kujamiana kabla ya ndoa. Hata hivyo, hakutaka kumwaibisha au kumfedhehesha hadharani bali kwa nia njema pia asingelimwoa. Kwa hiyo, waamuzi wake bora ulikuwa ni kumtaliki. Yusufu angeliweza kumwaibisha na kumdhalilisha.

**Kumwacha kwa siri**. Yusufu hakutaka kumfedhehesha hadharani (Hes.5), lakini kam mtu mwenye haki, angeliweza kumwoa na hilo lingechafua jina la familia yake. Kama mtu mwenye rehema hakutaka kumdhalilisha mwanamke aliyempenda.

**1:20 Basi alipokuwa anafikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kuchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu**

**Malaika akamtokea** = miujiza imehusika - mpango wa Mungu umetendeka. Kitu cha maana sana kuhusu tukio hili ni kuona kuwa kipindi cha ukimwa wa kushangaza (karibu miaka 400, kutoka Malaki hadi hapa) na Mathayo anatilia mkazo katika ndoto. Tutakuwa tukijadili jambo hili zaidi katika sura chache za awali zijazo.

**JUU YA UKIMYA WA MANABII**

Katika kipindi hiki cha kati cha maagano walitambua kuwa hawakuwa na nabii yeyote ylue. Angalia: *1Makabayo 4:46*

"Hivyo wakavunja madhabahu na kulaza mawe chini ya mlima wa nyumba, mahali pa maagano, hata nabii atakapokuja na kuamua (nini cha kufanya) kuhusu hayo."

*1Makabayo 9:27*

"Na kulikuwa na adha kuu katika Israeli, ambayo haikuwahi kutokea tangu wakati ule nabii alipokuwepo kwao."

*1Makabayo 14:41*

"Wayahudi na makuhani walipendezwa kuwa Simoni awe kiongozi wao na kuhani wao mkuu milele, hata atakapokuja nabii mwaminifu atakapoinuka."

"Kutoka Artashasta kufikia muda wetu huu historia kamili imeandikwa lakini haihesabiwi kuwa na thamani ukilinganisha na maandishi ya kale, kwa sababu ya kushindwa kurithiana hasa kwa manabii." Josephus, Against Apion 1.8.

"Maelezo haya ni sahihi na yanaambatana na vitabu vyetu. Kwa maana mwishoni yameandikwa kwamba Nebukadneza, katika mwaka 18 wa kutawala kwake, aliliteketeza hekalu letu, ambalo kwa miaka hamsini halijakuwepo, ambalo katika mwaka wa pili wa kutawala kwake Koreshi msingi uliwekwa, na hatimaye, katika mwaka wa pili wa kutawala kwake Dario lilikamilika." Josephus, Against Apion 1.21.

Mafungu haya yanaonyesha kwamba Wayahudi walijua tofauti kati ya manabii wa Mungu na manabii wa uongo. Walitambua kwamba hapakuwepo manabii wa kweli tangu kipindi cha Malaki hadi kipindi cha Agano Jipya. Hivyo basi, kujitokeza kwa Zakaria na kwa Yusufu ni kwa maana sana.

**Angalia**: Hakika Zakaria, baba yake Yohana Mbatizaji, alikuwa ndiye wa kwanza kuzungumza

na Mungu kwa zaidi ya miaka 400 ya ukimwa. Ndiye aliyetumika hekaluni, na ndiye aliyechelewa hekaluni. Halikuwa jambo la kawaida kuchelewa hivyo. Kwa sababu watu walingojea nje kupata baraka. Waliamini kwamba alikuwa mbele za uso wa Mungu nao aliokuwa awabariki (mara atokapo nje ya hekalu) wangelipokea baraka za kipekee. Hiki ndicho kiini cha Yohana Mbatizaji kujulikana sana.

Wayahudi waliamini kulikuwa na njia mbalimbali ambazo Mungu alizungumza nao:

1. **Kwa kupiga kura** (Mith.16:33).

2. **Urimu na Thumimu** (Kut.28:30). Mawe haya, yaliwekwa katika kifuko kifuani mwa Kuhani Mkuu, aliahidi Mungu kwamba angezungumza na watu wake. Neno la Kiyahudi linamaanisha "nuru na mianga," likionyesha kwamba Mungu angetoa nuru kwa swali watu wake walilomwuliza.

3. **Ndoto na maono**. Hili lilikuwa jambo la kawaida sana. Ndoto hutokea mtu anapokuwa amelala, maono wakati akiwa macho.

Kwa Mathayo kusema jambo hili lilitukia **katika ndoto** anaonyesha kwamba ilitambuliwa kwa ufunuo toka kwa Mungu. Hii ni miujiza, Mungu akijidhihirisha mwenyewe katika maisha ya watu. Angalia kwamba Yusufu anatafakari hayo, lakini amechukuliwa na usingizi akaota ndoto mara malaika akamtoa hofu zake. "**Usihofu**." Asihofu nini? Kuna mambo mawili labda Yusufu aliyahofu:

1. Kudharauliwa kutoka nje - kwa kumkubali mwanamke aliye mzinzi.

2. Kwa kumwoa mwanamke ambaye pengine si mkweli (tena).

**1:21 Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."**

**Yesu** = □ = YEHOSUAH (pia kutoka shina la neno la Kiebrania linalotajwa kama "Yoshua" na "Hosea") - Bwana ni Mwokozi - (linalingana kabisa). Alikuwa awaokoe watu kutoka katika dhambi zao. Ulikuwa huo ni mpango wa Mungu tangu awali.

**1:22 Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema,**

**Litimie** = , moja ya wazo linalotokea mara kwa mara katika Mathayo. Ni mara ya kwanza neno hili kutokea na linatumika mara kumi na tatu katika kitabu cha Mathayo. Neno linamaanisha "kutimilika." Anachosema Mathayo ni hivi ndivyo unabii wa Agano la Kale ulivyotabiri, na hivi ndivyo ilivyonenwa lipate **kutimia**. Alikuwa ni Bwana, aliyesema, alinena kupitia kwa nabii. Ni ukweli kabisa huo na tunapaswa kuwakumbusha watu hivyo tunapofundisha maagano yote mawili la Kale na Jipya. Wengine wanasadiki kuwa haya ni mawazo tu ya mwandishi. Basi inatupasa kusisitiza kwamba **ni Bwana** anayenena mambo haya.

## VIPIMO VYA KUMAANISHA MAANDIKO

**1* Maana ya kawaida, kihistoria na ya kuzingatia mazingira:**

Kimsingi hili maana yake ni kwamba lilitabiriwa, na lingelitimia siku moja. Kwa mfano, Eze.26 na unabii wa Tiro, au Isaya 53 na unabii wa Yesu. Mifano ya aina hii ya unabii ni Math.2:6

(Mik.5:2; Math.3:3 (Isa.40:3); na Math.10:10 (Mal.3:1).

**2*  Maana kamili au ya kiroho - utimilifu mara mbili:**

Hii inamaanisha kwamba fungu katika Agano la Kale litapata kutimilika zaidi au kutambulikana katika Agano Jipya. Mfano wa hili ni Mathayo 2:15 (Hos.11:1) na 2:18 (Yer.31:15).

**3*  Maana ya kimafumbo:**

Gal.4:21-31 (kufananisha). Sara = muungwana, Hajiri = Wayahudi kuendelea kubakia watumwa wa Sheria. Isa.11:1 - shina au chipukizi.

**4*  Utimilifu mara mbili & mfano - mara mbili au kitu chenyewe:**

Kwa mfano ni katika kitabu cha Waebrania hekalu kama mfano, na kanisa kama kitu halisi.

<u>Swali:</u> Ikiwa Myahudi, pasipo kupata msaada wowote ule, "Nikamwita mwanangu atoke Misri," wangetafsiri vipi?

<u>Jibu:</u> Ingelikuwa ahadi ya kwamba Mungu mara nyingine tena angewaokoa watu wake kutoka utumwani au vifungoni.

<u>Swali</u>: Ikiwa Myahudi, yeye binafsi, angesoma Yer.31:15 katika mazingira yake, angetafsirije?

<u>Jibu:</u> Utumwa wa Babeli.

Mungu alilitambua hili lakini alikuwa daima na mpango. Mungu alituma mtu wa kufunua au mwalimu wa kufundisha - Yesu alikuwa mwalimu huyo. Bila ya yeye kuja ingelikuwa vigumu kuelewa mpango mzima wa Mungu. Mitume hawakuelewa maana halisi ya maandiko hadi Yesu alipofufuka na kuwafunulia akili zao.

<u>Swali:</u> Ni jinsi gani Mathayo alitambua kwamba Yer.31:15 ilitimia?

**1:23  Tazama, bikra atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Immanueli; yaani, "Mungu pamoja nasi."**

Nukuu hii inatoka Isa.7:14. Mazingira ya kihistoria ya Isa.7:14 ni hii: katika kipindi cha ufalme uliogawanyika (wakati wa utumishi wa Isaya), falme mbili (Israeli na mfalme wake, Peka; Shamu na mfalme wake, Resini) walipigana na ufalme wa Yuda na mfalme wake, Ahazi. Ahazi, alionyesha kutokuwa na imani kabisa katika Mungu, akaamua kukimbilia Ashuru kuomba msaada, hata ingawa Mungu alimwahidi ulinzi iwapo angemtumani. Isaya alijaribu kumhakikishia kwa kumweleza kuwa hawa vinga vya moto viwili ni wafalme wawili (Resini na Peka), na kwamba wako tayari "kuondoka;" watatoweka, wasiweze kumhangaisha tena Ahazi. Basi, Mungu anasema mipango yao haitafanikiwa.

Ili kumhakikishia Ahazi kusudi la Mungu la kumsaidia, alimwomba Ahazi aombe ishara aipendayo. Ahazi alikataa "kumjaribu Bwana," lakini kiuhakika alikuwa tayari ameazimu akilini mwake, tena kutokufanya kama Isaya na Bwana walivyomtaka afanye. Basi, Isaya akamwambia Bwana hata hivyo atakuonyesha ishara - *Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara, Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli. Siagi na Asali atakula, wakati ajuapo kuyakataa mabaya na kuyachagua mema. Kwa maana kabla mtoto huyo hajajua kuyakataa mabaya na kuyachagua mema, nchi ile, ambayo wewe unawachukia wafalme wake wawili, itaachwa ukiwa* (Isa.7:14-16).

Yesu ndiye, kwa namna ya pekee, aliyetimiza unabii huu.

Kwa jinsi Mathayo anavyolitumia fungu hili tunaweza kujifunza ukweli wa Biblia mwingi:

1. Yesu alizaliwa na bikira - Math.1:25; Lk.1:34.

2. Kuzaliwa kwa Yesu ni utimilifu wa unabii wa Agano la Kale - Isa.7:14

3. Yesu ndiye Imanueli wetu Joh.1:1,14.

**1:24 Naye Yusufu alipoamka katika usingizi, alifanya kama malaika wa Bwana alivyomwagiza; akamchukua mkewe;**

Yusufu alisadiki alichoambiwa na kutendwa na malaika, kusema ukweli, kumwoa mkewe hata ingawa amekuwa na mimba. Tunapaswa kumshukuru sana mtu huyu! Alionyesha kiwango kikubwa cha imani na moyo mkuu. Namna gani alivyovumilia kudharauliwa? Je, familia yake aliifedhehesha? Maswali ya majibu hayo Biblia haijibu.

**1:25 Asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe; akamwita jina lake YESU**.

Huu ndiyo msitari unaoonyesha kuwa alikuwa bikira, na maandiko yanafundisha wazi kwamba Mariamu alikuwa bikira. Kama maandishi mengine yanavyothibitisha, katika Kiyunani hasa inasomeka kama "hakumjua kabisa." Ukweli ni ule ule hata katika Lk.1:24 - "sijui mume." Kwa nini ni muhimu kuzaliwa na bikira? (1) Inadhihirishwa Mungu kuingilia kati kimuujiza katika mambo ya wanadamu ili apate kumwokoa mwanadamu (Yoh.3:16); (2) Ni kueleza kuwa Yesu ni Mungu, kwa maana alipata ujauzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; na (3) hufafanua kuwa Yesu ni mwanadamu, aliyezaliwa na mwanamke (Ebr.2:14). Kama vile Yusufu walivyoonywa, akamwita mtoto **Yesu**. Kama ilivyotajwa katika 1:21, jina Yesu maana yake "mwokozi."

## SURA YA PILI

**2:1 Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalem, wakisema,"**

**Herode** - angalia taarifa za maelezo ya ukoo. Herode aliwekwa mfalme wa Wayahudi na Baraza kuu la Rumi mwaka 37 K.K. kufuatana na Josephus, *Jewish Wars*, uk.1, 282-285. Alilijenga upya hekalu, na alikuwa rafiki wa Kaisaria.

## WATAWALA WA MAHALI MAHALI

1. Arkelao (6 K.K. - 4 K.K.).

Alimiliki Uyahudi, Samaria na Idumia. Utawala wake ulikuwa wa mateso sana hata Wayahudi na Wasamaria wakaungana kutuma ujumbe Rumi kuomba utawala wake uondolewe. Augusto akamwondoa na kumhamishia Vienna Gailo.

2. Herode Antipasi (4 K.K. - 39 B.K.).

Alimiliki Galilaya na Perea. Ndiye yule aliyenyang'anya mke wa nduguye na baadaye akamkata kichwa Yohana. Na pia ndiye alikuwepo wakati Yesu akishitakiwa. Alihamishiwa Lioni Gailo ambako alifia huko.

3. Filipo (4 K.K. - 34 B.K.).

Alimiliki jimbo la Iturea na Trakoniti, Lk.3:1. Nchi yake ni pamoja na upande wa kaskazini-mashariki mwa Palestina. Kaskazini ilipakana na Abilene na Kusini ilipakana na Dekapoli. Ilijumuisha pamoja na Bashani ya kale na Ilauran, na nchi za ukanda kuzunguka usawa wa Herman. Filipo, akiwa kinyume na wengine katika familia yao, alikuwa mtu mpole sana na alitawala ufalme wake vizuri sana. Aliujenga mji wa Kaisaria Filipo juu ya maeneo ya kale ya Manias na akauita kwa jina la mfalme lake mwenyewe. Alikufa mwaka 34 B.K.

4. Lisania.

Alimiliki Abilene, hivyo akapauita kutoka Abila, mji wake mkuu. Hakuwa mmoja wa wana familia ya Herode. Baada ya kifo chake, utawala wake aliongezewa Filipo. Na baada ya kifo cha Filipo, Herode Agripa alimiliki sehemu aliyoongezewa Filipo.

<u>Maliwali wa Rumi 6 B.K.- 42 B.K.</u>

1. Pontio Pilato alikuwa liwali wa sita (wengine hudai wa tano) wa Uyahudi na aliikalia ofisi tangu 27 - 37 B.K. (Wengine hudai 26-36 B.K.).

2. Herode Agripa I - 37-44 B.K.

3. Maliwali wa Rumi 44-66 B.K.

Alipokufa Herode Agripa I, serikali ya Uyahudi ilirejea kwa mawakili ambao miongoni mwao alikuwa Feliki (Matendo 24) na Festo (Matendo 25). Herode Agripa II alikuwa na umri wa miaka kumi na saba tu baba yake, Herode Agripa I alipokufa. Kwa hiyo, Uyahudi iliwekwa chini ya uangalizi wa maliwali hata kufikia Wayahudi walipoasi mwaka 66 B.K. Ingawa Herode Agripa II hakuwahi kutawala katika eneo la Wayahudi, alikuwa na utawala wa karibu wenye kuhusiana na historia ya Agano Jipya (Matendo 25:26). Katika mwaka 48 alimiliki ufalme wa mjomba wake, Herode wa Chalcis, na katika mwaka 53 Klaudia alimpatia majimbo ya kale ya Filipo na Lisania.

Josephus*, <u>Antiquities</u>, uk.27, 317.*

Baada ya wajumbe wa Wayahudi kujaribu kumshawishi Kaisaria Augusto juu ya uovu wa Herode Mkuu na uovu wa aliyembadili Arkelao ambaye aliua Wayahudi 3,000 katika mkutano wa hekaluni, Nikolasi alimtetea Herode na haki yake Arkelao kuwa mfalme. Baada ya kusikiliza pande zote, Kaisaria aliahirisha baraza na siku chache baadaye akamwondoa Arkelao asiwe mfalme hasa, lakini akamkabidhi nusu ya eneo ambalo lilikuwa chini ya Herode, na akamwahidi kumzawadia cheo cha kuwa mfalme iwapo angethibitika kuweza kutenda vyema eneo hilo. Eneo lingine lililobaki likagawanywa katika mafungu mawili na akayakabidhi kwa wana wengine wawili wa Herode, Filipo na Antipasi, wa pili huyu aligombea haki ya kutawala eneo lote pamoja na la ndugu yake Arkelao.

**Mamajusi** = *magoi*; makuhani - wenye hekima - hasa wanajimu wenye ujuzi, kutafsiri ndoto, na mambo mengine ya uganga. (Angalia <u>Arnt and Gingrich</u>, <u>Lexicon</u>, uk. 486). Mapokea kutoka kwa waandishi mbalimbali wa awali kabisa wanasema kuwa walikuwa wafalme watatu (mamajusi), bali maandiko yamenyamaza juu ya idadi au jinsi walivyokuwa ila tu yanadai walikuwa mamajusi.

**Mashariki** - ya Uajemi au Babeli.

Mathayo ndiye mwandishi pekee anayeandika kutembelea kwa mamajusi. Habari hii inalingana kabisa na kusudi lake Mathayo, kwa kuwa anataka kuonyesha jinsi Wayahudi walivyokuwa na mashaka kuwa Yesu ni Masihi, lakini baadhi hawakuwa na shaka. Mamajusi hawa, kwa ujuzi wao wote, waliweza kuona dhahiri kwamba mtoto alikuwa wa pekee.

**2:2 Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliona nyota yake mashariki, nasi tumekuja tumsujudie**.

**Yuko wapi ... mfalme**. Herode pia aliitwa "mfalme wa Wayahudi" (mst.1) na asingependa kushirikiana cheo chake na yeyote. Agano la Kale linasema wazi kwamba Masihi angekuwa mfalme (Yer.23:5; 30:9; Zak.9:9), ingawa si mtawala mwenye jeshi hodari waliyemtarajia Wayahudi.

Ibada = (proskuneo) - kubusu miguu, au kuanguka miguuni - sio lazima iwe kuabudu ingawa mazingira kwa kawaida yanaonyesha wazi kama iliyokusudiwa ni ibada (ama tendo la heshima). Neno hili linatokea mara 11 katika kitabu cha Mathayo - 1:8; 4:9; 4:10; 8:2; 9:18; 14:33; 15:25; 18:26; 28:9; 28:18). **Ibada** ni wazo la ufunguo katika Mathayo, likiwa na mtazamo mkuu unaoonekana katika 4:10. Hawa mamajusi makuhani wanakwenda kumwabudu Yesu na hawaoni aibu kusema hivyo! Mamajusi wanaonekana kutarajia Wayahudi wote kumwabudu huyu mfalme mpya aliyezaliwa. Watakuwa walifadhaika kuona kwamba watu wake Yesu wenyewe hawakumtambua kuwa Masihi.

**2:3 Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.**

**Makuhani wakuu** imetumika kwa namna ya uwingi: pamoja na jamaa zake kuhani mkuu ambao walikuwa katika Sanhedrin (Baraza kuu la Kiyahudi) - ukijumuisha pamoja na kuhani mkuu aliyeongoza, wale walichaguliwa, wanaume wazima washiriki kutoka katika familia zilizojulikana za kikuhani.

**Herode...aliposikia hayo**. Herode alikuwa mtu mwenye mashaka mengi hata Yerusalem ilijaa wapelelezi. Herode alidhania Yesu angemnyang'anya ufalme na kiti chake. Wayahudi, kwa upande mwingine, wangelifurahi kuona serikali ya Rumi ikiangushwa na Masihi mwenye jeshi imara, hasa Wazelote. Walikuwa madhehebu ya kijeshi ya Kiyahudi ambao walimsubiri Masihi mwanajeshi kuja.

**Alisumbuliwa**. Kwa kuwa watu wa Yerusalem walimfahamu Herode alivyo (alikuwa na tabia ya kumwua yeyote aliyempinga), waliingiwa na hofu jinsi Herode angepokea taarifa kuhusu huyo mfalme. Sehemu ya kwanza ya karne ya kwanza, kulikuwa na ghasia za Wayahudi wakijaribu kujitoa katika mateso - damu nyingi za Wayahudi zilimwagika. Mazungumzo yote yaliyohusu mfalme mpya "Lugha ya Kimasihi katika Daudi" yalimaanisha vita kwa Wayahudi - kwa namna ambayo haikuwahi kuonekana kamwe, na hakika, vilitokea mwaka B.K. 68-70. Yerusalem (na Masada wakati fulani baadaye) uliangamizwa. Hivyo walishikwa na hofu nyingi jinsi Herode angefanya.

**2:4 Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi?**

**Waandishi** = walionakili Sheria, watafsiri miongoni mwa Mafarisayo - walikuwa na nafasi katika baraza la Sanhedrin. Hawa wangelikuwa na ufahamu juu ya kuzaliwa Masihi anayekuja. Walikuwa wakitafakari juu ya ahadi aliyoahidiwa Daudi 2 Sam.7.

**Kristo** = mpakwa mafuta. Akififikiri juu ya ahadi aliyoahidiwa Daudi, Herodi alitambua kwamba

kuja kwa wageni hawa waliongozwa na nyota, na kulingana na mafundisho ya Agano la Kale, hatimisho lake la pekee lingelikuwa mfalme huyu mpya asingelikuwa mwingine bali Kristo (Masihi).

**2:5 nao wakamwambia, katika "Bethlehemu ya Uyahudi;" kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,**

Viongozi wa Kiyahudi walijua ingawa kidogo kwamba maandiko yalitaja mahali ambapo Masihi angelizaliwa. Walitambua kuwa katika mji mdogo maili chache kutoka Yerusalemu ndipo mahali Masihi angelizaliwa. Pia walitambua kwamba yale yaliyoandikwa katika maandiko na manabii yalikuwa yamevuviwa.

**2:6 "Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; kwa kuwa kwako atatoka mtawala atakayewachunga watu wangu Israeli."**

Agano la Kale lilitaja mahali maalum ambapo Mwokozi angelizaliwa! Nukuu hii inatoka katika Mika 5:2. Angalia hatumii neno "litimie" hapa. Kwa nini? Kwa kuwa itapingana na jinsi Mathayo anavyolitumia neno hili la pekee la Kiyunani.

Wakuu = viongozi - maliwali - watu wenye mamlaka. Katika muundo ya kiarifa neno hili limetumika kuelezea viongozi wa kijeshi.

**2:7 Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota.**

**Hakika**. Aliwataka mamajusi wamweleze muda nyota ilipoonekana. Kama angekiri kweli kutaka kumwabudu mfalme mpya, Yerusalem yote ingelitambua unafiki wake.

**2:8 Akawapeleka Bethlehemu, akasema, "Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie.**

Hakuna sababu ya kufikiri kwamba mamajusi walitilia shaka imani ya mfalme. Hata hivyo, inawezekana kwamba waliona jambo hili kutowavutia wenyeji wa Yerusalem, pengine walidhania kwamba taarifa hazikuenea vya kutosha za kuzaliwa kwa mtoto Kristo.

**2:9 Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota walioiona mashariki ikawatangulia, ikasimama, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto**.

Ingawa hata wengine hutia shaka jinsi Mungu alivyoweza kutenda hili (angalia maelezo juu ya "Maoni ya Nyota") ni moja mifano ya Mungu akitenda chochote atakacho ili kufanikisha mapenzi yake.

**2:10 Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno**.

Mamajusi walifurahia Mungu akitenda kazi katika maisha yao. Walifurahia kwa sababu ya mwongozo walioupata toka kwa Mungu. Kadhalika walifurahi kuwa na fursa kumwona mtoto huyo wa pekee.

**2:11 Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipofungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane.**

**Dhahabu**. Madini ya thamani - yakini hayajasafishwa, au kuwa katika vito, n.k.

**Uvumba**. Sandarusi (gum) nyeupe iliyo na manukato mazuri sana, inayopatikana katika miti aina mbalimbali ya Uarabuni.

**Manemane** = smurnan - ni neno lilo hilo "Smirna;" iliyozalishwa na kuuzwa katika mji huu - utomvu wa sandarusi kutoka katika miti, "Balsam Odendron Myrrha;" yenye harufu nzuri na iliyotumika kuhifadhia maiti - Ufu.18:13; Yoh.19:39; Wimbo 3:6.

Hii inaonyesha jinsi walivyomwamini Yesu kuwa mfalme, kwa maana wale tu wa ukoo wa kifalme ndio waliopewa zawadi bora kama hizo.

**2:12 Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudi Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.**

Katika ndoto waliambia mamajusi chakufanya. Yusufu pia alikuwa na ndoto (1:20), ikionyesha tena muujiza wa Mungu akiingilia kati. Mpango wake umetekelezwa.

**2:13** Ndoto ya tatu.

**2:14 Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda ake Misri;**

Ulikuwa umbali wa maili 100 hadi mpakani mwa Misri; maili 200 hadi Mto Nile.

**2:15 Akakaa huko hata alipokufa Herode; ili litimie neno lililonenwa Bwana kwa ujumbee wa nabii, ikisema, "Kutoka Misri nalimwita mwanangu."**

Mara nyingine tena tunaona neno "litimie" (pleroo). Jambo hili linadhihirisha unabii kutimia mara mbili. Hos.4:1 ni kutimia kwingine kwa neno "litimie" (pleroo). Kwa Mathayo neno **litimie** lina wazo ndani yake Mungu akitekeleza makusudi yake - mpango wake aliotangulia kuupanga unatekelezwa - kwamba maana ya kiroho ya maneno haya ya Agano la Kale yanatekelezwa katika Yesu.

**2:16 Ndipo herode, alipoonywa ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhabika sana, akatuma watu akawauwa watoto wanaume waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi.**

**Uhakika wa muda**. Luka anasema usiku Yesu aliozaliwa wachungaji walimwendea kutoka makondeni kumwona mtoto katika hori la kulia ngo'mbe. Mathayo haonyeshi jambo lolote juu ya wachungaji hawa. Inawezekana kwamba Yesu alikuwa na miaka miwili kwa maana 2:11 panasema walimwendea nyumbani na wala si katika zizi la ng'ombe.

**2:17 Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii Yeremia, akisema,**

Litimie - mpango wa milele - Efe.3:11 (aina 3 tofauti za unabii):
- Mst.6 - moja kwa moja,
- Mst.15 - mafumbo (lakini wenye utimilifu katika matukio mawili),
- Mst.16 - utimilifu mara mbili au katika matukio mawili.

**2:18 Sauti ilisikiwa Rama, kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako.**

Huu pia ni unabii uliotimia mara mbili. Angalia maelezo katika “Vipimo vya maana ya Maandiko.”

Rama ulikuwa mji katika Benyamini. Nukuu hii asili yake Yer.31:15 ikilenga utumwa waBabeli.

**2:19 Hata alipofariki Herode, tazama, malaika w Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri,**

**Ndoto**. Ni mara ya nne sasa malaika wa Bwana kumtokea. Hii inazidi kudhihirisha matukio ya mwanadamu yakingiliwa na nguvu za kimiujiza.

**Herode** alikufa akiwa na umri 70 (alitawala miaka 37).

**2:20 Akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto.**
**2:21 Akaondoka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli.**
**2:22 Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Uyahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya,**

Hii ni mara ya tano malaika wa Bwana ametokea katika ndoto. Jimbo hili lilitawaliwa na Arkelao kutoka mwaka 4 K.K. Josephus, Wars 2, uk.94-97 anasema, “...alikuwa mtu mbaya mwenye ushawishi mkubwa kuchukua hatua kisiasa.”

**2:23** Angalia Waamuzi 13:5-7 - sehemu pekee katika Agano la Kale tunapoona fungu linalofanana. Katika kutimiza mpango wa Mungu angekuwa Mnazareti na angewaokoa wanadamu kutoka dhambini. Inawezekana pia kuwa kuna uhusiano na Isa.11:1, ambapo neno “shina” Kiebrania ni HETZER, ambalo neno “Nazareti” linatoka.

## SURA YA TATU

Katika Luka 3:1 tunajifunza muda wa mambo haya kutendeka. Kama huu ni mwaka wa 15 wa kutawala kwake Tiberio, tunatazamia karibu miaka 28 baada ya tukio la sura ya 2 kutukia. Miaka hii inachukua kipindi kirefu, ambacho kinastahili tukitaje. Injili haipo kuelezea historia toka kipindi fulani hadi kipindi cha Yesu. Wanatupatia mpangilio bora wa maisha ya Yesu pamoja na matukio na mafundisho muhimu ili kutufundisha na kuthibitisha ukweli. Kazi ya Roho Mtakatifu hapa imedhihirika kwa kutupatia mambo muhimu hata ingawa tungelipenda kujua zaidi. Kuna maandishi karibia mwishoni mwa karne ya kwanza yanayosimulia kuhusu Yesu, akiwa anafinyanga njiwa kwa udongo wa mfinyazi, na kumtia hai. Bila shaka, haya ni moja ya hadithi za uongo kuhusu maisha ya Yesu utotoni. Kuna wengini wanaotamani kuona zaidi, bali tulichonacho kimehifadhiwa na Roho Mtakatifu kwa njia ya maandishi kitabuni.

**3:1 Siku zile alliondikea yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema,**
**3:2 Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia**.

Neno **tubu** ni neno lililoundwa kwa maneno mawili katika Kiyunani - META na NOEITE - maneno yenye maana “kugeuka akili.” Mahubiri ya Yohana yalihitaji kugeuka, kama vile mahubiri ya manabii katika Agano la Kale, na ndilo Yohana analifanya hapa. Ameitwa “Mbatizaji” kwa kuwa Mungu aliyemwamuru kubatiza. (Angalia Math.21:23ff). Yesu anawatia mashakani wakuu hao washindwe kujibu mamlaka ya ubatizo wa Yohana. Waliamua kutokujibu lolote kwa maana wangejishtaki wenyewe. Jibu sahihi ni, “Ulitoka kwa Mungu.” Ingawa

kulikuwa na batizo zingine miongoni mwa Wayahudi kabla ya ule wa Yohana, ulichukua sura mpya kufuatia mafundisho ya injili.

Yohana aliwataka **wageuke** - watubu - kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Karibia ni "angiken." Maana yake "umesogea karibu" au "umejongea jirani." Wale waliokuwa wakimsikiliza Yohana wangeelewa hili kuwa na maana kadhaa. Muda umekaribia, au umesogea jirani? Mathayo atalijibu swali hili kuhusu kukaribia kwa ufalme. Lakini kwao hawa aliokuwa akiwafundisha hawakuelewa hili. Walakini ukweli ni "umekaribia" msingi wa kutosha kwa watu kuanza kutafakari juu ya maisha yao.

**3:3 Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, "Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheeni mapito yake".**

Isa.40:3 ndipo aliponukuu. Yohana alikuwa na kazi maalum ya kufanya, na hiyo ilikuwa kuwaandaa watu. Msitari huu umenukuriwa kwa sababu Yohana amekuja na kutaka watu watubu. Lakini, fungu hili ni mfano kwa watu wa kale walivyokuwa wakiandaa njia kwa ajili ya wafalme wao, wakiangalia kuwa visingelikuwepo vikwazo barabarani kumzuia mfalme kusafiri. Yohana, kwa maana ya kiroho, ataandaa mioyo na akili za watu hawa kwa ajili ya Kristo ajaye, na alifanya hivyo barabara!

**3:4 Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singe za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu.**

Angalia ulinganifu wa Yohana na Eliya - 2Fal.1:8; ndiye yeye, kama tutakavyoona, utimilifu wa unabii. Moja ya jambo linalochanganya ni, Yoh.1:21 ambapo watu wanauliza, "U Eliya wewe?" akasema, "Mimi siye." "Mbona basi wabatiza?" Hawakuelewa mamlaka yake. Yohana anasema kuwa yeye siyo Eliya lakini katika Mathayo 17:10, baada ya Eliya na Musa kujitokeza wakiwa pamoja na Yesu mlimani alipogeuka sura, Yesu anasema kuwa Yohana ndiye Eliya. Basi, walikuwa wakimtarajia Eliya *kuja katika mwili*, na Yohana alitambua kile walichotarajia. Katika Mal.4:5 Yohana alikuwa ni *roho* ya Eliya yule ajaye na kutengeneza mambo kabla ya kuja Masihi. Mathayo anadhamiria kufanya juhudi ya kuunganisha Yohana na Eliya. Yohana alikuwa mtu wa nje ambaye hakutafuta ofisi ya kustarehe ndani. Alikuwa mtu aliyejitoa wakfu kuzitafuta roho.

**3:5 Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yordani;**

Neno la Kiyunani "pas" limetumika kwa ajili **wote**, lakini hapa halina maana kila mtu mmoja. Itakuwa si vyema kufikiri kwamba watu wote maeneo yale walimwendea, ingawa kulikuwa na idadi kubwa waliomwendea. Tatizo halipo katika Kiyunani, bali katika tafsiri, kwa maana tunaelewa "wote" kama kila mtu. Mazingira ndiyo yanadhihirisha ikiwa inamaanisha "wote." Neno la Kiyunani lililotumika hapa lingemaanisha "wote," iwapo tu mazingira yangeonyesha hivyo. Neno hili limetumika mara nyingi kwa jinsi ya kusifia kuonyesha idadi kubwa, sio likiwa na maana bayana kila mtu. Lk.7:30 tunaelezwa wanasheria na Mafarisayo walipinga shauri la Mungu - baadhi, na sio wote.

Josephus anaeleza kwamba Yohana alijulikana sana hata Herode Antipasi akahofu kuzuka kwa ghasia. (Antiquities 18:.5.2). Walibatizwa Yordani kwa kuwa huko kulikuwa na maji tele. Angalia Yoh.3:23.

**3:6 naye akawabatiza katika mto Yordani, huku wakiziungama dhambi zao**.

***Tofauti katika Batizo hizi.***

| **Yohana** | **Injili** |
|---|---|
| Wayahudi tu | Mataifa yote |
| Kwa ajili ya toba na ondoleo la dhambi Mk.1:4 | Kwa imani na toba kwa ajili ya ondoleo dhambi |
| Uliwarejeza Wayahudi katika agano la kale | Unawaleta wote katika agano jipya |
| Ulitazamia mbele Kristo Math.3:11 | Ulimwangalia Kristo kwa nyuma |
| Haukufutiwa na kipawa cha Roho Mtakatifu | Ulifuatiwa na kipawa cha Roho Mtakatifu |
| Siyo katika jina la Kristo | Katika jina la Kristo Math.28:18-20 |
| Sio katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu | Katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu |

Kanisa la awali lilibatiza kwa jina la Yesu - Matendo 2:38; 8:35,36; 10:48. Paulo alisema kuwa kuna ubatizo mmoja tu - Efe.4:4. Ubatizo huo mmoja lazima uwe ubatizo wa maji - 1Pet.3:21 na mifano yote katika Matendo 8:36. Katika Matendo 18:25 Apolo alielewa ubatizo wa Yohana tu ingawa ubatizo wa Kristo ulikuwa tayari umefundishwa na kutekelezwa. Hivyo basi, alipaswa "kuelezwa njia ya Bwana kwa usahihi zaidi." Katika Matendo 19:1-7, ikifuatia mafundisho ya Apolo, waliobatizwa kwa ubatizo wa Yohana (yaani baada ya kifo, na mafundisho ya ubatizo wa Yesu) waliamuriwe wabatizwe tena - Matendo 19:5. Usitumie fungu hili kufundisha kwamba waliobatizwa wakati wa Yohana Mbatizaji walibatizwa tena. (Angalia maelezo katika Yohana). Wale wote katika Matendo 19 waliamuriwa kubatizwa tena kwa kuwa walibatizwa wakati ule wa Yesu ulipokuwa tayari ukitenda kazi. Tunalitambua hili kwa sababu ulitendeka kwa sehemu katika kitabu cha Matendo. Kazi ya Yohana ilikuwa ni kuwaandaa watu kumwendea Kristo, sio kubatizwa katika jina la Kristo. Ubatizo "mmoja" unaozungumzwa katika kitabu cha Waefeso ni ubatizo wa Kristo.

**Huku wakiziungama dhambi zao**. Jambo hili halikuwa geni. Katika Agano la Kale ungamo lilitendeka kwa kutoa sadaka za dhambi - Hes.5:7. Ilikuwa pia ni muhimu kwa ajili ya wokovu - Zab.32:5; 51:1ff; Mith.28:13; Ezra 9:6ff; Dan.9:5ff; katika Agano Jipya angalia 1Yoh.1:9; Rum.10:9,10. Kwa kuziungama dhambi zao kukiri hadharani kulifanywa ili kupatana na Bwana. Waliungama hadharani kuonyesha waliacha kutenda dhambi tena.

**3:7 Hata alipoona wengi miongoni mwa Mafarisayo na Masadukayo wakiujia ubatizo wake, aliwaambia, Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja?**

Mafarisayo na Masadukayo hawakuwa tayari kugeuka kwa vyovyote. Mathayo anarejea Mal.4:5,6. Fungu hili pia linazungumzia Kristo kuja, na Eliya. Inadhihirisha kwamba kuja kwake

Masihi kusingelikuwa baraka zote. Wayahudi walidhania kuwa hasira yake ilikuwa kwa ajili ya Mataifa tu.

**Wazao wa nyoka** = nyoka. Wasomi wanafikiri ni aina fulani za nyoka katika Palestina; urefu futi 2-5, unene nchi 1, zenye vichwa bapa, rangi ya njano pamoja na madoa ya kahawia marefu, zenye sumu kali. Kijana wa jangwani angelifahamu nyoka hawa. Yaani Yohana anamaanisha kwamba viongozi wa Kiyahudi walikuwa wamejaa hila, uovu, ujanja, na uchungu. Maneno **"hasira itakayokuja**" ni fungu linalofurahisha kujifunza. Paulo, katika Rum.2:4-5, anazungumzia kuhusu siku ya hasira, na ufunuo wa ghadhabu (hasira ya Mungu) ikiwajia wale wote wasio na mioyo yenye toba. Linga.Rum.1:18; 5:9; Efe.5:6; Yoh.3:36; 1Thes.1:10; Ufu.6:16,17.

**3:8 Basi zaeni matunda yapasayo toba**

Ubatizo bila toba haufai kitu. Watu ni lazima kuzaa "matunda." Matunda ni namna nyingine ya kusema *matendo ya haki*. Kuna wengine wanaodhania kwamba mahali popote Biblia inapozungumzia matunda, inamaanisha kuwaokoa watu kwa Kristo. Walakini hiyo siyo njia sahihi. Watu wanapaswa kuzaa matendo ya haki - Isa.3:10; 10:12; Yer.17:10; Math.7:16,20; 12:33; 21:43. Tunatambua kama Wakristo kuwa na matunda ya Roho, Gal.5:22, lakini Luka anatoa maelezo ya msingi juu ya mahubiri Yohana alifundisha. Kuna makundi matatu yanayouliza swali, "Yatupasa tufanye nini?"

1. Makutano - Lk.3:10,11 - Yule aliye na kitu na amgawie asiyenacho.

2. Watoza ushuru - Lk.3:12,13 - Msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamuriwa.

3. Maaskari - Lk.3:14 - Msidhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo, tena mtoshewe na mshahara wenu.

Mfano mzuri unaolingana na huu ni Yakobo 2:14-26.

**3:9 wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, Tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.**

Yohana anasema kwamba ni zaidi ya kuwa tu mzao wa Ibrahimu ili kumpendeza Mungu. Kama alama ya kuwaonyesha Wayahudi walivyofikiri uhusiano wao na Ibrahimu uliwanufaisha, ebu na uchunguze:

**<u>Nukuu kutoka Kitabu cha Mafundisho cha Wayahudi (Talmud)</u>**

"Abrahamu amekaa kandoni mwa milango ya Kuzimu, na kutoruhusu Mwisraeli yeyote mwovu kupita huko."

Inamwakilisha Mungu akimwambia Abrahamu:

"Ikiwa wanao wangelikuwa miili bila mishipa na mifupa, ujira wako ungeshinda."

"Mwisraeli mmoja anathamani zaidi mbele za Mungu kuliko watu wote waliokuwepo na watakaokuwepo."

"Dunia iliumbwa kwa ajili ya Waisraeli (ya Mwisraeli).

*Ijara za Baba,* Mekilta Beshallah 4:30 *(*Linga.Justin*, Dialogue with Trypho,* 140:2).

**3:10 Na shoka imekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni**.

**Na shoka imekwisha kuwekwa penye mashina ya miti**. Hili linaelezea ukweli wa kwamba hukumu imeanza na i-juu ya kila **mti** usiozaa. Yohana anasema kusita kwao kunaweza kuwaletea mauti. Ikiwa mtu hazai matunda ya toba, ingemsababishia mauti. Shoka inasimamia hukumu ya Mungu juu ya wanadamu. Mafarisayo na Masadukayo wamejifunga na yale wanayotenda, hawakuwa wakifanya mapenzi ya Mungu. Walitambua hilo, lakini hawakutenda yapasavyo.

**3:11 Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto**

Yohana atazungumzia mambo mawili.

1. Kusudi la ubatizo wake - wapate kutubu, na kuwaandaa kuingia katika ufalme ujao;

2. Kufafanua wazi kushinda kwao kumwelewa kuwa alikuwa Kristo. Alikuwa tu akimtengenezea njia "Yeye anayekuja" - Mal.3:1, Unabii wa Kimasihi.

**Wala sistahili hata kuvivua viatu vyake**. Katika familia za Kiyahudi zenye uwezo watumwa walibeba viatu vya mabwana zao. Yohana anasema huyo ni mkubwa zaidi na mwenye uweza kuliko yeye mwenyewe hata hastahili kuvichukua viatu vyake.

**Roho Mtakatifu na Moto**. Fungu hili limechanganya watu wengi sana.

1. Wengine wamedhania kwamba Yesu asingelibatiza kwa maji. Kuna mafungu mengine mengi ambayo yanaonyesha kuwa hivyo sio kweli, na hivyo basi ubatizo wa Kristo hauna kitu kingine isipokuwa maji - Matendo.8:36.

2. Kwa Roho Mtakatifu. Matendo 2 panaonyesha maana ya kubatizwa katika Roho Mtakatifu na katika Matendo 11:15 Petro anadai kwamba ilitokea kwa Kornelio kama ilivyotokea kwao pale mwanzo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu umetukia mara mbili.

3. Watu wengi (hasa makundi ya Kipentekoste) wameomba kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na moto, walakini sivyo hivyo wanavyotamani kupata. Neno la Kiyunani kuhusu **moto** ni "puri." Katika mst.11 tunasoma ubatizo wa Roho Mtakatifu na moto. Katika mst.10 tunasoma miti isiyozaa matunda, ikikatwa, na kutupwa katika **moto**. Na hiyo ni hukumu. Mst.12 "Pepeto lake li mkononi mwake, ... bali makapi atayateketeza kwa **moto** usiozimika." Hii ni hukumu. Hatuwezi kudai moto katika mst.10 na 12 unamaanisha jambo moja, na kisha mst.11 kudai kitu kingine tofauti. Kwa hiyo anazungumzia maoni aina mbili za ubatizo wa Yesu. Hili halihusiana kabisa na ndimi za moto katika Matendo.

Mstari 12 unafanana na yale yanayozungumzwa Ufu.20:15, "Alitupwa katika lile ziwa la moto." Moto katika Mathayo mistari yote hiyo inamaanisha - HUKUMU. Yesu ana mitazamo miwili katika huduma yake; kufanya kinachookoa watu, au kufanya kinachosababisha wapotee. Jambo lilo hilo litasababisha wengine kutubu, wakati huo huo wengine wataifanya mioyo yao kuwa migumu na kutotubu. Mawazo ya kutakaswa katika moto ni potofu, kwa maana hiyo ingekuwa tofauti na kinchoongelewa katika mazingira haya.

**3:12 Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake gharani mwake, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.**

Pepeto lake - kama jembe lenye meno la kukokotea taka (rake) au fimbo ya panda ya kupangia majani yaliyokatwa (pitchfork), ilitumia kupepetea ngano uliyovunwa na kuiludika uwandani. Makapi, ambayo ni mepesi, upepo ungeliyapeperusha. Nafaka, zikiwa ni nzito kuliko, zingelianguka uwandani. Maneno "moto usiozimika" yanapinga mafundisho mawili ya uongo:

1. Mafundisho ya wokovu kwa ulimwengu mzima - Mungu atamwokoa kila mtu,

2. Mafundisho ya maangamizi - mtu kutoweka kutokuwepo. Uzima wa milele hautahitajika iwapo adhabu itakuwa ya muda kitambo tu, lakini moto huu ni "usiozimika," ikionyesha kwamba adhabu itakuwepo kadiri moto utakavyokuwepo. Linganisha Math.25:46.

**3:13 Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe.**
**3:14 Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?**

Yohana alifahamu na kutambua kikamilifu kuhusu Yesu kuwa ndiye, kama mtu mwenye dhambi, alivyohitaji msamaha wa dhambi uliohusiana na ubatizo (Yesu) wake.

**3:15 Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali**.

Msitari huu watu wengi wanashindwa kuuelewa. Yaani maana yake hilo ni kwamba Yesu, akitambua kuwa yeye ni mwanakondoo asiye na dhambi, sadaka kamilifu, alistahili afanye yale Mungu aliyoamuru. Katika kuona kuwa Yesu anaeleza umuhimu wa kubatizwa, basi ni muhimu zaidi kwetu sisi kubatizwa? Tunahitaji dhambi zetu zioshwe. Yesu alihitajika tu kwa sababu Mungu aliamuru, angelikosa ikiwa asingetii Mungu alichomwamuru mwanadamu afanye. Mungu anafungua mlango kwa kizazi kipya. Ubatizo haukuamuriwa katika Agano la Kale. Yesu alibatizwa kwa kuwa uliamuriwa na Mungu. Watu walipaswa wamtii Yohana alichofundisha, kwa maana ilikuwa Sheria ya Mungu. Yesu alifanya hivi kutimiza haki yote. Zab.119:172 ni mfano mzuri katika hili, "Ulimi wangu na uiimbe ahadi yako, maana maagizo yako yote ni ya haki." Hilo ndilo limetendwa hapa na Yohana Mbatizaji. Hakika Mungu anatarajia watu kuelewa hilo kwa kuwa katika Math.22 Yesu anauliza ikiwa ubatizo huo ulitoka kwa wanadamu au kwa Mungu.

**Basi akakubali** - hilo linadhihirisha kwamba Yesu alibatizwa.

**3:16 Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake**;

Neno la Kiyunani lililotumika kufafanua kitu kinacholingana na kingine ni "hos." Ni <u>mfano</u> wa hua, siyo hua halisi. Lk.3:22 inaondoa mashaka yote - Roho Mtakatifu akashuka "kwa mfano wa kiwiliwili kama hua." <u>Hakuwa</u> hua bali kwa <u>mfano</u> wa hua.

Tunalinganisha ushahidi wa kwamba Yesu ni Masihi, na tulichokiona katika 3:1-12 ni utimilifu wa aliyeitengeneza njia ya Masihi. Yohana alikuwa ndiye Eliya ajaye. Mathayo alikuwa akijaribu kuwastajaabisha wasomaji kuhusu huyo alivyo. Katika sura 11 na 17 atatueleza kwamba Yohana ndiye huyo Eliya. Ubatizo wa Yesu umekuwa zaidi na unabii wa Masihi Wayahudi wasingeshindwa kufahamu hilo.

Isa.11:2 anasema, “Na roho ya Bwana atakaa juu yake...” - fungu ambalo Talmud bayana inakiri kuwa ni fungu la Kimasihi. Mafungu yote haya katika Agano la Kale yamefafanuliwa wazi katika Talmud yakimhusu Masihi. Hivyo basi Wayahudi wangeuelewa ubatizo wa Yesu na kushuka kwake Roho juu yake. Luka, katika Matendo 10:38 anasema Yesu alitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, na Mathayo anatueleza kwamba Yesu alifanya miujiza kwa Roho. Injili hii imekuwa zaidi na habari kuhusu unabii huu, na Talmud inakiri mafungu haya ni ya Kimasihi.

**3:17 na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye**.

Ukweli kwamba sauti ilitoka mbinguni ni jambo la msingi kwetu ingawa majadiliano yanaendelea kuhusu ama sauti kusikika na kila mtu au la. Jambo muhimu katika Mathayo ni lile kinachotokea mbinguni. Hapo baadaye katika Mathayo watu watomba kupewa ishara kutoka mbinguni, kwa sababu waliamini nguvu za shetani zisingeliweza kufanya lolote angani - Math.16:1. Msitari huu ungekuwa ushahidi zaidi kwa Wayahudi. “Mwanangu mpendwa.” Kuna mambo matatu yaliyoelezwa hapa kuhusu Yesu:

1. *Yeye ni Mwanawe* - Zab.2:7, fungu dhahiri la Kimasihi. Angalia Ebr.1:5 na Mdo.13:33.

2. *Anayependwa* - Isa.42:1. “Mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye...” Mwanawe atapendwa.

3. *Anayependezwa naye* - Isa.42:1; 44:2. Tena, utimilifu wa Kimasihi.

Mambo matatu yanayomweleza Yesu yote yanamdhihirisha Yesu kuwa Masihi.

Katika Zab.2:1-7 Daudi anamtaja Mwana wa Mungu kuwa “Mtiwa mafuta wake.” Yesu alifanyika kuwa Masihi alipobatizwa, na Roho wa Mungu akawa juu yake. Kufikia hatua hii alikuwa ametiwa mafuta tayari, na ukweli kwamba Mungu anapendezwa naye umetimiza matarajio yote yake na huyo ndiye asiye na hatia. Hata kufikia Math.28:18-20 ambapo Yesu anasema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.” Tunapozungumzia juu ya kupakwa mafuta, tunatakiwa kuchukua muda kujifunza Agano la Kale kuelewa jambo hili. 1Sam.10:7 - Sauli alitiwa mafuta, hakutwaa kiti cha enzi hadi hapo baadaye. 1Sam.16:13 - jambo kama hilo lilitendeka kwa Daudi, ambaye alitwaa kiti cha enzi baadaye sana.

Kwanza kabisa Yesu alitiwa mafuta, huduma ikafuatia, na akapata mamlaka baada ya kufufuka. Katika Matendo 10:38 Petro anasema, “Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu; naye akazunguka huko na huko...” Petra bayana anajumuisha haya pamoja. Ilikuwa baada ya kufufuka Yesu akapewa mamlaka yote. Haya yote yalikuwa moja ya mipango yake Mungu. Yesu ndiye aliyetiwa mafuta, na alikuwa na kazi za kuzitekeleza kwanza, na kulikuwa na wakati wa kushughulikia kwanza. Lk.3:23 anatufafanulia kuwa Yesu alikuwa mwenye umri kama miaka thelathini wakati huo. Ni jambo la kuvutia kuona kwamba Roho Mtakatifu alishuka kwa mfano wa hua kisha akamwongoza jangwani ili ajaribiwe katika sura 4:1.

## SURA YA NNE

**4:1 Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi**.

Ukweli wa kwamba aliongozwa na Roho inaonyesha ilikuwa kusudi la Mungu kwamba Yesu angelipitia maudhi hayo, majaribu haya. Aliongozwa hadi mahali ambapo angejaribiwa. Mungu si ndiye mjaribu, bali anaruhusu ajaribiwe.

***Angalia maelezo ya nyongeza juu ya Shetani.*

**4:2 Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.**

Inaonekana kushangaza kidogo kwamba Yesu angefunga kwa kipindi kirefu na **kisha** kuona njaa. Tunapaswa kuelewa kwamba miili yetu inatenda kazi kwa namna fulani kunufaika na hili. Matumbo yetu yanapoanza kuunguruma tunahusisha hivyo na njaa, lakini hivyo ni kufungua matumbo kwa chakula kilichobakia. Mwili unakuwa hauhitaji chakula wakati huo. Waliozoelea kufunga wanaweza kwa urahisi kufunga kwa kipindi cha muda huo. Inaposemekana kwamba, "**Mwisho akaona njaa**," inaonyesha kwamba wakati wa kufunga. Kwanza, mwili unatumia ghara ya akiba (mafuta yake) ikiwa hautapata chakula. Kisha, yakisha tumika yote, mwili unaanza kula misuli. Inapotukia hivi, maumivu ya njaa ya kweli yanaanza na mwili unanza kujiila wenyewe na maumivu ni makali. Fungu hili linatufunza kwamba Yesu ana uzoefu wa kufunga, lakini baada ya siku 40 usiku na mchana, mwili wake ulifikia hatua ambayo ulianza kula misuri. Kwa kuwa mwili, kufikia hapa, unahitaji chakula kuliko wakati mwingine wowote ule, basi ukawa wa mpango wa yule mwovu Shetani kusubiri muda huo kumjaribu Yesu. Shetani hupenda kutujaribu sisi wakati tuwapo dhaifu. Angalia kuhusu kufunga: wakati Agano Jipya haliamuru kufunga, Wakristo bado wanaona faida kubwa ya kufunga. (Angalia maelezo: Math.6:16 Yesu anasema "Nanyi mfungapo..." akiona kwamba watu wa kiroho watufunga). Angalia <u>faida za kufunga</u>:

1. Tunapofunga matumbo yanakuwa yangali bado yanatembea, kwa maana mwili unakuwa ukijisafisha wenyewe. Kufunga ni kuzuri kwa ajili ya mwili. Vyakula vyetu vimejaa kemikali, tunazihifadhi na zinatusababishia matatizo. Kusafisha kwa kufunga ndiyo hatua kuyaondoa yatoke katika mifumo yetu.

2. Kwa nyongeza, kufunga ni kupata maarifa bayana kiroho. Kama kawaida mfungaji anajitoa wakfu kutokula muda wa kula kwa mambo ya kiroho, hivyo kiroho hunufaika.

3. Pia, kuna faida ya kujitia nidhamu. Wafungaji hujifunza kujizuia wenyewe moja ya mahitaji ya msingi ya mwanadamu - chakula. Wakishafaulu vyema kufanya hivi, wanaweza kuona ni jinsi gani wana uwezo wa kutawala tamaa zao.

**4:3 Mjaribu akamjia akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.**

Neno **"ikiwa**" hapa lipo katika daraja la kwanza la tungo tata na kiusahihi linamaanisha "kwa kuwa." Shetani hamtilii shaka Yesu kuwa ni mwana wa Mungu. Inatakiwa itafsiriwe kama, "Kwa kuwa wewe ni mwana wa Mungu" hivyo basi, kwa kuwa wewe ni Mwana wa Mungu, Shetani anasema, una uwezo kugeuza mawe haya kuwa mkate na kukufaa juu ya njaa yako. Shetani anajaribu kushambulia eneo ambalo Yesu ni dhaifu. Hili bado lingali jaribu analopenda shetani kwa maskini. Ikiwa Mungu anatupenda, kwa nini basi tunahofu juu ya chakula - kwa nini tuna njaa daima? Watu wanapaswa kuelewa kwamba kufanikiwa kimwili/ vitu ndicho kipimo cha kuonyesha upendo wa Mungu kwetu (agalia Lazaro katika Lk.16). Yesu asingelitumia miujiza kutimiza matakwa yake ya mwili.

**4:4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu**.

Kumb.8:3 ndipo aliponukuu. Mapenzi ya Mungu ni muhimu kuliko chakula. Yesu hakufanya miujiza kwa ubinafsi, wala Paulo (2Kor.12), wala yeyote yule aliyetenda miujiza. (Epafrodito, Fil.2:25-27; Trofimo 2Tim.4:20).

**4:5 Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu**,

Jaribu la pili. Wasomi wamejaribu kujadili juu ya eneo hili jaribu lilipotendeka. Ilikuwa ni eneo la juu la hekalu. Wengine wanadhani kuwa ilikuwa karibu na Bode la Kidroni, na wengine wanafikiri kuwa mkabala na hekalu - upande wa Magharibi - eneo lililoitwa "kinara." sababu ya kumleta hapo ilikuwa Yesu awe na mwinuko mrefu wa kunguka, hata kubainisha wazi kwa watu wote kwamba miujiza ilitendeka.

**4:6 akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, atakuagizia malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.**

**Ukiwa** - ikimaanisha "kwa kuwa."

Angalia hata Shetani anaweza kunukuu maandiko - Zab.91:11, 12 ndipo nukuu ilipotoka. Lakini, hata ingawa Shetani anaweza kunukuu maandiko, hayatumii vyema. "Basi nenda. Jitupe chini. Malaika watakuwepo pale." Mtoa maoni mmoja alisema kuwa Waalimu (Rabbis) walifikiri Masihi ni mtu ambaye angesimama juu ya kinara cha hekalu, mwanga ungemmulika, na angeelea hewani kuelekea chini kwa watu. Maandishi hayo yangekuwa ndio msingi kwa hili, lakini hakuna mtu anayejua kwa uhakika.

**4:7 Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako**.

Shetani alitambua ingelikuwa dhambi kumjaribu Mungu kwa njia hii. Nukuu hii imetoka Kumb.6:16. Watu walikosa maji na wakamlaumu Musa kwa kuwaleta huko wafe. Walimwamuru Musa awapatie maji kuona kama Mungu kweli alikuwa pamoja nao. Walimjaribu Mungu kuona kama alikuwepo mbele yao. Yesu asingelimwamuru Mungu afanye miujiza kwa sababu ya kitendo cha upumbavu chake mwenyewe.

Fafanuzi: Wengi hudai, "Huu pengine sio muda wangu wa kufa." Pengine Mungu anatarajia wewe uishi muda fulani, lakini kama unaamua kujilaza chini ya reli za treni linalokuja, muda wako utabatilika. Inamaanisha kwamba wakati huu wa Yesu yeye hakutazamia maono, n.k. kumpatia nguvu. Alipojaribiwa, hakukubali! Yesu alitengemea neno **lililoandikwa**. Yesu alipambana na majaribu kama mwanadamu (Fil.2:6,7), akatumia silaha ambayo Mungu amempatia mwanadamu (Efe.6:17) - neno la Mungu, upanga wa Roho. Hawa alianza kwa njia nzuri, lakini hakudumu katika hiyo, na akaanguka katika majaribu aliyojaribiwa na Shetani.

**4:8 Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake**,

Ufalme ni wazo la ufunguo katika injili, basi tunapaswa kuangali mstari huu kwa uangalifu sana. Ufalme ungekuwa jaribu kwa sababu ya fahari na utukufu (ingawa bure), aina hiyo ya nguvu. Yesu angeweza kutafakari: "Kwa kuwa mimi ninaenda kuwa mfalme vyovyote vile, kwa nini nisifanya hivi? Basi kutakuwa na nini iwapo nitatenda kosa dogo? Naweza kutenda mema mengi baadaye." Watu wengi wametenda mabaya wakijipofusha akili kwamba mema fulani yatatoka humo (k.m. uongo akiamini kwamba utaleta matokeo mema, etc.)

**4:9 akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia**.

Hapa kuna neno lingine la ufunguo, **ibada**. Mamajusi walimwabudu Yesu, na Yesu ameombwa kuanguka chini na kumsujudu Shetani. Ilikuwa ni ahadi kubwa sana mbele ya macho ya Shetani ambaye ndiye, hakika, mfalme wa dunia hii. Lakini lilikuwa jambo dogo mbele ya macho ya

Yesu, alyeumba ulimwengu. Yeye ndiye muumba wa ulimwengu huu. Shetani anaweza kutuahidi vitu vikubwa hata leo. Anafanya hivyo hakika, kutujaribu ili kutulaghai tuingie majaribuni, na ahadi za shetani zinaweza kuwa kubwa kwa wana wa dunia, lakini ni ndogo kwetu sisi tunakwenda kuwa na utukufu wa uzima unaokuja (Rum.8:17,18) warithi pamoja na Kristo (Fil.3:7, 8). Hii ndiyo njia tunapaswa kuyaona majaribu. Tunapaswa kutokutazama kwa jinsi ya kibinadamu, bali kwa jinsi ya kiroho. Tunapata anasa fulani hivi sasa, lakini tutakuwa na na furaha isiyoelezeka ikiwa tutabakia waaminifu kwa Mungu. Ikiwa tutaangalia mambo kwa macho ya kiroho, tutakuwa na matarajio sahihi. Paulo anaelezea kama hivi. "Nia ya roho hufuata mambo ya roho, na nia ya mwili hufuata mambo ya mwili, kwa hiyo tunapaswa kuwa na nia ya kiroho" Rum.8:4-14.

**4:10 Ndipo Yesu akamwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake**.

Yesu alimwita Ibilisi "Shetani" ambalo ni neno lenye maana "adui" au "mpizani." Yesu anamwona jinsi alivyo kabisa. Hapendezwi na mambo mema yaliyo akilini mwa Yesu. Wala hana mapenzi mema nasi akilini kama anavyoendelea kutujaribu kutenda dhambi. Shetani, ikiwa alielewa mpango wa Mungu, angelitambua kwamba dhambi moja ingeliharibu mpango wa Mungu wa kumwaokoa mwanadamu. Alimjia Yesu na namna tatu za kumfanya Yesu aweze kuanguka.

Tunampa Shetani nguvu asizostahili. Yeye haoni kila jambo, wala hafahamu kila kitu, na wala hajui ni nini kilicho akilini mwetu. Njia pekee anayojua tunaudhaifu ni kwa kutuchunguza. Yakobo 1:13,14 anasema tunajaribiwa tunapovutwa na tamaa zetu wenyewe. Shetani, kwa uchunguzi, anatambua udhaifu wetu ulipo, lakini kusema kwamba ana nguvu za kutawala akili zetu ni jambo asiloweza kufanya, kwa sababu iwapo anajua tulichonacho akilini mwetu, atakuwa basi na uwezo wa Mungu - ambao huo hana!

Wakati huo huo, hatupaswi kudharau nguvu zake! Ni simba aungurumae kama Petro anavyosimulia (1Pet.5:8). Iwapo, kupitia uchunguzi, Shetani anatambua kwamba tunakuwa na macho ya kutangatanga tumwonapo mwanamke amevalia kisasa, basi atatuletea mwanamke aliyevalia kisasa, akitupatia sisi nafasi ya kutazama zaidi. Mungu wetu ametupatia sisi njia ya kujikinga na majaribu, siyo kuruhusu tamaa ikae akilini mwetu. Ikiwa tuna mawazo ya kimwili tukiwa peke yetu, hayo ni mabo yetu wenyewe. Shetani hausiki na hilo. Ni ukosefu wa kujitawala mwenyewe. Tunapaswa kukabiliana na matatizo hayo. Angalia Mik.2:1 - wakusudio kutenda maovu na kuwaza mabaya vitandani mwao. Je, Shetani alitambua waliokuwa wakifikiri? Hapana, ila anajua kuwa watu wana tamaa mbaya. Tunatenda dhambi kwa sababu ya tamaa zetu wenyewe, na si kwa sababu Shetani ametusababishia. Mtu angeweza kuondolewa mapepo lakini, wangerejea tena (kama katika Math.12:45), ikidhihirisha nguvu mtu anazoweza kuwa nazo juu ya majaribu na dhambi.

Je, Shetani alitambua kwamba angeliharibu mpango wa Mungu ikiwa Yesu angekosa? Pengine. Inawezekana aliligundua hili kutoka maandiko ya Agano la Kale. Yawezekana, basi, kwamba alitaka tu kumvuta atende dhambi, kama vile anavyotaka watu wote watende dhambi.

Tunapaswa kushukuru pia kwamba jambo hili ni kweli, majaribu halisi kwa Yesu. Mwandishi wa Waebrania anasisitiza kwamba Yesu alistahimili nguvu kamili na uwezo wa majaribu ya Shetani (Ebr.2:10ff). Hili lilifanyika ili kwamba awe msaada wa wote wanaojaribiwa (Ebr.4:16-18). Ingawa Yesu alihitaji mkate kweli, asingekubali jaribu ili kupata huo. Maana yake ni hii: Yesu alitambua nguvu ya majaribu. Shetani alipomjaribu afanye hivi, Yesu akataka kufanya vile, na akaachia hapo. Hakufuatilia na kisha kutenda dhambi. Ni lazima liwe jaribu, kitu alichotaka hasa kutenda, la sivyo fungu katika Waebrania lisingekuwa na maana. Majaribu na dhambi ni

vitu viwili tofauti. Ni mtu gani ajuaye majaribu, ni mtu yule anayeyakubali, au ni yule anayeyapinga? Yule anayepinga. Jaribu haliwi tena jaribu kwa yule aliyetenda dhambi. Yesu alikabiliana na nguvu kamili za majaribu zikimjia na alitambua ni jinsi gani vigumu kuyashinda mambo hayo. Angalia 1Kor.10:13. "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu." Tunaweza kupata nguvu kutokana na hilo na majaribu kuyashinda pia! Iwapo hatuwezi, hakuna wakumlaumu bali sisi wenyewe.

***Angalia makala: Kujaribiwa kwa Yesu*

Lengo limewekwa kwetu na neno moja la Kiyunani. *Teleios*. Neno hili limetafsiriwa "kamilifu" au "komavu." Hili ndilo lengo lake Mungu kwa wanawe - Yak.1:2-4. Tunapofikiri juu ya majaribu na jinsi yatendavyo kazi ndani yetu, tukiyakubali, mara ya pili majaribu yakija, tunakuwa dhaifu kidogo. Kuna hatua za kwenda kuyakubali hata kuwa kama katika 1Tim.4:1,2 ambao walifikia hatua ya kufa dhamiri zao. Ikiwa tabia ya kutenda dhambi tumeizoea tunafika mahali ambapo "haiwezekani tena kutufanya upya hata tutubu" - Ebr.6:6. Kwa maana nyingine, njia ya kutufikisha utu uzima (teleios) ni kukapinga majaribu kwa kutokutenda dhambi, na wakati mwingine tunakuwa na nguvu nguvu bado. Mfano: Kwa wengi, kupitia kipindi cha ujana, kunywa pombe pengine lilikuwa jaribu kubwa. Walakini, kwa kuendelea kukataa jaribu la kunywa, tunajikuta wenyewe kuwa na nguvu hata linakuwa si jaribu tena! Basi tunaweza kukua na kuwa na nguvu katika nyanja zingine. Shetani hawezi kutushambulia mahali tulipo na nguvu, bali pale tulipo dhaifu. Mungu, ingawa hivyo, anatutaka kuwa wakamilifu. Ukamilifu ndilo lengo la Mkristo. Tunatia madoa huduma zetu za kiroho tunapoanguka katika majaribu.

Washindani katika michezo, ni muhimu kushambulia udhaifu alionao mshindani wake. Mtu anapofanikiwa kufanya hivyo, yaelekea akapata ushindi. Hii ndiyo njia Shetani anaitumia. Tunakuwa dhaifu maeneo fulani fulani, basi anashambulia katika maeneo hayo ili atushinde. Lakini Mungu anatupatia silaha za kuvaa (Efe.6:10ff) - silaha ambazo mishale yenye moto ya Shetani haiwezi kupenya. Hawezi kushinda hayo! Ufahamu katika neno la Mungu utasaidia katika kukabiliana na majaribu. Yakobo anasema kumpinga Shetani na atatukimbia (Yak.4:6). Hawezi kutuachia iwapo hatutampinga. Neno ndicho kitu pekee kinachotenda kazi kuyakabili majaribu. "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi" Zab.119:11. Daudi aliamini nguvu ipatikanayo katika neno. Hii inatoa sababu kubwa ya kudondoa maandiko. Neno la Mungu likiwa miyoni mwetu, na tunalitafakari tunapojaribiwa, tunaweza na tutashinda. Neno lile, lililopandwa ndani, linaweza kuokoa - Yak.1:21.

**Msujudie Bwana Mungu wako na yeye pekee umwabudu**. Angalia kwamba Yesu ni mmoja walikubali kuabudiwa (Math.28:9,17; Ebr.1:6), bali pia alisema umwabudu Mungu peke yake. Hili ni dhihirisho kwamba Yesu ni Mungu (Yoh.1:1; 20:28). Katika mst.8 Shetani anazungumzia falme za duniani lakini mtazamo wa Yesu wote ni juu ya ufalme wa mbinguni. Hili ni wazi kama tunavyotambua tofauti kati ya Mungu na Shetani. Yesu amependezwa na ufalme wa mbinguni, na Shetani katika ufalme wa dunia. Mpango wa Mungu umetekelezwa. Yesu anathibitisha kuwa ni Masihi. Tuna ukoo, kuzaliwa kimuujiza, kuokolewa kwa Yesu mkononi mwa Herode, mamajusi, kutumwa kwa nabii, kutiwa mafuta kwa Yesu, adui wa Yesu kumkabili na majaribu na kushinda kwake.

**4:11 Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia**.

Huu ni moja ya utimilifu wa Yesu kuwa Masihi (Isa.53) kama tunavyoona kwamba Yesu ni mpatanishi wa dhambi, akiwa yeye mwenyewe bila dhambi. Baadhi ya Wayahudi walishindwa kuelewa Masihi kutokuwa na dhambi, lakini wengine walielewa. Katika Isaya, Mungu alichukua mapigo tuliostahili kila mtu wetu. Katika 1Yoh.2:15-17 tunaona kwamba kuna vyanzo aina tatu vya dhambi: tamaa ya mwili, tamaa ya macho, kiburi cha uzima. Vyote hivi vilikuwepo katika

majaribu ya Yesu. (Pia, vilikuwepo kwa Hawa katika bustani ya Edeni).

*Tamaa ya mwili* - geuza mawe haya yawe mkate.

*Tamaa ya macho* - falme hizi zote zitakuwa zako.

*Kiburi cha uzima* - malaika hawa wote watakuja na kukuokoa.

Luka anaogeza (4:13) kwamba Shetani akamwacha hata fursa nyingine (akamwacha kwa muda). Ni makosa kusema kwamba Shetani alimjaribu mara moja na kukata tamaa. Alimjia tena Yesu ili kumjaribu Yesu atende dhambi. Lakini, kila mara, alishinda. Ebu angalia mpangilio sahihi. Mateso yalitangulia kwanza, kisha **malaika** wakaja kumfariji. Ndivyo ilivyo hata kwetu. Sasa tunapingana vita, lakini sio wakati wa kuvunjika moyo (Gal.6;9) kwa maana pumziko likuja baadaye. Huu ndio daima utaratibu wa mambo katika mpango wa Mungu. Kama vile mwandishi wa Waebrania anasema, kuna mapumziko ya Sabato baadaye - Ebr.4:1-6.

**4:12 Basi Yesu aliposikia ya kwamba Yohana amefungwa, alikwenda zake mpaka Galilaya**;

Hakuna maelezo zaidi Yohana ameelezwa isipokuwa sura zingine baadaye, katika sura 14 ya Mathayo, tunajifunza kuhusu baadhi ya mahangaiko yake. Hatujifunzi kwa kufuata nyakati katika kitabu cha Mathayo. Maana yake hapa ni kwamba wakati Yohana amefungwa, Yesu aliendelea kufanya kazi yake. Anafanya mabmo yote aliyotakiwa afanye.

**4:13 Akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji uliko pwani, mipakani mwa Zabuloni na Naftali**;

Hii ni Bahari ya Galilaya. Nazareti iko kati ya Bahari ya Galilaya na Mediterania. Yesu alielekea Mashariki. Kapernaum iko nchani Kaskazini kabisa mwa Bahari ya Galilaya.

**4:14 Ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema,**
**4:15 Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa,**
**4:16 Watu wale waliokaa katika giza wameona mwanga mkuu, nao waliokaa katika nchi na uvuli wa Mauti mwanga umewazukia.**

Hii ni Isa.9:1-2, na ni mfano mwingine wa *pleroth* (timiza). Kitu kizuri ajabu katika mpango wa Mungu kimetimia. Kikubwa na kizuri ajabu!

**Watu wale waliokaa katika uvuli wa mauti** - watu ambao kiroho wako karibu na maangamizi, na Yesu amekuja kuleta nuru kwa watu. Yeye ndiye rehema na upendo wa Mungu. Mathayo hatuelezi jinsi haya yote yalivyotimia. Wale walio gizani na dhambini walikuwa wapate nuru ya upendo wa Mungu na msamaha.

**4:17 Tokea wakati hyi Yesu alianza kuhubiri, na kusema, tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia**

Ikiwa tunatazama nyuma katika 3:2, hivi ndivyo hasa Yohana alihubiri. Jambo hili linamwunganisha Yesu na huduma ya Yohana. Katika Yohana 3:26 Wanafunzi wa Yohana wana mashaka kuhusu kuondoka kwa watu kwenda kwa Yesu. Wanaamini kwamba Yesu amejulikana zaidi ya Yohana, na wana mashaka kuwa hivi sivyo kama mpango waliousikia kwa Yohana. Ingawa bado Yesu na Yohana walifanya kazi pamoja. Yohana aliiandaa njia, hivyo basi Yesu

alikuwa aendeleze pale Yohana aliachia, akizihubiri habari njema za ufalme wa mbinguni.

**4:18 Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili, Simoni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi.**
**4:19 Akawambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu**

Hii ni mara ya kwanza kutokea moja ya maneno ya ufunguo katika Mathayo - **nifuate**. Siyo tu nia ya Mathayo kuthibitisha kuwa Yesu ndiye Masihi, bali pia baada ya kuuthibitisha ukweli huo, kuwaonyesha watu kitu cha kufanya juu ya ukweli huo. Ikiwa yeye ndiye Masihi, watu wanapaswa kumfuata! Na wanafanyeje hivyo? Hili litakuwa moja ya masomo makuu aliyofundisha kitabu kizima. Hapa kuna mafungu yote yenye neno hili la ufunguo: 4:20,22,25; 8:1,10, 19,22,23; 9:2,9,27; 10:38; 12:15; 14:13; 16:24; 19:2,21,27,28; 20:29,34; 21:9;26:58;27:55.

Tunaona wazo juu ya "kufuata" mara ishirini na tano. Katika mistari kadhaa kufuata ni jambo la muhimu mno. Zamani za kale mtu alipompata mwalimu ambaye alimvutia mno, angeliacha kazi yake kumfuata mwalimu huyo. Kufuatana na hili, tunapaswa kuamua kuwa Yesu kuwa ndiye Masihi. Ikiwa tutatambua kuwa ndiye yeye, basi ni lazima kuamua kuwa tunataka kulipia gharama zitakazo tugharimu tukimfuata - Math.16:24.

Kuna mambo mengi yametendeka kabla ya hili ambayo Mathayo hayaandiki. Hatupaswi kudhania kwamba Yesu ghafla anajitokeza na mara moja watu wanamfuata. Hivi sio kweli. Tunachokiona katika injili ya Yohana kinatupatia picha kamili zaidi jinsi mtu walivyoalikwa kumfuata. Yesu tayari alikuwa na ushuhuda na uthibitisho wa Yohana Mbatizaji. Hili ndilo lingekuwa faraja kubwa kwa watu kumfuata. Kisha tuna neno la kutoka kinywani. Kwa mfano, Adrea na Petro walimtambua Yesu katika matukio fulani, na kumsikia akifundisha. Katika Yoh.1:40ff. Andrea anamleta Petro ili amwone Yesu. Kwa nini wafanye hivyo, kumfahamu Yesu mara moja tu kuwafanye waache kila kitu? Usisahau kwamba Petro alikuwa mtu aliyeoa ambaye angelikuwa na majukumu zaidi juu yake. Kwa hamu kubwa inaweza kuwa ni moja ya sababu, lakini pia walikuwa na mawazo potofu juu ya Yesu kuwa ndiye Masihi wa ufalme wa duniani...ufalme wa kimwili. Wayahudi walimwona kuwa angelichagua kundi linalomzunguka, ambalo lingepata utajiri na mamlaka makubwa, hivyo kutamani kuwa sehemu ya ufalme wa duniani kungekuwa ndiyo sababu ya kufuata. Ikiwa Petro alifikiri kuhusu kuacha mali zake, ingelikuwa kwa kuwa alitarajia faida kubwa. Kupendezewa kwake faida binafsi kumeonekana katika Math.19:27 ambapo Petro alijitokeza mbele na kuuliza swali, "Tazama sisi tumeacha vyote, tukakufuata; tutapata nini basi? Petro alikuwa tayari (kama na wanafunzi wengine) na mawazo kuwa wangepata nini, lakini katika Math.19 wanaanza kuona hawatapata kile walichodhania.

Katika 21:3,4 Petro anasema, "Naenda kuvua samaki." Kisha Yesu, mst. 15, anamfundisha Petro habari ya upendo. "Je...wewe wanipenda kuliko hawa?" "Lisha wana-kondoo wangu." (Nenda kafanye kazi!") Ikiwa Petro anafikiri kurudi tena kuvua samaki, ameshindwa kuelewa. Katika Lk.5:1-10 Petro amekuwa mvuvi muda wote, na Yesu anasema, "... shusha nyavu zako." Idadi kubwa ya samaki walivuliwa. Petro alipoona hivyo akasema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi." Kutokana na hivyo Yesu akamwambia kuwa atamfanya kuwa mvuvi wa watu. Alimwambia kile ambacho angefanya siku za mbeleni. Walakini, wanafunzi walitarajia vyeo vya madaraka na tunzo. Mfano mwingine ni habari ya Yakobo, Yohana na mama yao katika Math.20:20-28.

Marko 1:16-20 anatupatia habari zingine za kuitwa kwa wanafunzi wake. Hizi ni sababu mbili za msingi kwa nini Kristo alichagua wapole na wasiosoma (lakini sio wajinga) kuwa wanafunzi wake:

1. Akili zao zingelikuwa huru toka katika chuki bila sababu (prejudice), na zaidi zilizokuwa tayari kupokea ukweli mpya. Unawezaje kufikiri Yesu kuchagua waandishi na Mafarisayo - "Wajuao-kila-kitu" - kuacha kila kitu walichonacho na kumfuata? Yesu aliwatambua ambao walikuwa rahisi kufundishwa. Hakuna faida sana kujaribu kushughulika na watu wale "wajuao kila kitu."

2. Uweza wa injili ulitambulikana zaidi kwa udhaifu wa watumishi wake. Angalia Matendo 4:13. "...watu siosoma ma wasio na maarifa..." hazina ya vyombo vya udongo..." Linga. Zak.4:6.

**4:20 Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata.**
**4:21 Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwamo chomboni pamoja na Zebedayo baba yao, wakizitengeneza nyavu zao; akawaita.**
**4:22 Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata**.

Mwaliko umetolewa na wanaupokea. Kwa nini wafanye hivyo? Kwa sababu wanaona thamani ya kumfuata Yesu. Hakika hili linazidisha kusadiki sifa zaYesu. Wale waliomwona na kumsikia ni wale waliomwamini na kumfuata. Ukweli wa kwamba mara moja walimfuata unaonyesha kwamba walikuwa tayari kwa ajili ya wito.

**4:23 Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na koponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.**

Yesu anafundisha mahali ambamo watu wa dini wangeenda, na kujifunua mwenyewe kwa wale waliokuwa wenye juhudi katika dini. Linganisha haya na Lk.4:15. Hii ni mara ya kwanza Mathayo anatumia neno injili katika kitabu hiki. Injili maana yake, "habari njema" na 24:14 anasema injili hii ilipaswa ihubiriwe duniani kote. Hotuba ya Mlimani ni mfano bora wa injili yf ufalme ambayo Yesu anafundisha katika sinagogi.

"Na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Hapakuwa na ugonjwa ambao Yesu hakuweza kuuponya. Hili ni jambo la maana ambalo Mathayo ataliendeleza katika kitabu kizima.

**4:24 Habari zake zikaenea katika Shamu yote; wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na maradhi mbalimbali na mateso, wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponya**.

Kurudia rudia kwa uponyoji kumefanyikwa kwa sababu ya kusisitiza. Mathayo hataki tukose kuona uweza mkubwa wa Yesu aliouonyesha katika uponyaji. Aliwezaje kufanya hivyo? Kwa nini hakuweza kushindwa hata mmoja? Maana yake ni hapakuwa na mtu yeyote aliyekuwa na tatizo la aina yeyote ile Yesu alishindwa - hata magonjwa ambayo madaktari hawakujua ni jinsi gani ya kuyatibu. Yesu aliweza kuyatibu yote. Hata wale waliokuwa na roho chafu zilizowakalia ndani ya miili yao, Yesu aliweza kuponya.

Biblia inatufundisha masomo mengi kadhaa ya maana; kwa mfano, 1Pet. 2:6 ananukuu kutoka Isa.28:16. "Kwa ajili ya hayo Bwana, Mungu, asema hivi, Tazama, naweka katyika Sayuni jiwe la pembeni, teule, lenye heshima, na kila amwaminiye hatatahayarika (hataona aibu)." Paulo pia anaelezea hili katika Rum.9:32,33; 10:11; Efe.2:20. Maana yake ni hii: Fanya kila uwezacho kumwendea Yesu! Watu hawa ambao walikabiliwa na maradhi mbalimbali ya kiafya pengine walipata shida kubwa kuweza kumfikia Yesu. Halikuwa jambo jema kusafiri walipokuwa

wagonjwa, hasa ilipowalazimu kutembea, au kusafiri kwa kupanda wanyama (pendine kipindi kibaya cha hewa, na kwa siku kadhaa!) Wangelipata nini wakishafika kwa Yesu? Hakika hawakuvunjwa moyo! Hivyo, kuna maana ya kiroho iliyofanywa kwa msingi wa maajabu ya kimwili iliyotendwa na miujiza ya Yesu. Haikujalishwa ni shida ya namna gani, Yesu aliweza kutatua tatizo. Iwapo anaweza kuponya kimwili, anaweza pia kuponya kiroho. Hivyo basi ikiwa mtu anamwendea Yesu, hawezi kuvunjwa moyo.

**4:25 Na makutano mengi wakamfuata, kutoka Galilaya, na Dekapoli, na Yerusalemu, na Uyahudi, na nga'mbo ya Yordani**.

Ng'ambo ya Yordani itakuwa upande wa Mashariki. Hata upande ule injili ilisambaa, na watu walimjia kumwona.

Tupo karibu na kuanza <u>sehemu tano za mahubiri</u>. Lakini kwanza ebu na tuanze na <u>sehemu ya uponyaji</u>. Mbili hizi zinaenda pamoja, na zinahusiana.

Kwanza, angalia sehemu zote za uponyaji katika Mathayo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 4:23,24 | |
| 2. | 8:16 | Yesu aliwaponya wagonjwa wote. |
| 3. | 9:35 | Akiponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina. |
| 4. | 12:15 | Yesu alitambua hivi...na akawaponya wote |
| 5. | 14:14 | |
| 6. | 14:35,36 | |
| 7. | 15:30 | |
| 8. | 19:2 | |

Kuna sehemu nane za uponyaji, na katikati ya kila moja zipo sehemu tano za mahubiri. Katika sehemu za mahubiri Yesu atatilia mkazo "ufalme" na "Baba." Baada ya mahubiri unatokea uponyaji. Cha nini kiolezo hiki? Kwa sababu Mathayo anatoa msingi imara kwa ajili ya kumfuata Yesu. Miujiza unawasogeza watu kwa Yesu, na mafundisho yanawaonyesha kinachotakiwa kwao ili wawe miongoni mwa "ufalme wa mbinguni" na kutambuliwa watoto wa "Baba" aliye mbinguni.

Kwa hiyo, Mathayo anawakilisha kiolezo hiki:

1. Miujiza
2. Fuata
3. Mafundisho
4. Fuata
5. Miujiza

Mzunguko huu ndio anaoutumia Mathayo. Miujiza na mafundisho yanaenda hatua kwa hatua. Miujiza ndiyo iliyowawezesha watu kufuata, kisha angewafundisha. Na wakisha fundishwa, pengine wasingelikuwa na uhakika wa kutaka kumfuata, hivyo basi angelifanya miujiza zaidi, ndipo wangemfuata, na angewafundisha. Wakati wote anawafundisha maana hasa ya kumfuata. Mzunguko huu katika injili ni muhimu. Hiyo ndiyo sababu tunajifunza sehemu ya uponyaji. Mara nane Mathayo anasisitiza "uponyaji" wa kila mtu. Wanapomfuata, wanajifunza zaidi kuhusu uponyaji wa kiroho.

## SURA YA TANO

Matumizi ya sura 5 ni kwamba kuna watu wengi wanaotoka sehemu moja hata nyingine lakini waiokuwa wanafunzi hasa (wafuasi waliojitoa wakfu). Wanahitaji kujifunza. Tuna watu leo wanaomfuata Yesu kutoka "sehemu moja hata nyingine." Wanahudhuria kanisani kawaida, lakini maisha yao hayaonyeshi kuwa ni wanafunzi kweli wa Yesu. Kipindi cha juma hawaishi maisha ambayo yampasa mwanafunzi kuishi.

**5:1 Naye alipowaona makutano, alipanda mlimani; na alipokwisha kuketi, wanafunzi wake walimjia;**
**5:2 Akafumbua kinywa chake, akawafundisha, akisema**,

sehemu hii inalingana karibu na Lk.6:20-49, mara nyingi inayojulikana "Hotuba ya Uwandani." Hii imetajwa "Hotuba ya Mlimani." Kuna ulinganifu mkubwa, pengine kuonyesha kwamba Yesu alifundisha mambo yale yale zaidi ya mara moja. Kuna mambo katika Hotuba ya Mlimani yaliyosambaa katika injili ya Luka, hakika, karibu sura nane tofauti.

**5:3 Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao**.

***Angalia karatasi kuhusu heri hii*.

**Heri** =. Wengine wametafsiri kama hivi "furaha" au "kupongezwa." Hivyo si sahihi. Neno hili *makarios* linamaanisha kwamba watu hubarikiwa kwa sababu wana <u>*haki kwa Mungu*</u>, na <u>*wamekubaliwa na Mungu*</u>. Wanatenda mambo ambayo yanampendeza Mungu na wanatambua wametenda mapenzi yake, kwa hiyo ni wale ambao upendo wa Mungu unakaa.

Zab.1...Heri ni yeye anayependezwa na sheria ya Bwana.

Kumb.33:29...Israeli imekuwa heri kwa sababu ni taifa lililookolewa na Bwana, na Mungu yu pamoja nao.

Zab.32:1...Heri waliosamehewa dhambi zao.

Yak.1:12...Heri wanaostahimili majaribu.

**Maskini wa roho**. Kuna walio maskini, ambao hawana vitu vingi. Maskini hawa ni maskini wa roho, wanatambua kwamba wanaupungufu wa vitu kiroho. Ambapo wenye kiburi na majivuno na wenye makuu hawatambui hitaji lolote. Wameridhika na kufurahia jinsi mambo yalivyo. (Kwa mfano Mafarisayo.) Mtu aliye maskini wa roho anatambua hitaji lake kuu kwa Mungu. Lk.6:24,25 Yesu anatoa ole kwa walio matajiri kwa maana hawaoni hitaji la kumhitaji Mungu. Hapa kuna mtu aliye maskini, siyo kifedha, bali katika roho.

**Ufalme wa mbinguni ni wao**. Utajiri wote wa kiroho wote unapatikana katika ufalme. Mtu anapotambua hitaji lake kiroho na kumgeukia Mungu, Mungu anampatia kile kinachohitajika.

**5:4 Heri wenye huzuni; maana hao watafarikjika**.

***Angalia maelezo ya nyogeza katika heri*.

**Huzuni** - juu ya kushindwa kwao, kukosa kwao wenyewe, na kwa ajili ya maovu ya duani.

**Watafarijika**. Watafarijika wanapofanya jambo fulani kupokea msamaha. Kuhuzunika ni ishara ya kutubu (Yoeli 2:12,13) kwa huo msamaha umepatikana. (1Yoh.1:9 - Mungu ni mwaminifu na haki kutusamehe.)

**5:5 Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi**

**Wenye upole** = nyenyekevu (tulivu). Haina maana ya udhaifu. Musa alikuwa mpole kuliko watu wote duniani - Hes.12:3. Unyenyekevu maana yake kuwa chini ya mapenzi ya mwingine. Hivyo basi, kwa hakika, mtu mnyenyekevu ni aliye na nguvu nyingi; mtu aliyeweza kujitiisha na kuwa chini yeye mwenyewe, na ndipo kwa kujitolea anatitoa mwenyewe kwa wengine, akiondoa "unafsi" ukae mbali naye. Mmoja wa waandishi wa kwanza wa Kiyunani anatumia neno hili kama kumwongoza farasi. Kuzitawala nguvu.

Watairithi nchi. Wakati wanaoamini utawala wa miaka elfu moja duniani wanahusisha fungu baada ya hukumu, inawezekana Yesu alikuwa na mitazamo miwili akilini mwake:

Kwanza, angeliweza kurejea kurithi "mbingu mpya na nchi mpya," kama katika 2 Pet. 3:13 na Ufu.21:1. "Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake." Kwa nini Yesu anasema namna hii?

Pili, Yesu angelikuwa akitaja ahadi iliyotajwa nyumba katika Sheria ya Kale katika Kumb.28:1-25. Ahadi ya nchi walipewa watu wa Mungu, na kwa kadri walivyodumu kutenda mapenzi yake wangedumu kupokea ahadi hiyo. Maana yake ingelikuwa hivi: nyenyekea chini ya mapenzi yake au hamtapata baraka zake.

**5:6 Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa**.

**Wenye njaa na kiu kwa ajili ya haki**. Mtu ambaye hajisikii kiu au njaa atakuwa ama anaumwa au amekufa! Hivyo mtu asiyejisikia njaa au kiu kwa ajili ya haki ama amekufa kiroho au amekufa.

**Haki** maana yake kutenda haki ya Mungu, kile ambacho Mungu amejulisha kama haki. Siyo kitu tunachokisikia tuhudhuriapo mikusanyiko katika mikusanyiko. Ni kitu tunachotenda na kuwa hivyo! Wakristo hujisikia njaa na kiu ya kumpendeza Mungu. Math.6:33 ni nyongeza nzuri sana ya fundisho hili...tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake. Yesu alikuwa hapedelei zaidi vyakula vya mwilini, bali chakula chake kilikuwa kutenda mapenzi yake aliyempeleka - Yoh.4:31-34. Alionyesha maana hasa ya "kuwa na njaa kwa ajili ya haki."

**Watashibishwa**. Vyakula vya mwili vinashibisha kwa kitabo, tena huja muda ambao tunahitaji zaidi. Mana toka mbinguni ilikuwa ikusanywe kila siku. Basi hamu ya kula kiroho inahitaji kudumu kulishwa, na Mungu anaahidi chakula kuwepo na tayari. Atatupatia kile tunachohitaji. Mungu anaahidi kutushibisha njaa ya roho zetu.

**5:7 Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema**.

**Wenye rehema**. Mtu mwenye rehema ni anayetoa, au anayefanya, jambo fulani kwa mwingine bila kudai chochote kwa mtendewa. Hili linhusiana na kupenda na msamaha. Hauwezi kupokea rehema hata nawe ukuwa mwenye rehema (6:12). Inalingana kabisa na kumsamehe mtu fulani. Katika 6:2 tunaona kurudiwa kwa neno hili lililotafsiriwa "rehema." "Unapotoa sadaka" - hasa unapofanya tendo la rehema." Mwenye rehema, wanaotenda matendo ya upendo kwa wengine, wanaweza kutarajia kupata rehema wao wenyewe.

**Maana watapata rehema**. Kwa mambo kadhaa wanayo shirikiana na wengine, Mungu ataona kwa hayo, wenyewe kunufaika nayo.

**5:8 Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu**.

**Wenye moyo safi** = weupe, watakatifu. **Moyo** katika Biblia mara nyingi ni akili, chombo cha kufikiri. Kutenda mapenzi ya Mungu lazima kuwe zaidi ya kutenda tu. Lazima kutoke moyoni (kwa unyoofu, kweli) na siyo kwa kujionyesha nje tu. Mafarisayo waliitwa "kuta zenye kupakwa chokaa" katika Math.23:25,27. Yesu anataka wanafunzi wake kuwa zaidi ya hivyo. Ebr.12:14 ni makala mengine kwa hili.

**Kwa maana watamwona Mungu**. Angalia Ebr.12:14. "..na huo utakatifu na, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao. Katika 1Yoh.3:2, ili kuweza kumwona Mungu mtu ni lazima awe safi. 1Pet.1:14ff - "Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu." Mungu anatuita tuwe watakatifu, na ikiwa tumekwenda kusimama mbele zake, ni sharti tuwe safi! Na iwapo tuko hivyo tunaweza kutegemea kumwona Mungu. Kinyume chake, Isa.59:1,2, "Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu." Dhambi zetu zinatuzuia kuona uso yake.

**5:9 Heri wapatanishi; maana hao wataitwa wana wa Mungu**.

**Wapatanishi**. Yesu analishughulikia hili katika 5:21-26 - akizungumzia juu ya magomvi baina ya watu. Wakati huu Wayahudi wanakaribia wakati wa vita vya Kiyahudi. Mauaji wametendwa na Wazelote. Kuna hamu ya damu, na jamii ya Kiyahudi imegawanyika katika makundi. Yesu anadai heri ni kwa wale wanaunda na kufanya upatanisho. Kupatanisha kunahitaji juhudi...mara nyingi juhudi kubwa. Neno la Kiyunani "wanatenda amani." Wanafanya au kutenda, amani kwa kutenda yapasayo amani, ama kwa maneno au kwa matendo.

**Wana wa Mungu** = kuwa na tabia kama Baba. Tunapofanya haya, tunafanyika kama Baba aliye mbinguni. Mungu ni Mungu wa amani (1Thes.5:23), na anawachukia wanaoharibu amani (Mith.6:19). Angalia pia kwamba hapana "amani kwa wabaya" (Isa.48:22); 57:21). Yesu ameitwa pia "Mfalme wa Amani" (Isa.9:6; Efe.2:14).

**5:10 Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao**.

Wanaoudhiwa kwa ajili ya haki. Ikiwa tunafanya mapenzi ya Mungu na kuteseka kwa ajili ya hiyo, ndipo tutaurithi ufalme wa mbinguni. Hapa hazungumzii kuteseka kwa ajili ya matendo yetu yasiyo haki. Petro anazungumzia hayo katika 1Pet.2:20 - hakuna faida ikiwa unatenda dhambi na kuteseka kwa ajili ya hiyo, lakini mkitenda mema na kuteseka, hiyo ndiyo haki mbele za Mungu. Rum.10:3 ni mfano mzuri. Paulo anamweleza Timotheo katika 2Tim.3:12, "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." Yesu alisema, "Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatendea manabii wa uongo mambo kama hayo" - Lk.6:26. Basi, kuna mateso ambayo yanaambatana na haki. Katika mistari kumi tumezungumzia kuhusu **ufalme wa mbinguni** mara mbili. Kama ilivyotarajiwa, Masihi ana mambo ya kusema kuhusu ufalme.

**5:11 Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu**.

"Kwa habari yangu mambo haya yatatukia:

1. **Watakapowashutumu ninyi** - 1Pet.4:14. Ikiwa tunashutumiwa kwa ajili ya jina la Kristo, ni heri kwetu. Hili linahusisha maudhi ya kushutumiwa kwa matamshi, walakini pia inaweza kupelekea kunyanyaswa kimwili. Basi jambo la pili ni:

2. **Kuwaudhi ninyi**. Haya yanaweza kuwa maudhi ya kimwili na kiroho, lakini hasa Yesu anamaanisha mateso ya kimwili hapa.

3. **Kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu** = maudhi ya matamshi na matokeo yake. Tunaumia iwapo sisi tumeshutumiwa kwa uongo.

**5:12 Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu**.

Tunazungumzia kufurahi duniani. U-heri tunaofurahia sasa ni kitu fulani kinachodhihirika chenyewe kwa furaha ya nje, kwa kuwa tumeahidiwa thawabu kubwa mbinguni. Tunaweza tusiwe na thawabu yoyote duniani. Thawabu anayoifikiri siyo ya kidunia. Rum.8:28 ni mfano mzuri kwa hili. Fungu hili halina maana kuwa mambo yote hutendeka vema katika uhai huu. Rum.8:18 panafundisha mateso ya uhai huu si kitu ukilinganisha na utukufu utakaofunuliwa. Mtu anaweza kumpenda Mungu, na kuwa mtumishi wa kweli, lakini mambo yasimwendee vema. Lazaro alikufa akiwa mgonjwa, mwenye njaa, lakini mwenye haki - Lk.16:16. Tunafuraha kwa kuwa kile tulichonacho katika uzima ujao, siyo kwa kuwa tumeahidiwa vitu sasa, ingawa kuna mistari ambayo inaonyesha Mungu atatujali sasa; kwa mfano 6:23,24.

**Ndivyo walivyowatenda manabii kabla yenu** - njia imekuwa hivyo daima, na njia itakuwa daima hivyo. Watu watawaudhi daima manabii wa Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo!

**5:13 Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.**

Chumvi wakati wa kale ilitumika njia mbili kimsingi, ambazo zote masomo kiroho:

Kwanza, chumvi ilitumika *kukifanya chakula kiwe na radha nzuri*. "Maneno yenu na yawe na neema siku zote, yakikolea munyu," - Kol.4:6. Maneno yenu "yawe na radha nzuri," yenye kupendeza wasikiao. Yesu anaonekana akiwa na fikra hizi, kwa maana anatumia neno "radha."

Pili, chumvi pia ilitumika kwa *kuhifadhia.* Chakula, kwa mfano nyama, ikiwa kililitiwa chumvi, kisingeharibika mapema.

Wakristo ni "chumvi" ya Mungu kwa hiyo wanapaswa kuwa ndio wanafanya uhai huu, dunia hii, mahali salama pa kuishi, zaidi "pa kupendeza." Ikiwa maisha yetu hayatafanya mahali penye kupendeza, ndipo tutakuwa hatufanyi yale Mungu anatutaka tufanye. Tunapaswa kuwa ndiyo tunaoleta mabadiliko! Mazuri yalipo katika dunia siku hizi ni kwa sababu ya Ukristo; sheria zetu, hospitali zetu, mashirika ya misaada, na watu mmoja mmoja wanaotenda matendo mema wamevutwa na sheria ya Mungu. Wakristo hujitahidi kuwa wema na wenye kusaidia, kama vile "Msamaria mwema." Si jambo geni geni kuona wasio amini Mungu kudhihaki Ukristo? Lakini imekuwa ni kwa sababu ya ushawishi wa Ukristo kila kitu chema kipo duniani. Je, Madeline O'Hare, aliyejitahidi sana kuufuta Ukristo, tambua kwamba ni Ukristo uliojenga hospitali aliyokwenda alipokuwa mgonjwa? Wakristo ni watu wanaouvutia ulimwengu kutenda mema.

Tunatambua kwamba sisi, kanisa kama kusanyiko, kutenda kazi njema ingawa wakati fulani tunasahau au tunajifanya hatuoni ukweli kwamba *mimi ndiye* mmoja ninayewe kuleta mabadiliko. Francis Schaffer, mwanafilosofi wa kale, alilionyesha kanisa kama "halina onyesho" kwa vipindi kadhaa katika historia ya Marekani; k.m. kipindi cha mageuzi ya maswala ya kujamiana, kukua kwa uchumi na matumizi mabaya, manyanyaso (utumwa), n.k. Kanisa halikuonyesha nguvu ya kupinga maovu hayo. Wakristo ni lazima kupinga kutokubali vitu visivyo halali mbele ya macho ya Mungu. Walakini Wakristo ni sharti wasimame ndani ya sheria inavyoruhusu kufanya. Shida tuliyonayo siku hizi ni mamlaka ya Biblia. Wanadamu hawaiheshimu kama ipasavyo na jinsi inavyoamuru.

**5:14 Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani**.

Kusudi la nuru ni kuwawezesha watu kuona. Wakristo pia ni "nuru" Mungu. Tunataka watu waone ukweli na nuru zetu, maisha yetu, yanapaswa yafunue ukweli wa Mungu.

Mji ukiwa juu ya mlima. Watu wanaweza kuuona kutoka pande zote.

**5:15 Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani**.

Fikiria juu ya upumbavu wa kuwasha taa na kuificha nuru yake. Taa inawashwa ili watu waweze kuona. Sababu zipi, zingemfanya mtu aifunike, na kuondoa kitu hicho ambacho kingesaidia wengine kuona? Ukristo ni sharti uwe kwa namna hiyo. Bila kujali mtu yuko wapi duniani, anapaswa kuwaonyesha wengine nuru ya Ukristo wake. Yesu sasa anaonyesha mambo ya kuzoelea kutenda kutokana na hili.

**5:16 Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele za watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni**.

**Nuru yenu na iangaze** - kwa nani? Mbele za watu, kwa kusudi - kubainisha - **wapate kuyaona matendo yenu wenu mema**. Tunataka watu waone nuru, kwa hiyo tunaihifadhi mahali ambapo wanaweza kuiona. Kanisa, ikiwa litakuwa nuru, ni lazima liwe mahali ambapo litaonyesha wengine jinsi lilivyo, na kile linachofundisha (1Tim.3:15) - nguzo na msingi wa kweli! Kanisa ndilo linaloinua juu ukweli ili kila mtu auone. Ikiwa kanisa halifanyi chochote kuwawezesha wengine waone ukweli, ndipo litakuwa haliwashi taa iangaze. Na ikiwa mtu hafanyi mambo hayo, akuwa hawashi taa yake. Kuna tofauti "kuwasha nuru yako" na "taa yako iangaze." Hatupaswi kutenda matendo yetu ili tuonekane na watu kama, Yesu anavyosema katika sura 6, au kutukuzwa na wanadamu. Tunapaswa kuwa watu tunao dhihirisha haki, na tunatakiwa kukumbuka kwamba kwamba tunawasha nuru ili wengine waone. Ikiwa Ukristo na maisha yetu daima ni siri, ndipo hatutatekeleza fungu hili. Mji uliojengwa juu ya mji, watu huuona, na huujia. Sababu ya kuufanya Ukristo wetu uonekane ni kwamba watu wauone, na wamwendee Kristo.

**Wamtukuze Mungu** siyo sisi wenyewe. Watu wengi - wakiume na kike - wamejiingiza katika mtego wa kutamani kutukuzwa na wengine kutokana na huduma zao. Bali, wanapaswa kumtukuza Mungu kwa kutenda matendo yao. Kinachoongelewa hapa ni nia. Nuru yenu na iangaze - ili wengine waweze kuyaona matendo yenu, lakini wamtukuze Bwana. Watu wanapaswa kujihusisha, na kutenda, kutumia nuru zao kuwavutia wengine. Paulo anawatumia wa Makedonia kama mfano; sadaka yao kuu kwa kujitoa wao kwanza kwa Bwana, na kisha fedha walizotuma - 2Kor.8:1; Fil.4:15,16.

**5:17 Msidhani ya kuwa nalikuja kuiitangua torati au manabii, la, sikuja kutangua, bali kutimiliza**.

Hili ni neno la Kiyunani *pleroo*, kutimia. Akishazungumzia haya, mtu anaweza tayari kuelewa kile Yesu anaongolea hapa. Alikuja kutimiliza, kuhatimisha, kufunga Agano la Kale kwa kuwa Sheria ya Kale isingekamilika bila ya kuja kwa Masihi na yote aliyokuwa ayafanye.

**5:18 Kwa maana, amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie**.

Yesu anaeleza bayana kungekuwa na muda ambao herufi ndogo kabisa au yodi vingetoweka, na muda huo ni “yote yatakapotekelezwa.” Wasabato wanautumia msitari huu kufundisha kwamba Sheria ya Kale haitaondoka hata mbingu na nchi ziondoke. Hivyo si kweli! Mbingu na nchi zingeondolewe kwanza kabla ya kuondolewa kwa Sheria ya Kale *pasipo kutimilika*. Lakini Yesu aliitimiza, hakika!

Sheria ya Mungu isingeweza, na haitaweza, kuondolewa hata iwe imetekeleza kilichoamuriwa kutendwa. Paulo anaeleza hivi katika Gal.3:21-29. Mstari 24 ni ufunguo - Sheria ya kale ilikuwa kiongozi kutuleta sisi kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa njia ya imani; na sasa imani imekuja hatupo tena chini ya kiongozi. Sheria ilikuwa inatuleta kwa Kristo na ikishafanya hivyo, hapo hatuihitaji tena.

Yesu anasema, kwamba **<u>hata</u> yote yatimie**, hakuna ambacho kitaondolewa. Wasabato wameigawa Sheria makundi mawili: za Kawaida na Amri. Wanaamini kwamba kilichopigiliwa msalabani ni sheria za kanuni. Haiwezekani kuthibitisha kwamba kulikuwa na tofauti, au kuwa aina hizi mbili zilikuwepo. Kwa mfano, angalia Lk.2:28ff. Mariamu amekuja kutoa hua wawili wengine imewachanganya juu ya “Sheria za Kawaida,” au “Amri za Bwana.” Wanaoshika mafundisho ya Sabato wanasema hii ilikuwa Sheria ya Kawaida, ambayo iliondolewa na Kristo. Lakini Luka anataja kama “Sheria ya Bwana” (mst.39), ambayo ingeangukia katika maagizo ya “Amri.” Tofauti haipo; Sheria imefungwa pamoja. Ni jinsi gani Myahudi aliikumbuka siku ya Sabato? Hakujua ni jinsi gani ya kufanya hata alipokwenda nje na Kutoka 20. Hakuna Msabato yeyote ambaye anaweza kujibu swali hili, “Ni vitu gani unafanya siku ya Sabato? Kadhalika hawawezi kuthibitisha kwamba amri kumi zilitolewa “hapo mwanzo.” Kumb.5 anathibitisha kwamba Sheria “hawakupewa...baba zao, bali sisi...”

Mafungu yanayoonyesha kwamba Sheria zilikuwa zidumu milele yanatumia neno la Kiebrania *olam* ambalo pia linahusisha uvumba, ukuhani, na vitu vingine kadha wa kadha. Wasabato wanasema fungu liliandikwa juu ya mawe kwa kishada cha Mungu linamaanisha milele lakini ikiwa hivyo ndiyo kweli, basi hivi vitu vyote ni lazima vidumu milele. *Olam* maana yake muda maalum, uliojulikana na Mungu pekee. Mtu hana haki ya kusema kwamba Mungu aliziondoa sheria, isipokuwa Mungu ndiye anaweza kuamua kufanya hivyo! Basi,
Sheria zilikuwa zikae kwa kipindi cha muda usiojulikana. Mungu hakuwaeleza katika Sinai kuwa Sheria hizi zingelidumu kwa kipindi cha muda wa miaka 1400, lakini alitambua kwamba ingelikuwa hivyo. Walikuwa hawaelewi nyakati. Mhu.1:3,4 anaeleza kwamba nchi ingedumu *milele*. Mashahidi wa Yehova pia wanafundisha fundisho hili. Neno tena ni *Olam,* muda maalum uliojulikana na Mungu pekee. Mtu angesemaje kwamba mbingu na dunia zingedumu milele? Hata mmoja! Mungu pekee ndiye anaweza kusema hivyo, na ikiwa angependa kuwa, mbingu na nchi kudumu milele. Ebu angalia vitu hivi Agano la Kale linasema kuwa vingelidumu “milele” - *olam*.

1. Kut.12:14 ...Pasaka
2. Kut.30:8 ...Uvumba
3. Kut.29:42 ...Sadaka za kuteketeza
4. Kut.40:15 ...Ukuhani, na
5. Law.3:17 ..Sadaka za amani.

Ingeliweza kuwa kwa kitambo lakini, pia ingeliweza kuwa milele. Ikiwa Mungu alitaka ziwe za milele, zingekuwa hivyo. Mungu alitaka waelewe kuwa Sheria aliwapatia zingekuwa na ukweli kwa ajili yao, watoto wao, na wajukuu wao. Hii inaeleza sababu iliyomfanya Yesu awe na wakati mgumu sana kuwaondoa watu kutoka katika Sheria za Kale.

## MTAZAMO WA MANENO YA YESU YENYE UVUVIO

Akisema juu ya Sheria, Yesu anasema, hata herufi ndogo (yodi, alama ya Kiebrania) au nukta ndogo (taw, herufi ya Kiebrania) zitaondoka. Yesu anakubali neno kwa neno la uvuvio. Hakuna kilichoandikwa ambacho kisingetekelezwa, na chochote kilichoandikwa kiliandikwa kwa sababu Mungu alitaka kiwepo! Na, hakuna hata kimoja kingeliondoka hata vyote yatimie.

**5:19 Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni**.

Neno vunja limetafsiriwa "legeza" au "asi." Waalimu (Rabbis) walizihesabu jumla amri 613 katika Sheria za Kale, na kuzifanya zingine kuwa muhimu kuliko zingine. Yesu anasema kuwa yeyote atakayelegeza (kuona nyepesi kuliko - 16:19; 18:18) atakuwa katika ufalme lakini atakuwa **mdogo** katika ufalme. Hili halina maana kwamba, kwa kuwa hakuchukulia sheria moja kuwa ina umuhimu sawa na nyingine, wakaamua kutokuzitii. Walizitii, isipokuwa walifikiria kuwa zinauzito mdogo kuliko sheria zingine (angalia Math.23:23).

**Atakayezitenda**. Mtu anayetaka hasa kuwa mkubwa katika ufalme wa Mungu atatakiwa kuzitenda sheria sawasawa na zinavyostahili. Tusielewe vibaya kwamba ikiwa mtu anadharau na kulitumia isivyo halali neno la Mungu atakuwa katika ufalme, bali hatainuliwa juu katika "ngazi ya wote." Hatutaweza kuwa na thamani kubwa ikiwa hatuichukulii makini sheria ya Mungu. Ikiwa tunataka tuwe watu wa thamani mbele za Mungu, tutashika Sheria Zake, na kuwafundisha wengine kuzishika pia.
Hii ni mara tatu nne anataja juu ya ufalme wa mbinguni.

**5:20 Maana nawaambia ya kwamba, Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni**.

Yesu ameanzia daraja moja (ile ya waandishi na Mafarisayo) na sasa anawapeleka watu katika daraja nyingine. Ikiwa hawazishiki sheria zote na kuwafundisha wengine kufanya yayo hayo, hivyo watakuwa katika daraja ile ile ya waandishi na Mafarisayo. Moja ya mafundisho ya kuogofya yanaonekana Yesu anaposema kwamba iwapo haki yenu haizidi ile ya waandishi na Mafarisayo, hamwezi kuingia katika ufalme. *<u>Huu ndio mstari wa ufunguo katika Hotuba ya Mlimani</u>*; taarifa ya hoja au wazo kuu kwa ajili ya Hotuba yote. Kila hotuba na kila makala ya muhula yanahitaji kuwa na taarifa moja ambayo inafafanua kinachokwenda kuwasilishwa. Msitari huu ndilo kusudi lake hilo. Waandishi na Mafarisayo walikuwa "wenye mamlaka," kundi bora kabisa ambalo ndilo liliratibu sheria ambazo kila mtu aliziangatia na kuzinukuu. Hawa ndio wanaotajwa katika Math.23 ambao walivaa hirizi (kasha lenye maandiko0 mikononi mwao. Vilitengenezwa ili vifunika mkono yao yote, wakidhani ndio kuwa na haki zaidi. Vichwani mwao kulikuwa na utepe ulioshikila kasha zikiwa na maandiko ndani: "kama utepe katikati ya macho yako..." Kumb.6:4-9. Mambo haya yalifanyika kutilia mkazo (na kuonyesha) haki yao, lakini haki hiyo haikuwa sahihi. Haki yao ilikuwa na unafiki. Kufuatana na Rum.10:3ff walijaribu kuithibitisha haki yao wenyewe na kuunda miongozo yao wenyewe, na kutokutambua ile ya Mungu. Hata hivyo, haya yangelikuwa ni maneno ya kushangaza sana na Yesu. Lilikuwa hili ni kundi bora; watu wa kiwango cha juu katika ulimwengu wa dini, na Yesu anawambia watu kuwa ni lazima haki yao izidi ya hao; wakijitahidi kila siku kutenda yale Mungu alitaka yafanywe, lakini waandishi na Mafarisayo walikuwa hawafanyi hivyo.

***Angalia mchanganuo katika sehemu ifuatayo*

Kila ulinganifu utaanza kwa, "Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, bali mimi nawambieni."

Ndivyo walivyotenda kwa sheria ambayo Yesu anawashutumu. Ulinganifu wa kwanza:

**ULINGANIFU #1 - Hasira**

**5:21 Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu**.

Hapa imefunuliwa tatizo waliyokuwa nayo watu. Watu wa kawaida hawakusoma maandiko na ndiyo maana anasema **mmesikia**. Waliisikia sheria, na tafsiri ya sheria toka kwa waandishi na Mafarisayo. Huu ni mfano mzuri wa kutaka kujifunza Biblia. Watu hawa walifundishwa sheria, lakini pamoja na mapokeo ya waalimu (Rabi). Walipata tafsiri toka kwa Mafarisayo. Walipaswa kujifunza wao wenyewe.

**Usiue**. Maneno ya kwanza katika maelezo haya yanatoka Kut.20:13, na moja ya amri kumi. **Itampasa hukumu** (mahakama) inatoka Kumb.16:18. Yesu anasema kwamba kuna mambo zaidi ya kufanya katika sheria hizi si tu tafsiri ya waandishi na Mafarisayo.

**5:22 Bali mimi nawaambieni, kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanam ya moto**.

**Lakini mimi nawaambia**. Yesu alifundisha kama mwenye mamlaka - Math.7:28ff

**Itampasa baraza**. Yesu anaigawa dhambi ya hasira katika makundi matatu:

1. *Hasira tulivu*. Mtu amemchukia ndugu yake, lakini yu kimwa, au imwkuwa kwake tu. Mafarisayo walidai ikiwa mtu aliua alistahili mahakama, lakini Yesu anasema kwamba ikiwa mtu ana hasira, hivyo anahatia.

2. *Kumfyolea*. Ikiwa mtu atamwambia nduguye "Raka" (mpumbavu, kichwa kitupu, hauna lolote) - hasira ya kutamkika, Yesu anasema, atakuwa na hatia mbele ya mahakama kuu, Sanhedrini.

3. *Kumwapiza*. Akisema, "wewe mpumbavu" itampasa jehenamu ya moto. Neno "mpumbavu" linaweza kuwa lisimaanisha kama "si lolote" kwetu, lakini neno hili ni wazo lenye maelezo mazito. Watafsiri wengi wanaamini hili ni kumshutumu mtu leo; ukimlaani mabaya yamtokee, ukiapiza kwa maneno ya kuhukumu; maneno yakutosha kukupeleka jehenamu.

Dhambi ina hatua, Mungu anailezea kwa namna ya "mbegu." Inaanza kwa hasira inayowaka moto, kisha hukua. Mtu mwenye chuki huifuta hasira, kisha huanza kuwaza mabaya kumtokea adui yake. Ni moyoni ambapo mtu hushindwa kujizuia, na kushindwa kujizuia kunamletea kupoteza roho yake. Yesu anasema haki ya kweli *inatoka ndani*. Mtu anapaswa kuweza kuona haki kupitia katika unafiki wa Mafarisayo - Math.7:20. Walikuwa na haki ya nje, lakini mafundisho ya Yesu si kujionyesha kwa nje tu bali ya ndani.

**5:23 Basi ukileta sadaka yako madhahabuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako**,

Anaendeleza mawazo yake juu ya hasira.

**5:24 Iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako**.

Tunapaswa kuelewa kwa Mungu uhusiano mzuri na watu wengine ni muhimu mna kuliko ibada yenyewe. 1Yoh.4:19-21 “Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.” Ikiwa mtu atasema, “Nampenda Mungu, na anamchukia ndugu yake, ni mwongo.” Yohana anasema kwamba hatuwezi kumpenda Mungu pasipo kupendana sisi, na tusipopatana sisi, hatuwezi kumpenda Mungu.

Ebu fikiria kumwabudu Mungu, na Mungu anasema, “Sitaki wewe uabudu. Ondoka na kwanza tatua shida na nduguyo, na <u>kisha</u> njoo utoe sadaka yako.” Huyu ni mtu aliye na daawa na nduguyo, kisha <u>wewe</u> unaenda na kupatana. Hatuwezi kugombana baina yetu na tuwe na ushirika na Mungu. “Heri wapatanishi, kwa maana wataitwa wana wa Mungu.” Kuna wakati watu watakuchukia bila wewe kujua sababu. Lakini unapaswa kujaribu kupatana. 1Tim.2:8 - “Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali...pasipo hasira wala majadiliano.” Watu wengi katika kusanyiko wako katika hali ambayo kuna magomvi mengi hata kufikia mtu mmoja kusimama upande mmoja na mwingine wa pili, wakichukiana. Lakini Paulo anasema, hamwezi kufanya hivyo. Mungu anahitaji wewe kujirudi na kisha umwabudu, na Yesu anasema kwamba yapo na mambo mengine yaliyo muhimu zaidi. Hatuwezi kuwa na uhusiano sahihi na Mungu ikiwa hatuna uhusiano sahihi na ndugu.

**5:25 Patana na mshitaka wako upesi, wakati uwapo pamoja naye njiani; yule mshitaki asije akakupeleka kwa kadhi, na kadhi akakupeleka kwa askari, ukatupwa gerezani**.

Bado anajadili juu ya hasira.

**5:26 Amini, nakuambia, Hutoki humo kamwe hata uishe kulipa senti ya mwisho**.

Habari ya kufurahisha hii, na nyepesi kuelewa tunapotambua kuwa ni moja ya “ULINGANIFU #1 -Hasira.” Mtu anayechochea ugomvi anaendea taabu zaidi. Hapa kuna aliyepelekwa mahakamani, pengine kwa kuwa hakuizuia mapema hasira yake. Akiwa njiani anakutana na mshitaki wake. Ni jinsi gani afanye?

**Patana na mshitaki wako upesi**. Hapa kuna namna ya kukabiliana na hali, basi jitahidi kufanya urafiki. Hili linaonyesha sababu ya kuzuia ndimi na fikra zetu. “Jawabu la upole hugeuza hasira” - Mith.15:1. Kwa kupatana, hasira hupungua pia. Mith.22:24 anasema, “Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi...”

Hutoki humo ka,we hatya uishe kulipa senti ya mwisho. Utapata unachostahili. Biblia ina maonyo mengi juu ya kuwa mwangalifu na maneno. Angalia Math.12:36,37. Uwe mwangalifu kwa maneno <u>yako</u>. Kwa maneno <u>yako</u> utatoa hesabu.

**<u>ULINGANIFU #2 - Uzinzi</u>**

**5:27 Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini**;

Kut.20:14. Hivi ndivyo amri kumi zinaamuru.

**5:28 Lakini mimi nawaambia, kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini moyoni mwake.**

Mara nyingine tena, Yesu anaenda kinyume na waandishi na Mafarisayo walivyofundisha. Neno uzinzi ni “moikeuo” ambalo linamaanisha mahusiano ya kujamiana nje na vifungo vya ndoa. Pia mtu ambaye hajaoa akijamiana na mwana ndoa ni mzinzi. Mafarisayo walifundisha kwamba tendo lenyewe ndilo dhambi. Sasa tunaona ulinganisho wa Yesu.

**Mimi nawaambia...amekwisha kuzini moyoni mwake**. Yesu anasema yeyote amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani azini. Mungu aliumba mwanamume, na anapomuona mwanamke anayevutia, wakati fulani huamsha tamaa ya ngono. Lakini hapa ndipo panapaswa aweke msitari wa kubainisha tabia sahihi ya Mkristo na ambayo siyo. Ikiwa ataendelea kutazama, na kisha kuwazia, anakuwa na hatia ya kuzini moyoni mwake. Hakuna kosa kwa kutazama mwanzoni, bali kuendelea ni tamaa na dhambi. Ni nani ataua? Ni yule asiyeizuia hasira yake. Mtu atakayezini kadhalika ni yule asiyeizuia tamaa yake. Kuitia akili nidhamu ni muhimu! - Ayu.31:1. Ayubu hakuruhusu haya yatendeke. Ni lazima tusiruhusu haya!

**Angalia Rocky Mountain Christian, Sept. 80 Series, "Kama nionavyo."

Ikiwa mwanamume atamtamani mumewe, je amtaliki kwa uzinzi? Jawabu linaonekana kuwa "hapana" kwa sababu zifuatazo:

1. Yesu anaongezea kwa kusema **moyoni mwako** ambapo hutenganisha toka kitendo chenyewe cha uzinzi.

2. Hili siyo tendo lenyewe hasa la uzinzi, ambalo hilo linahitaji watu wawili (Yoh.8:4).

3. Dhambi ya uzinzi inahitaji watu wawili kuwa mwili mmoja )1Kor.6:16).

4. Sababu: Je, tumpeleke gerezani mtu yeyote ambaye ana hasira (mwenye hatia ya uuaji?) Pia, je hatujawahi kutamani kwa hali yeyote ile, ikiwa ni pamoja na wanawake?

Hili haliondoi umuhimu wa fungu hili. Mungu atamwesabia hatia mtu yeyote mwenye tamaa. Kwake yeye, dhambi ya tamaa inamatokeo sawa sawa kama uzinzi. Wakristo ni lazima aizuie tamaa yake - Fil.4:8.

**5:29 Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanam**.

**Jicho lako la kuume** (hata mkono - v.30) ilichukuliwa na Wayahudi kama ulio na thamani zaidi.

Akiendeleza wazo la tamaa, anasema, "Likikukosesha, ling'oe ulitupe."

**5:30 Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanam**.

Hapa anaongeza **mkono wa kuume**.

***Angalia makala.*

Maana yake Yesu hapa ni: Ni vyema kupoteza kitu upendecho sana maishani kuliko roho ya mtu. Math.16:26, "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Yesu anazungumzia jitihada ambayo mtu inampasa kufuata maisha bila dhambi. *Kukata halisi* kitendo hiki kungelifanya kanisa kuwa hospitali. 1Thes.5:22 tunaamuriwa "jitengeni na ubaya wa kila namna." Kung'oa jicho au kukata mkono hakutomzuia mtu kutenda mambo haya. Hivyo kutenda kitendo halisi hasingetatua tatizo, bali mtu anapaswa kuwa tayari kuondoa dhambi maishani mwake. Hivyo basi, tunzo kubwa ya mali haina thamani kuliko kupoteza roho zetu. Fanya kila uwezalo, jilinde kwa uwezo wako wote kutotenda dhambi!

## ULINGANIFU #3 - Talaka

**5:31 Imenenwa pia, mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka**;
**5:32 Lakini mimi nawaambia, kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwona yule aliyeachwa, azini**.

Tena, angalia kanuni anayotumia Yesu. Wazi anajadili mambo ya aina moja - haki ya Mafarisayo ikilinganishwa na anyoizungumza Yesu. Mishnah sehemu iitwayo "Gittin." Katika hiyo kuna "Hati ya Talaka" ikijumuisha shule tatu za maoni yaliyozungumziwa:

1. Maoni ya shule ya Shammai - ilifundisha kwamba mtu angemtaliki mkewe ikiwa ni mwasherati.

2. Shule ya Hillel - ilifundisha hata ikiwa angeunguza chakula mume angemtaliki mkewe. Angalia Kumb.24:1.

3. Shule ya Akiba - ilifundisha ikiwa mtu amemwona mzuri kuliko yeye ("hakupata kibali machoni pake"), angelimtaliki.

Shule ya Shammai inakubaliana na mafundisho ya Yesu. Marko sura 10 inazungumzia swala la talaka kwa upande wa mwanamke. Talaka iliruhusiwa katika Uyahudi, na ilichukua hatua rahisi katika hiyo mtu aliyetalikiwa alipata hati ya talaka (iliyoitwa pata). Hapakuwa na maoni juu ya utakatifu wa mahusiano ya ndoa, au madhara ya tendo hili. Hati hii, ambayo alikabidhiwa mwanamke mkononi, ilisomeka "Nenda, uko huru kuolewa na mume yeyote" (Gittin 9:3). Hati ilimlinda kutoka katika kushutumiwa kuwa mzinzi ikiwa angeolewa tena. Yesu anaenda kinyume na uhuru ambao Sheria ya Musa ilitoa. Mafundisho yake juu ya kutaliki na kuona tena itakuwa zaidi thabiti, kama tunavyoona hapa na katika Math.19:1-9. Yesu anakuja na tangazo lenye mamlaka - "Kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uashareti akaoa mwingine, azini." Maana yake anatazama kwa namna kuu mbili:

1. Inaaminika kuwa mwanamke anaweza kuoa tena. Mume, aliyefunua aibu hii mbaya, lazima awe na wajibu wa kuchukua kwa kumtaliki mke. Lakini, ikiwa tu atamtaliki kwa sababu nyingine mbali na ile ya **uasherati** - kukosa uaminifu kindoa. Hivyo basi, anatofautisha mafundisho ya waandishi na Mafarisayo kwa kusema kuwa haipaswi talaka itolewe wakati wowote, isipokuwa ikiwa uasherati umetukia.

2. Yesu anataka mtu anayemtaliki mkewe afikiri kwa makini sana juu ya madhara ya tendo hilo. Kuna madhara aina mbili ya moja kwa moja:

    a. Anaweza kumlazimisha kuingia katika hali ya uzinzi - kwa maana angeolewa bila kuwa na sababu inayokubaliwa na Mungu. Walakini, ikiwa angemtaliki kwa sababu ya uzinzi, kosa lingelikuwa lake mwenyewe. Kiusawa, ingelikuwa dhambi kwake (ya uzinzi) ikiwa angeamua kuolewa tena - hata ingawa hakuwa na haki ya kimaandiko kuolewa tena.

    b. Anaweza kuishia kuwa katika ndoa ya uzinzi, kwa kumwoa mtu mtu aliyeachwa na mtu mwingine (kwa hiyo basi si jambo huru bila masharti kuoa tena).

Ikiwa una hatia na umeachwa, lazima uishi maisha ya useja, au utafute njia ya kupatana na mwenzi wako - 1Kor.7:10-11.

Unaweza kuona kutokana na hili, na sehemu katika Mathayo, jinsi Sheria ilivyotumiwa vibaya ili

ikidhi walichotaka. Angalia jinsi swali lilivyoulizwa katika Math.19:3, . "..kwa kila sababu ...?" Hili linaonyesha nia mbaya waliyokuwa nayo waandishi na Mafarisayo. Wangelipenda uhuru wa kutaliki kwa kila sababu. Yesu hatakuliana na uovu wao na nia ya kujiangalia wenyewe.

Kuna watu wanaojadili kwamba talaka ikitendeka kifungo cha ndoa huondolewa. Lakini fungu hili haliruhusu hatimisho kama hili. Yesu anasema **naye amwoaye yule aliyeachwa azini**. Itakuwaje uwe **uzinzi** ikiwa alikuwa hafungwi kwa mwingine? Haiwezekani. Kwa hiyo, katika mtazamo wa Mungu, bado anafungwa. Iwapo angeoa mwingine ingekuwa ni kuzini.

## ULINGANIFU #4 - Viapo (5:33-37)

**5:33 Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiape uongo, ila mtimizie Bwana nyapo zako**;

Neno kiapo linahusisha nadhiri au mikataba (Law.19:12; Kumb.23:21; Hes.30:2; Mhu.5:4-5). Tunachofundishwa na mafungu haya ni, kwamba mtu anapotoa kiapo au nadhiri, anapaswa kuitunza kwa kuwa Mungu ni shahidi wa maneno ambayo yanatoka kinywani mwako, na atamwesabia hatia mtu yeyote ambaye amedai kutenda jambo. Kut.20:7 ni moja ya mafungu yasiyoeleweka vizuri zaidi. Inazungumzia juu ya kuapa kwa jina la Bwana, kutoa nadhiri, kisha kutotekeleza. Hivyo ni kulitaja jina la Bwana bure. Umuhimu wa kutoa ahadi zaidi kulijulikana kwa kutoa nadhiri. Jinsi ilivyonenwa ilitambuliwa kwa ama kutekelezwa ama la. Math.23:16-22 - "Mtu atakayeapa kwa hekalu, si kitu; bali mtu atakayeapa kwdhahabu ya hekalu, amejifunga." Mtu atasema, " Naapa kwa hekalu nitakulipa." Wala halipi deni lake. Kisha angedai, "Oho, lakini niliapa kwa hekalu, na wala si kwa dhahabu ya hekalu." Yesu anafundisha tusifanye viapo vya uongo kwa Bwana. Usiahidi ahadi na usiweze kuzitekeleza.

**5:34 Lakini mimi nawaambia, usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu;**
**5:35 Wala kwa nchi, kwa maana ndiyo pa kuwekea miguu yake; wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndiyo mji wa Mfalme mkuu.**
**5:36 Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.**
**5:37 Bali maneno yenu yawe ndiyo, ndiyo; siyo, siyo; kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu**.

Kuna mambo mengi ya kuyaangalia hapa:

1. Kristo na Paulo walikula kiapo. Angalia Math.26:63,64; 2Kor.1:23; Rum.1:9; 1Thes.5:27; Fil.1:8; 2Tim.4:1ff; 1Kor.15:31; Ufu.10:5,6. Anachofanya Yesu ni kuonyesha kuwa viapo asili yake ni Mungu. Neno la Mkristo linapaswa kuwa kifungo chake. (Kila mtu anatakiwa afungwe kwa maneno yake!) Ikiwa tutasema "ndiyo" ndipo watu watajua kutekelezwa kilichosemwa. Katika Math.23 watu walikuwa wakijaribu kuitumia vibaya sheria. Yesu anasema hakika watu wenye haki watatenda waliyosema. Watu wenye haki ni wenye kutumainiwa, wasiotoa kiapo au "kuapa" juu ya kitu chochote kile.

2. Anaonyesha kuwa viapo asili yake ni Mungu hata mwisho. Kila kiapo ama ahadi inamlenga Mungu hasa.

## ULINGANIFU #5 - Kisasi (5:38-42)

**5:38 Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na jino kwa jino**;

Hii ni nukuu kutoka katika Sheria ya Musa - Kut.21:34; Law.24:20. Kusudi la msingi la Sheria hii ilikuwa kumwezesha mtu kutafakari kwa makini kuhusu jambo kabla ya kulitenda. Ikiwa, kwa kuridhia ghadhabu, mtu amempiga mwingine, na kumuumiza jicho, ndipo mtenda angepoteza jicho lake. Au ikiwa, kwa kutupa jiwe lililosababisha mtu kupoteza mkono wake, ndipo hata yeye yatamkuta aliyetupa jiwe. "Angalia kabla ya kuruka." "Fikiria mbele."

Waandishi na Mafarisayo waliigeuza hii kuwa sheria ya kisasi. Kusudi la asili ya sheria ilikuwa kutoa hukumu inayostahili kwa mahakama iliyotambulika, ambayo ndiyo ingeamua iwapo "jicho kwa jicho" ilikuwa ni haki inayostahili. Mafarisayo waliliangalia hili kama njia ya kujilipizia kisasi.

**5:39 Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili**.

Tunaona mfano huu kwa Yesu mwenyewe. Alitendewa vibaya, lakini hakujibu kwa kulipiza kisasi binafsi, ingawa alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Msishindane maana yake "simameni kinyume." Hapa haina maana kutojitetea binafsi; katika hali ya kushambuliwa. Katika Ukristo kuna namna mbili za kufanya ikiwa mtu anakutendea vibaya.

1. Samehe, na

2. Mwachie Mungu alipize kisasi. Rum.12:14-21 "Maana kisasi ni juu yangu; mimi nitalipa, anena Bwana." Hivyo, tunapaswa kuachia mikononi mwa Mungu haki. Tunapoendelea kusoma katika Rum.13 tunaona kwamba Mungu ameruhusu serikali kutoa adhabu. Inakubalika, hivyo basi, Wakristo kuitumia serikali ikiwa haki inahitajika kutolewa.

**5:40 Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia**

Hapa kuna mtu ambaye anataka hasa kutwaa kila kitu chako. Mpatie bila kuwa na mawazo ya kulipiza kisasi. Jamii ambayo imeweka akili zake kulipiza visasi imejivuna kuelekea maangamizi yake. Ndicho kinachotukia katika ulimwengu wetu wa leo; mtu anamtendea ovu mwingine, na anaona lazima kulipiza kisasi kwa mikono yake mwenyewe.

**5:41 Na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili**.

Manyanyaso haya yalikuwa ya kiserikali, kwa sababu sheria ya Rumi ilikuwa askari wa Rumi angelimtaka mtu kumbebea mzigo au silaha maili **moja**. Wayahudi walikuwa na alama za maili kando ya barabara hata inchi kutoka majumbani mwao. Walipoifikia inchi hiyo, walitua mzigo. Yesu anasema, ikiwa wanakushurutisha kuenda maili moja, nenda **mbili**. Ebu fikiria jinsi maaskari wangestaajabu! Mtu kwenda maili ya ziada; wala siyo kufikiri juu ya kisasi na kusimama juu ya haki yake mwenyewe; bali kuonyesha roho ya namna tofauti - kutumika badala ya kutumikiwa; kuonyesha tabia tofauti kabisa. Wazo la kwenda maili mbili - ile "maili ya ziada" - inatoa masomo ya ziada makubwa leo. Fikiria juu ya yafuatayo:

***KWENDA MAILI MBILI***

Math.5:41

**1. WENGINE HUENDA MAILI MOJA NA SI ZAIDI.**

A. Kuna wale watakaofanya tu vile Mungu alivyowaamuru - na si vinginevyo.

B. Wanataka kutenda kadri ilivyo kidogo iwezekanavyo.

**2. WENGINE WANAJARIBU KWENDA MAILI YA PILI KABLA YA KUMALIZIA YA KWANZA.**

A. Kuna wale ambao wanataka kupata sifa ya maili ya pili bila ya kwenda maili ya kwanza ya utumishi.

B. Ni lazima tufanye kila kitu Mungu anatutaka tukifanye katika maili ile ya kwanza.

**3. WENGINE WANAKWENDA MAILI YA KWANZA MARA MBILI.**

A. Wengine wanafuata haki katika fikra zao wakitenda yale Mungu ameyaagiza, lakini pia wanajaribu kurudia rudia yale yale.

B. Mtu akiwa anafanya kile alichoagizwa na Mungu (k.m. amebatizwa), hapaswi kufanya tena na tena.

**4. WENGINE HUENDA MAILI ZOTE YA KWANZA NA YA PILI.**

A. Kuna wale wanaojali kile walichoamuriwa na Mungu kufanya.

B. Hawa ni wale pia wanaotaka "kwenda zaidi ya na kushinda wajibu walioitiwa."

C. Wanafanya hivyo kwa sababu ya upendo wao kwa Mungu. Efe.4:1; 5:2; 5:15f.

**5:42 Akuombaye, mpe; naye atakaye kukopa kwako, usimpe kisogo**.

Yesu anazungumzia kitendo cha kutoa cha uhakika; siyo kutoa kwa chuki kwa kuwa umelazimishwa kufanya hivyo. Tumeitwa kuwa mawakili wazuri (2Thes.3:10) na tunapaswa kutoa kwa kadri ya mahitaji ya mtu, tupatapo fursa hiyo - Gal.6:10. Efe.4:28 anazungumzia kuhusu kusudi la kufanya kazi - ili tuwe na mahitaji ya kuwasaidia wenye mahitaji. Sheria ya Agano la Kale juu ya kukopesha ilikuwa kama kutokutarajia kupata riba mtu alipoanzima fedha kwa nduguye (Law.25:36; Kumb.23:19ff; Kut.22:25). Yesu anazungumzia juu ya kanuni hii katika Lk.6:34 - "Ikiwa mmewakopesha watu huku mkitumaini kupata kitu kwao..." Katika mazingira haya Yesu anazungumzia kuhusu "kujipiga-piga mgogoni wenyewe" katika kufikiri kuwa tumetoa sadaka kwa kuwakopesha wengine. Bali, hata wenye dhambi (Mataifa) wanafanya vivyo hivyo, basi hatufanyi tofauti na wao. Ukristo ni lazima uwe hatua mbele ya hayo. Yesu anajumuisha uwezekano wa kutokupata hata kile tulichoazima.

Kanuni ilivyowekwa na Mungu katika Agano la Kale, kuna jambo fulani kuhusu kanuni hiyo. Kuitendea kazi hiyo leo: ikiwa natambua ndugu anahitaji, nikawa na fedha ya kumwazima, ndipo ninapaswa kumwazima bila riba. Hitaji halisi halihitaji riba - Law.25:36. Kumb.23:19,20 inazungumzia kumtoza riba mgeni. Kut.22:25 ni mahali pengine panapozungumzia hili kwa mujibu wa sheria. "Ukimkopesha mtu maskini, katika watu wangu walio pamoja nawe; ...wala hutamwandikia faida." Basi je, Wakristo wanapaswa kuwasaidia Wakristo wenzao kwa kuwakopesha pasipo riba? Hivyo ndivyo Mungu anatarajia kutoka kwa watu wake chini ya Sheria ya Kale. Ilikubaliwa kumdai mgeni (k.m. wasio Wakristo) riba, lakini si kwa ndugu.

**ULINGANIFU #6 - Kisasi (5:43-48)**

| Mafarisayo | Yesu |
|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mpende Jirani yako | 1. | Mpende adui wako |
| 2. | Mchukie adui yako | 2. | Waombeeni wanaowaudhi |
| | | 3. | Hivyo mtakuwa kama Baba yenu |

**5:43 Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, umchukie adui yako**;

Hili jambo la kipekee katika ulinganifu wa sita kuwa katika Law.19:18 **mchukie adui yako** si moja ya Sheria ya Kale. Hii ilikuwa nyongeza, au mapokeo, kwa sheria.

**5:44 Lakini mimi nawaambia, Wapendeeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi**,

Neno **upendo** ni "agapata" (sawa kama lilivyo Efe.5:25 ambapo waume wameambiwa kuwapenda wake zao). Ni aina ya upendo wenye kukusudia. Upendo, unafafanuliwa kama kutenda chochote kile kwa kadri ya mapenzi ya wengine. Tunachagua kufanya hivyo. Tunatenda chochote kile kwa uwezo wetu kwa ajili ya mapenzi ya wengine - 1Yoh.3:16-18. Wakristo wanapaswa kuwapenda adui zao. Tunajitahidi kadri tuwezavyo kwa ajili ya wengine. Tunapenda, kwa kuwa tunawafikiria mema mioyoni mwetu maadui zetu. Tunatenda kila kilicho chema kwa ajili yao. Tunatenda kwa juhudi zetu zote. Jinsi ya kuenenda kwa Wakristo ni bayana. Kuna watu wengi wanaosimama kama maadui wa Ukristo na Kanisa la Bwana. Namna Mkristo anavyopaswa kuwa na upendo na kutenda wema. Hivi ndivyo Yesu alivyowatendea madui zake. Nasi tunapaswa kutenda hivyo. Ukimpenda mtu fulani utatakiwa kumwombea. Ni vigumu kumchukia mtu unayeendelea kumwombea.

Huo ndio mfano wa kwenda maili mbili. Maili ya pili ni maili ya upendo. Mungu anatutaka tutumike siyo kwa lazima, bali kwa upendo.

Waombeeni wale wanaowaudhi - leta jina la mtu mbele za Mungu, ukimwombea kwa Mungu kumsaidia, mbariki na kumsamehe kama vile Yesu alivyofanya msalabani.

**5:45 Ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki**.

**Wana**. Biblia inapozungumzia kuwa wana wa Mungu hasa inakuwa inazungumzia juu ya tabia. Kwa kuwa Mkristo lazima awe na tabia ya Baba yake aliye mbinguni, hivyo anapaswa kumpenda adui yake na kuwaombea wanaomwuudhi. Ni jinsi gani Mungu anatupenda? Mfano uko hapa.

**Maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki**.

Mungu huwabariki si tu walio wake, bali hata walio sio wake. Wengine wanatumia fungu hili kufafanua madai ya kujibiwa maombi kwa wale walio nje na Kristo. Mungu huwabariki wote, lakini baraka hizo hazithibitishi kuwa Mungu anawakubali wote. Wengine wanaweza kuwa waovu na wasio haki. Kufuatana na Mith.15:9,29, "Bwana yu mbali na wasio haki; bali huisikia sala ya mwenye haki."

**5:46 Maana mkiwapenda wale wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo?**

Ikiwa tunafanya sawa na wasio haki wafanyavyo, hapo tutakuwaje bora na kuliko wao? Ikiwa utanipenda mimi, ni rahisi kwangu kukupenda wewe. Kitu cha pekee katika Wakristo ni kwamba

tunapenda na kufanya mema kwa wale wasiotupenda, na si wema kwetu. Hakika, wale hasa wanajaribu kutudhuru ndio tunaopaswa kuwapenda. Ikiwa tunawapenda tu wale wanaotupenda, hatuko tofauti na wao.

**5:47 Tena mkiwaamukia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo**?

Salaam ni ishara ya urafiki. Mataifa walisalimia wale waliowafahamu, na sio wale wasiowafahamu. Yesu anasema ni rahisi kwetu kuwapenda "ndani ya marafiki" zetu. Kuwa rafiki ni jambo ambalo Wakristo wanapaswa kuwa kwa wote; kutoka nje, kufika nje, kuzungumzia. Ni mara ngapi tumefanyika marafiki na watu kwa sababu ya kuzungumza nao - wale tuliowafahamu, kadhalika wale tusiowafahamu?

**5:48 Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.**

Fungu hili limekuwa rahisi kupotoshwa. Wengi hudhania kwamba tunapaswa kufikia ukamilifu, lakini hakuna jinsi ya kufanya hivyo - Rum.3:10,23. Katika mazingira, hapa inazungumziwa kuwa na upendo mkamilifu. Tunaweza kupenda kama Mungu anavyopenda. Tukiwapenda maadui zetu kwa kadri tunavyotaka Mungu kutupenda sisi, ndipo tumetiliza mst. 48. Anapozungumzia ukamilifu wa Baba aliye Mbinguni anazungumzia kuhusu upendo kamili. Upendo wetu unakuwa hauna thamani ikiwa hatuonyeshi zaidi ya Mataifa. Ru.13:8 - "Msiwiwe na mtu kitu chochote, isipokuwa kupendana." 1Yoh.4:19-21 - "Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza."

## SURA YA SITA

**6:1 Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni**.

**Haki** ni jambo la <u>kufanya</u> katika Mathayo. Lakini katika Warumi si kitu cha kufanya, ni jinsi sisi <u>tulivyo</u> kwa sababu ya vile Mungu alivyotufanya sisi. Mungu anatufanya kuwa na "haki," anatuhesabia haki katika Warumi. Hivyo sivyo ndivyo Mathayo analitumia neno hili.

Kuna maeneo manne ya haki Mathayo anayajadili.

1. Katika kutoa sadaka - 6:2-4.
2. Katika sala - 6:5-15.
3. Katika kufunga - 6:16-18.
4. Katika mali - 6:19-33.

**Angalieni**. Maonyo haya yanapaswa kuhamashisha mawazo yetu hasa juu ya kutenda haki mbele za watu ili **tuonekane** nao. Tunapaswa kuwa makini sababu ya kufanya na nini tunafanya. Tunatakiwa tuangalie kilichofanywa, na jinsi gani kimefanywa. Ni kwa nini tunafanya mambo hayo? Tunataka tuonekane na watu?

**Thawabu**. Matendo yetu ya Ukristo yanatakiwa yafanywe kwa sababu tunataka kumtukuza Baba aliye mbinguni, na siyo kwa sababu tunataka kupokea utukufu toka kwa watu. Hili litatusaidia kuelewa Math.5:16 panaposema nuru yenu na iangaze. Sasa Yesu anatueleza sisi watu tusitende matendo mbele ya watu. Tofauti yake ni ipi? Tofauti ndiyo sababu hasa. Ni kwa kusudi la kutukuzwa kwa matendo yao. Wanataka waone na watu na kuwatukuza, na watu wanapopata utukufu huo, ndipo Baba yao wa mbinguni hatawapa thawabu. Iwapo tumetenda matendo mema,

na wengine wanayaona tuliyofanya, na kumtukuza Mungu, hicho ndicho Yesu anataka. Ikiwa kile tukifanyacho kwa Bwana kimefanywa ili tuonekane na watu, ndipo tunakuwa kunaiba utukufu toka kwa Mungu. Tunanyang'anya kutoka kwa yeye anayestahili, siyo sisi. Kufuatana 6:19-21 tunataka kuweka hasina mbinguni.

**6:2 Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu**.

**Sadaka**. Neno hili linatokana na "eleeos." Tuliijadili hii katika 5:7 ikiwa na maana "rehema." Tafsiri ya "New American Standard Version" inasomeka "matendo ya upendo." Hili ndilo tunalolizungumzia. Angalia neno hili lilivyotukia.

Math.5:7; 6:2; 9:13, 27; 12:7; 15:22; 17:15; 18:33; 20:30,31; 23:23. Anachozungumzia Yesu ni jambo mtu analomtendea mwingine, ambalo linalopelekea kutoa vitu kwa kuhurumiana. Maana yake katika Mathayo kwamba kumfuata Yesu kunahitaji wanafunzi wake wawe na namna maalum, na hiyo ndiyo ya kutoa. Wanapaswa (tunapaswa) kuwa watu wa lkutoa, wenye upendo, watu wenye kuhurumiana. Hivyo, tungelisema kwamba mtu aliye mchoyo sana basi huyo siyo mwanafunzi wa Yesu. Mtu aliye navyo, lakini hawashirikishi wengine, amepoteza maana halisi ya uanafunzi. Mtu anayetenda jambo fulani kwa ajili ya mwingine, na anatangaza kwamba amefanya hivyo, anataka wengine wamwone. Yesu anasema:

**Wamekwisha kupata thawabu yao**. Kuna huzuni kubwa katika hili, kwa maana Mungu alitarajia kuwapa thawabu watu hao. Lakini, kwa kuwa wamepata thawabu toka kwa wengine, Mungu tena hanuii kuwapati yoyote ile. Je, usingelipenda Mungu akupatie thawabu kuliko thawabu ya wanadamu?

**6:3 Amini, nawaambieni, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto, usijue ufanyalo mkono wako wa kuume;**

Kutoa kwetu si kwa kujionyesha hadharani - ili kuonekana. Kunatendwa katika upendo na nia ya kumtumikia yeye. Maneno yanayodai kuwa mkono wa kushoto usijue kile kinachotendwa na mkono wa kulia ni lugha ya mafumbo, ikisisitiza tabia ya watu wa Mungu waliyonayo wanapotumika.

**6:4 Sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi**.

Mungu anaona na kujua. Angalia sehemu inayozungumzia Baba, ambayo itajadiliwa mwishoni mwa Hotuba ya Mlimani. Maana yake hapa ni, Mungu ndiye tunayetaka atuone sisi, na hakuna kitu ambacho tutafanya ambacho hataona na kujua. Ufunguo uko katika tabia zetu - tabia ya kwamba yote yametendeka kwa utukufu wa Mungu. Tunaweza kuona katika hili kwamba kuna mambo mengi ambayo mtu anaweza kufanya sirini, wakati wengine wanamazoea ya kujitoa hadharani. Kuna wakati ninapomsadia mtu mwingine yanatakiwa yawe matendo yangu binafsi, wakati kwa upande mwingine, kutakuwa na wakati ambapo yatakuwa matendo ya hadharani. Yesu anajaribu kuonyesha uwiano, na kusisitiza sababu ya mtu kufanya anachofanya. Tunaweza kuwaonyesha watu kwamba Yesu anafanya mambo kupitia wengine bila ya kutaja majina na, kwa kufanya hivyo, tunampa Mungu utukufu.

Ni huzuni kuona tumefikia kiwango cha kutokumtukuza Mungu, bali mwanadamu. Walakini, tunapaswa kuona kilichotendeka. Tunatakiwa kumsifu Mungu kwa ajili ya watu hawa na matendo yao mema, lakini siyo kuwatukuza watu wenyewe. Hatupaswi kumwibia Mungu utukufu ambao ni hake yake na kuwasifia watu kwa matendo wanayotenda.

**6:5 Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amini, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao**.

Hasemi kwamba "na kama utasali." Anatambua kwamba wenye haki watasali!

Msiwe kama wanafiki. Sehemu muhimu zilizojulikana Yerusalem ni **mitaani** na katika **masinagogi**. Kusudi la kusali kwao katika maeneo hayo ilikuwa watu wawaone. Walikuwa ni wanafiki kwa kuwa walikuwa wakiigiza tu kuwa na haki - wakisali ili waonekane na watu.

**Thawabu yao "kikamilifu"**. Je, unatambua kwamba umepata thawabu yako kwa kusali kwako? Ni thawabu gani Mungu anatoa? Kusikia. Ndiye anayesikia sala. Ndiyo thawabu ya kwanza tunayoitaka.

**6:6 Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakuzaji**.

Yesu hana maana kwamba hatutakiwi kuomba hadharani, bali wenye haki wanaishi wakiomba kwa siri. Tunatambua kwamba Mungu anaona na kusikia **ndani vyumbani** kukiwa hakuna mtu karibu nasi. Kama mtoto wa Mungu tunazungumza na Baba. Anapenda tunapomweleza yeye pekee.

**Atakujazi**. Atazijibu sala zetu. 1Yoh.5:14,15 - "Tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia..."

**6:7 Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi**.

Tena, fikra ambazo wanafunzi wake watakuwa nazo wasalipo. Mataifa walipenda kurudia-rudia mambo yale yale tena na tena; **kukariri** kama Waislamu wanavyotumia, rosali, kitabu cha sala. Yesu anataka sisi tujue jinsi Baba anavyoona kuhusu sala. Hatupaswi kurudia rudia *kusiko na maana* yeyote. Sala inaweza kurudiwa na ikawa na maana. Kutoa shukrani zetu kwa ajili ya chakula kunaweza kuwe kukariri maneno bure; lakini tukiwa tunakumbuka kwamba Mungu ndiye mpaji wa vitu vyote, na tunashukuru, hawezi kutushutumu kwa sala zetu. Tunapaswa kufikiri kuhusu sala zetu; mazingira, tabia tunayoionyesha tunapoomba.

Wakidhania. Hii ndiyo sababu ya kurudiwa-rudua kwao, kuiamusha miungu yao isikie.

**6:8 Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba**.

Hakika, kwa mtazamo wa mara moja, tunaweza kuona ufahamu wa asili wa Mungu kujua mambo yote. Anatambua kabla hatujaomba neno lolote. Anajua kile tunachotaka kusema. Hivyo, ndipo, kwa nini tusali ikiwa Mungu anajua tayari? Sala ni kwa ajili yetu sisi! Sala ni kwa ajili ya faida yetu. Ikiwa hatusali, tunakuwa hatuonyeshi imani yetu kwa Mungu.

Kwa nini kusali, ikiwa Mungu anajua tayari haja zetu?

1. *Kwa sababu tumeamuriwa kusali*. Ni mapenzi ya Mungu kwamba tusali. Angali Math.6:9; 1Thes.5:17; Fil.4:6; Rum.12:12.

2. *Kwa sababu tumeambiwa tutapata tukiomba*. 1Yoh.5:14,15. Kuna mfano mzuri wa

jambo hili 2Fal.19. Hezekia alihofu vile mfalme wa Ashuru angeutenda ufalme wake jinsi alivyoutenda tayari Ufalme wa Kaskazini wa Israeli - akiuangamiza. Hezekieli ndipo akamwomba Mungu. Angalia sala hii. Kisha angalia majibu ya Mungu. “Kwa kuwa umeniomba juu ya Senakeribu, mfalme wa Ashuru, mimi nimekusikia.” Kama Hezekia asingemwomba Mungu, hivyo Mungu asingemjibu. Bali alisali, ma Mungu akamjibu!

3. *Kwa kuwa ni jambo jema kwetu*. Inatusogeza tumkaribie Mungu. Ni vizuri kutamka tunayohitaji. Kukiri ni jambo jema kwa nafsi zetu. Ni jambo jema kwa maana inatusaidia kutanguliza uzima wetu na kupata vitu katika matarajio yake sahihi. Tunasali, tukijua kwamba Mungu anajua kile tunachohitaji. Tunasali, kukitambua kwamba Mungu anajua tunayohitaji.

Hili linatufariji kwa kuwa tunapojisikia kwamba hatuwezi kusali, tusipokuwa tayari kujieleza jinsi tunavyojisikia, haijarishi kwa maana Mungu anajua - hasa tunapokuwa tuna majonzi. Pengine hatuwezi kutamka jinsi tunavyojisikia, lakini Mungu anajua. Hili ni faraja - Rum.8:26ff.

**6:9 Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje**,

Mara nyingi hii imejukana kama sala ya Bwana, lakini hasa ni sala ya *wanafunzi*.

**Salini hivi**. Kimsingi hiki ni kiolezo cha yaliyomo katika sala.

**Baba yetu**. Tunapaswa kushukuru ukweli wa kwamba tunamwendea Baba yetu - tukitambua na kufahamu uhusiano uliopo kati ya Baba yetu na sisi wenyewe. Yesu aliwataka Wayahudi (nasi) kumwona Mungu kama Baba. Mfano mzuri ni uhusiano ule uliopo baina ya baba zetu wa duniani - “wazazi” wetu - hatusiti kuongea nao kitu chochote kile. Mungu ni Baba mkamilifu kwetu kumwendea kwa njia hii.

**Aliye mbinguni**. Yesu anaweka tofauti bayana iliyopo kati ya baba zetu na Mungu. Ni Baba yetu aliye mbinguni. Yeye ni Baba yetu, lakini sio “dadi wetu” - neno linalotumika kwa njia fulani lililo na heshima kidogo. Kunahitajika kuwa na kipimo cha tunayemwendea.

**Litukuzwe** = maalum, juu ya kila jina. Limetakaswa, takatifu, tukufu. Yesu anatutaka sisi tuianze sala kwa sifa; tukitambua, kufahamu na kutamka kwa maneno kwamba Mungu ni mkuu, kwamba jina lake ni kuu kuliko, na kwamba jina lake ni juu ya kila jina. Yeye ndiye pekee. Jina *lake* litukuzwe. Hatumwendei mtu yeyote. Huyu ni Mungu mwenye enzi! Mungu ni mmoja anayepaswa kuheshimiwa. Jina lake ni tukufu, na hivyo ndivyo tunavyopaswa kutambua tunapoanza sala zetu.

**6:10 Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe, duniani na mbinguni**. Huu ni ulinganifu wa Kiebrania. Ufalme wako uje na mapenzi yako yatimizwe inasema jambo moja. Mungu anapotawala kama mfalme, raia wake wanatii wao wenyewe chini ya utawala wake, kwake. Kile Yesu anatusisitiza tusali hapa ni kwamba mapenzi ya Mungu yaliyotajwa kwa mwanadamu yafanyike duniani. Ndiyo maana anasema, “Duniani kama ilivyo mbinguni.” Malaika mbinguni wanafanya kile Mungu anataka. Wanatii jumla kwa Mungu. Yesu analitambua hili kwa kuwa alikuwa kule, na ameshuhudia kuitikia kwao wito wa Mungu. Wakristo ni lazima waige tabia ya malaika. Mungu akisema, wanatenda. Hivyo basi, sisitizo liko juu ya **mapenzi yako** yafanyike. Ndivyo hivyo Yesu aliomba akiwa bustanini - Math.26:39.

Hasa hili siyo kuomba kanisa lingekuja. Inauhusiano kidogo na hilo. Ni sala ya kwamba utawala wa Mungu ungetawala duniani. “Mapenzi yako yafanyike” ni wakati uliopo, kitendo kinachoendelea. Tunataka yafanyike iwezekanavyo kabla ya kanisa na pia baada ya kanisa.

Hivyo tunaomba mapenzi ya Mungu yafanyike kwa mwanadamu kutendwa na mwanadamu. Ni mapenzi ya Mungu kwamba kanisa lianzishwe na kwa maana hiyo ni kweli, bali maana ya jumla ni kwamba mapenzi ya Mungu yafanyike duniani. Si kinyume na maandiko kusali kuhusu hivyo. Tunapaswa kusali kwamba Mungu atawale duniani kama vile mbinguni.

Angalia tunapoendea sehemu ya nne ya mambo yaliyomo katika sala, tunaeleza shida zetu na mahitaji yetu. Utaratibu Yesu anaofundisha ni somo kwetu. Kwa bahati mbaya, tunaanza kwa kawaida kueleza shida na mahitaji yetu kwanza. Yesu hatufundishi njia hii. Tunapaswa (1) kumsifu Mungu; (2) kusali kwa ajili ya kazi ya Mungu na kisha (3) kusali kwa ajili ya mahitaji.

**6:11 Utupe leo riziki yetu**. Jambo la kufurahisha kuhusu sehemu hii ya sala ni siyo kiwango cha mahitaji tunayoyahitaji, bali omba kwa ajili ya riziki ya **siku** ya **LEO**. Hii linalenga kwa Wayahudi wakitangatanga jangwani. Mungu aliwapatia kila siku mana waliyohitaji. Walitakiwa wajifunze kumtumaini Mungu siku hadi siku, na siyo kukusanya ghalani vitu ili wasijali kuhusu Mungu kuwabariki kwa mwezi mwingine. Kila siku tunapaswa kumgeukia Mungu katika mahitaji yetu. Jamii zetu zenye mali zimeharibu nguvu ya maneno haya. Ebu fikiria kwamba unaishi katika jamii ambayo matumbo yanaunguruma kwa njaa, na hujui ni wapi ungepata chakula. Ndipo hapo unapopiga magoti na kuomba chakula cha siku ya leo. Leo nitaomba baraka kwa Bwana. Hili linadhihirisha unyenyekevu. Angalia 6:33,34. Kufanya hivi katika jamii yenye vitu vingi ni vigumu. Lakini tunatakiwa tutambue kwamba Mungu anaweza kuziondoa baraka zake. Tunapaswa kushukuru kwamba tunavyo vile tulivyonavyo, na Mungu wetu ametukirimia.

**6:12 Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu**. Tulijieleza mahitaji yetu, shida zetu, na sasa tunaeleza mahitaji yetu ya kiroho. Tunahitaji msamaha wa Mungu, na tunaweza kumwendea yeye kwa ajili ya hili kwa sababu ya kitenzi cha wakati uliopita cha tungo uliyofuata ya pili: **Kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu**. Tunamwendea Mungu tukimwomba msamaha, pale tu tukishawasamehe tayari wengine.

**6:13 Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina**.]

Hesabu 6:24-26 ni sala ya Israeli kwa ajili ya ulinzi wa kiroho, ambalo ndilo sehemu ya mwisho ya yaliyomo katika sala ya wanafunzi. Katika maandishi ya Kiyunani kuna (definite article), "utuokoe na yule *'the' mwovu*." Hivyo inaweza kuwa na maana kutulinda na Ibilisi. Haibadili hasa maana, iwe Ibilisi au mwovu. Tunamsihi Mungu kutusaidia kuepukana na chochote kitakachotenga na neno lake na mapenzi yake. 1Kor.10:13 tunahakikishiwa, "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu..." Na 2Thes.3:1-3, "tuombeeni...tukaokolewe na watu wasio haki, wabaya ...kuwalinda na yule mwovu." Paulo anasema Mungu atafanya hivyo, na tunatakiwa kuomba kwamba ataweza. Hii ndiyo asili ya sala tunayoitegemea kuisikia kila mara - kutulinda na yule mwovu. Tunasikia kuomba msamaha, na kwamba Mungu atatuepusha na baadhi ya mambo. Mungu anatusaidia kwa kumwondoa Shetani katika njia zetu. Pia atatusaidia kutulinda tusiingie katika njia yake.

**Kwa kuwa ufalme ni wako**. Pengine hili si sehemu katika injili ya Mathayo. Haipatikani katika maandishi bora ya kale, lakini haifundishi jambo lililo potofu. Katika Lk.11:2-4 sala hii imerudiwa, na hatimisho hili haipatikani katika sala hiyo. Na hata halipatikani mahali pengine popote katika Agano Jipya. Pengine hili liliingizwa na baadhi ya waandishi walionakili maandishi. Maandishi yote ya awali hayana maneno haya. Angalia fungu hili katika Kiyunani msitari 13. Wenye ujuzi wanasoma bila ya "Kwa kuwa wako..." fungu {A} kusomeka - na hii inamaanisha kuwa yamekuwa na uhakika 98% yaliyosemwa kuwa ndiyo yaliyoandikwa katika asili.

**6:14 Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu aliye mbinguni atawasamehe ninyi**.
Yesu anaongezea juu ya kile alichojadili mapema. Neno "kwa maana" inarejea yale aliyotaja katika mst.12. Yesu anaweka bayana mambo ya kawaida, lakini yenye mvuto mkubwa, ukweli wa Biblia: kusamehe. Watu wa Mungu ni lazima wawe na tabia hii, ambapo jamii ya kale (na hata ya sasa) walikuwa na tabia kama watu wenye kinyongo. Ukristo unamfanya mtu alitutenda vibaya kinyume nasi kusamehewa (Kol.3:13), kuchukuliana na kusameheana. Sisi ndiyo hasa watu wa aina hiyo: Efe.4:32 - "Mkisameheana kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi..."

Lk.17:3,4 anasema, "...akitubu msamehe." Je, Biblia inatutaka sisi kumsamehe mtu ikiwa hatubu? Ikiwa mtu atatukosa na hana nia ya kutubu, hatuhitajiki kumsamehe. Angalia Yesu katika usemi aliosema msalabani. "Baba uwasamehe." Watu hawakupokea msamaha hata walipotii ya aliyofundisha Petro katika Matendo 2:38. Yesu anaelezea tabia yake na nia yake ya kusamehe. Hii ndiyo njia tunapaswa kuwa nayo.

Ikiwa mtu anaishi dhambini, na ikiwa tunasamehe dhambi hiyo bila ya kumtaka mtu huyo kufanya kama Mungu anavyotaka - "kuzaa matunda" - ndipo tutakuwa hatuwashawishi kutenda kama Mungu anavyotaka. Ebu fikiria juu ya nidhamu ya kanisa. Katika Math.18 Yesu anatueleza jinsi ya kusaidia wengine kurejeza maisha yao katika njia ya Mungu. Ndilo kusudi la nidhamu. Fungu katika Luka linasema akikujia na kutubu, ndipo umsamehe. Ndivyo Mungu anavyotutendea tunapomwendea kila wakati tukiomba msamaha. Ndicho kilichoonekana msalabani. Yesu alitamani kuwa wasamehewe, lakini wasingelisamehewa hata walipotenda jambo fulani kuonyesha kwamba walikuwa tayari kutubu kile walichomtenda Kristo. Angalia anachosema Petro katika Matendo 2.

**6:15 Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu**.
Tunatakiwa kuwa watu wa kusamehe na kuwa na tabia kama ya Mungu. Hili ni lazima lifanywe ili kupata msamaha wa Mungu sisi wenyewe.

**6:16 Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao, ili waonekane na watu kuwa wanafunga. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao**.

Sheria ya Musa aliwataka kufunga mara moja kwa mwaka - siku ya upatanisho (Law.16; Hes.29:7). Kusudi la kufunga lilikuwa ni kuitesa nafsi kwa ajili ya lengo maalum, kama vile kuomboleza, au kwa ajili ya kujifunza na kutafakari. Kufunga ni ile hali iliyo na maana ya kiroho. Na kwa kuwa ina nia hii, kufunga kwetu ni kati yetu na Mungu, si kuwatangazia watu wengine. Hutendeka kwa hiari, na Wakristo wambao wanataka kujitesa nafsi zao kwa kuzingatia ya rohoni. Hii ilikuwa moja ya maisha ya kanisa la kwanza - Matendo 14:23.

**Ili waonekane na watu kuwa wanafunga**. Hawajisumbui na jinsi wanavyoonekana nje kusudi kila mtu awaone kwamba wanafunga.

**Wamekwisha kupata thawabu yao**. Hawatapata thawabu yoyote toka kwa Mungu kwa hili. Mfarisayo, katika Lk.18:12, akijidhania kuwa mwenye haki na kufunga mara mbili kwa juma.

**6:17 Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani, unawe uso**;

Yesu anaona kwamba wangefunga. Hakuna mahali katika maandiko panapoonyesha kwamba kufunga kumeamuriwa. Ni jambo la hiari la kujitolea. Yesu alikuwa akiongea na watu

waliokuwa kawaida wakifunga kama sehemu ya maisha yao. Ingelikuwa jambo jema leo kufunga. Kwa maelezo zaidi angalia Math.4:2.

**Jipake mafuta kichwani** - ujihadhari mwenyewe usije ukawaonyesha watu kuwa umefunga. Tena, wanapaswa wasijue kwa njia yoyote ile. Hili jambo ni kati ya mtu anayefunga na Mungu.

**6:18 Ili usionekane na watu kwamba unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi**.

Fanya hivyo. Hakuna anayehitaji kufahamu kuwa anafunga, na Mungu atakujazi.

**6:19 Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba**

Huu ni mwanzo wa aina nne ya *vitu*. Jambo ambalo mara kwa mara watu katika karne ya kwanza walijali ni ulinzi wa mali yao. Kulikuwa na aina mbili ya mali walizojali; mavazi na fedha. Mavazi yangeharibiwa na nondo, na fedha zingeliwa na kutu. Nyumba zao zilijengwa kwa udongo, ambazo zilikuwa rahisi kuvunjwa na kubomolewa rahisi kuingia ndani.

**6:20 Bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi**;

Sisitizo kubwa katika maisha ni kufanya mapenzi ya Mungu, kutenda haki ili kuonekana mbele za Mungu. Ikiwa haki yetu imekubaliwa na Mungu, na siyo tumetenda ili kutazamwa na watu, ndipo tutakuwa tunaweka akiba katika "banki ya Mungu ya mbinguni." Sisitizo letu linapaswa kuwa juu ya mambo ya kiroho, na kutenda mambo kwa kusudi la kiroho. Matendo yetu yana njia ya "kuhifadhiwa" kwa kuwa anasema:

**Wekeeni hazina** - fanya hivyo, tena na tena, ukiwa na usalama wa kutokupoteza thawabu hiyo. Imehakikishwa katika "benki" ya Mungu.

**6:21 Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwa na moyo wako**.

Ikiwa tunautumia muda na maisha yetu kwa ajili ya vitu vya duniani, ndipo maisha yetu hayatakuwa kama Mungu anavyotaka. Hatuwezi kutumia muda wetu wote duniani na kusema kwamba mioyo yetu iko pamoja na Mungu. Fungu hili ni la ufunuo kwa kuwa unaweza kueleza upendo wa mtu na matakwa yake kwa kuangalia hazina yake. Karibu kila kitu watu wanachofanya kinaonyesha hazina zao zilipo. Hazina ya aina yeyote ile - pesa, mashua, nyumba, n.k., ndiko mioyo yetu inakowekwa, kwa kuwa ndiko mapenzi yetu yanakowekwa.

**6:22 Taa ya mwili ni jicho, basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru.**
**6:23 Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!**
**6:24 Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana mawili; kwa maana atamchukukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali**.
Kama mali ndilo somo katika mst.20,21, na mali ni somo katika mst.24, ndipo mst.22,23 pia itakuwa inazungumzia kuhusu mali. Hili linatusaidia kutafsiri mafungu ambayo kwa wengi ni magumu.

**Taa ya mwili ni jicho.** Jicho linaruhusu taswira ya ndani ya mwili.

**Likiwa safi ...nuru**. "Safi" = "zima" au "lenye afya," lenye kutuwezesha kuona barabara.

Wakristo wanaona fedha kama kifaa cha kusaidia kundeleza kazi ya Bwana, na kutusaidia mahitaji yetu ya msingi; sio kitu cha kufanyia anasa sisi wenyewe. Jicho likiwa safi, litaona vitu kwa mtazamo sahihi.

**Lakini jicho lako likiwa bovu...giza**. Giza katika Biblia inawakilisha dhambi na ujinga. Haya ndiyo anayoyajadili Yesu. Hatutaona vitu kwa njia ile ipasayo kuwa na, matokeo yake, tutajaa na mambo ambayo si ya utauwa. Tunapoona sawa sawa, tumekuwa na tabia aliyokuwa nayo Ayubu - Bwana anatoa na kutwaa.

**Likiwa giza...si giza hilo**. Unaona vitu kwa mtazamo wa uovu, mtu anakuwa gizani na kuwa mwovu zaidi. Mtu ni lazima aanze na jicho lililo safi, lakini laweza kufifia na kufifia hata kujaa uovu, choyo, dhambi, tamaa ya fedha, kama wale katika 2Tim.3:2 (tamaa ya pesa). Mtu anapaswa kuwa makini sana.

**Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili**. Mtu aliye na jicho safi ni yule anayemtumikia Mungu; na yule aliye na jicho jeusi ni yule amtumikiaye Shetani. Hakuna mtu atakaye mtumikia Mungu na Shetani.

**Hamwezi kumtumikia Mungu na mali** - utajiri, milki nyingi, au fedha. Ikiwa maisha yote ya mtu ni utajiri, basi mwili wote umeharibika. Kuna watu wanaoweza kuwa matajiri, pengine kwa maarifa ya biashara au urithi, na katika kila jamii, kupata fedha nyingi, watu wanahitajika kufanya kazi kubwa kwa bidii - muda wa nyongeza, hata siku za mwisho wa juma, n.k. Kile tukipendacho ndicho tunachojitoa maisha kwa hicho na kuzingatia; na wala siyo tunachosema kuwa tunapenda, bali kile tunachoonyesha kukipenda. Watu wachache sana wanaweza kudai kwamba wanapenda fedha na kumchukia Mungu. Naweza kusema, “Nampenda Mungu.” Je, nampenda? Je, nashindwa kuhudhuria ibada kwa sababu ya kufanya kazi muda wa ziada? Kwa nini tunapokuwa na mkutano wa injili, au tunapokuwa na mchango maalum, sipendelei kusaidia? Ni jinsi gani tunadhihirisha kwamba tunapenda. Hatuwezi kumtumikia Mungu na mali. 1Tim.6:9,10 anasema tamaa ya mali ndilo shina la mabaya yote, na wale wote wanaotamani wanajichoma dhamiri zao kwa huzuni nyingi. Tunatamani kuwa nazo, kufanya kazi kwa ajili yake, kinachofuata ni kwamba tuko gizani. Ikiwa jicho linatamani utajiri, ndipo tamaa hiyo itaitia giza nafsi. Itaharibu moyo. Kama jicho linaruhusu nuru ya neno la Mungu, ndipo nafsi itajaa ukweli wa Mungu. Moyo itarejea usafi, mwanga wa mafundisho ya neno la Mungu.

**6:25 Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi**?

“Lakini ninatakiwa niilishe na kuivalisha familia yangu, na kuitunza.” Yesu anasema: **“Msisumbukie maisha yenu**. Hii ni mara ya kwanza neno **msisumbuke** Yesu analitumia kati ya mara tano zote. Mistari 25-34 anajadili juu ya wasiwasi - mtazamo wa Yesu katika eneo hili. Tunaliona neno katika 25, 27, 28, 31, na 34.

**Msisumbukie** - “acheni kuhofu” - kujisumbua ni kujali kusikokuwa kawaida, hasa juu ya mambo ambayo tunatakiwa tusijali, hasa aina hizi tatu kuu:
1. Chakula,
2. Nguo, na
3. Malazi.

Yesu analenga mahitaji ya mwanadamu ya msingi. Hatutakiwa kijisumbua kwa ajili ya hayo. Ni rahisi hili kusema kuliko kutenda! Haya matatu ndio msingi wa kuwepo mwanadamu. Lakini, walio wa kiroho wanatambua kwamba Mungu anajua tunahitaji mambo hayo, na atatujalia.

**Maisha je! si zaidi ya chakula**? Hili hapa anazungumzia kuweka kipaumbele - kuweka vitu katika mtazamo sahihi. Je, maisha si bora kuliko chakula kwa chakula na cheki ya malipo kwa cheki? Tunatia hofu zaidi juu ya vitu hivi? Si mahali pake sisi kuhofu juu ya vitu hivi, hivyo ni kazi ya Mungu. Avon Malone alisema, "Maisha bila Mungu hufupishwa kwa cheki za malipo, siku za mwisho wa juma, na mishtuko hafifu." Katika Yoh.4:34 Yesu alisema, "Chakula changu ndicho hicki, niyatende mapenzi yake yeye aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake."

**6:26 Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao**?

Ndege wa angani:
1. Hawapandi,
2. Hawavuni, na
3. Hawakusanyi ghalani.

Kamwe hawapandi, kamwe hawavuni, na kamwe hawakusanyi ghalani kwa ajili ya baadaye. Hili linahusiana na hazina ya mtu. Ndege hawafanyi hata moja yaliyotajwa hapo juu walakini Baba aliye mbinguni anawajali. Mungu huwapatia mahitaji yao yote.

**Ninyi je! Si bora kupita wao**? Taji ya uubaji wa Mungu ni mwanaume na mwanamke. Kila kitu kilumbwa kwa ajili yao. Kwa hiyo, kama Yesu atasema katika 7:11, "Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwaoa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?" Basi Mungu, Baba yetu wa mbinguni, ni mwenye kutaka kutoa alivyonavyo.

**6:27 Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua anaweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja**?

kipimo cha mkono mmoja ni karibu inchi 8 hadi 24. Tafsiri ya American Standard inasema, "kipimo cha maisha yake." Tafsiri ya King James inasema, "hata katika umbile lake." Hakuna, kwa kujisumbua, kuweza kujiongezea kimo chake. Wengine wanahofu juu ya afya zao wakati wote, na hakika, pengine hata huyafupisha maisha yao kwa ajili ya hilo.

**6:28 Na mavazi, ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya kondeni, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti**.

Kuwa na hofu juu ya mavazi huangukia katika mafungu mawili:
1. Je, itatosha?
2. Je, ni ya kileo? Inapendeza watu? Bora?

Fikirini. "Hayafanyi kazi" wala "hayasokoti" yanasimamia kujisimbua. Hapa kuna wazo la kujisumbua jinsi utakavyovaa vizuri. Maua ya kondeni ni moja ya vitu vizuri sana katika uso wa dunia, wakini hayajisumbui au kufanya kazi.

**6:29 Nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo.**
**6:30 Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba**?

Hakuna lililo gumu kwa Mungu kuyapamba majani ya kondeni, walakini ghafla hutoweka; maua hunyauka, na kuchomwa. Kwa Mungu hakuna la kushangaza, kwa sababu angeweza

kuyarudishia hali ya awali ikiwa anapenda hivyo.

**Huyavika hivi** au “hivyo ndivyo anavyoyavalisha.” “Yamevalishwa” vizuri. Ikiwa anaweza kutenda hivyo kwa vitu ambavyo mara moja anaviangamiza, je si zaidi kuwajalia watoto wake mahitaji yao vizuri zaidi?

**Imani haba**. Hii ni moja ya mara tano zote Yesu anazungumzia kuhusu “imani haba” (8:26; 14:31; 16:8; 17:20). Kuna watu waliowanyoge sana katika imani. Imani ni hali ya kutumaini au mategemeo. Kwa hiyo Yesu anazungumzia kuhusu kuhangaika, kujisumbua, au kuwa na wasiwasi kuhusu mavazi na malazi. Tunapaswa kufanya kazi, lakini ni lazima kumtumaini pia Mungu. Atatujalia vitu kwa kutupatia kazi, lakini mtazamo wetu lazima uzingatie kumtumikia Yeye. Ebu angalia tofauti iliyopo kati ya *imani haba* na *imani kubwa* katika Mathayo (k.m. 8:10).

**6:31 Msisumbuke, basi, mkisema, tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini**?

**Msisumbuke**. Amekwisha tueleza tayari kwa nini: Mungu atatujazi vitu hivi. Ni upumbavu kusema kwamba Mungu hajui au kwamba hatujalii kupata vitu hivi. Kadhalika ni upumbavu kusema kwamba Mungu nguvu zake zimepungua hata asiweze kufanya lolote juu ya hayo, kwa kuwa yeye ni mwenye uweza wote. Alituumba na anajua mahitaji yetu. Anatujali, na atatusaidia.

**Tuvae nini**? Mtu anaweza kuuliza swali hili na asitende dhambi. Ni hofu inayolifanya hili kuwa dhambi. Tunapaswa kujifunza kumtumainia Mungu.

**6:32 Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Mungu wenu aliye mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote**.

Mungu hapungukiwi na **kitu** chochote, anajua kila hitaji tulilonalo. Tunaweza kuachilia kila hitaji kisha **kutafuta** kitu kilicho muhimu zaidi: mst.33.

**6:33 Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa**.

Huu ndio ufunguo: **haki** (5:20). Haki ndilo wazo kuu katika hotuba hii. Haiwezekani mtu kuwa na haki wakati huo huo anajisumbua juu ya chakula na mavazi. Bali **“utafuteni kwanza ufalme wake**”, na **“haki yake”** ni maneno yenye maana moja. Hayo ndiyo tunayopaswa kuyatafuta.

**Tafuteni** inaonyesha kuwa ni tendo la *kuendelea* kufanya. Ni lazima kuendelea kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake. Ni jitihada ya siku hata siku, kama vile mtu anavyotafuta riziki kila siku. Tunasali kwa ajili ya mkate, na kumtumaini Mungu kujibu sala zetu, hivyo basi tutazingatia mambo ya mengine - mambo ya kiroho.

**Ufalme wake** - utawala wake. Hapa hazungumzii kanisa, bali tafuteni kwanza utawala wa Mungu katika mambo ya wanadamu.

Wengi hudai **ufalme** ni neno sawa kila lilipotajwa kama kanisa. Hivi siyo kweli. Ufalme ni utawala wa Mungu. Huo ndio Yesu anauzungumzia. Lakini ufalme “duniani” ni sawa kabisa na kanisa, kwa maana tuna mmoja - na mmoja tu - ufalme mmoja duniani, na huo ndilo kanisa. Tunapozungumzia watu wa ulimwengu, hawawezi kuwa katika ufalme wa Mungu, na wasiwe katika kanisa la Mungu. Mtu angeliwezaje kuwa katika ufalme wa Mungu na asiwemo katika kanisa la Mungu? Je! si Abrahamu, Isaka, na Yakobo wamo katika ufalme? Ufalme wa Mungu unajumuisha watu wote wa Mungu. Wafu na walio hai. Hivyo tunapozungumzia kuhusu ufalme tunapaswa kuchunguza kuwa ama tunamaanisha kanisa au la, ufalme hai duniani, au utawala

wake wote. Hapa kuna mifano ambayo tunapaswa kuichunguza:

1. Mfano wa magugu Math.13:37-43. Baada ya hukumu kutolewa, na Mwana wa Adamu kukusanya kutoka katika ufalme wake...ufalme wa Baba yao. Ufalme, baada ya hukumu, hapa haiwezekani kuwa anazungumzia kanisa.

2. 2Pet.1:11. *Ufalme* wa milele utaruzukiwa kwa ukarimu. Hapa hazungumzii kanisa. Huu ni utawala wa Mungu, ufalme wa Mungu. Kukubali utawala wake - ufalme wake utakuwezesha kingia katika ufalme wa milele. Hivi ndivyo inatakiwa "Ufalme wako uje" isimaanishe tu kanisa. Yesu hazungumzii hilo tu. Tunatakiwa daima kutafuata Ufalme wake. Hakika kuna mafungu ambayo yanazungumzia kanisa na ufalme kuwa kitu kimoja, lakini ni lazima mazingira ndiyo yatoe majibu. Angalia:

Math.18:16ff ufalme na kanisa ni mamoja. Kol.1:13 ..."kutuhamisha na kutuingiza katika ufalme wake..." Hili ni kanisa. Mk.9:1 anazungumzia kanisa. Kulikuwa na watu hasa walioshuhudia kanisa likianzishwa. Ufalme (kanisa) ulikuja kwa nguvu Roho Mtakatifu aliposhuka (Mdo.1:4ff), na Roho Mtakatifu alikuja siku ya Pentekosti (Mdo.2:1ff). Tunatafuta kwanza utawala wa Mungu na haki ya Mungu. Kumbuka 5:20 - lazima izidi **haki** ya waandishi na Mafarisayo. Hivyo maana yake hapa ni, tafuta kwanza utawala wake na kutenda anayotaka, na vitu hivi vyote atakujazi. Tenda haki yake. Na siyo ya mwanadamu, bali ya Mungu.

Na hayo yote ni chakula, mavazi, na makazi. Kumbuka, hii ni kanuni kuu. Lazaro (Lk.16) na wale waliotajwa katika Rum.8:31ff. hawakupata baraka hizi zote kwa kuwa ulikuwa mpango wa Mungu kwa uzima wao. Hatujui hakika ni nini Mungu amepanga kwetu - Mhu.9:1. Tunapaswa kuwa waadilifu, na kumwachia Mungu atende kilicho bora kwetu. Tunapaswa kukumbuka kwamba anatupenda bila kujali kushindwa kwetu - Rum.8:39.

**6:34 Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake**!

Basi inarejea ukweli wa kwamba Mungu anatujalia mahitaji ambayo mwanadamu anasumbukia.

**Kesho**. Kesho ni kitu fulani ambacho sharti tukishughulikie kinapotufikia. Kuhofu kuhusu hicho hakutaleta mabadiliko yoyote.

**Kila siku...yake**. Kila siku ina shida zake. Kusema kwamba Mungu ataondoa shida kutoka katika wale wanaotafuta kwanza, wanashidwa kuelewa kinachoongelewa hapa. Mungu hataondoa udhia. Heri wanaoudhiwa kwa ajili ya haki - Math.5:10,11.

Dhiki = "kakos" lenye maana ya maovu, misukosuko au mambo mabaya. Tunashughukia wenyewe na shida za leo, lakini hatuhofu shinda hizo. "Hofu huvuta wingu la kesho lije juu ya siku ya leo."

Kuna maana tatu kuu Yesu anazungumzia kuhusu hofu (kutoka katika 6:25-34).

1. Hofu ni - ya bure - mst.27,28. Haisadii lolote. Haitendi kazi yeyote! Kuhofu hakuna thamani yeyote!
2. Hofu - haitakiwi mst. 30. Haitakiwi kwa kuwa Mungu ameahidi kutujalia. Kwa nini kutia hofu katika mambo ambayo Mungu atatushughulikia?
3. Hofu - haifai - mst.32. Mambo haya yote Mataifa kwa bidii wanayasumbukia. Wana wa Mungu hawataonyesha kielelezo sahihi kwa ulimwengu iwapo watajisumbua au kuwa na hofu. Msijisumbue kwa neno lolote - Fil.4:6.

## SURA YA SABA

**7:1 Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi.** Usije ukawa mmoja ambaye anapitisha au kufanya hukumu. Neno hukumu ni "krinete" lenye maana kushutumu au kuhuku kwa kuona hatia. Ni kawaida kwa wanadamu kujisikia vibaya kuhusu dhambi za watu wengine. Hawapendi wanapohukumiwa na wengine, lakini wanadhani kuwa ni vyema kuwahukumu wengine. Katika Rum. 2 Paulo anawashutumu Wayahudi kwa maana waliwahukumu Mataifa kwa kufanya mambo yale yale wao nao walikuwa wakiyatenda. "Kwa hiyo wewe...huna udhuru...unafanya yale yale." Unadai kwamba mtu atakwenda Jehanamu kwa kuwa mwongo, lakini unaongopa. (Unafiki.) Wayahudi walikuwa wakihukumu bila kujichunguza kwa makini maisha yao wenyewe. Hakika walikuwa wakitenda dhambi zile zile ambazo Mataifa yalizifanya!

Sisi hatujishughulishi na kuhukumu. Yakobo 4:11,12 anaeleza kwa urahisi mno! "Msisingiziane, au kumhukumu ndugu yake...huwi mtenda sheria bali umekuwa hakimu...kuna hakimu mmoja." Hili je! maana yake ni kwamba hatupaswi kuhukumu kabisa, hata kidogo, au katika hali yoyote ile? La hasha! Ebu chunguza mafungu kadhaa:

Math.7:18-20 - "Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya...ndiposa kwa matunda yao mtawatambua." Hukumu imefanywa kuutambua mti ikiwa ni mwema au mbaya kwa matunda unaozaa. Hii ndiyo njia pekee tunavyowatambua watu kwamba ni wema au ni wabaya, kwa matunda wanayozaa. Tunapaswa kuhukumu kutokana na matunda mtu anazaa.

Yoh.7:24 - hukumu kwa hukumu ya haki, siyo kwa macho tu. Yesu anaema tunapaswa kuhukumu - lakini msingi ni lazima uwe ni wa haki. Mungu amekwisha kuhukumu, lakini sisi tunayachunguza matunda, na kutamka yale Mungu amekwisha kutaja tayari.

Gal.6:1 - Ikiwa mtu anamwona ndugu ameghafilika katika kosa lolote, lazima aifanye hukumu vile Paulo anavyosema kufanya hapa. Mtu aliye wa kiroho ni lazima amrejeza mtu huyo.

Math.18:15ff - Ni jinsi gani kanisa limtenge mtu ikiwa haliwezi kumhukumu mwenye dhambi? Hakimu anaangalia ushahidi na kisha kutoa hukumu - kuwa na hatia au la. Tufanya vile vile kama Gal.6:1 kusimamia ushahidi uliopo. Tunahukumu, hatuwalaumu, bali tuna haki kupitisha hukumu ambayo Mungu ameiweka tayari. Tukiwa hivyo tunaangukia katika mafungu wawili:

1. *Hatufanyi hukumu nje na neno la Mungu lilivyosema*. Kwa mfano, mhubiri anamwambia mtu kwamba ataenda jehanamu iwapo hatabatizwa. Mungu amesema tayari kwamba mtu anapaswa kubatizwa ili apate kuokoka 1Pet.3:21. Mtu anapotoa hukumu nami nikairudia kama ilivyotajwa, mimi siyo hakimu, mimi natoa taarifa. Ikiwa, katika mahakama ya wilaya hakimu akitoa hukuku kwamba mtu ana hatia, mimi sitakuwa hakimu ikiwa narudia alichotaja; mimi ni mtoa taarifa tu "kutaarifu" ukweli. Hatuchukui nafasi ya Hakimu tunapomwambia mtu kile Mungu ameshasema tayari. Hata hivyo, iwapo Mungu hajasema hatupaswi kuhukumu.

2. *Yesu anazungumzia kuhusu kuhukumu dhamiri ya mtu*. Nini mtu ananuia; nini mtu anachofikiri? Nini ilikuwa kusudi lake alipofanya hivi au vile? Kwa mfano, iwapo mtu ameshindwa kufika ibada ya jioni mtu mwingine anaweza kusema, "Pengine huyu ameenda kuwinda." Baadaye imejulikana kwamba alimsaidia mtu ambaye gari lake lilipata pacha tairi. Amekosa ibada kwa kuwa Msamaria mwema. Mtu mwingine anafungua kinywa chake na kutoa hukumu bila hata ya kuwa na ushahidi. Hizi ndizo hukumu ambazo tunapaswa kuwa makini nazo.

Yoh.3:17 "Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni...auhukumu ulimwengu..." Ulimwengu umekwisha kuhukumiwa kwa sababu hauna imani. Neno "krino" limetafsiriwa ama

"kupatikana na hatia" au "kuhukumiwa." Hicho ndicho ambacho Yesu anasema katika Math.7:1. Hatupo katika shughuli za kuhukumu. Hapa, katika Yohana, Yesu anasema wamekwisha hukumiwa tayari.

Warumi 14 anasimulia wenye imani kubwa wakiwahukumu wenye imani dhaifu. Walikuwa wakihukumu na mambo yaliyo nje na maandiko. Lazima tuhukumu kwa kutumia mwongozo tuliopewa na Mungu ama tutaishia kuchanganya na kujishutumu wenyewe kwa miongozo yetu wenyewe, ambayo siyo ya Mungu.

**7:2 Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa**.

**Kwa kuwa hukumu hiyo mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa**. Kama maamuzi yetu ni ya kikatili, kigomvi, na yenye huruma kidogo sana, hivyo tutarajie kupokea hukumu hiyo hiyo kutoka kwa Mungu.

**Kipimo chako**. Kukosa rehema na huruma kwa wengine kutasababisha sisi kukosa huruma na rehema toka kwa Mungu.

**7:3 Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndungu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii**?

Haki ya kweli haina nafasi ya kuwaonyesha wengine vidole. Hili huleta picha ya dharau tunapojaribu kuangalia hivi; mtu mmoja akiwa na boriti katika jicho lake mwenyewe akijaribu kuondoa kibanzi katika jicho la nduguye.

**7:4 Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe**?

Yesu, kama mwalimu mkuu, anahatimisha katika kufundisha somo hili juu ya ndugu. Iwapo tungeachia hapa, tungefikiri hatupaswi kusema chochote juu ya watu katika mambo ambayo wana matatizo. Yesu anatueleza kuwa lazima tujisafishe maisha yetu kwanza, kuhakiki tunajihadhari kwa ushuhuda wetu wenyewe wa kiroho.

**7:5 Mnafiki wewe, itoke kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako**.

Hasemi hatutakiwi kujihushisha na ndugu yetu. Anatueleza kushughulikia matatizo yetu wenyewe, ndipo tutaweza kuwasaidia wengine kutatua matatizo yao. Hatuwezi kuwashawishi wengine kutenda mema ikiwa maisha yetu yenyewe yanakiri dhambi na makosa. Yesu anasema tutakuwa na "sura mbili" ikiwa tuko namna hiyo (kama katika mst.5). Tunawashutumu wengine kwa matatizo yao, wakati huo huo kwa upande mwingine, tunakuwa na matatizo mengi tunakosa uwezo wa kumsaidia mtu mwingine.

Kutokana na mazoea, wanaopambana na matatizo yao wenyewe, na kujifunza jinsi ya kushinda udhaifu huo wana uwezo hata kumsaidia mtu mwingine. "Kibanzi katika jicho" kinahusu tatizo dogo, hasa ukilinganisha na matatizo ya mtu yaliyo mfano wa "boriti." Nikiwa nimekabiliana na udhaifu wangu mwenyewe, ndipo ninapokuwa bora kuweza kumsaidia mwingine. Yesu hasemi kusubiri hata tumekuwa wakamilifu kabla ya hatujamsaidia mtu mwingine. Kama ingelikuwa hivyo basi Gal.6:1 isingelitekelezwa.

...ndipo utakapoona vema kukitoa kibanzi katika jicho la ndugu yako... Mara nyingi tunatoa

hukumu, na wala hatutaki kwa nia njema kuwasaidia wengine. Tunaamuriwa kuungama dhambi zetu sisi kwa sisi (Yak.5:16) lakini mara chache tunafanya hivyo. Hivyo basi, hatujui udhaifu wa kila mmoja. Tunajidhani kuwa ndio sisi wenyewe, na kukabiliana na mambo kiroho, kwa kuwa hatuwaabii watu wengine. Kanisa lazima liwe wazi katika kuwasaidia kila mmoja, lakini ni kwa upendo na upole. "Hatupaswi kuangalia watu tofauti, bali kusaidia shida zao."

**7:6 Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua**.

"Lulu" ni neno lilo hilo katika Math.13:45, 46 - lule ya thamani kubwa. Mafarisayo wanautendea hivyo ujumbe wa Yesu. Hawautambui kama wenye thamani kama ulivyo hasa. Chakula kitakatifu ni kile kilicho kizuri kwa wanadamu, na chakula cha mbwa ni kile kisicho kizuri kwa matumizi ya mwanadamu. Mtu asitoe kilicho kitakatifu kwa mbwa kula. Maana ya kiroho ni, kuna wengine waliokwenda mbali hivyo, tunapoteza muda wetu kuwapatia wasichokitambua kama kitakatifu. Nguruwe atakanyaga kila kitu, ama kiwe lulu au tunda lililooza. Math.15:14 - waacheni.

Math.10:13,14 - "Na nyumba ile ikistahili, amani yenu iifikilie...la, kwamba haistahili, amani yenu na iwarudie ninyi...kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu." Usiwahubirie wasiotaka kusikia kile unachohubiri. Tito 1:15 inafundisha, "...lakini hakuna kilicho safi kwao walio wanajisi...akili zao zimekuwa najisi na nia zao pia." Ebu na tuyatazame haya kwa mitazamo miwili:
1. Mafarisayo kumsikia Yesu wanaweza kuyachukia maneno ya Yesu (hasa kwa kuwa wajiweka wenyewe kuwa waamuzi wa watu).
2. Somo kwa watu ni kujichunguza mioyo yao wenyewe na kuona kile kilichowekwa mbele zao (mafundisho ya Yesu) kuwa ni kitakatifu au la.

**7:7 Obeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa**
**7:8 Kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa**.

Yesu anabainisha mahusiano yaliyopo kati mtu na Baba. Hili ni jambo muhimu sana! Katika lugha ya Kiyunani vitenzi hivi "linear." Ni lazima mtu aendelee kuomba, kutafuata, na kubisha hodi. Katika Lk.18:1-8 ni mfano wa mjane aliyedumu kuomba. Alipata alichokuwa akiomba kwa kuwa alidumu kuomba, si kwa sababu aliomba mara moja tu. Kesheni mkiomba, kwa kuwa ukiomba mara moja unaweza usipate, lakini katika mazingira ya 1Yoh.5:14, 15, ni sharti iwe sawasawa na mapenzi yake. Ikiwa ni sawasawa na hivyo, inawezekana kudumu kwako ndiko kukaonyesha ama kupata au la. Yesu anafundisha asili ya upendo wa Baba, lakini wajibu wao si kukata tamaa. Ni mambo ya mtu binafsi kuamua kutokukata tamaa au la. Tena, katika 1Yoh.5, inakulazimu kuyajua mapenzi ya Baba. Huwezi kumwomba Mungu akusamehe makosa yako ikiwa hauko tayari kutubu na kubatizwa. Unaweza kuomba chochote utakacho lakini kama hutaki kutubu na kubatizwa hauwezi kupokea msamaha wa dhambi. Hilo ndilo 1Pet.3:21 anazungumzia.

**Hupokea**. Hasemi kwamba "inawezekana" bali anasema atapata. Ni kitu gani mtu atafute kwanza? Masihi na ufalme. Iwapo wataendelea kutafuta watapata. Pegine, katika uchunguzi wao wa kwanza kumtafuta Masihi walimkana yeye kuwa ndiye, lakini wakiendelea kumtafuta watampata Masihi wanayemtafuta. Ikiwa mtu anatamani kufahamu ukweli, ataupata! Yakobo 1:5 - Omba, kupata hekima, kuelewa majaribu. Panapokuwa na mambo tunayotaka kuelewa, tunahitaji majibu. Mungu ndiye mtoa hekima. Iwapo mtu anatafuta ukweli, ataupata. Hakuna mtu aliyewahi kuishi, au ataishi, akitaka kujua ukweli ashindwe kuupata. Mtu hajahukumiwa milele bado kwa sababu sijamhubiria. Mungu atamwinua mtu mwingine ikiwa mimi sitaki

kufanya hivyo. Ikiwa majirani zangu wanataka kujua ukweli, na siuhubiri ukweli huo kwao, Mungu atampata mtu anayetaka kufanya hivyo, lakini mimi nitawajibika kama mlinzi asiyefaa Eze.33:6. "Tafuteni nanyi m**ta**ona." Haitatokea kwamba mtu anayetafuta atashindwa kuona kwa kuwa mtu mwingine alishindwa kuhubiri kwake.

Kuomba, kutafuta, na kubisha inajumuisha sala ambazo ni bayana toka mst.9-11. Kunakujibiwa kwa sala. Dumu ikitafuta, ukiomba, na kubisha kisha utapata. Ikiwa mtu anapenda kujua, au anataka majibu, ndipo Yesu anawatia moyo.

**7:9 Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe?**
**7:10 Au akiomba samaki, atampa nyoka**?

Hakika hakuna baba mwenye mapenzi na mwanawe kutenda hivyo! Wala hata Baba yetu hawezi kufanya hivyo. Pengine Yesu anawashambulia tabia ya waandishi na Mafarisayo waliyokuwa nayo mbele ya Mungu. Hawakumwona Mungu kama Baba mwenye upendo kwa sababu ya utumwa, na mateso mengi waliyoyapitia tangu uhamisho. Linga. vitabu vya Hagai na Malaki.

**7:11 Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao**?

Hata watu waovu wangali wana baadhi ya matendo mema. Huwatendea mema watu wa kwao. Kulinganisha, Mungu anajali watu wake.

**Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwimbao**. Angalia anayestahili - kuwa Baba huwapatia wao **wamwombao**. Kwa nini? Kwa kuwa ni Baba yetu, na baba hupenda kuwapatia watoto wao zawadi bora. Yak.1:17 - kila kilicho chema na kizuri hutoka huko... Daima hutoa kilicho chema, na kila kilicho chema kimetoka katika mkono wa Mungu. Tunaimba nyimbo, "Ebu na uhesabu baraka zako," na kuwa na orodha ya vitu vyema vyote. Yesu anatuhamasisha kwamba tuombe. Ni kitu gani unaweza kukitaja ambacho hawezi kutoa jibu? Kila kitu tuombacho, anaweza kutujibu.

**7:12 Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana, hiyo ndiyo torati na manabii**.

Yesu anazungumzia kuhusu njia Mungu anavyoitikia kwa wamjiao na jinsi awatendeavyo mema. Tunapenda kutendewa mema, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwatendea wengine. Tunapenda zawadi bora, hivyo basi tunapaswa kufikiria kile tunachowatendea wengine. Hii imeitwa *sheria ya dhahabu* na ndivyo ilivyo, kama watu wengi walivyoitaja, na ni rahisi sana, lakini yenye mafundisho makubwa. Kwa nini? Kwa sababu, tukitii msitari huu mmoja, tungeweza kutatua matatizo mengi ya wanadamu! Ikiwa kila mtu angeyakabili maisha kwa njia hii, ebu fikiria jinsi maisha haya ambavyo yangelikuwa. Ni kitu gani ungelipenda utendewe? Mtendee hivyo kwa mwingine - Math.6:14, 15.

**Torati na manabii**. Anajumuisha hapa mafundisho yote ya torati na manabii. Linga. pia Math.22:37-40. "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yot, na kwa akili zako zote...na jirani yako kama nafsi yako..."

**7:13 Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo**.

Yesu anahamasisha watu waingie kupitia "mlango mwembamba," ingawa hata hajaeleza ni mlango huu mwembamba ni upi. Yerusalemu ilikuwa na milango mingi, baadhi mipana na

baadhi miembamba. Iliyojulikana zaidi ni milango mipana katika njia pana. Mtu asingelipenda kupitia njia nyembamba, hasa kwa sababu za wevi na wanyama pori, n.k. milango ilikuwa moja ya kuta, iliyoundwa kwa ajili ya usalama na hivyo ikapelekea kutokuwa na mipana mingi. Watu waliizoea milango hiyo, na Yesu kutokana na hiyo anafundisha masomo ya kiroho.

**Njia ni pana ...upotevuni**. Hii ni njia isiyostahili mtu kuwemo, ingawa ni rahisi kusafiri kwayo. Ni rahisi kwa kuwa inarahisisha njia, na yenye kupendeza. Ni njia pana, isiyo na vikwazo vingi. Ni njia ielekeayo katika **maangamizi**.

**Nao ni wengi waingiao kwa mlango huo**. Kuna idadi kubwa ya watu duniani, lakini kundi kubwa halitaokoka kwa kuwa wanachagua njia rahisi. Ebu fikiria juu ya maisha ya Mkristo ya kawaida. Kipi ni rahisi, kutumia pesa yako mwenyewe, au kutoa kiasi kikubwa kwa ajili ya kazi ya Ukristo? Kipi ni rahisi, kupiga baadhi ya simu, na kutembelea, au kukaa nyumbani na kupumzika katika kiti? Mifano mingi katika maisha inatuonyesha ni rahisi kutenda mambo katika njia ya Shetani. Huo ndio mwelekeo ambao dunia inaelekea - njia pana. Ukristo unahitaji kujitia nidhamu mwenyewe na kujikana mwenyewe.

**7:14 Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionayo ni wachache**.

Nyembamba = "nyooka" katika tafsiri ya King James. Neno lina maana ya "taabu" au "dhiki nyingi." Njia kutoka Yeriko kwenda Yerusalemu ilikuwa nyembamba, yenye kona-kona, njia yenye miamba chini ya milima na unyevunyevu. Mbali na ukweli huo ilikuwa njia ngumu, yenye mwinuko mkali. Watu hawa walifahamu ugumu wa kusafiri njia kama hii, hivyo wangelielewa hili la kwamba **nao waionao ni wachache**. Wachache wanaosafiri katika njia hii, anasema, **"waionao."**

Mtu angelipaswa kuitafuta ili aione. Na akiisha kuiona, ilipasa kubakia humo. Ni jambo la kuhuzuni juu ya ukweli wa Biblia kwamba mabilioni ya watu walioishi duniani katika karne zote, ni wachatu tu watakaopata uzima wa milele. Kuna makundi mengi ya dini leo yanayofundisha kuwa watu wote wa dini wataokolewa. Madai haya hayalingani na mafundisho ya Yesu.

**7:15 Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali**.

Ulimwengu wa karne ya kwanza (kama ulivyo wetu) ulijaa walimu wa uongo. Kwa hiyo, wenye haki wanatakiwa kuwa makini sana. Waalimu wa uongo hawatangazi kwa wote, "Mimi ni nabii wa uongo." Wanakuja kwa mavazi mithili ya kondoo - laini, yasioumiza, nyororo. Paulo anawaonya wazee katika Matendo 20:28 ili wakeshe kulilinda kundi kwa kuwa mbwa mwitu wakali wataingi kanisani. Yesu anawaonya watu kuwa macho na waalimu wa uongo. Kilicho muhimu ni jinsi wanavyokujia. Wanaonekana wenye amani, wenye kupenda, wenye sifa zote za kuwa marafiki. Shetani ni nyoka mjanja, na anaitambua njia bora ya kuwadanganya watu kuamini kisicho kweli. Je, wanajitambua kuwa manabii wa uongo? Wengine ndiyo, kama waliotajwa katika 2Tim.3:1-5, lakini wengine wameongozwa vibaya tu, wamedanganyika. Mafungu mengine yanayoonya juu ya manabii wa uongo: Fil.1:10ff wakihubiri kwa wivu na fitina. Wanachohubiri ni kweli bali hawana nia njema.

1 Tim.1:7 wanaotilia mkazo yale wasiyoyafahamu . 1 Tim.4:1ff mafundisho ya mashetani yatafundishwa. 1 Pet.3:16, 17 wanaogeuza na kupotosha maandiko. Kuna watu wengi wanaamini yale wanayofanya kuwa ni sahihi. Lakini wengi wanafanya kwa kuwa wamedanganywa. Math.24:24 - kudanganya, kama yamkini, hata wateule. 2 Kor.11:14 - Shetani anajigeuza na

kuwa mfano wa malaika wa nuru. 2 Pet.2:1 - manabii wa uongo kati ya watu.

**Kwa ndani...mbwa mwitu**. Katika fafanuzi ya Yesu kuhusu walimu wa uongo hunyofoa watu hata kuwa vipande vipande. Mbwa mwitu mkali ni yule anayeng'ata na kunyofoa vipande vipande ili kujilisha mwenyewe. Hakuna nia njema hata kidogo ndani ya waalimu hawa wa uongo. Wanamawazo maovu tu akilini mwao. Kuna wengine wanaowasifia walimu wa uongo. Na husema, "Walakini kuna mambo mema mengi wanatenda." Lakini, ikiwa mafundisho yao yatawapeleka watu jehanamu, ni tofauti ipi matendo yao mema yataleta?

**7:16 Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti?**

Yesu atasema tena katika mst. 20 **"ndiposa mtawatambua kwa matendo yao"** - maana halisi. Zabibu...je? Mpanzi anapanda akitarajia matunda toka kile alichopanda. Hatarajii kwenda katika miiba ya mwituni na kuvuna zabibu njema. Lazima tuwaone waalimu wa uongo kwa mtazamo wa Mungu na si kwa mtazamo wetu. Iwapo mtu amemtii Oral Roberts au Billy Graham yeye si mtoto wa Mungu, bali mtoto wa shetani.

**7:17 Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya.**

Hatusemi, "Angalau unazaa matunda." Iwapo ni mbaya, ni mbaya; haufai kitu.

**7:18 Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri**.

Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya. Mkristo mwema hawezi kuzaa matunda mabaya. Upande mwingine, mti mbaya kuzaa matunda mema. Mwalimu wa uongo hawezi kuzaa matunda mema. Ni matunda gani tunazaa? Je, ni mti mwema au mbaya? Matunda mema ni yale ya roho - Gal.5;22, 23; upendo, amani, saburi, n.k. Hivi ndiyo vitu ambavyo watu wanapaswa kuviona vinatoka kwetu.

**7:19 Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni**.

Badala ya kuacha mfano huu pasipo kuhatimisha, Yesu anamalizia kwa kusema miti mibovu itakabiliana na Mungu katika hukumu na kukatwa. Math.3:10 Yohana anasema mambo yanayofanana. Shoka umewekwa chini ya mti tayari kukata na kutupwa katika moto.

**7:20 Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua**.

Hivi ndivyo utakavyotambua. Yesu anafafanua jinsi ya kumtabua mwalimu wa uongo. Anasema matunda yao ndiyo yatatambulisha jinsi walivyo. Hivyo basi, tunatakiwa kuwa wachunguzi wa matunda. Tunapaswa kuhukumu kwa kile mtu anachofanya; ni chema au kibaya?

**7:21 Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni**.

Neno "Bwana" ni "kurio" kwa Kiyunani. Ni neno lenye maana katika injili ya Mathayo. Neno hili mara nyingi limetumika sawa na YAHWEH katika Agano la Kale la Kiebrania. "Adoni" ni neno la Kiebrania lenye maana "Bwana." Hivyo Yesu anasema, **"Si kila mtu"** asemaye, kurio, kurio. Hili ni la kuvutia, kwa maana Yesu anadai mamlaka kwa ajili yake mwenyewe. Sasa anasema, unaweza kuniambia MMI, Bwana, Bwana. Mwalimu, mtawala, kiongozi, yote hayo yanalenga maana ya neno "Kurio." Rum.10:9,10 tunapaswa kumkiri Yesu kama Bwana. Fil.2:10ff Kila ulimi utakiri.

Kutamka maneno matupu haileti maana yeyote. Hatuwezi kuuingia ufalme wa mbinguni ikiwa tutatamka tu kwamba Yesu ni Bwana. Tunachofanya ni kusema "Bwana, Bwana" na **halafu kufanya mapenzi** ya Baba aliye mbinguni.

Wengi hudai kwamba kinachotakiwa ni imani tu. Lakini Yesu hakubaliani na hilo. Alisema mtu ni lazima **AFANYE** mapenzi ya Baba, na Agano Jipya ndiyo mapenzi yake. Ni mapenzi yake kwetu kutenda matendo mema, Efe.2:10, na ikiwa hatutendi mapenzi yake, hatuwezi kuingia katika ufalme wa mbinguni. Wokovu haupatikani kwa sababu *tumestahili* kutokana na tulichofanya kwanza, bali tunatenda matendo hayo sawasawa na Baba yetu aliye mbinguni ametuamuru kuyafanya. Na, kwa kuwa hatuwezi kuyatenda kikamilifu hivyo tunapatikana na hatia (Yak. 2) ya kuvunja sheria - wavunjaji wa sheria. Kwa kuwa hivi ni kweli na wote tumetenda dhambi, tunahitaji neema ya Mungu. Hii nidyo njia pekee, hatustahili wokovu wetu, lakini hilo halina maana kwamba hatutakiwi kujitahidi kwa uwezo wetu wote kufanya yale Mungu anataka sisi tuyafanye. Neema imewekwa kwao *wanaojitahidi* kutenda yale Mungu anataka ingawa hawawezi kikamilifu. Rum.6:1-3. Mtu asitarajii neema kuzidi ikiwa anadumu kukaa katika dhambi. Wengi huamini kwamba mtu akishaokoka, basi ameokolewa daima, lakini hivyo siyo kweli. Hatuwezi kukaa kudumu katika dhambi na neema izidi. Ni lazima tulitendee kazi neno la Mungu na amri zake na Yesu atafafanua hili katika Math.7:24-27. Yak.2:14-26 - imani peke yake haitoshi. Lazima mtu atende kazi ya Mungu.

**7:22 Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi**?

Mara ya mwisho tumeona WENGI ilikuwa mst.13 (mlango mpana). Wengi wanaoiendea njia pana wanaamini wanastahili wokovu, hata ingawa hawajawa watiifu. Kutakuwa na watu siku ya hukumu ambao watastajabu watakapohukumiwa. Kuna aina tatu ya watu wametajwa ambao wamefanya mambo katika jina (Yesu) **LAKO**. Lakini, kwa kuwa wanatenda isivyo baadhi ya mambo Yesu anasema hajawatambua.

1. **Hatukutoa unabii kwa jina LAKO** - Hawakuwa wakijipadisha wenyewe daraja. Unabii wao ulifanywa kwa mamlaka ya Yesu.

2. **Kutoa pepo kwa jina LAKO** - Hawakujaribu kuchukua sifa ambazo hazikuwa zao za kutolea mapepo. Walifanya hivyo kwa mamlaka ya jina la Yesu.

3. Katika jina **LAKO** kutenda miujiza mingi - kutenda kwao miujiza kulifanyika kwa mamlaka ya Yesu na jina lake lenye uweza mwingi. Watu wengine wanadhani kuwa hawa watu hawakutenda miujiza. Na kama sivyo, basi hata Yesu hakufanya. "Matendo ya miujiza" ndivyo inavyosomeka katika Kiyunani, na ni msemo wa aina hiyo hiyo anaoelezea miujiza aliyofanya Yesu. Huo pia unafanana na Ebr.2:3, 4 - ishara, miujiza na matendo ya nguvu nyingi. Hivi ndivyo mitume na Yesu walifanya; miujiza, nguvu fulani za kuvunja asili. Mara nyingi hatufikirii kuwa ilikuwa hivi. Upande mwingine tunaamini kulikuwa na walipagawa na mapepo, lakini hatutambui kuwa walikuwepo waliotenda miujiza ambao kwa asili walitoka kwa *shetani*. Katika maandiko wakati mwingine nguvu za Mungu na zile za Shetani mara nyingi zimedhihirika zikikabiliana kipindi cha wakati mmoja. Kwa mfano, kipindi cha Musa, Shetani pia aliruhusiwa kudhihirisha nguvu zake kupitia kati ya wachawi - Kut.7:11. Walikuwa hawafanyi "mazingaobwe" tu, bali walikuwa wakitenda miujiza, kama vile Musa. Katika karne ya kwanza Kristo na mitume walitenda miujiza. Manabii pia wa uongo walitenda miujiza na, kama Yesu anavyosema, katika jina LAKE. Lakini walikuwa hawaifanyi kwa njia sahihi. Math.24:24. "...nao watatoa ishara kubwa na maajabu." Yesu anasema waalimu wa uongo watawajia na kutenda miujiza kama vile walivyomwona yeye na mitume wakifanya. Miujiza ya Shetani hailingani na hiyo. Miujiza ya Yesu ilikuwa mikubwa zaidi; isiyotofautina kwa hali

fulani, katika viwango na katika ukuu wake. Mungu alikuwa angali akilazimisha watu wachunguze yale alifundisha kuona kama ni kweli ama la. Miujiza ya Yesu ilithibitihs kwamba alitoka kwa Mungu kwa kuwa ilikuwa mikuu zaidi, kama vile Musa aliweza kupita kiwango cha waganga walivyofundisha.

Zaka.13:2. Unabii - “Nitakatilia mbali majina ya sanamu katika nchi...pia nitawafukuza manabii, na roho ya uchafu, watoke katika nchi.” Atawaondoa manabii wa kweli, na atakapowaondoa watoke katika nchi, kadhalika atawafukuza pepo wachafu. Haya yote yanazungumzia kipindi cha Masihi. Hii ni katika siku ile, siku ya Masihi. Kutatokea wakati ambao hivi vyote vitaondolewa.

1 Kor.13:8ff. Lazima kuwe na kipindi ambacho kazi za miujiza zingekoma. Hakuna nguvu za miujiza kuvunja asili leo zinazofanywa ama Mungu au Shetani. Ushawishi wa Shetani katika jamii zetu unazidi, lakini nguvu za kuvunja asili imeondolewa. Miujiza ilikuwa na kusudi, na kusudi hilo ilikuwa ni kuthibitisha neno la Mungu (Mk.16:20; Ebr.2:1-4). Kulikuwa na ushawishi wa miujiza katika karne ya kwanza. Manabii wa uongo walikuwa wakitenda mambo makubwa katika jina la Yesu ili watu wawafikirie kuwa walitoka kwa Mungu. Lakini Yesu aliwaonya, nasi, kwa kuwaangalia wangelijua manabii ya uongo kwa jinsi yalivyo matunda yao wazaayo. Walikuwa wakitenda mambo makuu, lakini maisha yao hayakuwa na utiifu katika mapenzi ya Mungu. Sheria ya Musa inazungumzia manabii wa uongo. Katika Kumb.13:1, 2 ikiwa mtu angefanya ishara au maajabu na ikatukia kama alivyonena, kisha akasema, “Twende tukaitumikie miungu mingine,” Mungu anasema, msifuate. 1 Yoh.4:1-6. Lazima wafundishe sawasawa na mitume walivyokuwa wakifundisha.

**7:23 Ndipo nitawambia dhahiri; Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu**.

Kuna na watu wasiojulikana na Yesu hata ingawa wanatenda mambo ya mengi katika jina lake. Wanamtambua yeye, lakini yeye hawatambui wao.

**Ondoka kwangu**. Kama matokeo ya kutokufuata Sheria ya Mungu, hawakutambuliwa na Yesu. Hawatapata ruhusa kukaa mbele ya Yesu (1 Thes.1:7-9). Kinyume chake ni kweli. Anayetenda mapenzi yake, anamjua. Yesu alisema katika Yoh.14:15, “Mkinipenda mtashika amri zangu.” Tunadhihirisha upendo wetu kwa utiifu wetu. Matendo 19:13, 14 wana saba wa Skewa walijaribu kumtoa pepo kwa jina la Yesu. Mith.14:12; 16:25. “Kuna njia ionekanayo kuwa njema.” Hili ni jambo la msingi limetokea mara mbili, pengine ili kutufanya tuzingatia kwa makini uwezekano wa mtu kuweza kudhania anaamini kwa moyo na bado akapotea.

Kuamini kwao watu hawa katika Math.7 siyo ndicho tunakijadili hapa, bali yale walikuwa wakifanya. Pengine walidhania kuwa sahihi, lakini haikuwa sahihi. Wengi leo wanaona mambo mengi mema yakitendeka katika jina la Kristo na wangeliona kama unawakwaza iwapo ungesema kuwa wamepotea. Angalia hawa mambo wanayofanya ni yale yale. Hawatendi mapenzi ya Baba. Wanaonekana kama wanatenda yaliyo haki, lakini sivyo. Kuna watu wengi katika madhehebu wanaotafuta ukweli na Yesu anasema ikiwa wanatafuta, wataupata. Lakini iwapo hawatafuti, ndipo hawataupata ukweli. Sababu ni kwamba hawatafuti. Je, ukweli unaweza kujulikana? Ikiwa sivyo, basi tusingelikuwa na uwezo wa kutambua jema na baya. Iwapo hatutendi yaliyo sahihi, basi tunapaswa kubalidilika. SISI ni akina nani? Kuna uchaguzi aina mbili tu. Sisi ama tu kanisa la karne ya kwanza au sisi ni madhehebu kati ya madhehebu. Ikiwa sisi siyo kanisa lile Kristo ametaka tuwe, basi hatustahili kuwepo. Yesu atawahukumu watu wa dini ambao hawatendi mambo jinsi Mungu anataka yafanyike. Ni makanisa mangapi ambayo yanajumulishwa? Efe.2:19-22. Kristo ni jiwe kuu la pembeni. Kanisa ni lazima lijengwe juu ya msingi (mafundisho) ya mitume na manabii Kristo mwenyewe akiwa jiwe kuu la pembeni. Hakuna njia nyingine.

**7:24 Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba**;

Hatujaacha hasa kinachozungumzwa mst. 21. Yeye afanyaye mapenzi ya Baba ataingia. Wote **wasikiao** na **kufanya** (**"tenda"** hasa ndilo neno, sawa pia katika mst.21). Tunamsikiliza Yesu kama anavyowakilisha hotuba hii. Mapenzi yake na mapenzi ya Baba yake yote ni mamoja. Yeye ni msemaji wa Mungu. Yohana anasema yeye ndiye Neno la Mungu (Yoh.1:1). Yesu ni kama vile Mungu anachotaka kusema kwetu.

**Kila mtu**. Yesu anajumlisha kila mtu awezaye kusikiliza maneno haya. Math.13:9 - "Mwenye masikio na asikie." Mungu ametupatia sisi vyombo ambavyo kwa hivyo husikia na kuelewa kilichoagizwa. Wajibu wa kutenda tulichoagizwa ni juu yetu sisi. Hili hasa linafundishwa kwa watoto, walakini pia ni muhimu sana kwa watu wazima. Hekima imedhihika nyumba inapokuwa imejengwa juu ya mwamba imara. Je, tutajenga juu ya kitu kilicho imara? Yeye asikiaye na kutenda ni mtu mwenye hekima. Tunapenda kuwa na vitu bora sisi wenyewe ili kwamba dhoruba katika maisha ishukapo, tutasimama thabiti.

**7:25 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.**

Hili linafafanua vitu vinavyoshambulia ujenzi wa mwanadamu. Sababu ya kusimama imara ni kwamba ilijengwa juu ya **mwamba**. Iwapo mtu anasikia neno na anatenda sawasawa, hatahofu kuhusu udhia katika maisha kwa kuwa kwa jinsi msingi wa maisha ulivyojengwa juu yake.

**7:26 Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga**.

Yeye asikiaye na hatendi sawasawa ni mtu mpumbavu ajengaye maisha yake juu ya vitu ambavyo si imara na si salama.

**7:27 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa**.

Ikiwa tunataka kuonekana wenye hekima, ndipo tutatii maneno ya Yesu. Ikiwa tunataka kuwa wapumbavu, tutafuata njia za ulimwengu. Kujenga nyumba juu ya msingi wa mchanga ni ujinga, kwa kuwa yote itaanguka uvua ikija, na juhudi yote tuliyoifanya itakuwa ni kupoteza muda. Unaweza kujenga kitu cha gharama mno, nyumba nzuri na kutumia maisha yako yote kufanya hivyo. Tunafanya hivyo katika maisha yetu. Ni lazima tujenge juu ya kitu fulani imara - mapenzi ya Mungu, na siyo juu ya kitu kisicho thabiti cha duniani. Tunaimba wimbo wa Edward Mote ambao kibwagizo chake kinaimbika, "Juu ya Kristo, Mwamba Imara, Nasimama; Mingine yote ni mchanga unaozama, misingi mingine ni mchanga unaizama." Ni ajabu, na rahisi kukumbuka, hatimisho la Hotuba ya Yesu ya Mlimani!

**7:28 Ikiwa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake**;

Hapa ni sehemu ya kwanza ya maneno ya ufunguo - **"alipoyamaliza maneno hayo..." Walishangaa mno kwa mafundisho yake**; sababu inapatikana...

**7:29 Kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao**.

Yesu alikuja akidhihirisha uweza na mamlaka ya mafundisho yake. Mamlaka ni wazo la ufunguo katika injili hii. Ikiwa Yesu ndiye (na hasa ndiye) Masihi, atatenda (anafanya) kwa mamlaka. Yesu amedhihirisha mamlaka yake katika sura 7. Sasa, katika sura 8, atadhihihirisha mamlaka juu ya asili na ufalme wa roho kwa kutenda miujiza, ukiwa ni uthibitisho mwingine kuwa yeye ni Masihi.

***Kuna Mafungu Saba yenye vitu Viwili Viwili katika Sura ya Saba***.

1. Hakimu wawili (1-5). Mwenye boriti na mwenye kibanzi, au mtu anayeondoa kwanza,
2. Wasikilizaji wawili waovu (6),
3. Baba wawili (7-12),
4. Milango miwili (13, 14), au njia mbili,
5. Waalimu wawili (15-19),
6. Miti miwili (15 - 19), na
7. Wajenzi wawili (24 - 27).

## SURA YA NANE

Kama ilivyotajwa mapema, Mathayo anasimulia kwa mpangilio wa mzunguko au kielelezo katika injili yake, akisisitiza miujiza, wafuasi, mafundisho, wafuasi, miujiza, ingawa si lazima daima kwa mpangilio huo. Katika mst.1 makutano wakamfuata, kwa sababu ya muujiza uliofanywa katika sura 4, na mafundisho yenye mvuto ya sura 5-7. Sasa, Yesu atathibitisha madai yke ya kuwa Masihi kwa mfululizo wa miujiza ya nguvu. Tutaziita sura 8-9 kuwa ni "sura za miujiza," kwa sababu zote mbili zimejaa miujiza yake.

**Angalia mpangilio wa sura 8 na 9 - sura za miujiza**.

a. Zote mbili zina miujiza aina tano.
b. Zote mbili zina sehemu ya miujiza (8:16, 9:35)
c. Zote mbili zinashughulikia mambo ya pekee ya miujiza.

**Katika sura 8 Yesu anadhihirisha nguvu yake juu ya**:

a. Wenye ukoma (1-4) - nguvu juu ya ulimwengu wa vitu vinavyoonekana.
b. Mtumishi wa akida wa kikosi (5-13) - uweza juu wakati na nafasi.
c. Mama mkwe wa Petro (14-15) - uwezo juu ya ulimwengu wa vitu visivyoonekana (kwa macho).
d. Kukemewa kwa pepo (16, 28-34) - uweza juu ya ulimwengu wa kiroho (ufalme wa shetani).
e. Dhoruba kuu (23-27) - uweza juu ya Asili.

Hakuna miujiza ambayo isingeangukia kati ya aina hizi kuu. Yesu anadhihirisha uweza wake mkuu katika kila hali. Huo ndio muundo unaopatikana katika sura 8, ikionyesha kwamba Mathayo hapendelei mpangilio wa nyakati.

**8:1 Naye alishuka mlimani, makutano mengi walimfuaaa.**
**8:2 Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa**.

Ukoma ulikuwa ni moja ya magonjwa mabaya katika kipindi Biblia. Ni ugonjwa wa ngozi ambao unaharibu taratibu, ngozi kwa ngozi, mwili hata mtu anavuja damu hata kifo. Hata siku hizi mwenye kutawaliwa na ukoma hufungwa bandeji mwilini, akipewa ulinzi wa kila namna. Ilikuwa haiwezekani mtu mwenye ukoma kutakasika (Law.13, 14).

Ukoma ulikuwa ugonjwa wa kuambukiza (ingawa aina nyingine haiambukizi). Inaonekana ule ulioongelewa zaidi katika Biblia ulikuwa hasa wa kuambukiza. Mungu alisema kuwa mtu yeyote atayemgusa mwenye ukoma angelinajisika. Ukoma ulikuwa na mambo mawili:

1. Walijifunika mwili, (hasa vinywa vyao, kuzuia mate kumtemea mtu yeyote).
2. Kupiga kelele, walipokuwa wakisafiri, wakisema wao ni najisi. Inawezekana kuwa na ukoma mkononi au kiganjani mwako tu, au inaweza kufunika sehemu kubwa ya mwili.

**Akamsujudia**. Neno hili ni lile la "kuabudu." mwenye ukoma huyu alimjua Yesu vya kutosha kustahili kuabudiwa.

**Ukitaka.** Tunaweza kuona maumivu, upweke, kukataliwa, na kutengwa kwa mtu huyu. Alitambua kwamba Yesu ana uweza wa kumponya, lakini hajui kama anataka kumfanya hivyo. Kwa kusoma tu ombi la kusihi la mwenye ukoma huyu, tunaweza kumwona akikaribia kumgusa Yesu. Yesu angemkatalia ungekuwaje?

**8:3 Yesu akanyosha mkono wake, akamgusa, akisema Nataka; takasika. Na mara ukoma wake ukatakasika**.

**Akamgusa**. Ulichukua muda gani wa Yesu kumgusa mtu huyo? Wenye ukoma hawakuzoelea kuguswa na mtu wa aina yeyote. Yesu kunyosha mkono na kumgusa ilikuwa ishara ya upendo na huruma ambavyo hakuwahi kuvipata hapo mwanzo, au kwa muda mrefu hakupata.

Je! jambo hili lilimfanya Yesu kunajisika? Makutano walikuwa wakiangalia, na kujiuliza wenyewe swali hili. Wataona kuwa Yesu hakunajisika, kwa kuwa kugusa kwake kutakatifu kulisababisha kilicho najisi kuwa safi. Ndivyo Yesu anachotutendea sisi. Anatugusa katika hali yetu ilinajisi, na kwa kupitia mguso huo, tunatakasika.

Yesu haendi kufundisha maneno mengi, bali anasema, **"Nataka, takasika."** Ingawa Yesu hatumii neno "mamlaka" hapa, uthibitisho wa mamlaka ya Yesu ni dhahiri, kwa sababu anachofanya tu ni kunena na kutokea kama alivyosema. Miujiza hii ingeonekanaje; uumbaji wa mwili upya? Hili litakuwa lazima ni tukio la kustaajabisha! Hatujui jinsi utakaso ulivyotukia, lakini neno "mara" ni la msingi. Kama anavyoandika Mathayo, wasomaji wake lazima wavutiwe na ukweli wa kwamba **"mara"** ikatokea, tena likisisitiza mamlaka ya Kristo (na pengine kudhihirisha kwamba hayo havikuwa viini macho).

**8:4 Yesu akamwambia, Angalia, usimwambie mtu; ila enenda zako, ukajionyeshe kwa kuhani, ukaitoe sadaka kama alivyoamuru Musa, iwe ushududa kwao**.

Kwa nini asimweleza mtu yeyote? Kuna maoni aina nne yaliyotolewa.

1. Pengine hakutaka idadi kubwa kumfuata yeye kwa lengo mbaya.

2. Ingelimletea pengine matatizo mtu mwenyewe, na Yesu anataka kuzuia kutakataliwa na jamii mtu huyu katika uhai wake. Linga. Yoh.9:34 - kipofu alitolewa katika sinagogi.

3. Ingelitia mkazo zaidi katika miujiza, badala ya mafundisho. Yeye anataka mafundisho ndiyo yawe malengo makuu. Math.12:15ff.

4. Ingelipandisha upinzani wa Kiyahudi (Math.21:15). Hili linaendana na maelezo yaliyoelezwa mara nyingi katika injili ya Yohana - "Saa yangu haijawadia." Hakika Yesu alikuwa na ratiba. Wengine wangeliweza, pengine katika kumuunga mkono Yesu, wangeingilia utumishi wake.

Yesu hakutaka iwe hivyo.

**Ukajionyeshe kwa kuhani**. Kufuatana na Law.13:49 na 14:2 hivyo ndivyo sheria ilivyoamuru. Yesu alikuwa akimweleza kufanya yale Musa aliyoamuru. (Maelezo: Yesu wazi aliamini kwamba Musa ndiye aliandika. Hakukubali mawazo yanayotia shaka uandishi wa Musa.) Ingawa Yesu alikuwa analeta sheria mpya, kamwe hakufundisha watu wasitii sheria ya Musa.

**8:5 Hata alipoingia Kapernaumu, akida mmoja alimjia**,

Hapa ni upande wa juu wa Galilaya, karibu na bahari ya Galilaya. **Akida** - Afisa wa Rumi juu ya watu 100. Wakati hili linafanana na Lk.7, lakini haifanani na habari ya Yoh.4:46ff, ambako kuna tofauti kubwa. Akida, alikuwa hasa, siyo Myahudi. Alikuwa Mrumi aliyemwesabu Myahudi kuwa duni. Kwa kuwa Mrumi kungelihitaji unyenyekevu wa hali ya juu kumwendea Yesu kuomba msaada. Lakini alipenda kunyenyekea mwenyewe. Kwa nyongeza, lazima alisifiwa kwa kuona (na kuamini) nguvu za Yesu.

**8:6 Akamsihi, akisema, Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana.**
Bwana...anaumwa sana. Neno hili Bwana ni "kurios." anamsihi na kumwomba Yesu; akinyenyekea hasa mwenyewe kwa kumwendea. Anaonyesha tabia ambayo hatuioni katika viongozi wa Rumi - kuona huruma kwa wengine. Anamjali mtumishi wake. Hii haikuwa kawaida. Alikuwa na moyo mwema, na mmoja anayeweza "kumeza majivuno yake."

**8:7 Yesu akamwambia nitakuja, nimponye**.

Ni umbali kiasi gani unazungumzia? Kapernaum, au nje? Haileti tofauti yoyote kwa Yesu, amependa kusafiri. Mara moja anaelezea nia yake ya kwenda.

**8:8 Yule akida akamjibu, akisema, Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona**.

Hathubutu kuharibu muda wa Yesu. Pia, hathubutu kuona anastahili kuwa mtu kama Yesu kwenda katika nyumba yake. Kila kitu kuhusu akida ni utiifu. Ni mtu mwenye mamlaka kubwa, lakini angali mnyenyekevu sana. Kadhalika anaonyesha ufahamu mkubwa juu ya uweza wake Yesu.

Tungali bado hatujaona kufikia hapa kutueleza kwamba Yesu alihitajika awepo mahali pale ili muujiza kutendeka. Alitambuaje akida hili? Hatujui. Alitambua mamlaka alipoona, aliona katika Yesu.

**8:9 Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, nenda, huenda; na huyu njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya.**

Yesu alistaajabu.

**8:10 Yesu alipoyasikia hayo, alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, Amini, nawaambieni, Sijaona imani kubwa namna hii, kwa ye yote katika Israeli**.

Yesu anawaambia wale waliokuwa wakimfuata, siyo kwa akida.makutano waliomfuata Yesu kutoka sehemu moja hata nyingine wametiwa changamoto kufikiri juu ya alichofanya mtu huyu.

**Amini, nawaambieni, sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli**. Haya ni maonyo juu ya Israeli, kwa kuwa huyu anayaona katika Yesu yale Wayahudi hawayaoni; mamlaka yake, uhakika wake, uweza wake. Anaona katika akida imani, kusadiki, na tumaini. Anamatumaini makubwa katika Yesu kuliko Mwisraeli yeyote yule. Hivyo ndivyo alivyoonyesha. Kustaajabu huko ni moja ya mara chache alivyostaajabia imani ya mtu fulani.

**8:11 Nami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashriki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni**;

Hili linarejea mawazo ya Wayahudi juu ya chakula baada siku ya hukumu juu ya Mataifa. Wayahudi waliamini kwamba Masihi angekuja, pigana na Warumi na kuwashinda katika vita vikali, na kuanzisha utawala wa Kimasihi katika Yerusalem; ufalme ulio sawa na ule wa Daudi.

**8:12 Bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno**.

Mara nyingine tena anawaeleza makutano. Wale watakaotoka "mashariki na magharibi" ni watu wengine wasio Waisraeli. Wazo kama hilo lingewaudhi Wayahudi! Kufikiri kwamba Mataifa kukaa pamoja nao mezani na watu kama Abrahamu, Isaka, na Yakobo ingelikuwa chukizo sana.

"Ufalme wa mbinguni hapa" siyo kanisa hapa, kwa nini? Kwa sababu Abrahamu, Isaka na Yakobo wako ndani ya ufalme, lakini hawako ndani ya kanisa. Lakini wana wa ufalme, Wayahudi, wale walipaswa kumiliki ufalme huu watatolewa nje. Hawatahitajika kuwepo humo.

**Giza la nje**. Mathayo anatumia msemo huu mara mbili nyingine katika injili - Math.22:13; 25:30. Giza la nje ni sawa sawa na kumaanisha kuwa nje ya kambi, nje ya zizi, nje ya wokovu, nje ya ufalme. Hakika hataji mahali pa kupendeza. Hasa Yesu anapopataja ni Jehanamu.

**Kulia na kusaga meno** ni msemo unayojitokeza mara kwa mara katika Mathayo: 13:43, 50; 22:13; 25:51; 25:30. Kulia kunaweza kusababishwa na maumivu makali, yawezekana yakawa maumivu ya ndani, kwa sababu ya upumbavu wao wa kumkana Yesu. Kusaga (kukereza na kusaga) meno ni hali ya kuwa na maumivu. Hapo hapatakuwa mahali pa kufarijika. Maelezo hayo ni kinyume kabisa na kuwa mezani pa Abrahamu, Isaka, na Yakobo. Wazo hili ndilo walikuwa nalo Wayahudi kuhusu ufalme; kupurudika na kula, kwa amani na kuwa na mafanikio makubwa. Sasa Mataifa wataupokea wakati Wayahudi watatupwa mahali pa mateso makubwa.

**8:13 Naye Yesu akamwambia yule akida, nenda zako; na iwe kwako kama ulivyoamini. Mtumishi wake akapona saa ile ile**.

Hivyo basi akida, kwa sababu ya imani yake, atapata kile alichoomba. Angalia kwamba mtumishi alipona **saa ile ile**; alipona mara moja. Yesu aliweza kuponya kupita wakati na nafasi. (Mfano huu ni wa pili wa kuponya).

**8:14 Hata Yesu alipofika nyumbani kwa Petro, akamwona mkwe wa Petro, mamaye mkewe, amelala kitandani hawezi homa**.

Fungu hili ndilo linalothibitisha kwamba Petro alioa - hauwezi kuwa na mama mkwe pasipo kuwa na mke. Pia tunafahamu kuwa kulikuwa na wengine waliooa. 1 Kor.9:5 Paulo alisema kuwa alikuwa na haki ya kuchukua mke kama mitume wengine, pia alisema kuwa alikuwa mzee - 1 Pet. 5:1. Mtu ni lazima awe na mke ili aweze kuwa mzee katika kanisa la Bwana - 1 Tim.3:2.

**8:15 Akamgusa mkono, homa ikamwacha; naye akaondoka, akawatumikia**.

Hii ni mara ya pili tunasoma kwamba Yesu "alimgusa." Pia tunaona mara moja matokeo yanaonekana kutokana na Yesu kumgusa mkono.

Naye akaondoka, na kuwatumikia. Nini tunafanya Yesu akiyagusa maisha yetu? Tumesamehewa, tunamtumikia kama mama mkwe wa Petro alivyofanya. Tunatumika kwa sababu ya upendo, kwa sababu ya shukrani kwa yale tuliyotendewa.

**8:16 Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi**.

Tunaona uweza wa "neno" la Yesu. Yesu aliwaponya "wote." Hapakuwa na hata mmoja ambaye hakuweza kumponya. Mathayo hataki tushindwe kuelewa kwa nini? Msitari unaofuata unatueleza sababu.

**8:17 Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua magonjwa yetu**.

Mpango mtakatifu wa Mungu unaenda kutimilizwa kupitia Yesu. Angalia Isa.53:4.

**8:18 Naye Yesu alipoona makutano mengi wakimzunguka, aliamuru kuvuka kwenda ng'ambo**.

Tena, anataka wamsikilize. Katika utangulizi wa injili, tulionyesha jinsi *kumfuata* likiwa ndilo wazo kuu la UFUNGUO. Sasa, kwa mara ya kwanza, Mathayo atatusaidia kuona maana ya kuwa mfuasi. Ina maana zaidi tu ya kufuatana Yesu kutoka mji huu hata mwingine.

Maelezo:
**8:19 Mwandishi mmoja akamwendea, akamwambia, mwalimu, nitakufuata ko kote uendako**.

**Nitakufuata**. Huyu ni mtu mwenye mamlaka fulani katika jamii ya Kiyahudi. Tunaweza kuvutiwa na waandishi kutaka kwao kumfuata Yesu kokote alikokwenda. Ingawa, ni wazi kutokana na jinsi Yesu alivyomjibu alikuwa na mawazo tofauti kuhusu maana halisi ya "kokote" ilivyo; nini hasa cha kufuata. Je, tuko tayari kumfuata Yesu "popote aendako?"

**8:20 Yesu akamwambia, Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake**.

kwa khiyo, ili mtu awe mfuasi wa Yesu mtu lazima afanye mambo mawili:
1. *Kuhesabu gharama ya kuwa mfuasi*. "Mwalimu nitakufuata ko kote uendako." Lakini Yesu anauliza, "Je, umefikiria juu ya hili? Mbweha na ndege ni bora kuliko mimi. Sina hata mahali pa kulaza kichwa changu." Je, mwandishi alifikiria ufalme wenye raha na mali? Pengine. Yesu anamwambia ahesabu gharama.

2. *Weka kipaumbele* - Yesu lazima awe wa kwanza. Angalia maelezo katika mst.22.

**8:21 Mwingine katika wanafunzi wake akamwambia, Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu**.

Ni jambo la kufurahisha kuona Mathayo anamwita **mwanafunzi** (mfuasi). Neno **mwanafunzi** maana yake ni "mfuasi," lakini kuna tofauti baina ya mfuasi na mwanafunzi wa kweli kweli. Hilo ndilo Yesu atalijadili.

**8:22 Lakini Yesu akamwambia, Nifuate; waache wafu wazike wafu wao.**

Angalia Math.6:33 Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake. Lazima mwanafunzi aweke kipaumbele. Mtu huyu anapaswa kufanya hivi. Kutafuta kwanza ufalme wa Mungu. Kuna watu wanaofikiri kwamba Yesu hakuwa tabia yenye huruma hapa kutokumpatia mtu huyu muda wa kwenda kumzika baba yake aliyekufa. Tunatambua, hata hivyo, kwamba wafu walizikwa siku waliyokufa, hivyo mtu huyu angelikuwa ameshughulikia shughuli kama hiyo anayomweleza Yesu iwapo kweli baba yake alikuwa amekufa. Baba yake pengine alikuwa mahututi, na anataka kumhudumia hata atakapokufa, na ndipo atakuja na kumfuata Yesu.

Ingekuwaje iwapo baba yake angeishi miaka 3 ½? huyu mtu angeikosa huduma yote ya Yesu! Sasa ndiyo wakati uliokubalika kuwa mwanafunzi! Hakuna kusubiri mpaka "hili" litendeke au "lile" litendeke. Lazima iwe sasa! Hii ni moja ya sehemu nne ambazo zinatueleza nini maana hasa ya kumfuata Yesu.

Ebu angalia jinsi tunavyoweza hili kulitendea kazi leo. Kila mtu ambaye anataka kumfuata Yesu ni sharti ahesabu gharama. Lazima awe na kiupambele. Je, kina kitu kingine chochote muhimu kuliko Yesu? Ikiwa kipo, hapo ndipo vipaumbele vyetu havitakuwa katika mpangilio sahihi.

**8:23 Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata**.

**Wakamfuata**. Aliwaeleza watu wawili waliomjia chakufanya, na jambo lingine tunalosoma ni watu **wanamfuata**. Na hili ni jambo la msingi, Mathayo hataki mtu yeyote ashindwe kulielewa hili. Yesu anatueleza tuhesabu gharama na kuwepa kipaumbele. Wanafunzi hawa wanasema wanataka, na wanafanya kama walikuwa wakipenda. Hawaelewi maana halisi ya "kufuata," bali wanafanya hivyo. Wanatambua kwamba wasingepata mahali pazuri pa kulala, na famili ungechukua nafasi ya pili. Hata hivyo, wanamfuata.

**8:24 Kukawa msukosuko mkuu baharini, hata chombo kikafunikizwa kwa mawimbi; naye alikuwa amelala usingizi**.

Yesu amechoka.

**8:25 Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia**.

Kumbuka karibu wanafunzi wanne walikuwa wavuvi. Walijua nini cha kufanya wakati wa dhuruba, lakini hawakujua nini cha kufanya na hii "dhoruba kuu."

**Tunaangamia**. Wanakabiliana na kifo, na wanajua kuwa Yesu anaweza kuwaokoa. Kuna somo lingine hapa. Iwapo anaweza kuokoa kimwili, kadhalika anaweza kuokoa kiroho. Iwapo mtu atamjia Yesu wakati wa dhoruba za maisha ikiwa pamoja na udhia na dhiki zake, Yesu anaweza kuokoa.

**8:26 Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? Mara akaondoka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu.**

Yesu alimwambia akida kuwa alikuwa na imani kubwa. Wanafunzi hapa wameshutumiwa kwa kuwa na imani haba. Jambo hili zuri, hasa ikiwa wametafakari yale Yesu alihatimisha punde katika Hotuba ya Mlimani. Mungu angeliwajalia. Walipaswa kutambua hivyo.

**Akaondoka...akazikemea**. Katika mst.16 alikemea pepo kwa kutumia neno. Sasa tunaona

anauwezo wa kutawala vitu vya asili vya dunia kwa kutumia maneno. Ikiwa Yesu aliumba akitumia neno, si jambo gumu akitumia neno kutuliza. Hivyo ndivyo Petro anasema katika 2Pet.3:5ff.

Maswali ni ya msingi sana katika kitabu cha Mathayo zingatia maswali yote yatakayoulizwa. Mengi ya hayo hatajibiwa. Kwa nini? Anataka tujiulize maswali yayo hayo sisi wenyewe, na kisha kupata majibu ya maswali hayo.

**8:27 Wale watu wakamaka wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii**?

**Huyu ni mtu wa namna gani?** Angalia swali halikujibiwa. Tunapojifunza tunatafakari kuhusu haya. Watu hawa walikuwa na uzoefu wa majini. Kupitia maisha yao yote hawakuwahi kushuhudia dhoruba hiyo, na kuinyoshea kidole tu ikakoma! Mtu huyu ni namna gani, kweli, hata upepo na bahari vinamtii? Waliwahi kumwona akiponya, lakini hawakuwahi kuliona hili hapo nyuma. Basi huyu ni mtu wa namna gani? Kama wasomaji, tunawezaje kujibu swali hili? Shwari **kuu** iliyotokea ilikuwa ni sawa na dhoruba **kuu** yenye ghadhabu.

**8:28 Naye alipofika ng'ambo, katika nchi ya Wagerasi, watu wawili wenye pepo walikutana naye, wanatoka makaburini, wakali mno, hata mtu asiweze kuipitia njia ile**.

Huu ni mwanzo wa muujiza wa tano na wa mwisho. Huu hapa utadhihirisha uweza juu ya ulimwengu wa kiroho. Angalia ulinganifu katika Mk. 5. Huu umetolewa kama mfano wa "synoptic problem" (angalia utangulizi). Tuna watu *wawili* hapa na mtu *mmoja* tu katika Marko. Pengine tatizo linajibiwa kiurahisi. Katika Marko, mmoja wa hao wawili ni msemaji mkuu au ndiye anayezungumziwa, na mwingine ni mhusika wa pili; ambapo Mathayo anataja tu kuwa walikuwa watu wawili. Hii siyo kuhariribu, bali inawekana kueleza. Marko anamtilia mkazo mmoja kati ya wawili. Hata siku hizi tunafanya kama hivyo tunaposimulia matukio.

Marko, katika injili yake, anatuelezea zaidi kuhusu vitendo vibaya alivyokuwa navyo huyo mtu, hata ilishindikana kufunga, na kadhalika. Kwa kuangalia walikuwa na nguvu nyingi kwa kupagawa na pepo waliowatia nguvu. Watu hawa jumla walitawaliwa, na kuongozwa na Shetani.

**8:29 Na tazama, wakapiga kelele, wakisema, Tuna nini nawe, Mwana wa Mungu? Je! Umekuja kututesa kabla ya muhula wetu**?

Wala swali hili halikujibiwa. Mawili yote ni muhimu.

1. **Tuna nini nawe, mwana wa Mungu?** Walitambua (kwa kuwa ni viumbe kutoka katika ulimwengu wa kiroho), Mungu mmoja wa kweli, na kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu. Hakuna cha kumtenda Yesu. Wao wametoka jumla katika ulimwengu wa mapepo wabaya, siyo katika ulimwengu wa roho wema. Linatusaidia hili kuelewa sura 12 Yesu alishutumiwa kwamba alitumia Belzeburi kukemea pepo wabaya. Hawapo katika utumishi wa Yesu wala upande wake. Wako kinyume na chochote Yesu anachojaribu kufanya. Huu ni utawala wa Mungu ukikabiliana na utawala wa Shetani - ugomvi mkubwa baina ya nguvu za mwovu na zile nguvu za mema. Katika Lk.17:21 Yesu anasema, "Ufalme wa Mungu uko katikati yenu" - hakika Yesu amekuja na uweza na mamlaka yote. Uweza wake Yesu ni mkubwa kuliko ule wa Shetani. Iwapo tutatii chini ya Yesu, kama Yakobo anavyosema katika 4:7, Shetani atatukimbia.

2. **Je, umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?** Muhula upi? Na jinsi gani walitambua kwamba alikuwa awatese? Kwa kumtambua Yesu, walijua mamlaka yake, na kwamba ndiye

huyo ambaye wangetoa hesabu zao siku ya hukumu. Mashetani walitambua kwamba watateseka kwa maana hawana tumaini kabisa. Mwandishi wa Waebrania anaelezea kwamba Yesu hawasaidii malaika, bali kwa watoto wa Abrahamu (Ebr.2:16). Viumbe vya kiroho vikikengeuka haviwezi kurejea kuwa malaika wa Mungu. Wakisha shuhudia uweza na utukufu (katika uumbaji) wa uumbaji na kisha wakakengeuka, hawawezi kupata fursa nyingine tena. Mapepo ni malaika waliokosa (Yuda 6 na 2 Pet.2:4,5). Ni vigumu kusema kwa nini kwa sababu Biblia haielezi. Pepo hawa wanatambua kwamba siku moja iliyoteuliwa watahukumiwa kuteswa.

**8:30 Basi, kulikuwako mbali nao kundi la nguruwe, wengi wakilisha**.

Yesu hayupo katika nchi ya Palestina, lakini ng'ambo ya Galilaya katika nchi ya Wagerasi.

**8:31 Wale pepo wakamsihi, wakisema, Ukitutoa, tuache twende, tukaingie katika lile kundi la nguruwe**.

Hili ni shurutisho la sentensi za daraja la kwanza, ikimaanisha "kwa kuwa wewe utatutoa." Pepo hakutaka akose mahali pa kukaa, hasa hawa wangelipendelea kukaa katika miili ya nguruwe kuliko kukaa mahali pasikuwepo miili yoyote. Walitambua kwamba Yesu alikuwa awafukuze; ndiyo sababu iliyomleta - kudhihirisha uweza wake juu ya Ibilisi na kazi za giza. (Math.12:43ff. - "wakitafuta pa kupumzika" ni mahali penye mwili wa kuumiliki).

**8:32 Akawaambia, Nendeni. Wakatoka, wakaingia katika kundi la nguruwe; na kumbe! Kundi zima likatelemka kwa kasi gegeni hata baharini, wakafa majini.**
**8:33 Lakini wachungaji walikimbia, wakaenda zao mjini**

Yesu alikubali ombi lao la kuwaingia nguruwe. Wakawaingia nguruwe, wakatelemka kwa kasi gegeni hata majini. Inasemakana kulikuwa na imani za kale zile (hakuna uthibitisho kuwa ni za kweli) njia pekee ya kuyashinda mapepo kwa kufa maji. Inaonekana hili kusadikika japo kidogo kutokana na Mk.5:13; Lk.8:33, mafungu yanayosisitiza kwamba **wakafa maji** au **wakaangamia baharini**. Lk.8:33 - "Pepo wakamtoka...wakafa maji." Math.12:43 - "...hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika." Je, tunaweza kutoa maoni kutokana na maelezo haya? Tunachoelewa ni kwamba Yesu alidhihirisha uweza wake wa kutawala, pia uweza wake wa kuangamiza. Inawezekanaje sababu iliyomfanya Yesu aruhusu pepo wabaya kuwaingia nguruwe ilikuwa hivyo ili kudhihirisha uweza wake wa kungamiza? Vyovyote vile, anafahamu kilichokuwa kitokee, aliruhusu. Yesu ni Bwana wa kuumba, na kwa sababu hiyo, anaweza kufanya hivyo kama apendevyo.

**8:34 Na tazama, mji wote ukatoka kwenda kumlaki Yesu; nao walipomwona, walimsihi aondoke mipakani mwao**

Pengine waliingia hofu kwa sababu ya uweza wake, siyo kwa sababu (kama wengine walivyodhania) waliogopa maangamizi mengine kutokea katika maisha yao. Pengine walitaka aondoke kwa sababu ya vitu vyao, au kwa sababu ya uwezo wake, walipaswa kuuliza maswali kuhusu mtu huyu. Watu walipomwona Yesu, kulikuwa na kitu ambacho kiliwafanya washikwe na fadhaa. Marko anaandika mistari 17 juu ya tukio hili, wakati Mathayo anaandika mistari 6 tu. Marko anatueleza kuwa, "Wakamwendea Yesu, wakamwona yule mwenye pepo...ana akili zake ... wakaogopa" - 5:15. Watu walihofia uweza wa Yesu, "Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao." - 5:17.

## SURA YA TISA

Sura hii ina miujiza mitano. Yote ni miujiza ya kimwili na inahusisha:

1. Mtu mwenye kupoza (1-9)
2. Msichana aliyekufa (18, 22-26),
3. Mwanamke mwenye kutokwa na damu (19-21),
4. Vipofu (27-31), na
5. Bubu (kiziwi) (32 - 34).

Katika mistari hii, magonjwa ya nje (kipofu, bubu), magonjwa ya ndani (kupooza, kuvuja damu), na mauti - aina tatu zikiwa na mifano mitano.

**9:1 Akapanda chomboni, akavuka, akafika mjini kwao**.

Hapa ni Kapernaum (Math.4:13).

**9:2 Na tazama, wakamletea mtu mwenye kupoza, amelala kitandani; naye Yesu, alipoiona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza, Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako**.

Kuna mambo mawili ya kuvutia hapa:

1. Wakamletea "wao" katika mstari huu ni wale walimjali rafiki yao hata kumbeba hadi kwa Yesu alipokuwa. Jambo la msingi kwa wanaodai "kutenda miujiza" siku hizi kuona kwamba Yesu alimponya huyu aliyepooza kwa imani "yao," na sio kwa imani yake yeye aliyeletwa kwake. Hao "watenda miujiza" wanaodai miujiza haitatendeka iwapo mtu hana imani ya kutosha wanapaswa kufahamu kwamba aliyeponywa hakuhitaji awe na imani yoyote ile.

2. Yesu hakumwambia mtu huyo ameponywa, bali alimwambia alisamehewa dhambi zake. Yesu anafundisha kwamba ni muhimu zaidi kuponywa kiroho kuliko kimwili.

**9:3 Na tazama, baadhi ya waandishi wakasema nafsini mwao, Huyu anakufuru**.

Walimshutumu Yesu kukufuru kwa sababu anayeweza kusamehe dhambi ni Mungu tu.

**9:4 Naye Yesu, hali akijua mawazo yao, akasema mbona mnawaza maovu moyoni mwenu**?
**9:5 Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, Umesamehewa dhambi zako, au ni kusema, Ondoka, uende**?
Tena, hakuna jibu lililotolewa, lakini lililo rahisi lingekuwa "umesamehewa dhambi zako" kwa sababu mtu asingeweza kuthibitisha kama ni kweli ama la. Yesu tena anatumia mambo ya mwili kuthibitisha anaweza kusaidia ya kiroho.

**9:6 Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (amwambie yule mwenye kupooza) Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako**.

Yesu anathibitisha kitu kimoja kwa kufanya kingine. Alitenda kazi ngumu zaidi (jitwike kitanda chako), akithibitisha kuwa alikuwa na uwezo wa kufanya kazi ndogo ya (kusamehe). Mamlaka ya Yesu yamedhihirika hapa. Majadiliano yametolewa na watu wengine kwamba mwizi msalabani hakutakiwa abatizwe, hivyo basi hata watu leo. Msitari huu, hata hivyo, unaweza kutusaidia kuelewa tukio hilo. Angalia:

1. Yeye (mwivi) aliishi chini ya Sheria ya Kale, hivyo basi sheria ya ubatizo haimhusu.

2. Yesu alikuwa na uwezo wa kusamehe dhambi. Ikiwa alitaka kufanya hivyo, angeweza

kufanya. Lakini alipopaa kwenda mbinguni, aliacha mpango wa jinsi sis kupata msamaha. Petro anaufundisha huo katika Matendo 2:38.

3. Hatuwezi kuthibitisha kwamba mwizi msalabani hakubatizwa. Pengine alibatizwa kwa ubatizo wa Yohana, au kwa ubatizo uliofanywa na mitume.

**9:7 Akaondoka, akaenda zake nyumbni kwake.**
**9:8 Makutano walipomwona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii**.

**Makutano walipomwona**. Wameingiwa na hofu (kicho), hawakuweza kuamini macho yao walichokiona. Wakamtukuza Mungu kwa kuwa hawakuwa na jinsi isipokuwa furaha kwa jilia yake aliyeponwa.

**Aliyewapa watu amri ya namna hii**. Mathayo anataka kuwashawishi Wayahudi waamini kuwa Yesu ndiye Masihi. Hii ingelikuwa ni sehemu muhimu sana katika kutekeleza lengo hilo. Watu walimstaajabia Yesu. Makutano wamesimama kinyume na waandishi (katika mst.3) ambao walimshutumu kwa kukufuru.

**9:9 Naye Yesu alipokuwa akipita huko aliona mtu ameketi forodhani, aitwaye Mathayo, akamwambie, Nifuate. Akaondoka, akamfuata.**

Siyo jambo la kutushangaza kuona kwamba Mathayo anaandika kuitwa kwake mwenyewe humu. Kuna mambo mengi ya maana kuhusu Mathayo, kama mwanadamu, zilizoandikwa katika maelezo haya. Kuna makala nyingi kutoka kwa Wazee wa Kanisa (church fathers) zilizoandikwa kuhusu Mathayo huyu. Biblia inasema kwamba alikuwa mtoza ushuru - Myahudi aliyeajiliwa na Warumi kukusanya kutoka katika watu wake mwenyewe. Kazi hii ilidharauliwa sana na Wayahudi kwa sababu ya:

1. Chuki bure yao kwa Warumi na yeyote aliyefanya kazi kwa Warumi.
2. Dharau ya kawaida juu ya kulipa kodi.
3. Watoza kodi waliokuwa si wadilifu; walizidisha viwango vilivyopangwa halali vya Rumi alivyotakiwa mtu kulipa. Yohana Mbatizaji aliwaambia watoza ushuru wasitoze zaidi ya iliyotakiwa Lk.3:12,13. Watoza usuru walikuwa wakijilimbikizia mifuko yao wenyewe toka kwa mali ya wengine.

Mchanganyiko wa pekee wa wanafunzi unafaa tuuangalie; Wazoleti, wavuvi, watoza ushuru, n.k. - watu walifanya kazi pamoja bega kwa bega, mbali na uhasama wa kawaida baina yao. Yesu ameweza kuleta amani na umoja toka kwa watu mbalimbali.

**9:10 Ikawa alipoketi nyumbani ale chakula, tazama, watoza ushuru wengi na wenye dhambi wakaketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake**.

Hapa tunaona marafiki wakila chakula pamoja. Idadi inawajumuisha watoza ushuru wengi na wenye dhambi. Wenye dhambi ni wale wasio na dini au wasiojishughulisha na Uyahudi. Wao hawakupendezwa na dini ingawa walikuwa Wayahudi. Yesu "anashirikiana" na watu wa "hali ya chini" katika jamii. Wapinzani wake walijenga hoja hii. Hapa ni fafanuzi nzuri kwetu sisi katika maisha yetu wenyewe tunapozungumzia kuhusu kuwa "duniani na pasipo kuwa wa dunia." Yesu alikuja kutafuta na kuokoa kilichopotea, walakini hicho hasa ndicho alichofanya - nasi ni sharti tufanye vivyo hivyo.

**9:11 Mafarisayo walipoona, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona mwalimu wenu anakula**

**pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi**?

Yesu hatendi kwa mfano wa Rabi, ambaye hakushirikiana na watu kama hawa. Wamekuja kufahamu kwa nini Yesu anafanya kama hivyo. Yesu amelizungumzia hili katika sura ya 11:16 - 19, "Lakini nitakifananisha na nini kizazi hiki...maana Yohana alikuja, hali wala hanywi, wakasema, 'Yuna pepo!' Mwana wa Adamu alikuja, akila na kunywa, wakasema, 'Mlafi huyu, na mlevi...'" Walimlaumu Yohana kwa kutokufanya chochote, pia wakamlaumu Yesu kwa kufanya mambo yayo hayo. Yesu anasema hawawezi kuridhika hata angefanya vipi hawawezi.

**9:12 Naye alipoosikia, aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi**.

Anafundisha kutokana na maisha ya kila siku. Waliowagonjwa kimwili wanahitaji msaada (daktari), pia wagonjwa kiroho wanahitaji msaada (Yesu). Kusudi la huduma yake Yesu nikuwafikia wagonjwa - kimwili, naam; lakini muhimu zaidi, kiroho.

**9:13 Lakini nenda mkajifunze kuhusu maana ya maana haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye akili, bali wenye dhambi**.

**Mkajifunza**. Ukweli ni kwamba hawakujifunza vya kutosha kwa sababu hawakujifunza kilichopaswa kujifunza. Kungelikuwa na baadhi wangeweza kunukuu sehemu hii ya maandiko, Hos.6:6. Kujua kinachozungumzwa na kukielewa ni mambo mawili tofauti.

Neno "huruma" ni "eleos" (kama katika 6:1 "jihadharini...msifanye wema"), matendo ya huruma au ya haki. Imetafsiriwa "huruma" lakini Yesu anasema anachotaka Mungu ni pamoja na wao kuwafikia watu na kuwasaidia. Kwa Wayahudi, Yesu anasema haya katika kujibu maswali ya nafsini mwao juu ya kula na kunywa na wenye dhambi. Hakuna miongoni mwa viongozi wa Kiyahudi wangedai kuwa wenye dhambi si wagonjwa. Lakini wasingekuwa miongoni mwa wanaohitaji msaada. Wanafuata Sheria ya andiko, lakini roho ya sheria imesahaulika. Anawataka wasiwe na dini isiyo na huruma bali wenye dini ya huruma.

**Sadaka** = taratibu za ibada za kusahihisha, Sheria ya andiko.

**Sikuja...wenye haki, bali wenye dhambi** = wanaojiona wenye haki kama vile Mafarisayo ambao hakutumwa awaite wao; watu ambao hawakutambua hata kwamba wamepotea na hakika walimhitaji Yesu. Daktari hatamsaidia mtu asiyemwendea ili atibiwe. Wenye dhambi walio na toba ndiyo walijua walimhitaji msaada.

**9:14 Wakati ule wanafunzi wake Yohana wakamwendea, wakasema, kwa nini sisi na Mafarisayo twafunga, bali wanafunzi wako hawafungi**?

Swali lililoulizwa halina uhasama ndani yake. Ni swali zuri. Yohana alisema tunafanya kazi kwa pamoja, lakini unaonekana unaenda tofauti, sasa tunataka tufahamu kwa nini hivyo. Ndipo Yesu anajibu katika mstari ufuatao.

**9:15 Yesu akawaambia, Walioalikwa arusini wawezaje kuomboleza, muda bwana arusi akiwapo pamoja nao? Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi; ndipo watakapofunga**.

Mara nyingi kufunga ni ishara ya kuomboleza. Wanafunzi wa Yohana walionekana zaidi kukubaliana na Mafarisayo, na hili halikuwa na maana. Kufunga kote kulifanyika kwa sababu ya kutafuta wokovu toka kwa Mungu, lakini sasa wokovu uko hapa - bwana arusi yupo hapo - hivyo basi si muda walioalikwa (mitume na wanafunzi) kuomboleza, bali kusherehekea. Mwokozi,

Masihi wao, Yesu, alikuwa kati yao na hawakumtambua! Siku zitakuja ambapo kuomboleza kutakubalika; wakati bwana arusi - Yesu - ataondolewa na kusulubiwa.

**9:16 Hakuna mtu atiaye kiraka cha nguo mpya katika vazi kuukuu; maana kile kilichotiwa huondoa kipande cha lile vazi, na pale kilipotatuka huzidi**.
**9:17 Wala watu hawatii divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama wakitia, vile viriba hupasuka; divai ikamwagika, na viriba vikaharibika; bali hutia divai mpya katika viriba vipya, vikahifadhiwa vyote**
.
Ikiwa tutaliangalia hili katika mazingira yake ni rahisi kuelewa. Viongozi wa Kiyahudi walimtaka Yesu alingane na tabia zao za kale jinsi ya kufanya mambo - njia ile Mafarisayo waliyafanya. Walifarijika na Sheria ya Kale, na walikuwa na maoni yao juu ya mipango na malengo ya Masihi. Sivyo kuwa walifikiria hili vazi la kale (Sheria ya Kale) haikuhitaji "kiraka" hapa na pale. Sheria ya Kale haikuwa kamilifu, lakini hawakuitaka kuitupa. Yesu alikuwa, hata hivyo, na utaratibu wa sheria mpya kabisa. Yesu haindi "kutia kiraka" katika Sheria ya Kale, atabatilisha na badala yake kuiweka sheria mpya.

Mistari hii miwili ni moja ya mafungu yasiyoeleweka zaidi katika Agano Jipya. Kuna waojaribu kuitumia mistari hii kutokukubaliana na mafundisho ya Biblia juu ya mfumo wa uongozi wa kanisa, madaraka ya mwanamke, vyombo vya muziki katika ibada, n.k. Hoja zinazotolewa ni kwamba mambo hayo ni "vazi la kale" na zinatakiwa kutupwa. Kutumia hivyo sehemu hii ni "kugeuza na kupotosha" Maandiko. Yesu alituachia yale ambayo daima yatafaa hadi atakaporudi tena (Ebr.13:8; Gal.1:8,9; Yuda 3).

**9:18 Alipokuwa akiwaambia haya, tazama, akaja jumbe mmoja, akamsujudia, akisema, Binti yangu sasa hivi amekufa; lakini njoo, uweke mkono wako juu yake, naye ataishi**.

Myahudi huyu alikuwa kiongozi wa sinagogi, na ilikuwa muhimu sana karibu kila jamii yenye idadi fulani kuwa na sinagogi, mahali ambao palikuwa ndio kituo kikuu cha kukusanyikia mjini hapo au jijini hapo. Hivyo basi, kuwa kiongozi wa kituo maalum hicho, ilikuwa ni fursa kubwa yenye mamlaka na heshima. Si jambo dogo mtu huyu mkubwa kumsujudia Yesu. Aliifahamu vyema ibada, kwa maana aliishuhudia hekaluni. Anaisimamia ibada kila siku katika sinagogi.

**Binti...naye ataishi**. Hii ni kuonyesha imani kubwa. Amehatarisha nafasi yake katika sinagogi, na hajali. Binti yake amekufa na anajua kwamba mtu huyu angefanya jambo fulani juu ya hili.

Amekufa sasa hivi inaonyesha alimwendea Yesu muda huo huo alivuta pumzi ya mwisho. Kuna dharura katika hilo yaani limetoka tu, na kwamba Yesu angali anaweza kufanya kitu fulani kufuatia lililotokea.

**Naye ataishi**. Siyo pengine, bali ataishi! Mtu huyu amekuwa mwanafunzi mzuri wa maandiko, macho yake hayajapofusha kama wengine wa wakati wake. Anatambua mkono wa Yesu unaweza kuponya kwa maana ameona hayo mara nyingi kwa mashaka.

**9:19 Akaondoka Yesu, akamfuata, pamoja na wanafunzi wake**.

Katikati ya mazungumzo yake na wanafunzi wa Yohana, wanafunzi wake na Mafarisayo, Yesu akainuka na kuondoka! Ghafla, amekatishwa.

**9:20 Na tazama, mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, alikuja kwa nyuma, akaugusa upindo wa vazi lake**.

Ni maumivu ya jinsi gani mwanamke huyu alivumilia! Miaka kumi na miwili ya maumivu ya ndani na kikwazo alichokuwa nacho kiini cha kumtia katika huzuni daima.

**Akaugusa upinde wa vazi lake**. Hes.15:38,39,40 panazungumzia kuhusu vishada katika mavazi "ili mpate kukumbuka na kuyafanya maagizo yangu yote, na kuwa watakatifu kwa Mungu wenu." Pengine hiyo ndiyo sehemu aliigusa katika vazi la Yesu - upinde au vishada. Septuagint inatumia neno sawa na tulilonalo hapa. Katika Mathayo 23:5 Mafarisayo walitanua matamvua ya mavazi yao. Vazi la Yesu dhahiri lilikunjwa kwa vishada. Kulikuwa hakuna kosa kuwa hivyo. Ilikuwa kutanua ndiko alikushutumu katika Math.23.

**9:21 Kwa maana alisema moyoni mwake, Nikigusa tu upindo wa vazi lake nitapona**.

Alikuwa akififikiri, "Sitakiwi hata kumsumbua. Ninacho hitaji ni kugusa tu moja ya vishada vya vazi lake, hapo nitakuwa nimepona!! Hii ilikuwa imani kama ya yule mkuu wa sinagogi aliyoionyesha. Aliamini kuwa angeliponywa.

**9:22 Yesu akageuka, akamwona, akamwambia, Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya. Yule mwanamke akaponywa tangu saa ile**.

Alimwamini Yesu angeweza kumponya, na hakika, alimponya. Ilikuwa ni imani yake iliyomponya. Hakuvunjika moyo; aliitumia fursa, kisha akaponywa. Tungeweza kuacha kuelezea kila muujiza na kuwa na maana moja. Tunaona katika simulizi Mathayo anazofanya kwamba Yesu ni Masihi aliyetabiliwa, na anatueleza kuwa Yesu ni mtenda miujiza aliyetabiriwa (Math.8:17). Maana hii imeelezwa kwa mapana zaidi, na tumepewa fafanuzi binafsi zikionyesha kuwa Yesu ndiye aliyechukua magonjwa yetu. Watu wanamwangalia Yesu, na kwa uchunguzi wanaamini kwamba anaweza kuwasaidia, ndipo wanapofanya jambo fulani. Wanaidhihirisha imani yao. Mathayo anajaribu kuwaelimisha Wayahudi wamwamini Yesu kuwa ndiye Masihi wao, lakini wanapaswa *kufanya* jambo fulani ili waweze kusaidiwa naye. Iwapo angewasaidia maradhi yao ya kimwili, kusingelikuwa na haja ya wao kuamini kwamba hawezi kuwaponya magonjwa yao ya kiroho.

Wote waliokuwa wagonjwa au kupagawa na pepo wabaya waliponywa. Walimwendea Yesu na hawakuvunjwa moyo. Tunaamini kwamba Yesu anaweza kutuponya maradhi yetu ya kiroho. Anaweza, na hatutakatishwa tamaa. Bali, ni lazima *tutende* sawasawa ili tuweze kupata baraka.

**9:23 Yesu alipofika nyumbani kwa yule jumbe, aliona wapiga filimbi, na makutano wakifanya maombolezo**.

Yesu alipofika hapo kulikuwa ghasia tupu.

Kelele bila mpangilio ilikuwa kulia, kuomboleza, kutoa sauti kuu, n.k. Jamii zetu kwa upande wetu zimekuwa tofauti kama za jamii za Kiyahudi katika kuomboleza. Wayahudi, kuomboleza kulilinganishwa na maafa. Kadri maafa yalivyokuwa makubwa ndivyo kuomboleza na kulia kulivyokuwa pia. Ebu fikiria idadi ya watu wangekwenda kwa binti wa mtu mkubwa huyu. Wapiga filimbi ni wale walikodishwa kufanya hivyo.

**9:24 Akawaambia, Ondokeni; kwa maana kijana hakufa, amelala tu. Wakamcheka sana**.

**Kijana** (msichana) = karasin = "msichana mdogo," msichana mwenye umri mdogo usio ule wa kuolewa.

Wakamcheka sana. Hawa ni waombolezaji wenye ujuzi na waliutambua mwili wa mtu aliyekufa

mara tu walipoona. Hii inadhihirisha kwamba watu hawa hawakuwa wakihuzunika hasa. Hakika wazazi wasingelicheka katika kipindi kama hiki. Lakini waliokodishwa kuomboleza wangelifikiri kwamba Yesu ni mwenda wazimu kwa kusema hivyo. Hili halifundishi "kulala kwa roho" kama wengine wanavyofundisha. Angalia marejeo katika habari ya binti yake Yairo katika Lk. 8:41ff. hasa mst. 55. Angalia pia marejeo katika habari ya Lazaro aliyefufuliwa toka kwa wafu - Lk.16.

**9:25 Lakini makutano walipoondoshwa, aliingia, akamshika mkono; yule kijana akasimama**.

Siyo kiini-macho hapa; alimwinua kwa mkono hapa, na mara moja akapona.

**9:26 Zikaenea habari hizi katika nchi ile yote**. Kumfufua mtu kutoka kwa wafu ni habari njema haswa. Hukuona haya kila siku!

**9:27 Yesu alipokuwa akipita kutoka huko, vipofu wawili wakamfuata wakipaza sauti, wakisema, uturehemu, mwana wa Daudi**.

Katika Yoh.9:39-41, baada ya Yesu kumponya mtu aliyezaliwa kipofu, Yesu alitoa maelezo juu yao walio vipofu hasa. Si wale wasioweza kuona kwa macho yao walio vipofu, bali wasioweza kuona kwa mioyo yao, macho yao ya kiroho.

**Uturehemu**. Hili ni "eleos," rehema, matendo ya upendo. Wanaomba macho yao yarejee.

Mwana wa Daudi. Wanamwita Kristo, Masihi; vipofu wawili wameweza kuelewa kwamba Yesu ndiye Masihi. Kweli hilo ni la maana sana!

**9:28 Naye alipofika nyumbani, wale vipofu, wale vipofu walimwendea; Yesu akawaambia, Mnaamini kwamba naweza kufanya hili? Wakamwambia, Naam, Bwana**.

Tunauliza swali lilo hilo. "Je, tunaamini kwamba Yesu anaweza kufanya hili? Kutegemea na jinsi tulivyojifunza tunasema kweli, lakini mioyo yetu imekuwa wazi kuliko Wayahudi waliokuwa wakisona haya. Wangali bado walimtilia mashaka Yesu, bali watu hawa wawili wanasema, "Naam Bwana." Tuna watu wengine hapa wanaoamini.

**9:29 Ndipo alipowagusa macho, akasema, Kwa kadiri ya imani yenu mpate**.

Ikiwa tutamwendea Yesu kwa imani tutapata thawabu.

**9:30 Macho yao yakafunguka. Naye Yesu akawaagiza kwa nguvu, akisema, Angalieni hata mtu mmoja asijue**.

Angalia Math.8:4 kwa ajili ya sababu pengine zilifanya asielezwe mtu.

**9:31 Lakini wakatoka, wakaeneza habari zake katika nchi ile yote**.

Hawafanyi makosa kwa kupuuza yale waliyoonywa na Yesu, bali wamefurahi mno na kuwa na shauku hawawezi kulinyamazia hilo. Hivyo ndivyo tulivyo katika imani yetu ya Ukristo. Ni vigumu kunyamaza kuhusu Bwana wetu.

**9:32 Hata hao walipokuwa wakitoka, tazama, walimletea mtu bubu mwenye pepo**.

Huu ni muujiza wa tano na wa mwisho katika sehemu hii. Katika sura 9, miujiza yote mitano imetegemea imani; ama imani ya mtu mwenyewe, au imani ya familia, au imani ya marafiki.

1. Imani ya marafiki wa mwenye kupooza.
2. Imani ya jumbe wa sinagogi.
3. Imani ya mwanamke mwenye kutokwa na damu.
4. Imani ya vipofu wawili.
5. Imani ya watu walioleta bubu kwake.

Katika matukio hayo yote imani *imetenda kazi*.

**9:33 Na pepo alipotolewa, yule bubu alinena, makutano wakastaajabu, wakasema, Haijaonekana hivi katika Israeli wakati wo wote**.

Watu walishuhudia miujiza hii ya ajabu na isiyopingika. Hawakuweza kulinganisha mahali popote. Katika Math.7:22 wengine wanatenda miujiza lakini si kama ya Yesu. Makutano si wajinga ambao wanaweza kuchukuliwa ovyo ovyo. Wamestaajabia kwa sababu wameona mambo hayo halisi yakitukia. Kuamini kwamba haya ni kawaida ni kuwafanya watu hawa kuwa wapumbavu. Watu wa tabia ya asili watadai kwamba Yesu anawaonyesha viini-macho tu. Makutano na Mathayo walishuhudia haya yote.

Mafarisayo walirudia tena kutia shaka kwao:

**9:34 Lakini Mafarisayo wakasema, Kwa nguvu za mkuu wa pepo atoa pepo**.

Lazima wawe na la kusema. Wanaamini kwamba kuna nguvu zivunjazo nguvu za asili imetendeka, lakini hawataki kumtukuza Mungu. Hivyo basi hawana njia nyingine tena. Jambo hili ni kumkufuru Roho Mtakatifu kufutana na jinsi Yesu alivyosema katika Math.12:31,32.

**9:35 Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina**.

Sura 9 inajumuisha aina zote za magonjwa na udhaifu. Yesu anaweza kuyaganga yote. Yesu anafundisha, na anaitumia miujiza kama msingi kwa kuwafundishia.

**9:36 Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji**

**Aliwahurumia** ni tabia (Isa.53) ambayo itadhihirika kwa Masihi. Katika Math.14:14 "Yesu akatoka...akawahurumia..." Hakika tumeona tayari katika Math.9:14 kwamba Mungu anataka rehema. Tutaliona hili tena tunapopitia kitabu kizima cha Mathayo.

**9:37 Ndipo alipowaambia wanafunzi wake, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache.**
**9:38 Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake**.

Kuna watu wengi wanaomwendea Yesu, siyo tu wanaoteseka kwa sababu ya magonjwa ya mwilini, bali pia mst.36 anasema, "walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji." Neno katika Kiyunani ni "taabika" na "teseka." Inawezekana toka kwa wawili wote, viongozi wa Kiyahudi na kwa Warumi. Watu hawana utawala na usimamizi mzuri, wamekata tamaa. Moyo wa Yesu unawahurumia. Anatumia njia hii kuwafundisha wanafunzi

wake:

**Mavuno ni mengi**. Kuna kazi nyingi ya kufanya na msaada ni finyu wa kusaidia.

Basi mwombeni Bwana. Wafanya kazi wengi wanahitajika - mambo ya kuomba kwayo!

## SURA YA KUMI

Katika Yoh.4, baada ya manamke Msamaria kwenda kuwaelea jamii yake, wanafunzi wake wanarejea na Yesu anasema katika mst.35, "...Inueni macho yenu...mashamba...kuwa yamekweisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno." Katika kuwahurumia makutano waliomwendea, anasema, "Angalieni kazi yote ile inayotakiwa kufanywa. Mwombeni Bwana atume wafanya kazi, lakini mimi nina kazi ya kufanya kwa ajili YENU sasa." Itakuwa kinyume na mpango wa Mungu kwetu sisi kumwomba Bwana atume watenda kazi, na sisi wenyewe hatuendi kufanya kazi. Ombeeni, naam, lakini pia toka kafanye kazi!

**10:1 Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoke, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina**.

Amri = - walipewa mitume juu ya roho wachafu...sawa na neno katika 9:35. Imejulikana kama "agizo maalum" lililokinyume na "agizo kuu" katika sura 28.

**10:2 Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya; Wa kwanza Simoni aliyeiitwa Petro, na Andrea nduguye; Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye;**
**10:3 Filipo, na Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru; Yakobo wa Alfayo; na Thadayo;**
**10:4 Simoni Mkananayo, na Yuda Iskariote, naye ndiye mwenye kumsaliti**.

Walikuwa wakijifunza orodha ya mitume, na kwa nini jina la Petro linaorodheshwa kwanza. Tunaposhindwa kuelewa kwa nini, tunatambua kwamba Petro, Yakobo, na Yohana ni moja mitume waliopendwa na Yesu.

**10:5 Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie.**

Sababu inapatikana mstari unaofuata.

**10:6 Afadhari shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli**.

Yesu alitambua kwamba injili ingehubiriwa kwa Mataifa muda si mrefu. Anawaeleza katika Matendo 1:8 jinsi ya kuenea kwa injili. Siyo kwamba Yesu hawajali watu wa Mataifa, anawajali, bali wakati utafika kwa ajili yao. Ni mpango wa Mungu kwamba Wayahudi wahubiriwe injili kwanza - Rum.1:16 "kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia." Kwa wakati huo, Wayahudi wapo mahali ambapo wanapaswa kutoa wakfu muda wao. Kipindi cha utumishi wa Yesu, ujumbe unatakiwa kuwawendea watu wa Mungu kwanza.

**10:7 Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, ufalme wa mbinguni umekaribia**.

Ufalme umekaribia. Uko jirani. Yesu anawataka wahubiri ujumbe ambao hata Yohana alihubiri (Math.3:2) ambao yeye mwenyewe aliuhubiri (Math.4:17). Kile Yohana alichoweza kufanya ni kuwatayarisha watu, Mungu anapenda kuwapatia watu wake mwenyewe fursa ya kwanza kusikia injili, kisha Mataifa watausikia. Paulo anafafanua katika Warumi kwamba mafundisho walikuwa

kwanza kwa Wayahudi, lakini kwa sababu ya kukataa kwao, wangekatiliwa mbali na kupewa Mataifa - Rum.9.

**10:8 Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo, mmepata bure, toeni bure.**

Anataja moja moja kazi aina nne. Wameshuhudia uponyaji wake, na wanatambua kwamba inawezekana. Yesu amewahakikishia kwamba miujiza inawezekana, na itatendeka!

Mmepata bure, toeni bure. Hawakufanya lolote kupata karama zake hizo, hivyo basi wanatakiwa wasitake faida kwa wengine vile vile. Msizuie kwa mtu awaye yeyote. Tayari Mathayo amebainisha ukweli wa kwamba Yesu aliweza kumponya kila mtu, watu wote. Wanafunzi wake ni sharti wafanye vile vile,

**10:9 Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipani mwenu**;

Kutengeneza pesa kutokana na kuponya kwao, ingelikuwa nafasi ya pekee kwa wanafunzi. Iwapo walikuwa tayari na fedha zingine, hakuna tatizo na hizo. Kusudi kubwa hapa ni kwamba wasiende nyumbani kuhakikisha wanachukua "fedha za safari." Watu watakaowasaidia watawapatia mahitaji yao yote.

**10:10 Wala mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala fimbo; maana mtenda kazi anastahili posho lake.**

Wale waowahubiria watawasaidia, basi kunatakiwa kuwe na kizuizi cha kufuata cha vitu vya kuchukua toka kwa wale walioponywa. Mfanyakazi anapaswa kuchukua vitu vyepesi safarini, na kuwezesha watu wengine kuwasaidia wakiwa "kazini."

1 Kor.9:14 - Paulo anasema mtenda kazi anastahili kusaidiwa.
1 Tim.5:18 - "Usimfunge kinywa ngo'mbe apurapo nafaka..." na mtenda kazi anastahili ujira wake . Gal.6:6 - "...amshirikishe...katika mema yote."

Ni miongoni mwa mipango ya Mungu kwamba watenda kazi wasaidiwe kwa kuihubiri injili. Kuna watu ambao watapinga kusaidia na wala hawataunga mkono kazi. Yesu anawazatiti jinsi watavyopingwa.

**10:11 Na mji wo wote au kijiji cho chote mtakachoingia, tafuteni ni nani humo aliye mtu mwaminifu; mkae kwake hata mtakapotoka**.

Hatuelezwi sisi anaposema kuwa **kustahili**, bali awali utumishi wa Yesu yalikuwepo mawazo ya nani anastahili na nani hastahili, kwa maana ya watu wenye kufungua mioyo yao mikunjufu wakikabiliana na mioyo midanganyifu ya Mafarisayo. Ni jambo jema kuuliza watu wa kiroho wanapokaa na kuishi nao mjini unakokwenda. Katika vijiji vidogo mitume wangetambua walio wa kiroho kwa kuwapokea.

**10:12 Nanyi mkiingia katika nyumba isalimuni.**
**10:13 Na nyumba ile ikistahili, amani yenu na ifikilie; la, kwamba haistahili, amani yenu na iwarudie ninyi**.

Ilikuwa desturi za Wayahudi kutakia heri nyumba waliyoingia humo. Wangesimama sehemu ya kizingiti na kusema baraka. Yesu anafundisha somo la kiroho. Mitume walifundishwa kuwaonyesha wenyeji wao heshima na uungwana. Walikuwa wawafundishe na kuzishiriki

baraka za Bwana za injili. Iwapo familia ilipenda kupokea neno, walipokea baraka zitokanazo na neno. La sivyo, baraka mitume walizotoa kwa familia zingekuwa juu yao wenyewe.

**10:14 Na mtu asipowakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule, kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu**.

Pengine sehemu ya pili ya fungu hii inatusaidia sisi kuelewa "kustahili." Ikiwa wanashindwa kuwakaribisha au kuwasikilizeni.

**Mtokapo...kung'uteni miguu yenu** = ishara ya kukataliwa; "Sina shughuli nawe, nawe huna shughuli nami." Paulo alifanya hivyo katika Matendo 13:51.

**10:15 Amini, nawaambia, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma na Gomora kustahili adhabu ya siku ya hukumu, kuliko mji ule**.

Watu wa mji, kundi zima likipinga ukweli, hilo jambo ndilo liletalo hasira ya Mungu juu ya yao. Kwa mfano, Sodoma na Gomora isingeadhibiwa iwapo wangekuwepo angalau wenye haki 10 miongoni mwao. Kwa kuwa hawakupatikana, miji iliangamizwa. Hivyo anawataka mitume watambue kuwa walikuwa mawakili wa Mungu, wanahubiri ujumbe wa Mungu, na ikiwa watapinga ndipo watu itawapa hasira ya Mungu.

**Itakuwa rahisi nchi...kuliko mji ule** (Math.11:21ff). Iwapo miujiza aliyofanya Yesu Korazini, Bethsaida, na Kapernaum ingefanywa katika Sodama na Gomora, watu wa Sodoma na Gomora wangetubu. Watu wengi walishuhudia miujiza aliyotenda Yesu hawakutubu, hivyo basi hukumu yao ni kubwa. Hili linaunga mkono fundisho la viwango vya adhabu Jehanamu.

**10:16 Angalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua**.

Mitume wametajwa kama kondoo - mwororo na mpole, wakati mbwa mwitu wanawakilisha ulimwengu - bila suluhu na katili.

**Busara** = hekima, makini, hasa katika kuzuia hatari.

**Wapole** = pasipo kuleta shari, safi, bila kuchokoza katika kila hali.

Jitengeni na ubaya (1 Thes.5:22) bali fanyeni yale mliyotumwa kufanya (Math.10:1).

**10:17 Jihadharini na wanadamu; kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga**;

Jihadharini na wanadamu. Mistari hii inawezekana iliwashangaza. Wakwenda katika mji, na kuponya wagonjwa na wenye ukoma, wakifikiria wangekaribishwa na kupendwa. Badala yake kuteswa na kupigwa - hata katika masinagogi!

**10:18 Nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme, kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa**.

Maneno haya ni kweli, "kuonywa mapema kunafanya uchukue tahadhaeri mapema." Wametambua hili kuwa lingetokea na isingeliwashangaza. Maadui zao wangeliwapeleka mbele ya wakuu na wafalme kwa lengo la kuadhibiwa kifo.

**10:19 Lakini hapo watakapowapeleka, msifikiri-fikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema**.

Aliwaahidi uweza wa kimiujiza ambao ungewawezesha kusema kilichotakiwa kusemwa kwa saa ile ile ilipohitajika. Ahadi hii inawafariji na kuondoa hofu kwa siku zijazo.

**10:20 Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu**.

Walikuwa vyombo vya Mungu. Alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyesema ndani yao. Tunapata hapa fafanuzi nzuri ya jinsi uvuvio ulifanya kazi. Mitume na manabii waliposema, yalikuwa ni maneno ya Mungu halisi yaliyotoka kinywani mwao (1Thes.2:13; 1 Kor.14:37; 2 Pet.1:20,21).

**10:21 Na ndugu atamsaliti nduguye ili auawe, na baba atamsaliti mwana, na wana watawainukia wazazi wao, na kuwafisha**.

Yesu ataliongelea hili kwa mapana zaidi katika mst.34. Lakini anawaandaa kujua jinsi mateso yatakavyokuwa makali yanayokuja; makali kiwango cha hata baina ya familia zitafarakana mmoja na mwingine, hata hatua ya kuuana! Tofauti za kidini zitafikia kiasi cha mtu kutaka mwingine auwawe na kutolewa kwa ajili ya kusudi hilo. Katika matukio fulani litafanikiwa.

**Na kuwafisha**. Katika Kiyunani bora ingetafsiwa na “ili wapate kuuwawa.”

**10:22 Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atayeokoka**.

Kwa kawaida watu watakaowapenda wanafunzi, marafiki, na kuwasaidia wataweguka na kuwa kinyume, sababu pekee...kwa sababu ya Yesu. Hapa kuna ufunguo:

**Lakini mwenye kuvumilia...ataokoka**. Mtu ni lazima awe na tabia ya “kudumu humo,” ya “kujilinda hata mwisho.” Hakuna thawabu kwake anayevumilia kwa kitambo tu, na kisha huacha. Angalia Math.24:9-13; Ufu.2:10; 2 Tim.4:7.

**10:23 Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu**.

Mitume walikuwa wasiyapoteze maisha yao. Walikuwa wayalinde kwa njia bora - kwenda mahali ambapo wangefanya kazi nzuri zaidi.

**Hamtamaliza...hata ajapo Mwana wa Adamu**. Hili ni fungu lingine gumu, lina fafanuzi aina tatu.

1. Maangamizi ya Yerusalem (Math.2429-31).
2. Mwana akija kutawala kama Mfalme katika siku ya Pentekoste.
3. Hukumu ya mwisho.

Yesu, Mwana wa Adamu, akija katika utukufu wa Baba yake (16:27). Hapa yametumika katika mazingira ya hukumu ya siku ya mwisho.

Katika Math.24:28-30 kuja kwa Mwana wa Adamu kunarejea kuangamia kwa Yerusalem. “Hamtamaliza miji ya Israeli...” Kuna muda maalum. Hivyo inawezekana kuja kutawala katika uongozi wake au kuanguka kwa Yerusalem. Kila maelezo mojawapo yanakubaliana yakilenga hayo.

**10:24 Mwanafunzi hampiti mwalimu wake, wala mtumwa hampiti bwana wake**.

Alivyotendewa mwalimu, mwanafunzi au mtumwa hatakiwi kudhani kwamba angetendewa vyema kuliko. Kama wanafunzi wa Yesu Kristo hatupaswi kutarajia au kudhania tunastahili kutendewa mema kuliko Yesu alivyotendwa. Tunapoteseka kukataliwa na kudharauliwa kutokaka na kuwa waaminifu, tunapaswa kufurahia kufanyiwa kama alivyotendwa - Yoh.15:20,21.

**10:25 Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba Belzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake**?

Iwapo walitendewa kama Mwalimu wao, wanaweza kutarajia kutendwa kama hivyo.

Beelzebuli = "Beelzebub" = "Mfalme wa inzi." Ikiwa kiongozi wa nyumba amenenwa hivi, wengine wote katika familia watatendwa vivyo hivyo (9:34).

**10:26 Basi, msiogope, kwa kuwa hakuna neno lililositirika, ambalo halitafunuliwa; wala lililofichwa, ambalo halitajulikana**.

**Basi** = kwa sababu ya yale yaliyoonywa katika msitari uliotangulia, **msiowaogope**. Hivi ndivyo mambo yangetukia, lakini msiogope. Neno "hofu" limetumika mara nne katika mistari inayofuata mitano.

Kila kitu kitatukia lakini ukweli ni lazima ukweli ujulikane. Mungu anaona hayo yote yakitendeka, na watenda maovu watawajibika kutokana na wanayotenda na kusema.

**10:27 Niwambialo ninyi katika giza, lisemeni katika nuru; na msikialo kwa siri, lihubirini juu ya nyumba**.

Waliyoambiwa sirini yalikuwa yahubiriwe hadharani.

**10:28 Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuua na roho; afadahli mwogopeni yeye awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu**.

Wanadamu wana uwezo, lakini ina mipaka yake. Katika jamii yetu kitu kibaya mtu yeyote anaweza kukifanya ni kutuua sisi. Yesu anasema hilo siyo ndilo jambo baya zaidi. Anatambua kwamba miili yetu haina lolote zaidi ya kuwa makazi ya kitambo tu.

**Afadhali mwogopeni...katika jehanamu**. Hapa ni "Gehenna" - adhabu ya milele. Mungu ana uweza ambao hakuna mtu anao - basi, tunapaswa kumwogopa yeye. "Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa" - (Mith.1:7).

Wengine hushindwa kuelewa maonyo haya ya kumcha Bwana kwa sababu ya 1Yoh.4:18 - "Katika pendo hamna hofu." Watu wengi huamini kwamba hatutakiwi kuwa na hofu ya aina yeyote ile. Lakini Biblia inatufundisha kwamba hofu hutuelekeza hata kufikia ukamilifu. Yohana anazungumzia pendo kamili ambalo linafukuzia mbali hofu katika hukumu. Mungu ndiye tunayepaswa kumcha! Ebr.12:29 "Maana Mungu wetu ni moto ulao." Katika Ebr.10:31 "Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai."

Alikuwa Mungu, katika Mlima Sinai, aliyewatetemesha Israeli. Soma Kut.20:18, 19. Katika mstari wa 20 Musa anasema, "Msiogope, maana Mungu amekuja ili awajaribu, na utiisho wake

uwe mbele yenu, ili kwamba msifanye dhambi." Watu wanapohofu ghadhabu ya Mungu husahihisha tabia zao. Kama wazazi tunaliona hili katika watoto wetu. Wanatii kwa sababu wanahofu adhabu ikiwa hawawajibiki. Lakini wakisha kuwa watu wazima wanatii kwa upendo na wala si kwa hofu. Hiyo ndiyo Mungu anayoitumia kutushughulikia. Tunakua na kuwa wazima hata kiwango cha kumtii. Uhusiano wetu na Mungu unatakiwa ukue ili kwamba tuweze kukua na kuwa wazima kufikia kiwango cha upendo ambao Wakristo wanapaswa wawe nao.
Neno kuangamiza halina maana maangamizi ya kutoweka kabisa. Kuna mafungu mengi yanayoonyesha adhabu itakuwa ya milele. Math.3:12 panazungumzia kuhusu moto wa milele ambao hauwezi kuzimika. Yesu anasema funza hawafi humo - Mk.9:44. Angalia pia Math.13:42; 25:41; Mk.9:48. Shetani hawezi kuangamiza nafsi; hana uwezo huo.

**10:29 Je! Mashomoro wawili hawauzwi kwa senti moja? Wala hata mmoja haanguki chini asipojua Baba yenu**;

**Shomoro** haina thamani kubwa, lakini Mungu anawajua na kuwapenda sana. Mmoja akianguka chini, anajua. Basi, anajali kiasi gani, na kuwajua, watoto wake?

**10:30 Lakini ninyi, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote**.

Hili ni fafanuzi bora kwamba Mungu anajali hata dakika dakika yenyewe moja ya kuwepo kwetu. Hivyo ndivyo anavyotujali na kutupenda.

**10:31 Msiogope basi; bora ninyi kuliko mashomoro wengi**.

**Msiogope basi**. Msiogope watu kwa sababu upendo mkubwa wa Baba mwenye uweza wote. Hili linahatimisha sehemu hii.

**10:32 Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni**.

Yesu alikuwa akizungumzia hofu juu ya wanadamu. Hofu huwafanya watu wafanye mambo ambayo hawawezi kufanya kwa kawaida. Mungu pekee ndiye anajua idadi ya watu wote, wa kike na kiume, wadogo kwa wakubwa, ambao wamerudi nyuma kwa sababu ya hofu. Yesu anasema kwamba bila kujali watu watavyokutenda, kama tunpenda kumkiri yeye mbelel za watu, tunaweza kuhakiki kwamba naye atatukiri mbele za Baba . Anatoa uhakika mkubwa kwamba iwapo tunamkiri yeye kuwa ni Bwana katika kila hali ya maisha, na kutegemea wokovu wake, ndipo atatupigania - Rum.10:9,10. Yesu, katika Mathayo, anazungumzia kujitoa maisha yote, mtu kumkiri daima kwa maisha na kwa maneno yake.

**10:33 Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni**

Kinyume cha hivyo ni kweli. "Kumkana" ni kinyume cha "kimkiri." Tunaweza kumkana Yesu katika njia mbili:

1. Kwa maneno kutamka hatutaki kumfuata yeye.
2. Kwa kukaa kimya. Mtu ambaye haonyeshi bayana utiifu kwa Yesu, na badala yake hasemi chochote, huyo hakika anamkana.

Atakayemwakilisha Yesu ni yule ambaye anamkiri yeye. Yeye aliyekazini, ni yeye anayekiri kwa kinywa chake mbele za watu na kwa maisha yake. Kumbuka katika Hotuba ya Mlimani, kwao wanaoasi sheria Yesu atawaambia, "Sikuwajua ninyi kamwe." Hatasema kwamba

anawajua (2Tim.2:12b). 1 Pet.3:15 tunaamuriwa kuwa tayari kutoa majibu juu ya tumaini lililo ndani yake. Watu wanataka kuona tunakiri kwa nini tunayotenda hivyo. 1 Pet.2:12 - tabia zetu zinakuwa sahihi mbele za Mungu. Math.5:16 - angalia matendo yetu mema.

**10:34 Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga**.

Watu walitarajia Masihi mwenye jeshi kubwa kuja na kuanzisha ufalme wa Daudi. Yesu anawaambia wasifikiri hivyo. "La! Sijaja kuleta amani, bali upanga." Yesu anataja tena gharama za kumfuata yeye.

**10:35 Kwa maana nilikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu;**
**10:36 Na adui wa mtu ni wale wa nyumbani mwake.**

Haya yanatoka Mik.7:6. Yesu anaelezea kuwa atakachofanya ni kikubwa kitaigawa familia katikati kwa sababu wana familia hawatakubalina na Mtu huyu analivyo. Yesu alikuja, kujua hivyo kungekuwa ndiyo kisa, na iwe hivyo hivyo! Watu watakiwa kufanya maamuzi, na moja ya maamuzi hayo ni magumu. Hatupendi watu wa nyumbani mwetu kuwa maadui zetu, lakini hivyo ndivyo inavyotukia tukitii injili. Hatuwezi kuruhusu uadilifu kwa familia zetu utugharimu sisi kukosa uzima wa milele mbinguni. Mungu ndiye pekee anayejua watu walimwacha kwa ajili ya familia zao.

**10:37 Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili**.

Hii ni mara ya kwanza kati ya tatu anazotumia neno **stahili**. Mtu anakuwa anastahili kwa Yesu? Ikiwa anachukua msimamo wa "imani pekee," hakuna jinsi. Walakini Yesu anasema kinyume na hivyo. "Ampendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili." Hivyo utiifu kwake lazima uzidi ule wa ndugu zetu duniani. Upendo mtu alionao kwa mwanawe au bintiye ni mzito na mkubwa kwamba hata hauelezeki kwa maneno, lakini hatakiwi awapende zaidi ya kumpenda Yesu au hatamstahili. Mtu anaweza kudai, "Hatutajadili kuhusu Yesu katika nyumba hii! Endapo unajisikia kufanya hivyo, sitamfuata." Na kama hivyo ndivyo, Yesu anasema mtu huyo anaipenda familia yake zaidi kuliko yeye, basi hamstahili. Ni jinsi gani mwanafunzi wa kweli wa nyumbani ashindwe kuzungumzia kuhusu yeye kwa wale wasiomfuata; na anapenda wapendwa wake waokolewe? Ni nafasi ya pekee kuishi katika familia ambayo kila mwana familia ni Mkristo!

**Anastahili**. Ni nani tunayempenda zaidi? Yesu au famila? Ni kweli kwamba upendo kwa Yesu unapaswa uzidi ule uhusiano tulionao duniani. Hasemi kwamba upendo wetu kwake uondoe upendo kwa wengine. Yesu alikuwa Mfalme wa Amani (Isa.9:6; yoh.14:27), lakini hazungumzii amani baina ya watu; anazungumzia juu ya amani ya ndani Wakristo walionao mioyoni mwao kwa sababu wanatambua kwamba wana mahusiano mema na Mungu. Tunaweza kuhitalifiana kwa nje, lakini wakati huo huo tukajisikia amani ya Mungu ndani; amani iliyowawezesha mtu kama Justin Martyr na wengine kuteswa hata kupata adhabu kali na kisha kifo.

**Upanga** = alama ya magomvi na wala si upanga halisi. Upanga huu ni neno lake, tunalokwenda kulitumia iwapo tutakuwa wanafunzi wake.

**10:38 Wala mtu asiyeuchukua msalaba wake akanifuata, hanistahili**.

Hii ni mara ya tatu anatumia neno **stahili**. Anazungumzia kila mmoja kuchukua msalaba wake.

Hii ni mara ya kwanza neno "msalaba" kutokea katika kitabu cha Mathayo. Mtu anaweza asiwe na magomvi na familia yake, hata hivyo anayo sadaka ya kuitoa. Yesu anatumia mfano ambao wangekuwa na uzoefu nao ambao mara nyingi walishuhudia kusulibiwa; mwenye kusulubiwa alikuwa aubebe msalaba wake mwenyewe. Kwa nini walitakiwa kubeba misalaba yao wenyewe? Walishurutishwa kufanya hivyo kama sehemu ya hukumu yao, kama vile Yesu alivyo shurutishwa kufanya. Wakristo kwa hiari lazima wachukue "misalaba" yao - chochote kinachoonekana kuwa fedheha, majaribu au kulemewa tunapomfuata Kristo.

Akanifuata. Hatuwezi kumfuta Yesu pasipo kuchukua msalaba migogoni mwetu. Kuna watu wengi wanajaribu kumfuta pasipo msalaba, na hawawezi kufanya hivyo. Lazima tuhesabu gharama, na gharama hiyo inaweza kuwa ni kupoteza maisha yetu wenyewe. Lk. 9:23 anaoongeza neno "kila siku." Hili ni jambo la daima. Yesu hamaanishi kwamba litakuwa jambo la muda kitambo tu. Mifano mingine ni: Rum.12:1 tunapaswa kuwa dhabihu zilizo hai, dhabihu na siyo vinginevyo. Gal.2:20 namna tunavyopaswa kuuona Ukristo wetu.

**10:39 Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza; naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona**.

Kama tunatilia manani katika vitu vyetu tunapoteza. Tunapofanya tu kile tunachotaka kufanya, ndipo tunapoteza uzima wa mbinguni. Lakini ikiwa hatuzingatii vilivyo vya kitambo na kupata vya kiroho, mbinguni kutakuwa kwetu. Ikiw atunatilia manani ufalme, tutafanikiwa. Maana yake ni kuweka kipaumbele. Ni kitu gani kilicho muhimu zaidi: mimi na ninachotaka kufanya; au Yesu na anachonitaka mimi nifanye? Shetani anataka sisi tusiushinde ubinafsi, mawazo ya kujiona wenyewe, lakini thawabu kubwa ni kumfuata Yesu.

**10:40 Awapokeaye ninyi, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi, ampokea aliyenituma**.

Hili linamhusu Baba. Kama mtu anataka uhusiano na Mungu, lazima amkubali Mwana wa Mungu. Hawezi kufanya hivi isipokuwa anakuwakubali waliotumwa na Mwana. Yesu anawaambia hawatapata anachokwenda kutoa Mungu isipokuwa kwanza wanawakubali wanafunzi. Ni jambo muhimu sana tunapojifunza, na kujaribu kuwafundisha watu wengine, ili tutambue mamlaka ya mitume. Tunatakiwa kupokea mafundisho ya mitume na Yesu ili tupate baraka za Mungu. Sababu ni hii, kuna watu wengine wanaosema leo kwamba tunatakiwa kuzingatia ya Yesu tu na wala si mitume. Hatuwezi kuzingatia ya Yesu na kuyadharau ya aliowatuma. Kama hatuyapokei mafundisho ya Petro na Paulo, ndipo tutakuwa hatujampokea Yesu.

Efe.2:20 "...mmejengwa juu ya msingi wa mitume...Kristo Yesu ni jiwe kuu la pembeni..." Kila kitu Mungu alichojenga juu ni katika msingi ambao mitume waliweka. (Hii ni pamoja na mtu kama Luka, Marko, Yakobo, na Yuda; wasio miongoni mwa mitume kumi na wawili, lakini walileta neno la Mungu kwa wanadamu). Kama upo mimbarini, na unahubiri Biblia, na watu hawapendezwi nawe, wangali wana wajibu wa kusikiliza ujumbe. Ikiwa hawataki ujumbe kwa sababu ya mjumbe, wanashindwa kumpata Yesu na Baba.

**10:41 Ampokeaye nabii kwa kuwa ni nabii, atapata thawabu ya nabii; naye ampokeaye mwenye haki kwa kuwa ni mwenye haki, atapata thawabu ya mwenye haki**

Mtu akimpokea nabii kama mnenaji wa Mungu, anamkaribisha yeye aliyemtuma - Mungu mwenyewe. Tena, atapata thawabu sawasawa na nabii. Kwa hiyo siyo sisi peke yetu tunaofanya kazi huko tutapata thawabu, bali pia watakaowapokea watapata thawabu. Kupokewa kuna mambo mawili:

1. Kuonyesha ukarimu, kutiwa moyo na, pengine, msaada wa kiroho (mst.12-14), kujumuisha ukarimu majumbani.
2. Kupokea ujumbe uliofundishwa.

**10:42 Na mtu awaye yote atakayemnywesha mmojawapo wa wadogo hawa ngaa kikombe cha maji ya baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amini, nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake**.

Wadogo hawa = "wanyenyekevu" (maelezo chini ya ukurasa 'footnotes' katika 'American Standard') mtu mwenye daraja la chini ya wengine; watumishi wake wanamtegemea, na kumtumaini yeye. Zawadi yenyewe siyo ndio muhimu. Ni nia ya kutoa. Ebr.6:10 "Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlililidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewhudumia watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia." Hili linatuonyesha mtu anaweza asiwe na vitu vingi vya kutoa, lakini karibu kila mtu anaweza kutoa kikombe cha maji kwa ajili ya mwingine. Anachukua angalau kitu chenye thamani ndogo anachoweza mtu kutoa na kusema kwamba kimetolewa katika upendo wa Ukristo, Mungu anaona na atampa thawabu mtu huyo.

## SURA YA KUMI NA MOJA

**11:1 Ikawa Yesu alipokuwa amewaagiza wanafunzi wake kumi na wawili, alitoka huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao**.

Yesu alikwisha waaeleza tayari kuomba wapate watenda kazi (9:38), sasa anatuma nje kufanya kazi! Wahubiri wanaosisitiza watu wengine wafanye kazi na kuhubiri, je wao wanafanya vivyo hivyo? Ni jambo la maana kuwaleza wengine na kisha kwenda kufanya kazi sisi wenyewe.

**11:2 Naye Yohana aliposikia huko gerezani matendo yake Kristo, alituma wanafunzi wake, kumwuliza**,

Mathayo anataja kufungwa kwake Yohana mara tatu; 4:12; hapa, na tena 14:1ff. Yohana alisikia kazi ya Kristo, sifa zake zimeenea hadi kwa wafungwa waliofungwa gerezani. Anatuma ujumbe wanafunzi wakaumwulize Yesu.

**11:3 Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine**?

Mara nyingine tena jinsi swali lilivyoulizwa (ikiwa njia ya kufundisha) katika Mathayo, moja ya swali muhimu sana.

**Wewe ndiye yule ajaye** = Masihi. "Au tumtazamie mwingine?" Kuna maelezo aina nne kutokana na uwezekano wa Yohana kuuliza hivi.

1. Alikuwa akitaka Yesu atangaze kuwa yeye ndiye Masihi kwa wazi zaidi.
2. Alikuwa na mashaka akilini mwake mwenyewe kuwa Yesu alikuwa Masihi, pengine kwa kuwa alikuwa gerezani, na mateso yaliyompata.
3. Alitaka wanafunzi wake sasa wamfuate Yesu.
4. Pengine alikuwa akihofia ikiwa kazi yake ya "kutayarisha" ilikwisha. Na ikiwa ilikwisha, angelipata madhara kutokana na uamuzi wa papara wa kiapo cha Herode (sura 14) kwa amani.

**11:4 Yesu akajibu akamwambia, Nendeni mkamweleze Yohana kile mnayoyasikia na kuyaona**;

Wanafunzi wa Yohana wamekabiliwa. Yesu anaainisha watakayoshuhudia:

1. Vipofu wanapata kuona,
2. Viwete wanakwenda,
3. Wenye ukoma wanatakaswa,
4. Viziwi wanapata kusikia tena,
5. Wafu wanafufuliwa, na
6. Maskini wanahubiriwa injili.

**11:5 Vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema**.

"Sehemu ya miujiza" inajumuisha aina hii ya miujiza. Mathayo anaandika habari zenyewe ya haya yote yakitukia. Kutoka namba moja hadi sita inahusisha unabii wa Kimasihi. Angalia Isa.35:5ff; 61:1ff.

Yamekuwaje haya kuwa majibu ya swali la Yohana? Yesu anatimiza maandiko ya Agano la Kale! Anatenda mambo yanayodhihirisha ukweli wa yeye kuwa Masihi. Ni jambo la kuvutia kuona hasemi, "Rudini na mkamwambie, 'Yesu amesema kuwa yeye ndiye Masihi!'" Yesu anataka watu wafikiri. Je yeye ndiye anayekuja? Nendeeni mkamweleze mnayoona na kusikia na amuaeni ninyi wenyewe, kama sisi sote tunavyopaswa kufanya.

**11:6 Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami**.

Hili linaweza kusomeka hivi, "Heri kwake ambaye sitabainisha kuwa ni kikwazo." Walio "heri" ni wale walielewa kazi ile Yesu aliyokuwa akiifanya na hawakuwa na sababu ya kutokufanya jinsi alivyofanya. Wayahudi, waandisho, na Mafarisayo hawakupenda jinsi Yesu alivyofanya mambo. Walitaka ajitangaze kuwa yeye ni nani. Hawakufurahia kujihusisha kwake na wenye dhambi, au jinsi alivyovuruga mapokeo ya Wayahudi. Kwao hao alikuwa kikwazo, basi hawakubarikiwa.

**11:7 Na hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, Mlitoka nyikani kwena kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo**?

Anazungumzia kuhusu mahubiri ya Yohana katika 3:1 na watu waliomwendea kumsikiliza. Huu unyasi unasimamia nini? Mtu aliyerahisi kushawishika au asiye madhubuti; asiye kaidi, kigeugeu.

**11:8 Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mwororo? Tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme**.

Pengine walitangulia kufahamu kuhusu Yohana angetoka ukoo wa kifalme, akivalia nguo ambazo jamii ya kifalme ilivaa. Yohana alikuwa mtu wa jangwani - sehemu kame; akivalia mavazi ya ngozi na manyoya ya ngamia (3:4).

**11:9 Lakini kwa nini mlitoka? Ni kuona nabii? Naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii**.

Pengine wengine walimtarajia mtu tofauti, na wakamkataa Yohana kwa sababu hakulingana na matarajio yao. Lakini wale wote waliokwenda kumwona nabii, walitambua zaidi kuwa nabii. Mstari wa 10 unaeleza kwa nini alikuwa zaidi ya nabii tu.

**11:10 Huyo ndiye aliyeandikiwa haya, tazama, mimi namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako mbele yako**.

Kulikuwa na unabii uliotabiriwa kuhusu Yohana katika Mal.3:1 tunapata wapi kutokana na unabii huu nabii mwingine hapa? Hakuna. Yeye ndiye alikuwa kusudi la unabii, na kwa hiyo kuwa unabii wa maana! Aliitayarisha njia ya Bwana! Ndiyo maana alikuwa mkuu kuliko wengine, akimzidi Isaya, Ezekieli, na hata Musa. Isipokuwa Yesu, alikuwa mkuu kuliko wote.

**11:11 Amin, nawaambieni, hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye**.

Yesu anamtolea sifa Yohana kuliko mtu mwingine yeyote yule. Ingawa hatujabarikiwa kwa kuona alichofanya Yohana, hii ni kuonyesha kwamba aliifanya kazi yake na akaifanya barabara. Ni sifa kubwa Yesu anaelezea kuhusu Yohana! Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko yeye.

Walakini aliye mdogo...ni mkuu kuliko yeye. Angalia mchanganua aina tatu kutokana na hili:

1. Yohana hakuwemo ndani ya ufalme. (Yesu anazungumzia kanisa hapa).

2. Ufalme (kanisa) na kuanzishwa kwake kulikuwa bado hakujatukia. Yohana alihubiri katika Math.3:2 ufalme "umekaribia" au uko jirani. Ulikuwa bado hajaja. Katika Math.16:18 ansema "Nitajenga (wakati ujao) kanisa langu", na katika mst.19 "Nita-(wakati ujao) kupa wewe ufunguo wa ufalme." Kuanzishwa ni wakati ujao. Iwapo ulikuwa tayari umekuwepo kufikia hapa, ndipo Yohana angelikuwemo ndani. (Maelezo: huu ni mfano mzuri kuruhusu mazingira yajitambue iwapo ni kanisa linaloongelewa au utawala wote wa Mungu. Katika mazingira haya unahusu kanisa. Yohana alikuwa ndani ya ufalme wa Mungu lakini si ndani ya kanisa).

3. Wale wote watakaokuwemo ndani ya ufalme (kanisa) watakuwa na nafasi kubwa kuliko ile ya Yohana (watabarikiwa zaidi). Alikufa kabla ya kanisa kuanzisha. Kuna baraka za pekee kwa wale wote waliomo katika kanisa la Kristo! Tumebarikiwa katika njia ile Petro anaelezea 1 Pet.10-12. Mara nyingi sana tunafikiria juu ya zawadi, na siyo baraka. Sisi tuliombele ya msalaba tunabarakiwa zaidi ya wale kabla ya msalaba, kwa kuwa tuna injili! Mitume na manabii walitamani kuuona wakati huu bila mafanikio. Bali sisi tumebarikiwa! Tumebahatika kuona jinsi mpango wa Mungu ulivyofunuliwa tangu mwanza wa uumbaji. Yohana hakubahatika kuona kanisa likienea duniani kote; mambo yote ya kuvutia siku ya Pentekoste. Sisi kama Wakristo tu wakuu kuliko au tumebarikiwa zaidi, kwa sababu tunaona mambo yote ambayo Yohana hakuweza kuyaona. Tunatambua hayo kuwa siyo thawabu, kwa sababu Yesu alisema hakuna aliye mkubwa kuliko Yohana.

**11:12 Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni unapatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka**.

Haya huchanganya wanafunzi wa Biblia kwa namna fulani. Yesu anatupeleka katika wakati maalumu - "kutoka Yohana hadi sasa" (muda huo anapozungumza), ufalme ulikuwa ukiteseka na wenye nguvu wauteka. Kuna uwezekano wa maana mbili wa kinachozungumzwa.

1. Katika NASB maelezo ya chini (foot note. "Huingia kwa nguvu" imetumika badala ya "kwa nguvu hupatikana." Inawezekana inamaanisha kwamba waliyoyapokea mafundisho ya Yohana walitamani kuwemo katika ufalme kwamba wakafanya jitihada kubwa kuingia kama watu wenye hasira wanavyoutwa mji kwa nguvu (Lk.16:16).

2. Inawezekana pia inamaanisha watu wanajaribu kuanzisha na kutengeneza kanisa njia wanayotaka. Yesu anasema sivyo hivyo (Yoh.6:15 walipojaribu kumfanya Yesu kuwa mfalme "kwa nguvu"). Watu hawana uwezo wa kumfanya ufalme kwa njia fulani yao. Kanisa lilikuwa katika hatua za kuanzishwa, na watu wengi walikuwa wanajaribu kuanzisha katika njia zao badala katika ile njia ya Mungu aliyotaka.

Pengine mfano mzuri wa jambo hili unapatikana katika Math.20:20,21 wakati mama yao Yakobo na Yohana alipojaribu kuwaombea madaraka wanawe mmoja kukaa mkono wa kulia na mwingine mkono wa kushoto wa Yesu atakapokuja katika ufalme wake. Ufalme ulikuwa bado haujaanzishwa, lakini ulikua katika hatua za kuanzishwa, kulikuwa na wengine walitaka kuwa na nafasi za vyeo.

**11:13 Kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana**.

Hatuna sababu ya kujua jinsi manabii wote na torati ilivyotabiri. Agano lote la Kale lilitarajia kuanza na yale Yohana alianza. Kulikuwa kuwe na mabadiliko makubwa katika mahubiri ya Yohana, na kuwasili kwake kungelikuwa ndiyo mwanzo wa "siku za mwisho."

**11:14 Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja**.

Fungu hili linarejea Mal.4:5. Wayahudi walitarajia Eliya kuvaa mwili. Ndiyo sababu Yohana anasema katika Yoh.1:25 kwamba yeye siyo Eliya. Bado walichanganyikiwa katika Math.16:13. Wengine walisema kwamba (Yesu) alikuwa Yohana Mbatizaji, Eliya, Yeremia, au mmoja wa manabii. Walikuwa hasa na mawazo ya Eliya kuvaa mwili.

Math.14:2 Herode alisema kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa amefufuka toka kwa wafu. Math.17:9-13 Mitume walimwona Eliya, na Yesu alisema kwamba Eliya alikuwa tayari amekwisha kuja. Walielewa kwamba alimzungumzia Yohana Mbatizaji. Alikuwa ndiye "Eliya yeye ajaye." Kanisa la Ulimwengu wote la Mungu linaamini Garmer Ted Armstrong kuwa ndiye Eliya ajaye. Lakini hivyo si kweli! Yesu anatueleza bayana kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa ndiye Eliya yeye ajaye!

**11:15 Mwenye masikio, na asikie**.

Yesu atarudia haya karibu mara mbili - Math.13:9,49. "Mungu amekuumbia kiungo sikio ambacho kwacho usikie, siyo kusikiliza tu. Pia kuelewa. Je, mmesikia nilichowaeleza kuhusu Yohana? Yeye ndiye Eliya! Kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyo, hivyo basi mimi ni Kristo."

**11:16 Lakini nitakifanisha na nini kizazi hiki? Kimefanana na watoto wanaokaa sokoni, wanaowaita wenzao, wakisema**,

Watoto wengine wanataka kucheza na wengine, lakini wengine hawataki.

**11:17 Tuliwapigia filimbi, wala hamkucheza; tuliomboleza, wala hamkulia**.

Wengine wanashauku la kufanya lolote lile, lakini wapo ambao hawataridhika na lolote lile. Kuna tofauti - wakiona kosa katika kila jambo lilitolewa.

**11:18 Maana Yohana alikuja, hali wala kunywa, wakasema, Yuna pepo**.

Hakuwapendeza watu kwa kuwa "hakushirikiana" nao kijamii.

**11:19 Mwana wa Adamu alikuja, akila na kunywa, wakasema, mlafi huyu, na mlevi, rafiki yao watoza ushuru na wenye dhambi! Na hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi yake**.

Kunywa na kula = akitenda kinyume kabisa na Yohana alivyofanya, Yesu alikataliwa kwa maana ya "kuzidi." Hakuna mtu atayefanya mambo kwa kumpendeza kila mtu.

Na hekima imejulikana kuwa ina haki kwa kazi yake. Hekima iliyokuwemo katika mafundisho ya Yohana na wokovu wa Yesu utakuwa umedhihirika katika maisha ya wote wanaoelewa na kutii. Kila mtu amepewa majukumu pekee ya kufanya, na kila mmoja atayatekeleza hayo!

**11:20 Ndipo alipoanza kuikemea miji ile ambayo ndani yake ilifanyika miujiza yake mingi, kwa sababu haikutubu**.

Watu *wasiotaka* kuamini, hawataamini! Walishuhudia uweza mkubwa ukidhihirika ambao ungeliwafanya watubu. Walakini hawakufanya hivyo. Waliiona miujiza hiyo lakini hawakuamini kwamba ilikuwa ya kweli, ama kutokumwamini yeye aliyeitenda.

**11:21 Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wangalitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu**.

**Ole** = onyo. Angalia kwa makini, uonywe Korezini na Bethsaida! Tiro na Sidoni ni miji ya Fonike: Korazini na Bethsaida ni miji ya Kiyahudi. Kama tunavyojifunza Matendo 21:3 na 27:3, tunajifunza kwamba Tiro na Sidoni ilikuwa tayari imepokea injili. Historia inathibitisha hayo aliyosema Yesu. Walifurahia kupokea injili. Watu wa Korazini na Bethsaida walishuhudia miujiza ya aina hiyo hiyo lakini hawakuwa tayari kutubu. Akaikemea ili itafakari kwa kiina kuhusu wanachofanya na kinachotendeka miongoni mwao.

**11:22 Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi kwa Tiro na Sidoni kustahili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi**.
**11:23 Nawe Kapernaumu, je! Utakuzwa mpaka mbinguni? Utashushwa mpaka kuzimu; kwa kuwa miujiza iliyofanyika kwako ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwako mji huo hata leo**.

Kapernaumu ulikuwa mji uliopendwa kwa sababu ulikuwa makazi yake Yesu (Math.4:13). Lakini hawatainuliwa mbele ya macho ya Mungu. Badala yake watashuka kuzimu. Kuzimu ni maangamizi, ukiwa, mauti. Itakuwa miji iliyokufa. Kwa nini? Kwa kuwa hawaamini na kutubu.

**11:24 Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu yake siku ya hukumu kuliko wewe**.

Linaloongelewa hapa ni **hukumu**. Sodoma iliangamizwa karibu 1900 K.K. (Mwa.18,19). Miji yote ilihukumiwa hapa, Korazini, Bethsaida, na Kapernamu ni miji ambayo iliangamizwa katika miaka 30 iliyofuata, na sasa ni magofu. Vipimo vya adhabu vimeonekana katika mistari hii, k.m. "Itastahimili adhabu...kuliko wewe." Angalia makala ya Cecil May. "Je, Kuna Viwango vya Adhabu na Thawabu?" Lk.12:47,48 anafundisha kuna viwango vya adhabu. 2Pet.2:21 anasema, "Maana ingelikuwa heri kwao kama wasingalifahamu njia ya haki, kuliko kuiacha ile amri takatifu waliyopewa." Bora wasingelijua kuliko kuijua? Bora kumkabili Mungu katika hukumu bila kujua, kwa maana watapokea kiwango cha adhabu kilicho kidogo. 2 Thes.1:6-9 panafundisha kwamba wote wasiomjua Mungu wataadhibiwa.

**11:25 Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nashukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga**.

Watoto = mitume, wanafunzi ambao hawana chuki binafsi. Rahisi kufundishwa. Mungu na ashukuriwe kuona kwamba kuna watu wa jinsi hii.

**Wenye hekima na akili** = welevu ambao kwa sababu ya hekima zao wenyewe, hawawezi kuona na kutambua kwa urahisi yale Yesu anasema. Tayari amesema katika mst. 15 yeye aliye na masikio na asikie, tena atasema pia katika 13:14, 15. Pia ananukuu kutoka Isa.6:9,10 - "Fulizeni kusikia, lakini msifahamu." Mungu ametoa fursa kwa kila mtu kusikia na kuamini, bali hawafanyi hivyo kwa sababu ya hekima zao wenyewe na welevu. Kutokana na msitari huu tunajifunza kwamba sisi pia tunapaswa kuwa wanyenyekevu na waliotayari kufundishwa, kuondoa chuki binafsi bila kuwa na mawazo ya mbele la sivyo sisi nasi hatutasikia na kuelewa...kama vile Mafarisayo.

**11:26 Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyopendeza mbele zako**.

Yesu anaona hekima jinsi Mungu anavyofanya kuwawekea kitu fulani mbele ya walio mfano wa mtoto kwa furaha na kupendezwa na shauku katika kuupokea ukweli.

**11:27 Akasema, nimekabidhiwa vyote na baba yangu; wala hakuna amjuaye Baba, ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana ampenda kufunulia**.

Mungu alimemfanya Yesu huyo awe na mambo yote yanayostahili ili kutimiza kazi aliyotumwa kwayo na Mungu alihakikisha kwamba alijitayarisha vya kutosha. 2 Tim.3:16,17 "Kila aandiko lenye pumzi lafaa...ili mtu wa Mungu awe kamili...amekamilika, amekamilishwa (ametayarishwa kikamilifu) apate kutenda kila kazi njema." Ukiwa na neno la Mungu hakuna ulichopungukiwa kutekeleza mapenzi ya Mungu.

**Ila Baba**. Baba ndiye hasa anayemfahamu mwana kikamilifu.
**Ila Mwana**. Mwana ndiye hasa anayefahamu Baba kikamilifu. Yoh.1:18- "Mungu Mwana pekee, aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua." Njia pekee ambayo watu wanaweza kumwendea Mungu ni kupitia Yesu. Yoh.14:9 "Aliyeniona mimi amemwona Baba."

Hatuwezi kuweza kujua Baba isipokuwa Yesu anamfunua kwetu. "Hakuna aliyemwona Mungu..." (Yoh.1:18) na, kwa kuwa hatujamwona yeye, hatuwezi kumjua. Lakini tunaweza kujua yale amefunua kwetu kwa kuwa Yesu alikuja kumfunua Baba. Wayahudi walikuwa hawana mawazo ya Mungu kuwa Baba. Hawakumjua yeye.

**11:28 Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha**.

Nira ambayo Mafarisayo waliiweka juu ya watu - mapokea ya wazee, na sheria za kawaida - mabmo ambayo wao hawakuweza kutenda (Math.23:2, 4).

**Nami nitawapumzisha**. Iwapo tu watamwendea, na kujifunza njia zake, wangekuweza kuwa huru toka katika nira hiyo nzito.

**11:29 Jitieni nira yangu, mkajifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu**;

Yesu anaondoa nira moja kuiweka nyingine. Hata hivyo, nira yake ni rahisi kubebwa kuliko ile nzito waliyoamuriwa watu kuibeba. Maneno haya yangewafariji. Watu walikuwa wakijitahidi kuwa wenye haki. Waliwamini waandishi na Mafarisayo kuwa ni waalimu wa Sheria za Mungu na waliamini, ili kumpendeza Mungu, iliwapasa kutenda kama walivyoamuriwa. Lakini Yesu anasema, ebu na niwafundishe jambo lililo bora zaidi. Hampaswi kubeba mzigo huu ambao ni mzito zaidi kumpendeza yeye.

**Ni mpole na mnyenyekevu wa moyo**. Angalia maelezo sura 5 juu ya "huruma." Yesu ni mwenye kupenda na mnyenyekevu wa moyo; kwa kutii kikamilifu mapenzi ya Mungu. Tunaweza zaidi kujifunza zaidi kwa mtu aliyemnyenyekevu kuliko mtu mwenye majivuno na kujikweza.

**Raha**. Hawakuweza kufanya kila kitu Mafarisayo waliwaamuru wafanye - ""...kongwa juu ya wanafunzi, ambalo baba zetu...hatukuweza kulichukua." - Matendo 15:10. Hawakuweza kushika amri za Mungu kikamilifu. Lakini kwa kuichukua nira yake Yesu, wangepata uzima wa milele - 1 Yoh.5:13.

**11:30 Kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi**.

**Nyepesi**. Neno hili linapaswa kujifunza. Watu wengi hawatafakari ni nini Yesu anamaanisha "nyepesi." 1 Yoh.5:3 - Amri za Mungu si nzito. Mungu hawezi kutupatia mambo ambayo hatuwezi kufanya. Neno "rahisi" maana yake ukweli kwamba yanapendeza, mambo yenye kufurahisha, mambo tunayotenda kwa furaha - maili ya pili ya upendo. Tunabeba nira kwa kuwa tunapenda kufanya hivyo. Nira Yesu anataka wawe nayo ni ile watakayopenda kuibeba. Walipaswa (tunalazimika) kubeba nira yake ili tupate raha. Katika nira ya Yesu walipata neema, amani, na furaha na furaha. Nasi tutapata. Angalia Fil.4:7; 1 Pet.1:8.

## SURA 12

**12:1 Wakati huo Yesu akapita katika mashamba siku ya sabato; wanafunzi wakaona njaa, wakaanza kuvunja masuke, wakala**.

Katika sura 8 mwandishi alisema, "Nitakufuata kokote uendako..." Siyo tu Yesu hakuwa na mahali pazuri pa kulala, bali hapa tunaona kuwa wanafunzi walishikwa na njaa. Waliacha msaada utokanao na kazi za kawaida za kuwapatia riziki. Wanajitoa sadaka. Kumb.23:25 kuyaparura masuke kuliruhusiwa na Sheria za Musa.

**12:2 Na Mafarisayo walipoona, walimwambia, Tazama! Wanafunzi wako wanafanya neno ambalo si halali kulifanya siku ya sabato**.

Haikuwa mujibu kisheria kulingana na Sheria ya Musa, bali ilikuwa hivyo kulingana na mapokea wazee waliwashurutisha watu. Juhudi yao kwa ajili ya Sabato iliwafanya waende kinyume na hati ya sheria, na kukataza mtu yeyote asifanye chochote siku ya Sabato. Yesu atatoa hoja tano kuonyesha kwamba walielewa vibaya Sheria za Mungu.

**12:3 Akawaambia, Hamkusoma alivyotenda Daudi, alipokuwa na njaa, yeye na wenziwe**?
****Angalia maelezo ya nyongeza juu ya sehemu hii.*

**Hamkusoma**. Anaonya. Ukweli ni kwamba waliwahi kusoma!

**12:4 Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, akaila mikate ile ya wonyesho, ambayo si halali kwake kuila wala kwa wale wenziwe, ila kwa makuhani peke yao**?

Yesu anarejea kwa 1 Sam.21:6. Umetajwa “mkate wa wonyesho” au “mikate ya maonyesho” kwa sababu iliwekwa hadharani. Mikate aliyokula Daudi ni ile iliyoondolewa, na siyo ile mipya iliyokuwa tayari kuwekwa mezani. Hata hivyo, kufuatana na Sheria ya Musa, ilikuwa iliwe na makuhani tu. Angalia Law.24:5-9. Mafarisayo wasingethubutu kumlaumu Daudi kwa kula mkate. Hawakuthubutu kusema kuwa Daudi alivunja Sheria. Lakini sasa wanatafuta makosa kwa wanafunzi wa Yesu kwa sababu wamevunja sheria isiyovuviwa ya mapokeo ya Wayahudi. Daudi dhahiri alivunja sheria, na wala hawakumlamu. Yesu hakutenda dhambi, lakini wakamshutumu. Mafarisayo ni vigeugeu.

**12:5 Wala hamkusoma katika torati, kwamba siku ya sabato makuhani hekaluni huinajisi sabato wasipate hatia**?

*Hoja ya pili*. Hapa tena Yesu anakemea kwa ukali. “Wala hamkusoma...?” Makuhani walikuwa na kazi nyingi siku ya Sabato (Law.24). Kwa wao ilikuwa ndiyo siku yenye kazi nyingi kuliko. Lakini Mafarisayo walifundisha kwamba mtu hawezi kufanya kazi siku ya Sabato. Makuhani walikosea mafundisho hayo kila juma! Shughuli kwa ajili ya kazi ya Mungu ilikubaliwa na kuruhusiwa.

**12:6 Lakini nawabieni, kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko hekalu**.

Hii ni *hoja # 3*. Kiyunani inasemeka hasa, “kitu kilicho” kikubwa kipo hapa, badala ya “yupo aliye,” kama inavyoonekana katika baadhi ya tafsiri zingine. Yesu hajizungumzii mwenyewe, bali kwa ufalme wa Mungu (linga.12:41,42). Ni nini kilichofanya hekalu kuwa kubwa, mawe au yale yaliyotendeka ndani ya hekalu? Mahubiri ya mitume kuhusu ufalme ni muhimu kuliko hekalu. Mafarisayo hawakujua ni nini kilicho muhimu - ni kitu gani hasa kikubwa. Unabii wote wa Agano la Kale ulilenga kufikia hapa hasa, mahubiri ya injili kuhusu ufalme, na Mafarisayo wanajali kuparura masuke siku ya Sabato. Wameshindwa kuelewa kusudi zima ya yanayotendeka.

**12:7 Lakini kama mgalijua maana ya maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingeliwalaumu wasio na hatia**.

Hii ni *hoja # 4*. Angalia kwa ukali anakemea, “Lakini kama mgelijua maana yake...” Kwa mara nyingine tena ananukuu Hos.6:6 (linga. Math.9:13). Kanuni hina maana yoyote ikiwa moyo si sahihi. Mungu alitaka sadaka lakini, zaidi ya hayo, alitaka moyo. Math.23:23 aliwashutumu Mafarisayo hao hao kwa kukosa kuwatendea rehema watu. Katika hoja yake ya nne ni kwamba wanavunja Sheria za Mungu kwa kutokuwa na rehema. Wanafunzi walistahili kupata rehema na huruma kwa kuwa walikuwa na njaa. Lakini badala yake walishutumiwa na kuhukumiwa.

**Msingeliwalaumu wasio na hatia**. Mitumea hawakuwa na hatia. Hakuvunja sheria ya Mungu yoyote, isipokuwa mapokeo ya wandishi na Mafarisayo.

**12:8 Kwa maana mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato**.

Hi ni hoja ya tano na ya mwisho. Yesu anarejea kwake mwenyewe. Yeye ni mtawala, au Bwana wa Sabato. Yesu, kama Bwana wa Sabato, atakwenda kutoa tafsiri sahihi ya Sheria ya Sabato. Sheria ya Sabato haikusema kwamba mtu ashinde na njaa. Mk.2:27 anasema, kwa nyongeza, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. Sheria ile Mungu aliitoa kwa ajili ya mwanadamu juu ya Sabato ilikuwa kwa ajili ya kumwongoza mwanadamu. Mungu hakumpatia mwanadamu nafasi ya kuongeza au kuondoa kutoka katika Sheria za Mungu za Sabato. Angalia Dan.7:13. Walielewa “Mwana wa Adamu” msemo kuonyesha Masihi. Yesu anawapa maonyo wanayostahili kusikia. Ikiwa Yesu ni Masihi je, hakuwa na haki ya kuieleza

Sheria ya Sabato?

**12:9 Akaondoka huko, akaingia katika sinagogi lao.**
**12:10 Na tazama, yumo mtu mwenye mkono umepoza; wakamwuliza, wakisema, Ni halali kuponya watu siku ya sabato? Wapate kumshitaki**.

Wanatambua Yesu anafanya miujiza na kumtega kumponya mtu kwa sababu walitaka kumshitaki. Iwapo anavunja mapokeo yao ya Sheria juu ya Sabato, hapo hatakuwa dhahiri si Masihi. Masihi hatavunja sheria.

**12:11 Akawaambia, Ni mtu yupi miongoni mwenu mwenye kondoo mmoja, na yule kondoo ametumbukia shimoni siku ya sabato, asiyemshika akamwopoa**?

Kondoo mmoja angekuwa na thamani ikiwa ni huyo tu unammiliki. Je, kuna yeyote ambaye, ikiwa alikuwa na kondoo mmoja, asingelivunja mapokeo yao kumshika na kumwopoa shimoni? Wangelitambua iwapo walikuwa waaminifu (na pengine walifanya kama hivi), hakika wangemshika na kumwokoa mnyama wao. Pengine wangefanya hivyo hata kama asingekuwa ni mmoja tu walionaye, bali wangefanya hivyo hata iwapo walikuwa na kondoo mamia! Huo ni mfano mzuri wa unafiki. Wanavunja mapokeo yao wenyewe, lakini hawataki wengine wafanye hivyo.

**12:12 Je! Mtu ni bora kuliko kondoo mara ngapi? Basi ni halali kutenda mema siku ya sabato**.

"Basi," ni hatimisho. **"Ni halali kutenda mema siku ya sabato."** Limekuwa jambo la kufanya au la kutokufanya kwa Mafarisayo. Yesu anaonyesha kuwa unachofanya ndiyo kilicho muhimu. Ni halali kutenda mema. Cotton Mather alisema, "Uwezo wa kutenda mema unalazimisha wajibu wa kutenda." Kuna ulinganifu katika Math.5:23,24 katika kutoa sadaka madhahabuni...nenda patana kwanza na kisha njoo utoe zawadi yako. Kama kuna jambo linalopaswa kufanywa, basi shughulikia jambo hilo. Sio kupuuza shughuli za ibada za siku ya Sabato, bali unapaswa kufikiri juu ya kutenda mema, bila kuhofia kushika mapokeo.

**12:13 Kisha akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako; akaunyosha, ukapona, ukawa mzima kama wa pili**.

Mkono wa mtu umeponywa mara moja! Yesu anafuata mafundisho yake mwenyewe: iwapo kuna jambo jema la kufanya, basi analifanya.

**12:14 Lakini wale Mafarisayo wakatoka wakafanya shauri juu yake jinsi ya kumwangamiza**.

Ni vipofu. Hawatambui uwezo na maana hasa ya mtu huyu mwenye kutenda haya. Wamekemewa na kudhalilishwa. Kiburi chao kimeharibiwa na wanashauriana jinsi ya kumwangamiza. Mamlaka yao yametiwa shaka na wanakwenda kufanya jambo fulani kuhusiana na hilo.

**12:15 Naye Yesu hali akiyafahamu hayo akaondoka huko; na watu wengi wakamfuata; a kawaponya wote**,

Hii ni ya nne ya "sehemu ya uponyaji."

**12:16 Akawakataza wasimdhihirishe**;

Mara tano katika injili ya Mathayo Yesu anaamuru watu wasiwaeleze watu kuhusu yeye (8:4; 9:30; 12:16; 16:20; 17:9). Hii ni mara ya tatu. Angalia maelezo juu ya 8:4 kuona kwa nini Yesu anafanya hivyo.

**12:17 Ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema**,

Hili linatudhihirishia ni kwa nini Yesu aliwaonya wasimtangaze. Mathayo ananukuu Isa.42:1-4 nukuu ndefu zaidi ya Agano la Kale katika Agano la Kale. Linaeleza hili sababu ya Yesu kutokujidhihirisha wazi.

**12:18 Tazama, mtumishi wangu niliyemteua; Mpendwa wangu, moyo wangu, uliyependezwa naye; nitatia roho yangu juu yake, Naye atawatangazia Mataifa hukumu**

Masihi atakuwa na Roho wa Mungu, na Roho huyo atajidhihirisha mwenyewe kwa miujiza na mafundisho.

**Naye atawangazia Mataifa hukumu** = kwa kila taifa. Atawafanya watu wajue yaliyo mema na mabaya, na hesabu watakazostahili kutoa mbele za Mungu. Mistari ya 19-21 inatupatia fafanuzi za kinachoongelewa katika mst.16, walikuwa wasimdhihirishe.

**12:19 Hatateta wala hatapaza sauti yake; Wala mtu hatasikia sauti yake njiani**.

Sababu za "Kutokudhihika kwa Masihi:"

1. *Hatateta* - kwa kutodhihirika kwake kunamsaidia kutokabiliana na Mafarisayo.

2. *Wala hatapaza sauti* - kwa unyenyekevu na utulivu akifanya kazi yake mwenyewe. Haikuwa dhamiri yake Yesu "kujipingia tarumbeta yeye mwenyewe."

3. *Wala mtu hatasikia sauti yake njiani* - huduma ya Yesu haikuwa kwa ajili ya kujitukuza mwenyewe. Alikuwa kutafuata na kuokoa kile kilichopotea. Alikuwa akipendezwa na wale wote waliokuwa wakutafuta ukweli.

**12:20 Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima, hata ailete hukumu ikashinda**.

4. *Hayuko hapa kuvunja na kuharibu* - "**Hata ailetapo hukumu ikashinda**." Yesu hataharibu kitu kilicho tayari kitoweka. "Mwanzi uliopondeka" u karibu na kutoweka na hasingeuvunja. "Wala utambi utokao moshi" u tayari kutoweka, walakini hatauondoa *hata* atakapoleta hukumu ikashinda. Ataponya na kurejeza, lakini kulingana na ratiba yake mwenyewe. Yohana anasisitiza hili katika injili yake. "Haujafika bado muda wangu." - 7:8.

**12:21 Na jina lake Mataifa watalitumania**.

Hili linahakiki ushindi wa Mataifa watakapo mtumaini. Hili ni la msingi kwa kuwa Masihi alikuwa mwenye kunyenyekea, mpole, na mwema mtu wa kuponya. Hakika Yesu ana vyote hivyo! Isaya 42 ilifikiriwa na Wayahudi kuwa ni fungu la Kimasihi. Angekuwa mwema kwa watu wake, lakini pia alitoa tumaini kwa wasio wateule wake Mungu (Wayahudi).

**12:22 Wakati ule akaletewa mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu; akamponya, hata yule bubu akanena na kuona**.

Ni fafanuzi nzuri anayoitoa Yesu akiwa na Roho wa Mungu. Yesu anawaponya wote katika mst.15 na hapa kuna fafanuzi nyingine juu ya hilo.

**12:23 Makutano wote wakashangaa, wakisema, Huyu si mwana wa Daudi**?

Wanajaribu kutafita sababu ya kuthibitisha kwamba Yesu siyo Masihi, mwana wa Daudi. Ni nini zaidi walitarajia Masihi kufanya? Katika Yoh.7:31 walisema, "Atakapokuja Kristo, je! atafanya ishara nyingi zaidi kuliko hizi alizofanya huyu?

**12:24 Lakini Mafarisayo waliposikia, walisema, huyu hatoi pepo, ila kwa nguvu ya Belzebuli mkuu wa mapepo**.

Wanajibu hivi kwa sababu wanajaribu kushika majani makavu. Watu wanauliza swali muhumu na la akili. Mafarisayo wanatakiwa kujibu na wajibu haraka sana. Basi wanasema hivyo.

Kumbuka, hawawezi kukataa miujiza iliyotendeka, lakini wanatafuta kupunguza makali yake wanampa Shetani kuwa ndiye mtendaji. Kwa kuwa nguvu ya kutolea pepo ilikuwa haionekani, ni jinsi gani basi mtu aliweza kuona inakotoka? Ni jinsi gani ungethibitisha kwamba haikutoka kwa Shetani? Baadaye watu wasiamini baada ya karne ya kwanza walisema kwamba Yesu alikuwa tabibu na kwamba yale aliyofanya yalikuwa viini macho (linga. Justin Martyr, Sialogue with Trypho 69, Origen, Angainst Celsus 1.28).

Yesu atajibu kwa mtiririko wa hoja kuonyesha kuwa mtu anaweza kufikiri haya na kutambua kwamba haikutokana na nguvu ya Belzebuli.

**12:25 Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yo yote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama**

**12:26 Na Shetani akimtoa Shetani, amefitinika juu ya nafsi yake; basi ufalme wake utasimamaje**?

*Hoja # 1*. Ni jambo lisiloleta maana kabisa kufikiri kwamba Shetani angefanya kazi kinyume na malengo yake mwenyewe. Basi lazima atawale mtu na akili zake. Kwa nini ajitapeli mwenyewe mafanikio yake. Siyo kwamba Shetani asingeliweza kufanya hivyo, ila ni kwamba hawezi kufanyya hivyo. Ufalme ukifitinika...hufanyika ukiwa - angalia kwamba Shetani ana **ufalme**. Ufalme ni lazima uwe na mfalme, raia, sheria, na nchi. Mambo haya manne Shetani anayo ikiwa ana ufalme. Haya tunaona hapa katika mistari hii miwili. Ufu.2:13 panaonyesha mahali kiti cha Shetani kinapatikana, mahali Shetani anakaa.

**12:27 Na mimi nikitoa pepo kwa Belzebuli, je! Wana wenu huwatoa kwa nani? Kwa sababu hiyo hao ndio watakaowahukumu.**

*Hii ni hoja # 2*. Je, wangeliwashitaki wana wao wenyewe? "Wana" wao hawa ni akina nani? Kuna uwezekano aina mbili:

1. Wanao wa kimwili ni wanafunzi wa Yesu na kati yao wanatenda miujiza.

2. Kwa maana pana zaidi, wana wa Israeli ni wana wao. Maana yake ni, je, mtawashtaki hawa kama watendao kwa nguvu ya Belzebuli? Wangelikuwa ndiyo wana wao. Je, watakuwa tayari kuwashtaki pia?

**12:28 Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia**.

Hii ni *hoja # 3*. Yesu kimsingi anasema, “Ikiwa, hasa, natoa pepo kwa Roho wa Mungu, nini maana yake?” Lazima itamaanisha kwamba yeye ni Mwana wa Daudi, Masihi, na kwamba ufalme wa Mungu unashinda dhidi ya utawala wa Shetani.

**12:29 Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake**.

Katika fafanuzi hii Shetani ndiye mtu mwenye nguvu. Mwivi hataiba kwa mwenye nguvu hata atakapomfunga kwanza, basi Shetani lazima afungwe, la sivyo atazitumia nguvu zake kupinga yale Yesu anafanya. Hawezi kumzuia Yesu asitoe pepo, hata akijitahidi kwa uwezo wake wote. Shetani anaona Yesu akiwatoa pepo ndani ya miili ya waliopagawa, na hawezi kuzuia kwa lolote.

**12:30 Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja nami anatapanya**.

Haiwezekani kuwa kati! Kuna falme mbili tu, na kila mtu yupo kati ya hizo falme mbili. Kumb.13:13,18 - ikiwa mtu atatabiri na yakafanyika kama alivyotabiri, na kisha akasema, “Msimtumikie Mungu,” umetambua kwamba unabii huo haukutoka kwa Mungu.

**12:31 Kwa sababu hiyo nawaambia, kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa**.

**Kufuru** = kukinenea kinyume kitu fulani au mtu fulani. Kusema maneno yenye kuharibu.

Ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa. Unatakiwa moyo mkaidi kusema kwamba Yesu alitenda miujiza akitumia nguvu za Shetani. Mtu anayesema hivyo anatupilia mbali ushahidi na kumpatia Shetani kuwa ndiye mtendaji.

**12:32 Naye mtu yeyote atakaye nena neno lo lote juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakayenena juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao**.

Mtu hawezi kumwita Mungu, Yesu, au Roho Mtakatifu pepo bila kuwa na moyo wenye ufisadi mno. Ikiwa utanena vibaya juu ya Roho Mtakatifu basi umepita mpaka ambao hauwezi kwamwe kugeuka. Haya ni sawa na yale katika Hos.6 - hawawezi kamwe kutubu. Siyo jambo lisilowezekana siku hizi kukufuru. Marko 3:30 ni fungu linalofanana. Kukufuru huku ni kuwa na hatia milele, kwa kuwa walikuwa wakisemam “Ana pepo mchafu.” Ilikuwa kuangalia wanachosema, na kusema hayo waliyosema ndiyo aliyowafanya wamkufuru Roho Mtakatifu. Watu leo wanaweza kwa ujinga kutamka maneno, walakini hawawezi kutamka kwa kuangalia miujiza ya Yesu. Hakuna mtu leo anaweza kufanya mambo yote mawili, hivyo hawawezi kutenda dhambi hii.

**Wala katika ule ujao**. Msamaha hautakuwepo hivi sasa hata milele. Kamwe hawatasamehewa.

****Angalia makala: “Dhambi ya Roho Mtakatifu.”*

**12:33 Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake kuwa mazuri; au ufanyeni mti kuwa mbaya na matunda yake mabaya, kwa maana kwa matunda yake mti**

**hutambulikana**.

Mti mbaya huzaa matunda mabaya tu, na mioyo yao pia imekuwa mibaya inanena hayo kinyume na Yesu. Mistari huu pia ni kuwataka wawe waadilifu. Ikiwa ni mti mwema basi uiteni mwema. Ikiwa mimi ni mwema, basi ninasema mimi ni mwema. Kazi yangu inaonyesha kuwa mimi ni mwema.

**12:34 Enyi wazao wa nyoka, mwawezaje kunena mema, mkiwa wabaya? Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake**.

Watu hawa walikuwa waovu; walio kama nyoka wa sumu, walioharibika kwa asili (3:7).

**Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake**. Walikuwa waovu kiasi hata cha kushindwa kutambua mema hasa, kuwa mema. Kwa nini? Kwa sababu yaliyokuwa mioyoni mwao yalikuwa mabaya kabisa, hakuna jema hata moja lingetoka kwao.

**12:35 Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya. Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana watakalonena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.**

Hazina ni jinsi mtu anatathimini yaliyo moyoni mwake. Thamani ya mtu mwovu ni mambo mabaya. Mtu yale anayotenda na kunena ("huzaa") ni ishara tosha kuona kwamba ni mtu mwema au mbaya.

**12:36 Basi, nawaambia, Kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.**

Maneno yanadhihirisha mawazo ya moyo. Yesu anasema mtu hatasema yasiyokuwemo moyoni mwake. Hivyo ndivyo watu watakavyotoa hesabu zao kutokana na yale wanayosema.

**12:37 Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa**.

Linga. Math.15:11-20. Hukumu itatengemea maneno ya mtu. Kwa maneno hayo mtu atakuhesabiwa kuwa mtu mwenye haki au mbaya.

**12:38 Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.**
**12:39 Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na zinaa chatafuta ishara, ila ishara ya nabii Yona.**

Wanaomba ishara ili waonekane kuwa wana akili timamu. Lakini Yesu anafahamu mioyo yao. Hawataki wapate ushahidi ili wawe na uhakika, bali ni kizazi kibaya na cha zinaa. Hawako tayari kuelewa; wanataka tu waburudishwe. Ishara anayowapatia ni ile ya Yona. Yesu anaamini kwamba Yona alikuwa mtu halisi, nabii, na habari ya Yona kuwa ndani ya tumbo la samaki usiku na mchana kwa siku tatu.

**12:40 Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa mchana na usiku katika moyo wa nchi**.

Hiyo ndiyo itakuwa ishara! Yesu anatoa mtazamo halisi uliofichwa wa kifo chake na kisha

ufufuo wake. Kama Yona alivyotoka katika samaki mzima, hivyo ndivyo Yesu atatoka mzima baada ya siku tatu akiwa chini ya ardhi.

Math.27:63 tunasoma, "siku tatu nitafufuka." Katika Mk.8:31 tunaona mchana na usiku mzima. Hivyo basi, kwa Wayahudi, hili halikupingana. Kwa maelezo zaidi, angalia: John Lightfoot, Commentary on the New Testament from the Talmud and Hebraica, vol.3, pgs.210, 11.

Hapa kuna baadhi ya mifano ya Biblia jinsi walivyohesabu muda: Mwa.7:12,17; 1 Sam.30:12,13, 1 Fal.12:5,12; Est.4:16; 5:1; Math.27:63,64.

**12:41 Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahuku kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri wa Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona**.

Yohana alihubiri karibu kutoka 760 - 800 K.K. Aliwahubiria miji ya wapagani Mataifa, Ninawi ilichofanya, ni kutii neno la Mungu. Sasa mtu aliye mkuu kuliko nabii yule yu katikati yao, na wanapuuza na kumkana. "Aliye mkuu" ni maneno sawa kama yalivyotajwa katika 12:6 - yakihusu ufalme wa Mungu. Ujumbe wa Yesu ni mkuu zaidi kuliko ule wa Yona. Yona hakutenda miujiza kwa watu wa Ninawi, lakini watu walitii. Yesu anahubiri ujumbe na kutenda miujiza, lakini hawatii hayo anayosema.

**12:42 Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahuku kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja toka pande za mwisho wa za dunia ili asikie hekima ya Sulemaini, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani**.

1 Fal.10:1ff - malkia wa Sheba. Sheba inapatikana nchani kusini kabisa mwa Uarabuni. Atasimama siku ya hukumu na watu wa Ninawi kwa kuwa alikwenda umbali mrefu kusikiliza hekima ikinenwa. Watu hawa walikuwa na Yesu kati yao, na hawakutaka kumsikiliza hata kidogo.

**12:43 Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo na maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate**.

Yesu anatumia hilo kama mfano, na siyo kama wazo juu mafundisho ya mapepo. Ni kweli kwamba roho chafu ilipumzika ilipompagawa mtu. Lakini, akimtoka mtu, anatafuta mahali pa kujipumzisha tena bila mafanikio. Rejea nyuma katika majadiliano yetu juu ya "pasipo maji."

**12:44 Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, akiona tupu, imefagiwa na kupambwa**.

Pepo anaamua kumkalia mara nyingine mtu (mahali pa kukaa, makazi) ambapo alikuwa mwanzo.

**12:45 Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu huyo hali ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kilicho kibaya**.

Akiwa amepata mahali pengine palipofagiliwa, pepo anakwenda kuwaalika wengine saba walio wabaya kuliko yeye mwenyewe. Maana imetumika ikilenga **kizazi hiki kibaya**. Hili linarejea na kuzidi katika ubaya kwa Wayahudi. Inawezekana walifanya mambo ya nje, marekebisho madogo, lakini bila toba hasa na kutenda haki. Hivyo wakawa wabaya zaidi kuliko mwanzo.

Siku hizi tunapowafundisha watu na kuwaleta kwa Kristo, tunataka kuwasaidia kuujaza akili zao na muda wao na mambo ya kiroho (linga.4:8 - yatafakarini hayo. Walizoelea kufanya mambo mengine, lakini sasa wanatakiwa kuzoelea wenyewe mambo ya kiroho. Roho mchafu ansingeweza kumwingia mtu ikiwa moyo wake umekaliwa na Roho wa Mungu na haki yake.

**12:46 Alipokuwa anasema na makutano, tazama, mama yake na ndugu zake walikuwa wakisimama nje, wataka kusema naye**.

Ndugu zake wametajwa katika Math.13:55, Yakobo, Yusufu, Simoni na Yuda.

**12:47 Mtu mmoja akamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kusema nawe**.

Walidhania kwamba Yesu angeacha mara moja kazi aliyokuwa akifanya na kukimbilia kuiona familia yake.

**12:48 Akajibu, akamwambia yule alimpasha habari, mama yangu ni nani?**
**12:49 Akawanyooshea mkono wanafunzi wake, akasema, Tazama, mama yangu na ndugu zangu**!

"Mwili na damu" hushikamana pamoja kwa uthabiti, lakini undugu wa kweli ni watu wanaotenda kazi kwa malengo mamoja. Ndugu zake Yesu hawakumwamini - Yoh.7:5. Hawakuunga mkono kile alichofundisha na kutenda. Yesu anawatambua wanafunzi wake kuwa familia yake kwa maana wengi wao - kama yeye mwenyewe - alikuwa na familia aliojitoa sadaka kwa Mungu.

**12:50 Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu**.

Undugu wa damu hauna umuhimu zaidi kama ilivyo kwa undugu wa kiroho. Undugu huu unatokana na utiifu, kutokana na kutenda mapenzi ya Mungu (7:21).

Watu wanahitajika kufanya maamuzi, ama kufuata mapenzi ya Mungu au yale ya familia yao. Ni lazima tuwajali Wakristo kwa kiwango cha juu zaidi kuliko familia zetu wasio Wakristo. Gal.6:10 "Tuwatendee watu wote mema, na hasa jamaa ya waaminio." 1 Tim.5:8 Mungu anatutaka sisi tujali familia zetu, lakini kiwango kisizidi wale wanaojitahidi kumpendeza Yesu.

## SURA 13

**13:1 Siku ile Yesu akatoka nyumbani, akaketi kando ya bahari**.

Hapa ni Kapernaumu, na ni maeneno ya Bahari ya Galilaya.

**13:2 Wakamkusanyikia makutano mengi, hata akapanda chomboni, akaketi; na ule mkutano wote wakasimama pwani**.

Watu wanazidi **kumfuata** Yesu. Huu ni mwanzo wa sehemu ya tano ya hotuba (13:1-52).

**13:3 Akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema, Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda**.

*Angalia makala katika "Mfano wa Mpanzi."*

“Mifano” (parable) linatoka katika neno la Kiyunani ambalo lina maanisha “kulinganisha kwa pamoja.” Neno hili lenyewe limeletwa moja kwa moja toka Kiyunani, *parabola*. *Para* likimaanisha kitu fulani kilicho pembeni ama kando, na *bola* ni kuweka. Tunaweka kitu fulani kando ya kingine. Tunafanya kuweka vinavyoonekana tukimaanisha vya kiroho. Yesu anajitahidi kufundisha hivyo akilenga ya rohoni.

*Angalia makala kwa maelezo zaidi juu ya mifano*.

Huu ni mmoja wa mifano saba. Sura ya 13 imetajwa haswa kuwa “sura ya mifano.”

**13:4 Hata alipokuwa akipanda, mbegu nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila**;

Katika ulimwengu wa kale mtu alibeba mfuko uliojaa mbegu. Angejaza mkononi mwake mbegu na kuzimwaga, zikisambaa. Watu hawa waliwahi kuona na kufanya kama hivi. Walielewa kwamba kulikuwa na mambo manne yangetokea juu ya mbegu, moja ya hayo ni kundi la ndege zilizomwandama mpanzi ili kuzila mbegu.

**13:5 Zingine ziangukia penye miamba, pasipokuwa na udongo mwingine; mara zikaota, kwa udongo kukosa kina**;

Walikuwa wameona mbegu zikiangukia juu ya mwamba na bila hata kuota mizizi.

**13:6 Na jua lilipozuka ziliungua; na kwa kuwa hazina mizizi zikanyauka**.
**13:7 Nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga**;
**13:8 Nyingine ziliaanguka penye udongo mzuri, zikazaa, moja mia, moja sitini, moja thelathini**.

Walitambua kwamba mbegu zinapoanguka katika aina mbalimbali za udongo, zingine zingezaa na zingine hapana. Sehemu kubwa zingeangukia juu ya udongo mzuri, hivyo kuzaa mazao mazuri. Hizi zote zinazotajwa kuwa udongo mzuri, ambazo zinazaa mazao.

**13:9 Mwanye masikio na asikie**.

Yesu anatumia msemo huu katika Math.11:15. Mtu anapaswa kusikiliza na kutafakari juu ya yale yaliyosemwa. Jinsi mtu anavyosikiliza ndivyo anavyopokea. Wote ni lazima wawe wasikilizaji makini.

**13:10 Wakaja wanafunzi, wakamwambia, Kwa nini wasema nao kwa mifano**?

**Nao** = walio nje na duara la wanafunzi. Walizoelea Yesu akiwafundisha kwa namna hii hivyo wakatatanishwa.

**13:11 Akajibu, akawaambia, Ninyi ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao hawakuzijua.**

Kwa kiwango fulani, wanafunzi walielewa “mafumbo,” yalifunuliwa kwao ili waweze kueneza ujumbe. Lakini “kwao” hayakufunuliwa bado kwa sababu walikuwa hawakuwa tayari kupokea, wala wasingeuhubiri.

**13:12 Kwa maana ye yote mwenye kitu atapewa, naye atazidishiwa tele; lakini ye yote asiye na kitu, hata kile alichonacho atanyang’anywa**.

Kama tutachukua nafasi zetu na kuzitumia, hivyo tutapewa nafasi kubwa kuliko. Lakini tukipuuza, ndipo hata nafasi tulizonazo zitachukuliwa. Kama wanafunzi wazuri wa Biblia tunatakiwa kuona haya katika mazingira ya kinachonenwa.

**Naye atazidishiwa tele** = nafasi zaidi wamepewa na Yesu. Ikiwa hawataitumia, hata walizokuwa nazo zitachukuliwa. Hivi ndivyo ilivyotokea kwa Yuda Iskariote. Kile alichopewa kilinyang'anywa.

**13:13 Kwa sababu hiyo nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa**.

Wanaona na kusikia lakini hawaelewi hasa kwa sababu ya "hali ya mioyo yao." Wamejipofusha wao wenyewe.

**13:14 Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, kusikia mtasikia, wala hamtaelewa; kutazama mtatazama, wala hamtaona.**
**13:15 Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya**.

Haya yanatoka Isa.6:9-11. Mungu alitambua watu wangeukataa ujumbe kwa sababu walikuwa na mioyo migumu, lakini Isaya aliendа na kuhubiri hata hivyo. Isaya aliuliza, "Hata lini?" Haya ni mazingira ya mistari iliyopita: hubiri hata yote yasikike au hata watu wote wasikie ujumbe!

Watu wafanywa kuwa wabaya zaidi, ndipo, kwa kusikia, kwa kuwa wamekwisha sikia bila kutii wakawa wabaya zaidi kuliko wasingelisikia kabisa. Angalia, kila mtu anamajukumu.

**Kusikia watasikia, wala hamtaelewa; kutazama...hamtaelewa**. Kwa nini? Kwa sabau ya uzito wa moyo. Wanajifanyia hivyo wenyewe. Ikiwa watu watalegeza tu mioyo yao, ikiwa watasikia, kuona na kugeuka, ndipo Mungu angewaponya.

**13:16 Lakini, heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na masikio yenu, kwa kuwa yanasikia**.

Wanafunzi wanasikiliza kweli, wakiwa na nia na mioyo mikunjufu. Wako tayari kujifundishwa.

**Heri** = waliokubaliwa na walio sahihi mbele za Mungu; walibarikiwa kwa sababu walitumia masikio na macho yao. Waliona, na kusikia!

**13:17 Kwa maana, amin, nawaambia, Manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi, wasiyasikie**.

Mmeona haya, na kunufaika nayo. Umebarikiwa kwa sababu unaweza kuwa sehemu ya jamii ambayo watu wa kale walitamani kuyaona na kuwa sehemu yake (1 Pet.1:10-12).

**13:18 Basi ninyi sikilizeni mfano wa mpanzi**.

Kama katika mst.9, hata sasa anawaalika wale wanafunzi kusikiliza.

**13:19 Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja yule mwovu, akalinyakuwa lililopandwa moyoni kwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia**.

Kwa kulinganisha na fungu hili Mk.4 na Lk.8, hatuoni maneno "asielewe nalo." Hili linapatikana

katika Mathayo tu. Watu husikia neno la ufalme, lakini hawaoni maana yake, hivyo Shetani huja kuliondoa neno lililopandwa mioyoni mwao. Angalia neno lilipandwa **mioyoni mwao**, katika akili zao. Alijua kilichosemwa. Katika Mk.4:15 Shetani huja kufanya kila awezalo kuliondoa neno ndani ya watu.

**13:20 Naye aliyepandwa penye miamba, huyo mdiye alisikiaye lile neno, akalipokea mara kwa furaha**;
**13:21 Lakini hana mizizi ndani yake, bali hudumu kwa muda; ikutukia dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara huchukizwa**.

Mtu anasikia ukweli na kukubali ukweli, lakini hajitoi wakfu kwa ajili ya ukweli huo au kutenda yaliyo haki. Kwa hiyo, udhia unaweza kuangamiza imani aliyomeza. Hakatai na kuasi juu ya ukweli, bali anakosa kuwa imara na ufahamu wa kukaa na kweli. Mtu mwenye imani kubwa anazitumia shida alizonazo kwa kumtia nguvu, na wala haanguki.

**13:22 Naye aliyepandwa penye miiba, huyo ndiye alisikiaye lile neno; na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mal;oi hulisonga lile neno; likawa halizai**.

Hapa kuna mtu anayeukiri Ukristo, lakini nguvu za dini yake imeharibiwa kwa sababu anataka mema katika falme zote mbili. Anataka fahari ya duniani, hasa udanganyifu wa mali. Lazima haya yazidi ushawishi ambao mali unao na jinsi unavyopingana na mambo ya kiroho (1 Tim.6:9, 10).

Ni jinsi gani mali yana udanganyifu? Yanakufanya wewe kitu cha kuabudu. Anaweka imani yako zaidi katika mali kuliko Mungu. Unadhania kuwa ni yako, na wala si ya Mungu. Kurithi katika udanganyifu ni kuwa na uhakika wa uongo. Hivyo ndivyo utajiri ulivyo. Hutudanganya sisi kuamini mambo ambayo si ya kweli (linga. Zab.52:7; Waebr.3:13; ! Tim.2:14; 6:17).

**13:23 Naye aliyepandwa penye udongo mzuri, huyo ndiye alisikiaye lile neno, na kuelewa nalo; yeye ndiye azaaye matunda, huyu mia, na huyu sitini, na huyu thelathini**.

Angalia kuwa katika mfano wa mwisho alikuwa akikiri Ukristo, walakini hakuzaa matunda. Yeye aminiye na kuelewa atazaa matunda.

**Huyu mia** = kiasi cha mara mia moja.

*Angalia makala: "Mpanzi."*

**MAMBO YA KUJIFUNZA**

1. MAFUNDISHO YOTE YANA MALENGO. Kupanda kumefanyika kwa kusudi la kupata matokeo halisi. Lazima tufikirie hili tunapotambua wajibu wetu kufundisha neno la Mungu.

2. KUNA AINA NNE ZA UDONGO (WATU). Udongo unawakilisha watu. Haya ni maelezo ya kuonyesha kwa vitendo kwetu sisi. Tunapowafundisha watu tunatakiwa kukumbuka kwamba kila mtu anaangukiwa kati ya makundi haya manne.

3. USIWE MWALIMU MCHOYO. Mpanzi huyu anapata kwa uhuru! Anachukua kwa mkono wake na kuziachilia zimwagike! Hakujali ni wapi mbegu zingedondokea. Walakini, mbegu nyingine zilidondokea katika udongo usiozalisha. Mungu anataka watu wa aina hizi nne kusikia neno, hatupaswi kuuhukumu moyo wa mwenye kusikia.

4. KUNA WATU AMBAO HAWAELEWI. Ni muhimu kutambua kuwa siyo kwamba hawawezi kuelewa, bali ni kwa sababu hawajakuwa tayari kupokea na kuelewa neno la Mungu - Isa.6:9,10. Watu hawa wana mioyo iliyofungwa, na hawatumii vile viungo ambavyo Mungu alituumbia kuelewa.

5. WENGINE HAWANA NGUVU. Ni kama katika mwamba. Wanasikia na kupokea neno, lakini wanashindwa kuliotesha ndani ya mioyo yao ili liweze kukua. Ni Wkristo wachanga na wanahitaji kufundishwa na kuongozwa.

6. WENGINE WENYE KUIGIZA DINI. Hawa ni wale wanaolipokea neno lakini hawazai matunda. Haachi; lakini kamwe hafanyi lolote! Hii siyo dini ya kweli. Dini ya kweli hutenda kazi, huzaa matunda. Dini ya kweli huzaa matunda ya roho, Gal.5:22. Yakobo 1:27 tunaelezwa kwamba dini ya kweli kuwatembelea yatima na wajane katika dhiki yao. Hawa siyo hasa waliongolewa au wenye dini.

7. WENGINE HUSIKIA NA KUZAA. Walio na moyo safi hukua na huzaa sana. Kuzaa matunda katika Ukristo ni jambo linalojidhihirisha lenyewe zaidi ya namna moja. Wengine hudhania kuwa ni kuwaleta tu watu kwa Kristo. "Kuzaa matunda" ni pale tunapozaa kitu fulani. Tunda la roho katika Gal.5 ni mifano bora ya aina ya matunda Mkristo mwema atazaa. Kwa kuwa ufalme wa Mungu ni shamba la mizabibu, fikiria juu ya mambo mbalimbali mtu anaweza kufanya ili kuzidisha uzalishaji. Ikiwa mtu amekuwa tayari ni Mkristo lakini ameanguka na mtu mwingine anamwendea na kumtia moyo. Mtu huyo anazaa matunda! Anajishughulisha katika kuokoa roho! Tunashawishi maisha ya watu mamia kwa mamia. Mafanikio hayahesabiwi kwa tatizo tu, bali pia kwa yale yameyafanya.

**13:24 Akawatolea mfano mwingine, akisema, ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake**;

Neno **umefanana** linapatikana mara kumi katika Mathayo, mara mbili katika Marko, na mara mbili katika Luka. Ni neno lililo muhimu kwa Mathayo. Kwa kuwa Wayahudi walipendezwa sana na ufalme, ni jambo la msingi Mathayo kujumuisha ufalme katika mambo aliyofundisha Yesu.

**Mtu...kondeni**. Mbegu ni njema, na mtu anayezipanda mbegu anapendezwa na kuona zinazaa mazao mazuri.

**13:25 Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda nagugu katikati ya ngano, akaenda zake**.

Kuna wakulima baadhi wanaojua kabisa anachozungumzia Yesu. Wakati wa ushindani, mtu anaweza kuzuia mazao ya jirani yake asiweze kupata mavuno mengi ili kwamba mazao yake mwenyewe yaweze kuwa na thamani. Gugu ni jani ambalo linaonekana kama ngano hata litakapokuwa, hapo ndipo utaona tofauti.

**13:26 Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu.**
**13:27 Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu**?

Alichukua tahadhari kuhakikisha kwamba mbegu ni njema, ndiyo maana iliwashangaza watumishi kuona magugu shambani.

**13:28 Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka**

**twende tukayakusanye**?

Watumwa wanataka kutatua matatizo yao mara moja. Hata hivyo, hawatambui kwa mapana madhara yatakayotokana na kuchukua hatua za haraka.

**13:29 Akasema La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo.**
**13:30 Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia mavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu**.

Tafsiri inaanza mst.39.

**13:31 Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na punje ya haradali, aliyoitwaa mtu akaipanda katika shamba lake**;

**Punje ya haradali** ni ndogo sana, lakini huota katika mti wa saizi kubwa. Kwa hiyo ufalme wa mbinguni unaanza taratibu bali hukua hata kuwa mkubwa. Kufuatana na Dan.2:44, 45, jiwe lisilofanywa kwa mikono litavunjavunja sanamu vipande vipande, na kuusimamisha ufalme ambao hautaangamizwa kamwe, lakini utadumu milele. Ufalme wa Mungu utaenea duniani nzima (linga. Kol.1:23).

**13:32 Nayo ni ndogo sana kuliko mbegu nyingine zote; lakini ikisha kumea, huwa kubw kuliko mboga zote, ikawa mti, hata nyuni wa angani huja na kukaa katika matawi yake**

Linga. Dan.4:12. Hizi ni baraka za kiroho zinazozungumzwa hapa. Watu wa Mungu watapata kimbilio katika ufalme.

****Angali makala: "Punje ya Haradali."*

**13:33 Akawaambia mfano wengine; Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyoitwaa mwanamke, akaisitiri ndani ya pishi tatu za unga, hata ukachachwa wote pia**.

Sasa anafafanisha mambo fulani ya wanawake. Pishi tatu, au vipimo, vya unga uliotumika kutengenezea mikate. Mara moja chachu ilisambaa. Basi katika mfano huu mfupi, Yesu anazungumzia jinsi ufalme utakavyoenea.

**13:34 Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno**;

Tusidhanie kwamba Yesu alizungumza na makutano kwa njia hii tu. Kabla ya mfululizo huu aliwafundisha kwa namna nyingine (k.m. 5-7), na baada ya haya atazungumza kwa namna nyingine (Math.23). Lakini, Mathayo anasema, katika matukio - na hii moja pekee - Yesu alizungumza nao kwa mifano.

**13:35 Ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali**.

Ananukuu Zab.78:2, Zaburi ya Asafu. Kwa hiyo Yesu anamwita Asafu nabii. Mtu alipokuwa msemaji wa Mungu, alikuwa nabii. Kuna maana mbili za msingi kutokana na fungu hili:

1. Masihi angenena kwa mifano. Yesu sasa anatimiza unabii huo.

2. Masihi atayazungumza mambo yaliyositilika tangu kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu. Yesu anafunua kusudi la milele la kanisa na wokovu. Unaufunua mpango wa Mungu. Waefeso 3 ni fungu zuri la kulinganisha.

**13:36 Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni**.

Yesu hawakemei kwa kuuliza swali hili, mara moja anaanza kuwajibu. Hata ingawa walishindwa kuelewa, walitaka kuelewa. Hawa ni watafutaji halisi. Wanapaswa kusifiwa kwa nia yao ya kutaka kujua. Tayari ameelezea maana ya mfano wa mpazi. Hivyo wanamatumaini kwamba Yesu ataeleza zaidi, na kweli anaeleza.

**13:37 Akajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu**;

***Angalia makala: "Magugu."*

**MAGUGU**

VITU VILIVYOTUMIKA KATIKA MFANO

1. MPANZI --------------------------- MWANA WA ADAMU
2. SHAMBA ------------------------- DUNIA
3. MBEGU NJEMA ---------------- WANA WA UFALME
4. MAGUGU ------------------------- WANA WA YULE MWOVU
5. ADUI -------------------------- IBILISI
6. MAVUNO ------------------------- MWISHO WA ULIMWENGU
7. WAVUNAJI --------------------------- MALAIKA

**13:38 Lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu;**
**13:39 Yule adui aliyepanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika.**
**13:40 Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia**.

Magugu ni wana wa yule mwovu. Watumishi wa Shetani watakusanywa na kuchomwa motoni (linga. 2 Pet.3:7). Moto ni alama ya Mungu juu ya hukumu mwisho wa dunia.

**Mwisho wa dunia** = siku ya hukumu.

**13:41 Mwana wa Adamu atawatuna malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi**.

Malaika ni wavunaji. Wavunaji huja na kukusanya nje na ufalme wake machukizo yote na wale wote walioasi. Mwana wa Adamu ndiye mpanzi, na mpanzi atatuma wavunaji.

Machukizo yote ni wazo la wenye kutenda makosa hata kufikia hatua ya kuwakwanza wengine. Neno hili limetafsiriwa haswa kama "vikwazo" katika Lk.11:6; 13:41 (hapa); 13:57; 16:23; 18:7,8.

**Na hao watendao maasi** = watu wasioshika sheria. Hao ni wavunjaji wa sheria. Watu hawa wanatenda makatazo wanayokanywa na Yesu wasifanye. Yesu anasema katika Math.7:23,

"Ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu."

**13:42 Na kuwatupa katika tanuru la moto, ndiko kutakuwa kilio na kusaga meno**.

Linga. 8:12; 13:50; 22:13; 24:51; 25:30. Haya ni maelezo juu ya watu walio katika mateso. Wako katika maumivu makali. Wanaishi kwa ajili yao wenyewe na kwa anasa, basi lazima wawajibike kwa uchaguzi wao, na kuteseka katika maisha yajayo.

**13:43 Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao**.**Mwenye masikio, na asikie.**

Mathayo anaweka tofauti kati ya ufalme wa Mwana (mst.41; 16:28; 20:21) na ufalme wa Baba (mst. 43; 25:34; 26:29). Pia angalia 1 Kor.15:24ff.

Angalia ufalme wa Mwana umekuwepo kabla ya kubaguliwa kwa wema na wabaya mst.41. Katika 1 Kor.15:24ff Yesu aaurejeza ufalme kwa Baba . Ufalme wa Mwana ni kanisa. Ufalme wa Baba ni utawala wote wa Mungu, siyo kanisa tu hasa. Dan.12:3 ananukuliwa - "watang'aa kama jua..." Wenye haki ni watu ambao watang'aa kama nuru katika ufalme wa Mungu kama walikuwemo katika ufalme wa Mwana. Siyo wale waliochukiza, lakini walikuwa wakishika sheria na kwa matokeo hayo watapokea thawabu.

**MASOMO**

1. SHETANI ANATENDA KAZI WAKATI WANADAMU "WAMELALA." Majina anayopewa Shetani katika Biblia ni kweli. Ametajwa kama nyoka katika Mwa.3, mdanganyifu kama Shetani. Ni simba aungurumaye anayetafuta mtu wa kummeza katika 1 Pet. 5:8. Mwenye hila katika Efe.6:11. Na mwenye hila na mjanja. Somo ni kwetu kukesha kama Petro anavyosema katika 1 Pet.5:8. Tunapaswa kuwa kama Paulo anavyoandika kwa Wakorintho: tusidanganyike kwa ujanja wake (Shetani) - 2 Kor.2:10, 11.

2. SHETANI NI MWEREVU. Wakati mwingine watu wanashindwa kuelewa ushawishi alionao hata wanapogundua kuwa wamechelewa. Hasara alizosababisha Shetani katika mfano huu haikufahamika mapema. Anapenda kufanya mambo ambayo baadaye hujidhihirisha bayana. Math.7:18-20 - mtu anashindwa kuutambua mti hata unapokuwa umezaa matunda. Hivyo ndivyo ilivyo kazi ya Shetani. Watu hujifanya kuwa wenye haki, lakini kwa hakika ni waovu. 2 Tim.3:5 wanajifanya kuwa na utauwa, lakini ni wabaya (cf. 2 Kor.11:14).

3. WATU WA MUNGU HUCHUKIA DHAMBI. Watumishi wa mwenye shamba wana wasiwasi juu ya haya magugu. Wanataka shamba liwe safi na wanataka jambo fulani lifanyike. Kazi hiyo ndiyo itakayofanywa na wavunaji wa Mungu. Watakusanya mabaya. Ni sharti tuwe na tabia njema ili kukabiliana na dhambi, chukia anachochukia Mungu, penda anachopenda Mungu (Rum.12:9) "Lipingeni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema").

4. LAZIMA MTU AFIKIRIE MATOKEO YA LILE ANALOTAKA KULITENDA (k.m. kungoa ngano). Mtu ni lazima afanye mambo kufuatana jinsi Mungu anavyoamuru; ikiwa ni kujitenga na mtu au vinginevyo. Watumishi angelikwenda shambani na kung'oa kila gugu, lakini angeling'oa pamoja na ngano njema. Mwenye shamba anataka kila mbegu njema hata iliyofichama ikiwezekana.

5. HATA HUKUMU IJAPO, KUTAKUWA NA WAIGIZAJI WAKATI WOTE BAINA YA WANA HALISI WA UFALME (linga. mst.47-50). Siyo mtu kwa sababu mtu anadai ni mwna wa Mungu haina maana ndivyo ilivyo (linga. 1 Tim.5:24, 25). Matendo ya watu wengine ni

dhahiri wakati mengine si dhahiri, lakini kila jambo litakuwa dhahiri. Yote yatafunuliwa dhahiri. Kwa kadri tujuavyo watu wanaoonekana kuwa “ngano” kwetu watabainika kuwa “magugu” siku ya hukumu. Maelezo: Rum.16:17 na 2 Thes.3:8ff ni mafungu yanayozungumzia juu ya wenye kukwaza wasikwenda sawasawa na utaratibu. Pia katika 1 Kor.5:1ff - nidhamu kanisani. Ikiwa mtu hayshiki mafundisho ya Agano Jipya, kanisa ni lazima lichukue hatua.

1. Watumishi wanataka kwenda na kuyaoondoa magugu.
2. Njia ya mwenye shamba ni kuyaacha hata mavuno yasije yakang’olewa na ngano. Lazima tufanye mambo kwa njia ile Mungu anapenda. Hatua za kufanya za kujitenga kama zilivyo katika Math.18:15-18 ndiyo tunayopaswa kuifuata hiyo. Ikiwa tutafanya tofauti na hivyo, ndipo tutang’oa pamoja na baadhi ya ngano - kuharibu nafsi njema. Hili ni somo muhimu zaidi katika kanisa!

**Ulimwengu** umegawanyika katika makundi mawili: wana wa ufalme, wana wa yule mwovu. Tunapozungumzia kuhusu wana wa yule mwovu wa dunia, mst.38, 39 panasema malaika huja na kuyakusanya, na yatateketezwa.

**13:44 Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile**.

**Ufalme wa mbinguni**. Hii ni mara ya tisa tuna maneno haya katika sura 13. Hata hivi sasa bado kuna mifuko ya fedha chini ya ardhi Palestina. Hii ndiyo njia walivyohifadhi fedha kule nyuma. Hazina iliyokuwa shambani ilikuwa inamilikiwa na mwenye shamba. Iwapo mtu alikuwa mwenye uadilifu, angelinunua shamba ili aweze kuwa na hazina iliyo shambani. Ukweli wa fungu linasema kwamba “huuza kila kitu” inaonyesha gharama kubwa aliyolipa ili kununua shamba hilo. Mtu ni lazima auze kila alichonacho kwa ajili ya ufalme! Hakuna kilicho na thamani! Ni hazina iliyo na thamani zaidi ya chochote kile ambacho mtu anaweza kuwa nacho. (Linga. Math.6:24; 8:18-22; 10:37-39; 19:21).

**13:45 Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara, mwenye kutafuta lulu nzuri;**
**13:46 Naye alipoona lulu ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua**.

Katika mfano wa kwanza, hazina (ufalme) ulipatika kwa nasibu, na inawezekana kulingana na Yoh.4:28ff (mwanamke Msamaria). Hakuwa akiutafuta lakini hata hivyo akaupata. Katika mfano wa pili, mtu huyu alikuwa akitafuta lulu ya thamani. Alikuwa akitafuta. Huu ni sawa na Towashi katika Matendo 8, mtu mwenye njaa ya kujua, akitafuta ajue. Mifano yote miwili inahatimisho moja: gharama kubwa ilihitajika! Na ikiwa mtu anataka kuelewa hasa ufalme, atatambua thamani yake haswa ilivyo. Yuko tayari kufanya kila kilicho muhimu, au analipia gharama yoyote ile ili kuupata.

**13:47 Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini, likakusanya samaki wa kila namna**;

Kuna vifaa aina mbalimbali vya kufulia samaki vilivyotumika kuvulia (kutoka ndoana hata juya). Juya lilitumika kukusanya kila kitu.

**13:48 Hata lilipojaa, walilivuta pwani; wakaketi, wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa**.

Ulinganifu huu unafanana na mfano wa magugu katika hilo kulikuwa mchanganyiko wa wema na wabaya.

**13:49 Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki**
**13:50 Na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuweko kilio n kusaga meno**

Hii ni hukumu yenye kuwatenganisha wabaya na wema (linga. Math.25:32ff. Atawatenganisha kama vile mchungaji anavyotenganisha mifugo yake).

1. WEMA katika mafundisho mbalimbali ya Yesu wameitwa kondoo, samaki wema, ngano.

2. WAOVU wameitwa magugu, mbuzi na samaki wabaya.

**13:51 Yesu aliwauliza, Mmeyafahamu hayo yote? Wakamwambia, Naam.**
**13:52 Akawaambia, Kwa sababu hiyo, kila mwaandishi mwenye elimu ya ufalme ya mbinguni amefanana na mtu mwenye nyumba atiaye katika hazina yake vitu vipya na vya kale**.

Mwenye nyumba ana ana amri juu ya vitu vipya na vya zamani. Kwa hiyo mwandishi aliye mwanafunzi anaweza kuchukua mafundisho mapya na ya kale na kupata habari zenye thamani kwa ajili ya anaowafundisha: ina thamani kwa sababu Yesu anataja kuwa **hazina**. Mwandishi anapaswa kuweza kuona jinsi gani Yesu anatimiza Agano la Kale. Anaona jipya, akilinganisha na lile la kale.

**13:53 Ikawa Yesu alipomaliza mifano hiyo, alitoka akaenda zake**.

Hii ni hatimisho ya sehemu ya tatu ya mahubiri.

**13:54 Na alipofika nchi yake, akawafundisha katika sinagogi lao, hata wakashangaa, Huyu amepata wapi hekima hii na miujiza hii**?

Hekima ya Yesu na uweza vilikuwa viwashawishi watu wa Nazareti kwamba alikuwa kama alivyodai kuwa.

**13:55 Huyu si mwana wa seremala? Mamaye si yeye aitwaye Mariamu? Na nduguze si Yakobo, na Yusufu, na Simoni, na Yuda?**
**13:56 Na maumbu yake wote hawapo hapa petu? Basi huyu amepata wapi haya yote**?

Yesu na familia yake ilijulikana vizuri mjini hapo. Walimtambua kwamba alilelewa nyumbani kwa seremala, na kwamba hakuhudhuria shule yoyote ya waalimu, hivyo basi alipateje ufahamu huo? Swali lingine ambalo halikuhitaji kujibiwa.

Basi huyu amepata wapi haya yote. Hili ni swali zuri sana. Tumeona ushahidi wa majibu kupitia sura 13 nzima. Wale wote waliokuwa wanafunzi wa kweli wangelitambua kwamba kufuatana na unabii wa Agano la Kale (linga. Isa.42:1) Yesu aliyapokea hayo kutoka kwa Mungu, kwa sababu alitabiriwa kuwa angelikuwa na Roho wa Mungu. Walimfahamu kama mwanadamu halishindwa kuona Uungu wake.

**13:57 Wakachukizwa naye. Yesu akawaambia, nabii hakusi kupata heshima, isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwao wenyewe**.

Katika mst. 41 Yesu ametangaza jinsi atakavyo kusanya "machukizo" yote. Neno lililotumika hapa ni sawa na **makwazo**. Wamekuwa machukizo kwa sababu ya Yesu.

Nabii hakosi kupata heshima...nyumbani mwake mwenyewe. Hii ni jambo la kuvutia katika kujifunza asili ya mwanadamu. Hasira ni matokeo yanayodhihirika mtu anapoona hana jinsi nyingine yoyote. Hawawezi kukataa mafundisho ua miujiza. Hawaelewi kabisa - wanakwazwa na yale Yesu ananena na kutenda - badala ya kuangalia ushahidi na kuamini.

**13:58 Wala hakufanya miujiza mingi huko, kwa sababu ya kutokuamini kwao**.

Hili ni la msingi sana kuthibitisha yaliyoelezwa hapo mwanzo. Miujiza ilikusudiwa kuwafanya watu waamini na ikiwa ilikuwa haizalishi imani, basi haikutendwa. Yesu hakutenda miujiza mingi Nazareti kwa sababu watu walimchukia bila haki. Alitoa uthibitisho wa kutosha ili waamini, walakini bado walikuwa bila imani. (Huu ni mfano mzuri wa kutupa lulu mbele ya nguruwe.)

## SURA 14

**14:1 Wakati ule mfalme Herode akasikia habari za Yesu, akawaambia watumishi wake**,

Mfalme Herode Antipas (kwa maelezo zaidi angalia maswala ya utangulizi juu ya Herode) alisikia habari kuhusu Yesu, miujiza, na mafundisho yake na mahubiri.

**14:2 Huyo ndiye Yohana Mbatizaji; amefufuka katika wafu; na kwa hiyo nguvu hizo zinatenda kazi ndani yake**.

Kazi ya Yesu alidhaniwa kuwa ni moja kati ya manabii na siyo ya Masihi. Kwa nini ilikuwa hivyo? Walikuwa wangali wakifikiria juu ya ufalme wa kimwili, na si wa kiroho. Kwa hakika Herode asingemwazia Yesu kuwa ni Masihi.

**14:3 Maana Herode alikuwa amemkamata Yohana, akamfunga, akamtia gerezani, kwa ajili ya Herodia, mke wa Filipo nduguye.**
**14:4 Kwa sababu Yohana alimwambia, si halali kwako kuwa naye.**
**14:5 Naye alipotaka kumwua, aliwaogopa watu, maana walimwona Yohana kuwa nabii**.

Makutano walimtambua Yesu kuwa nabii na kwamba alikuwa na wafuasi wengi sana miongoni umati. Alimweleza Herode kuwa haikuwa halali kumwoa Herodia kwa sababu ya mme wake wa kwanza. Filipo, alikuwa bado anaishi. Kadhalika mke wa Herode alikuwa hai. Tunatambua haya kutokana na historia.

**14:6 Hata ilipofika sikukuu ya kuzaliwa kwake Herode, binti Herodia alicheza mbele ya watu, akampendeza Herode**.

Salome alikuwa mpwawe Herode.

**14:7 Hata akaahidi kwa kiapo kwamba atampa lo lote atakaloliomba.**
**14:8 Naye huku, akichochewa na mamaye, akasema, Nipe hapa katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji**.
**14:9 Naye mfalme akasikitika; lakini kwa ajili ya viapo vyake, na kwa ajili ya wale waliokuwa wameketi chakulani pamoja naye, akaamuru apewe**;

Herode alikuwa ayashike maneno yake mwenyewe asije akaibika mbele ya waalikwa. Hakutaka

aonekane kama dhaifu kwa kuvivunja viapo vyake. Pengine wageni wake walitaka Yohana afe pamoja na Herodia vile vile.

**14:10 Akatuma mtu, akamkata kichwa Yohana mle gerezani.**
**14:11 Kichwa chake kikaletwa katika kombe, akapewa yule kijana; akakichukua kwa mamaye**.

Sasa sauti ya adui wa Herodia imenyamazishwa. Inawezekana alipata ahueni kutokana na hilo.

**14:12 Wanafunzi wake wakaenda, wakamchukua yule maiti, wakamzika; kisha wakaenda wakampasha Yesu hjabari**

Je, waliamini kwamba tukio hilo lingechochea hasira za Yesu? Hatuelewi nini walikuwa wakifikiri lakini, bila shaka, walijua kwamba lazima Yesu angelifahamu.

****Angalia maswala ya nyongeza juu ya ndoa.*
****Angalia makala: "Kuridhia Ndoa Isiyo ya Kimaandiko" na Hugo McCord.*

Herode na Filipo walikuwa ndugu. Herodias aliolewa na Filipo, lakini alimtaliki Filipo na akaolewa na Herode. Wengi wanadai kwamba ndoa yake kwa Herode ilikuwa uzinzi na ndugu. Yohana anasema, "Si halali kwako kuwa na mke wa ndugu YAKO." Hapo ndipo dhambi inapokaa. Wale wote wanaojadiliana kwamba ubatizo unaosha dhambi zote, na kwamba mtu anapaswa abakie katika hali ile ile aliyoitiwa, wanatakiwa watafakari fungu hili. Kwa nini Yohana asimwambie Herode abatizwe? Ubatizo unahitaji toba (Mdo.2:38). Ili Herode apate kutubu ilimlazimu kumwacha mkewe. Hivyo ndivyo Yohana alimwambia afanye. Ubatizo hautafanya uhusiano mchafu kuwa mtakatifu. Ndoa ya Herode kwa Herodia ilikuwa si halali, bila kujali kwamba Herode alibatizwa au la. Basi, asingeweza kubatizwa na "kubakia katika hali hiyo," yaani, katika ndoa isiyo ya kimaandiko.

**14:13 Naye Yesu aliposikia; hayo, aliondoka huko katika chombo, akaenda mahali pasipo watu, faraghani. Na makutano waliposikia, walimfuata kwa miguu kutoka mijini mwao**.

Yesu alikuwa akitaka kujitenga faraghani kwa kitambo, lakini watu wengi walipendezwa naye hata asiweze kupata fursa hiyo.

**14:14 Yesu akatoka, akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wagonjwa wote**.

Anajitoa mwenyewe kwa ajili ya wengine. Hii ndiyo picha haswa ya kujidhili kwake Kristo. Wakati mwingi tunasema, "Nastahili kuwa na muda wa faragha!" Lakini Yesu hakufikiria hivyo. Alikuwa ni mpaji na si mpokeaji.

**Akaponya wagonjwa wao**. Hii ni sehemu nyingine ya uponyaji. Hii ni sehemu ya #5 yetu ya uponyaji. Yesu alijisikia huruma na akaidhihirisha kwa kuponya wagonjwa. Yesu alikuwa mwenye huruma kitabia (Math.9:36).

**14:15 Hata kulipokuwa jioni, wanafunzi wake waklimwendea, wakasema, Mahali hapa ni nyika tupu, na saa imekwisha pita; uwaage makutano, aende zao vijijini, wakajinunulie chakula**.
**14:16 Yesu akawaambia, Hawana haja kwenda zao, wapeni ninyi chakula**.

Muda ulikuwa umepita sana. Wanafunzi waliwaona watu kuwa walihitaji kuondoka ili wapate

kununua chakula, lakini Yesu anawambia wawalishe watu.

**14:17 Wakamwambia, Hamna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili**.

Chakula hiki pengine kingetosha kwa mtu mmoja tu. Mikate mingine haikuwa mikubwa sana.

**14:18 Akasema, Nileteeni hapa.**
**14:19 Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano**.

Hili limefanyika katika njia ile ambayo kila jicho lingeshuhudia. Anabariki chakula, jambo ambalo ni kawaida. Ukweli wa kwamba Yesu anamsihi Mungu na miujiza inayotokea ni dhahiri. Inadhihirisha kuwa yeye alitoka kw a Mungu.

**14:20 Wakala wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate, vikapu kumi na viwili, vimejaa**.

Neno "vikapu" kwa Kiyunani ni "chombo kikubwa."

**14:21 Nao waliokula walikuwa wanaume wapata elfu tano, bila wanawake na watoto**.

Muujiza huu unapatikana katika injili zote nne - Mk.6, Lk.9, na Yoh.6. Roho Mtakatifu anawawezesha waandishi wote wanne kuandika muujiza basi una maana. Mathayo hahusisihi muujiza huu na Masihi, pengine kwa kuwa ilikuwa bayana zaidi hata isihitaji maelezo. Wayahudi walitambua ni nini Masihi angefanya.

Kut.16:13-21 Masihi angekuwa mfano wa Musa, na Musa aliwalisha watoto jangwani. Zab.78:19 "Je! Mungu anaweza kuandika meza jangwani?" Hili linazungumzia kutangatanga jangwani. Mungu alifanya nini? Yesu alifanya nini? 1 Fal.17:8-16 Eliya alimlisha mjane na mwanawe. Mbali na Agano la Kale kulikuwa na mapokea kwamba watu wangelishwa mana katika kipindi cha Masihi - 2 Baruku 29:8. Watu hawa hawakushindwa kuelewa jambo hili kumlenga Masihi.

**14:22 Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano**.

Mitume walitaka awaruhusu watu kuondoka katika mst. 15. Anafanya hivyo sasa, lakini ni baada tu ya kuwapatia chochote cha kufikiria juu yake - muujia dhahiri.

**14:23 Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwa jioni, alikuwako huko peke yake**.

Hivi ndivyo Yesu alikuwa afanye katika mst.13 baada ya kusikia kwamba rafiki na jamaa yake aliuawa kikatili. Kwa nini alijitenga mwenyewe? Je! kwa ajili ya uzuni? Yohana anatueleza kwamba mara baada ya muujiza huu, Yesu alitambua kwamba watu walitaka kumfanya mfalme. Iwe sababu yoyote ile...akaomba!

**14:24 Na kile chombo kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana kwa mawimbi; maana upepo ulikuwa wa mbisho**.

Umbali unakadiliwa kuwa futi 600.

**14:25 Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari.**

Zamu ya nne ilikuwa saa 3 - 6 kamili asubuhi. Wanafunzi pengine walichoka kutokana na kupambana na upepo ulikuwa wa mbisho.

**14:26 Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli, wakapiga yowe kwa hofu**.

Waliona nini? Mzimu fulani toka kwa wafu? Ukweli ni kwamba, waliongopa. Je! sisi tusingeogopa kama hawa walivyoogopa? Yesu kwa utulivu anatembea katika mawimbi makubwa yakimsukuma huku na huko.

**14:27 Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipe moyo ni mimi; msiogope.**
**14:28 Petro akamjibu, akasema, Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji.**

Petro alikuwa mtu mwenye harara. Hii ni moja ya matano ya matukio yanayomwelezea Petro. Mengine manne ni ya kukiri 16:13ff; Yesu alipogeuka sura 17:4ff; tukio linahusu kodi 17:24ff; na wakati wa kukana 26:69ff.

**14:29 Akasema, Njoo. Petro akaakashuka chomboni, akaenda kwa miguu juu ya maji, ili kumwendea Yesu.**
**14:30 Lakini alipouona upepo, akaogopa; akaanza kuzama, akapiga yowe, akisema, Bwana, niokoe**.

Petro ni mtu mwenye imani ya kutosha katika Yesu moja kwamba angeweza kufanya hivyo. Kumbuka katika sura ya 10 Petro yeye mwenyewe alitenda miujiza. Ni jambo lingine kwa yeye kutenda yale aliyoona mwingine akifanya. Hakika kwa upepo mkali, na mawimbi makubwa, kwa mtu kwenda juu ya bahari wakati huo, nafasi yake ya kuokoka hakuna. Bali Yesu anafanya hivyo, kwa hiyo Petro anadhani anaweza kufanya hivyo. Hili ni somo muhimu sana kwetu.

1 Pet.2:21 Yesu aliteseka kwa ajili yetu, akituachia kielelezo. Kumwamini Yesu na kuona uweza wake vingetutia sisi nguvu kwamba tunaweza kufanya mambo makubwa kadhalika. Ni kutembea kwa imani, kwa kutumaini, kusadiki katika uweza wake. Lazima tusijisumbue na kuwa na hofu za maisha, na kujiweka huru mbali na hofu. Ndipo tutakapoona kwamba tunaweza kuyakabili majaribu na dhiki kwa sababu Mungu atatusaidia kushinda.

Petro anafanya jambo ambalo sisi sote tunafanya. **Akaogopa**. Kwa kuwa Yesu aliweza kutuliza mawimbi (8:23) kusudi la habari hili imejadiliwa katika mst. 33.

**14:32 Nao walipopanda chomboni, upepo ulikoma.**
**14:33 Nao waliokuwamo ndani ya chombo wakamsujudia, wakisema, Hakika wewe u Mwana wa Mungu**.

Wakamwabudu na kusema, "Hakika wewe u Mwana wa Mungu!" Kulikuwa hakuna sababu ya Mathayo kuandika tena habari ya kutuliza dhoruba, isipokuwa kuonyesha kukua kwa imani na kuelewa kwa wanafunzi wake. Tunajifunza hili pamoja nao. Waliona bahari ikiamuriwa kuwa shwari, bali sasa kuna somo lingine la kujifunza. Waliuliza mapema kwamba, "Huyu ni mtu wa namna gani...?" Sasa hawaulizi swali hilo, bali wanajibu swali hilo. Wanaeleza asili ya Yesu ya kipekee. Yeye ni Mwana mbarikiwa wa Mungu, Mwana wa pekee.

Kuna kielelezo kinacholingana na yaliyotokea kwa Petro katika Math.26. Hapa, kama huko:

1. Petro anaikiri imani yake isiyoyumba kwa Yesu. Niamuru nije kwako juu ya maji, na
2. Kisha akaogopa. Petro, mwanafunzi, akapata wasiwasi.
3. Akashindwa na akaanza kuzama. (Katika Math.26 anamkana).
4. Kisha analia, au anaonyesha toba kwa namna fulani, na anarejeshwa tena.

Mara nyingine tena, matumizi ya swali katika mst.31 kuna maana. "Mbona uliona shaka?" kutembea juu ya maji ni jambo ambalo lilihitaji imani kidogo zaidi. Mashaka mara nyingi hujaribu kuzuia kufanya mambo makubwa kwa ajili ya Bwana. Tunautilia shaka uwezo wetu, au wa watu wengine katika kusanyiko. Kuona mashaka kunaweza kutuzuia sisi tusifanye mambo makubwa kwa Bwana.

**14:34 Na walipokwisha kuvuka, walifika nchi ya Genesareti**.

Watu walimtambua Yesu kokote alikokwenda, na mara walipofanya hivyo, wakamletea wagonjwa wote na wakaponywa.

**14:35 Na watu wa mahali pale walipotambua, walituma watu kwenda nchi ya zile za zilizo kandokando, wakamletea wote waliokuwa hawawezi;**
**14:36 Nao wakamsihi waguse hata pindo la vazi lake tu; na wote waliogusa waliponywa kabisa**.

Watu hawa wanadhihirisha kukua kwa imani yao. Mwanamke katika sura 9:20, 21 aliamini kwamba akigusa tu upindo wa vazi angepona, na Yesu akamsifia katika hilo. Watu hawa pia wanadhihirisha imani hiyo hiyo. Somo hili ni muhimu sana lenye maana kiroho. Nyosha mkono wako na mguse Mwokozi. Ana uwezo wa kuponya kiroho. Baadaye watu waliweza kulaza wagonjwa wao waguswe na kivuli cha Petro (Mdo.5:15) na kuchukua nguo na leso toka katika mwili wa Paulo kwa wagonjwa wao (Mdo.19:11, 12). Hii ni sehemu ya sita katika Mathayo.

## SURA 15

**15:1 Ndipo Mafarisayo na waandishi toka Yerusalemu walipomwendea Yesu wakisema**,

Watu wenye mamlaka kutoka Yerusalem wanaanza sasa kujihusisha.

**15:2 Mbona wanafunzi wako huyaharibu mapokeo ya wazee, kwa maana hawanawi mikono walapo chakula**.

Waliwashutumu wanafunzi kw kuvunja sheria katika sura 12 (bila mafanikio) na sasa wanamshutumu Yesu kwa kuvunja mapokeo. Mafarisayo waliamini mapokeo yalifunuliwa kwa Musa na Mungu, basi wakasimuliana kutoka kwa wazee kutoka kizazi hiki na kingine. Waliona kuwa ni sawa na Sheria. Mapokeo ya kuonya mikono kabla ya chakula yalipatikana katika Mishnah. Sehemu ya Yadaim katika Mishnah (neno Yad maana yake "mkono" na "im" ni uwingi). Wanafunzi wake hawaoshi mikono kulingana na *mapokeo*.

**15:3 Akajibu, akawaambia, Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?**

Waliamini kwamba mapokeo ni sawa na sheria. Yesu anawapinga waandishi na Mafarisayo kwa kuvunja kwao Sheria za Mungu wakitii mapokeo. Mapokeo hayo yalipinga neno la Mungu. Wanadamu daima wamejaribu kuunda maneno yao yalingane na neno la Mungu.

**15:4 Kwa kuwa Mungu alisema, Mheshimu baba yako na mama yako, na amtukanaye**

**baba yake au mama yake kufa na afe**.

1. Tungo la kwanza inatoka Kut.20:12.
2. Tungo la pili inatoka Kut.21:17 (siyo moja ya amri kumi).

Ingawa wanaweza wasiwe wamevunja nukuu ya sehemu ya pili (kwa kuwa hii ni lahisi kuitambua), lakini ujanja wao kuwatendea wazazi wao ulikuwa mbaya kama vile kulaani. Ndiyo sababu Yesu anazungumzia hili kwa kulinganisha.

Mheshimu ni neno ambalo linabeba maana nzito kuliko tunavyojadili kwa kawaida. Tunapofundisha watoto wetu, mawazo yao juu ya kuheshimu "kufanya sawasawa na jinsi (wazazi wao)" wanasema." Neno hili siyo "kutii." Neno ni "heshimu," siyo tu linamaanisha kutii, bali kuwa na tabia kupenda kutii, kunyenyekea chini ya mapenzi ya wazazi. Mungu anataka amri hizi kuwa katika maisha yote. Hapa sisi watu wazima tunavunja amri hizi! Walikuwa wawaheshimu baba zao na mama zao kwa kadri ya maisha yao, wakizitenda katika uzee wao na\au katika dhiki.

**15:5 Bali ninyi husema, Atakayemwambia babaye au mamaye, Cho chote kikupacho kusaidiwa na mimi ni wakfu,**
**15:6 Basi asimweheshimu baba yake au mama yake. Mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu**.

**Kusaidiwa na mimi ni wakfu** = "corban." Corban ni neno la ufunguo katika kitabu cha Walawi (limetumika mara themanini na tisa). (Hazina ya Kiyahudi iliitwa "corbana"). Waandishi na Mafarisayo walifundisha vijana kwamba kulikuwa na njia ya kujikinga na amri ya Mungu kwa kutimiza mahitaji ya wazazi. Walichotakiwa kufanya ni kusema kwamba chochote wazazi wangeomba kusaidiwa basi kilikuwa "Corban" au wakfu kwa Mungu. Kufuatana na mapokeo yao - na si Sheria ya Mungu - hii iliwawezesha watoto kuachwa huru na maagizo ya Mungu.

**Mkalitangua...mapokeo**. Waalimu (Rabi) walisema kwamba mapokeo yao yalikuwa ni "wigo ulioizunguka sheria" (Aboth 3:14). Waliamini kuwa mtu angeweza kukaa vizuri kabisa katika amri kwa kufuata mapokeo yao. Yesu anasema mapokeo yanasimama yakipinga Sheria ya Mungu.

**15:7 Enyi wanafiki, ni vema alitabiri Isaya kwa habari zenu, akisema,**
**15:8 Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami**.

Yanatoka katika Isa.29:13. Wana sura mbili. Ni wanafiki! Wanajifanya kuwa wenye haki, lakini mioyo yao imejaa nia mbaya. Walikuwa wakiziharibu sheria za Mungu kwa ajili ya faida zao wenyewe. Tunaiita hii "ibada ya midomo." Namna maneno yao wanavyotamka ni mazuri, lakini mioyo yao haiko ndani yake. Yesu anataka midomo safi na mioyo safi!

**15:9 Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu**.

Kulingana na maadiko kuna aina tatu za ibada.

1. Kuna ibada ya bure kama ilivyojadiliwa hapa.
2. Kuna ibada ya ujinga kama katika Mdo.17:23.
3. Kuna ibada kweli, Yoh.4:23,24. Hiyo ni katika roho na kweli.

Neno bure maana yake hakuna kitu, bila thamani. Mtu anaweza pia asiabudu kabisa kwa sababu haina faida yoyote. Mungu anasema katika Isa.1:13ff, "Msilete tena matoleo ya ubatili...siyawezi

maovu hayo na makutano ya ibada. Nanyi mkujuapo mikono yenu...sitasikia. Mikono yenu imejaa damu." (Linga. Mik.6:6-8). Tunapaswa kusali sawasawa na jinsi Yesu alivyofundisha, "Mapenzi yako yatimizwe." Lazima tufanye mapenzi ya Mungu katika utawala wake. Hii ni pamoja na kutenda mapenzi ya Mungu katika ibada. Ndiyo maana Yesu alisema, "...imewapasa ...kumwabudu katika roho na kweli."

Maagizo ya wanadamu = hakuna zaidi ya mawazo ya wanadamu. Lakini katika akili zao siyo mawazo, bali "mafundisho." Ni upumbavu kiwango gani kufunga kwa wengine yale tunayofikiria!

**15:10 Akawaita makutano akawaambia**

Yesu anazungumza na viongozi, lakini sasa ana jambo la kuwaeleza makutano. Anaenda kufafanua yale aliyowaleza wanafunzi katika mst. 14, "Wacheni." Amewakemea waandishi na Mafarisayo kwa yale wanayofanya na sasa anataka kutumia fursa hiyo kusema kitu fulani chenye thamani kwa makutano.

**Sikilizeni, mfahamu**. Hakuna sababu ya msingi kwao kutokuelewa yale Yesu anasema (linga. Efe.5:17).

**15:11 Sikilizeni, mfahamu; Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi**.

Neno "najisi" lina maana "kufanya kisiwe safi." Kula mikate na mikono michafu kusingenajisi mkate ama mlaji. Lakini mapokeo, maneno ya wanadamu yaliyo kinyume na neno la Mungu, hayo ndiyo yalimfanya mtu kuwa najisi! Kufanya mambo kinyume na Sheria ya Mungu itawafanya watu wasiwe safi na najisi mbele za Mungu.

**15:12 Ndipo wanafunzi wake walipomwendea, wakamwambia, Wajua ya kuwa Mafarisayo waliposikia neno lile walichukizwa**?

Walichukizwa = "kusababisha kujikwaa" (13:41, 57). Iliwachukiza wanafunzi kwamba Yesu aliwakwanza watu walioheshimiwa hawa toka Yerusalemu. Kama walivyo watu wengi leo, kuheshimu watu kulizidi jitihada yao kwa ajili ya kweli. Waalimu wa uongo wanatakiwa wapingwe kwa ajili ya kuwatoa watu katika wokovu.

**15:13 Akajibu, akasema, Kila pando asilopanda Baba yangu aliye mbinguni litang'olewa.**

Kila pando = fundisho, mwongozo. Mafundisho ya aina yoyote ile, mazoelea, na kanisa visivyoanzishwa (bila idhini) na Mungu vitang'olewa (angamizwa). Mungu alipanda Sheria zake, wala si mapokeo yao (Math.13:24-30).

**15:14 Waacheni; hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia wote wawili motoni.**

Kila kosa litashughulikiwa na Mungu. Yesu na wanafunzi wake wasingeliweza (na hatuwezi) kupoteza muda wetu kwa watu kama hawa na kusahau umati. Yesu hakufanya hivyo, akafundisha makutano. Hivi ndivyo Paulo anamweleza Tito kuhusu waalimu wa uongo - Tito 3:10, 11. "Mtu mzushi...mkatae...ukijua ya kuwa mtu kama huyo...amejihukumu hatia yeye mwenyewe." Hii si tu kuvunja ushirikiano nao. Bali, kujitenga nao; usipoteze muda wako nao. Sisi leo, kama walivyofanya wanafunzi, tutakabiliana na waalimu wa uongo. Ikiwa hatuna mawazo ya kukabiliana nao, tunapoteza nafasi ya kuwaokoa wengine. Tunapaswa kuwashawishi

wanaoweza kushawishika.

**15:15 Basi Petro akajibu, akamwambia, Tueleze mfano huo.**
**15:16 Yesu akasema, Hata ninyi mngali hamna akili**?

Mara nyingine tena Yesu anawapa changamoto ya kufikiri. Kuna ukweli katika Neno la Mungu lililo hazina iliyosititika ardhini, na haiwezi kufunuliwa wazi pasipo jitihada, kwa kujifunza, na kazi nzito. Biblia inaweza ikaieleweka! Baadhi ya yale Paulo aliyaandika yalikuwa magumu kuelewa, lakini tunaweza kuelewa kama tunajituma kufanya kazi fulani. Ikiwa hatujafundishwa, tunageuza na kupotosha neno lake tunajiletea maangamizi yetu wenyewe (2 Pet.3:14-18).

**15:17 Hajafahamu bado ya kuwa kila kiingiacho kinywani hupita tumboni, kikatupwa chooni**?

Chakula cha mwili huingia na kupita pasipo kuharibu hali ya mtu kiroho.

**15:18 Bali kitakacho kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimetiavyo mtu unajisi**.

Mambo yatokayo kinywani hutoka moyoni mwa mtu, na huathiri hali ya kiroho.

**15:19 Kwa maana moyoni mwa mtu hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo na matukano**.

Hakuna mtu ambaye amewahi kufanya moja ya makosa haya pasipo kuuathiri moyo. Kwa hiyo angalia nje (kilichotendeka). "Mtawatambua kwa matunda yao" - Math.7:20. Kuna mambo hasa yanayomtia mtu unajisi (linga. Gal.5:19-20).

**15:20 Hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula kabla mtu hajanawa mikono hakumtii mtu unajisi**.

Waadishi na Mafarisayo walizingatia zaidi mambo haya ya nje hata wakashindwa kuangalia zaidi ya ndani, mambo ya kiroho. Mambo ya kiroho ndiyo Yesu aliyazingatia. Katika Math.5, angalia ulinganifu aliofanya Yesu (k.m. "Mmesikia...nami nawaambia"). Yesu anauendea moyo.

**15:21 Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni. Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo**.

Sasa anaingia katika majimbo ya Mataifa kasikazini-mashariki mwa Palestina. Anakwenda kuhubiri, lakini kupitia. (Linga. 10:5, 6 walikuwa wahubiri kwa waliopotea Waisraeli).

**15:22 Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo**

Hili ni jambo la kushangaza! Mwanamke wa Mataifa, nje ya Palestina, alimtambua Yesu hata kumwita Mwana wa Daudi. Anaomba rehema (anamtaka amtendee jambo fulani).

**15:23 Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu**.

Huu ndio mtihani wa imani yake. Kwa mtazamo wa wanafunzi alikuwa akijaribu asikilizwe kitu

ambacho waliona wakizuie. Wanafunzi walitaka Yesu amsaidie hitaji lake ili aweze kuondoka na kuachana naye.

**15:24 Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli**.

Hakutumwa kwa watu wasio Waisraeli. Ilikuwa moja ya mpango wa Mungu kwamba huduma ya Yesu binafsi iwe kwa Wayahudi tu. Walikuwa ni taifa teule, na walipaswa kuwa wa kwanza kupokea faida ya injili na mahubiri yake.

**15:25 Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie**.

Hakati tamaa, bali anamsujudia na kumwabudu, akimsihi kumsaidia.

**15:26 Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa**.

Yesu hamdhalilishi huyo, akimsihi asaidiwe. Yesu alithibitisha ushupavu wa chuki za Kiyahudi. Yesu anaeleza tu mambo ya kawaida yanayotokea majumbani - chakula cha kawaida. Mbwa husubiri hata chakula kiwe kimekwisha, ndipo hula makombo. Katika kipindi hiki watoto (Wayahudi) wameshiba na mbwa (Mataifa) wangestahili kusubiri. Hakukwazwa na yale Yesu alimwambia, bali anaongeza maelezo yake katika hayo.

**15:27 Akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.**

Sasa anaonyesha imani kwa kutambua kwamba Yesu anaweza kufanya hivyo. Ameendelea kuomba kwa sababu ya imani yake kwa Yesu, na kwa sababu ya upendo wake kwa binti yake mdogo. Hakuweza kukata tamaa kwa sababu anajua kwamba mtu huyu ana uwezo wa kufanya jambo fulani kwake. Wakati chakula kinaliwa kunakuwa na makombo yanayodondoka mezani, na mbwa huyaokota. Alitambua kwamba Yesu alikuja kwa ajili ya Wayahudi, lakini asingeachilia makombo kuanguka kwa ajili yake? Imani hii ni kubwa!

**15:28 Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.**

Hapa kuna mfano mwingine ambao mtu ametajwa kuwa na "imani kubwa." Akida katika 8:10 alikuwa na imani kubwa na sasa mwanamke Mkananayo alikuwa na imani kubwa. Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba wote wawili ni Mataifa. Amezungumzia kuhusu "imani haba" katika 6:30; 8:26; 14:31; 16:8; 17:20; 21:21, na yote haya yanalenga kwa Wayahudi.

**15:29 Yesu akaondoka huko, akafika kando ya bahari ya Galilaya; akapanda mlimani, akaketi huko.**
**15:30 Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya**;

Hii ni sehemu ya saba ya uponyaji.

**15:31 Hata ule mkutano wakastaajabu, walipoona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli**.

Kizazi kipya kimeanzishwa na Yesu. Miujiza hii inadhihirisha kwamba Yesu kweli ni Masihi.

**15:32 Yesu akawaaita wanafunzi wake, akasema, Nawahurumia mkutano, kwa kuwa**

**yapata siku tatu wamekaa pamoja nami, wala hawana kitu cha kula, tena kuwaaga wakifunga sipendi, wasije wakazimia njiani.**

Nawahurumia - 9:36; 14:14; 15:32 (hapa); 18:27; 20:34. Kwa siku tatu watu wamemfuata Yesu, na hawana cha kula. Roho ya huruma ya Yesu isingeruhusu kuona wanateseka. Yesu ameahidi katika Math.6 mahitaji ya mtu ya kimwili Mungu atamjalia. Hapa yametolewa na mtumishi wa Mungu, Yesu.

**15:33 Wanafunzi wake wakamwaambia, Tupate wapi mikate mingi hapa nyikani, hata kushibisha mkutano mkuu namna hii**?

Kwa nini waliona mashaka baada ya kuwalisha 5,000? Kuna uwezekano mmoja kwamba wao wenyewe walishikwa na njaa hata kutarajia muujiza maalum kutendeka. Walikuwa wamezoelea usumbufu na kujitoa sadaka kuwa wanafunzi. "Tazama, sisi tumeviacha vitu vyote na kukufuata" - Lk.18:28.

**15:34 Yesu akawaambia, Mnayo mikate mingapi? Wakasema, Saba, na visamaki vichache,**
**15:35 Akawaambia, makutano waketi chini;**
**15:36 Akaitwaa ile mikate saba na visamaki, akashukuru akavimega, akawapa wanafunzi wake, nao wanafunzi wakawapa makutano**.

Yesu aliwaruhusu wanafunzi wagawe kwa kuwa walitaka kufanya hivyo, ingawa hawakutoa wao binafsi. Kuna furaha katika kushirikiana. Baadaye wangetoa wenyewe (kama ilivyo katika Mdo.20:35).

**Wakashukuru** = "wakabariki" lililotumika awali; wakimshukuru Mungu kwa ajili ya chakula.

**15:37 Waka wote wakashiba; wakayaokota masazo ya vipande vya mikate makanda saba, yamejaa.**

Kama ilivyo katika sura 14:20 watu 5,000, "wakala wote wakashiba." Kuna maana kiroho hapa. Mtu akimjia Yesu ili alishwe, atashibishwa. Hatahitaji zaidi na kutaka zaidi. Kuna kukamilika kabisa katika Kristo. Yesu alimwambia mwanamke Msamaria kwamba asingeona kiu kamwe.

**15:38 Nao waliokula walikuwa wanaume elfu nne, bila wanawake na watoto**.

Idadi iliyotolewa katika muujiza uliotendeka awali ni 5,000. Wanaeleza kuwa hili ni tatizo (synoptic problem) la waandishi wa maandiko wakitumia chimbuko moja kuandika, wanapata shinda kubwa kuelezea Mathayo akiandika kwanza 5,000 na baadaye 4,000. Mathayo anadhihirisha kwamba miujiza hii ilikuwa ya aina mbili tofauti.

**15:39 Akawaaga makutano, akapanda chomboni, akaenda pande za Magadani**.

Upande huu ni wa magharibi mwa Bahari ya Galilaya.

## SURA YA KUMI NA SITA

**16:1Wakamjia Mafarisayo na Masadukayo, wakimjaribu, wakamwomba awaonyeshe ishara itokayo mbinguni.**

Walimjia kwa lengo la kumtafutia makosa, misingi ya kumwua Yesu. Walitaka ishara **toka mbinguni**. Hii ni jambo la maana. Waliomba hapo mwanzo ishara, sasa wanaomba ishara iwapo

ingetoka kwa Mungu. Waliamini kuwa nguvu za giza haziwezi kuwepo mbinguni. Mioyo yao si sahihi, lakini hawataki kujifunza kitu chochote. Wanataka kumshitaki.

**16:2 Akajibu, akawaambia, [Kukiwa jioni, mwasema, kutakuwa na kianga; kwa maana mbingu ni nyekudu.**
**16:3 Na asubuhi, mwasema, Leo kutakuwa na dhoruba; kwa maana mbingu ni nyekundu, tena kumetanda. Enyi wanafiki, mwajua kuutambua uso wa mbingu; lakini, je! Ishara za zamani hizi hamwezi kuzitambua?] Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara; wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona. Akawaacha, akaenda zake**.

Waliweza kuelewa dalili za hali ya hewa, na kutabiri kwa usahihi nini kitatokea kwa masaa ishirini na nne na kadhalika. Lakini "ishara juu ya nyakati" ilikuwa kitu ambacho walishindwa kuelewa. Kwa nini wapewe ishara nyingine mpya wakati wanashindwa kuelewa zilizokuwa zikitendeka tayari? Kwa nini utende miujiza kwao hao asioweza kuelewa kusudi na maana ya miujiza?

**16:4 Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara; wala hakitapewa ishara, isipokuwa ishara ya Yona. Akawaacha, akaenda zake.**

Isipokuwa...ya Yona (Linga. 12:39-41). Walishakuwa wameona ishara za majira tayari. Iwapo walikuwa kweli wanatafuta ukweli, wangeweza kuona na kutambua ukweli. Tunaweza kusema sawasawa na siku hizi zetu. Sisi ni bora kutabiri hali ya hewa, lakini inatuwiwa vigumu kutambua ishara za mambo yanayoendelea baina yetu. Tunatakiwa kujiandaa zaidi kuona kichwa kibaya cha maovu kinapojiinua.

**16:5 Nao wanafunzi wakaenda hta ng'ambo, wakasahau kuchukua mikate.**
**16:6 Yesu akawaambia, Angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.**
**16:7 Wakabishana wao kwa wao, wakisema, Ni kwa sababu hatukuchukua mikate.**

Wanadhani kuwa Yesu anawaadhibu kwa kusahau kwao kubeba chakula.

**16:8 Naye Yesu akafahamu, akawaambia, Mbona mnabishana ninyi kwa ninyi, enyi wa imani chache, kwa sababu hamna mikate?**
**16:9 Hamjafahamu bado, wala hamkumbuki ile mikate mitano kwa wale elfu tano, na vikapu vingapi mlivyoviokota?**
**16:10 Wala ile mikate saba kwa elfu nne, na makanda mangapi mliyaokota?**
**16:11 Imekuwaje hamjafahamu ya kuwa si kwa sababu y mkate naliwaambia? Ila jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.**
**16:12 Ndipo walipofahamu ya kuwa hakuwaambia kujilinda na chachu ya mikate, bali mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.**

Ingawa hakusema kitu chochote tofauti, wakamwelewa sasa. Jinsi gani walifikia kuelewa haswa kutokana na alivyosema Yesu? Kwa sababu wanafikiria kiroho sasa na si katika vitu (kimwili). Wanaaza kuona sasa vitu kwa macho ya kiroho. Kusema kwamba mafundisho yalikuwa kama chachu inaonyesha kwamba Mafarisayo walikuwa na welevu mwingi hata kushutumiwa wazi wazi kwa mafundisho ya uongo. Walifundisha mafundisho ambayo taratibu yaliweza kuelekeza katika maangamizi; wakaikengeusha jamii taratibu na kuwapeleka watu kuhukumiwa. Math.23:3 "...basi, yo yote watajayowaambia, myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende." Lk.12:1 ni fungu linalolingana, lakini chachu hapo ni unafiki wa Mafarisayo. Watu wanapaswa kuwa makini kuelewa ushawishi wa mvuto na kupenyeza kwa kama hawa. Ni watu wenye nguvu nyingi!

**16:13 Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafuzi wake akasema, Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani**?

Hili limekuwa swali la msingi linaloulizwa wakati wote. Watu wanasemaje, siyo waandishi na Mafarisayo.

Maoni aina nne yametolewa.
1. **Yohana Mbatizaji**. 14:2 Herode alifikiria hivyo.

2. **Eliya**. Mal.4:5,6 aliahidi kuja kwake (Mk.6:15, Lk.9:8). Agano la Kale lilifundisha kwamba Eliya angekuwa ni nabii wa kutayarisha mapito ya Masihi.

3. **Yeremia**. Katika maandishi ya Apokrifa (Apocrypha) yanaonyesha kwamba mtu atakaye itayarisha njia ya Masihi atakuwa Isaya au Yeremia. Ndiyo sababu wametajwa hapa. Waliandika kipindi cha katikati ya Maagano walisema kwamba angekuwa Isaya au Yeremia (linga. 1 Maka.14:41). Ni wazi kutoka kwa Josephus kwamba vitabu hivyo hazikutaliwa kama GRAPHE (maandishi yasiyovuviwa, maandiko), bali yalikuwa muhimu kwa Wayahudi, na yalisomwa zaidi kama vitabu vya ibada.

4. Ama mmoja wa manabii. Maelezo sawa na yale ya Isaya au Yeremia. Uvumi mkubwa ulioenea hakumtaja Yesu kama Masihi.

**16:14 Wakasema, Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii.**
**16:15 Akawaambia, nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?**

Swali lingine la kuchoma moyo. Je, NINYI mnasemaje? Wanafunzi walikuwa naye kwa muda wa kutosha. Ikiwa walikuwa waaminifu wangetoa hatimisho sahihi. (Na kama sisi, wasomaji, tungekuwa waaminifu, tungeliweza pia kiusahihi kujibu swali hilo).

**16:16 Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai**.

Petro alikuwa na maana gani aliposema kwamba, “Wewe ni Kristo?” Alimwamini Yesu kuwa Masihi, mpakwa mafuta. Ni yule ambaye ametajwa kama Mungu Mfalme. “Wewe ni Kristo” ni kukiri kwa msingi haswa. Lakini Petro aliendelea, “Mwana wa Mungu aliye hai.” Petro anamtaja zaidi ya maoni yaliyovuma kumweleza uungu wa Yesu. Amekuwa akifikiri, na amefikia hatimisho ambalo halipingiki kwamba Yesu lazima ni Mwana wa Mungu.

Petro amekiri kwa namna mbili: Yesu ni Kristo (akirejea *ofisi* yake), na kuwa ni Mwana wa Mungu (anarejea katika *uungu* wake).

**16:17 Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damua havikukufunulia hili; bali Baba yangu aliye mbinguni**.

**Simon Bar-yona**. “Simoni ni jina lingine kwa “Petro.” Bar-yona maana yake mwana wa Yonas (au Yona) ambalo lilikuwa jina la baba yake Petro.

**Kwa kuwa mwili na damu...mbinguni**. Petro hakuwa na maono ya kimuujiza au hakuvuviwa kusema maneno haya. Petro alifanya ambacho waandishi na Mafarisayo hawakufanya. Hawakutambua dalili za majira. Mungu alikuwa akitoa ujumbwa kwa watu, akifunua jinsi alivyo kwa mafundisho na miujiza, na Petro akaona na kuelewa. Yoh.5:36 Mungu alitenda miujiza kupitia Kristo, hiyo ingelimwezesha Petro kufahamu kuwa Yesu alikuwa nani.

**Heri wewe**. Yesu hamwinui Petro kuliko wanafunzi wengine. Ni yeye tu aliyetangulia kusema kwanza; anauhusiano sahihi na Mungu kwa kuwa ameweza kutambua ujumbe wa Mungu. Petro alikuwa mwenye ujasiri wa kwenda mbele na kusema, na Yesu amependezwa na hilo.

**16:18 Nami nakwambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanis langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda**.

**PETRO** = *petros* = jiwe au changarawe.
JUU YA **MWAMBA** HUU - *petra*. Hii inamaanisha msingi mkubwa wa mawe wenye eneo kubwa. Math.7:24 mtu mwenye busara anajenga nyumba yake juu ya "petra," na si juu ya "petro." "Mwamba" ni ukiri aliofanya Petro, na wala si Petro mwenyewe. Kwa mamlaka gani Yesu atajenga kanisa lake? Ukweli wa kwamba yeye ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Hayo ndiyo yanampatia sifa za kujenga kanisa. Hiyo ndiyo sababu hakuna mwenye haki ya kujenga kanisa. Kukiri kunadhihirisha mamlaka ya Yesu. Kwa kuwa yeye ni Kristo na Mwana, ana haki. Msingi wa hili ni juu ya kile kilitamkwa, na wala si kanisa lijengwe juu ya Petro.

**NITALIJENGA** = Lingejengwa na Yesu na wala si mwingine yeyote yule.

**KANISA LANGU** = "ekklesia" = "walioitwa kutoka." Inachukua maana ya kikundi, kukusanyika, au mkutano. Yesu anatumia maneno ya kawaida ya kukusanyika kwa watu. (Linga. Matendo 19:41 ambapo mkutano -  au kundi - liliondoka). Neno la Kiebrania ni *kahal*, hii ni *ekklesia*; halina maana zaidi ya kundi la watu. Yesu anasema, "Nitalijenga kundi ama kusanyiko **LANGU**." Imani katika Yesu inatufanya sisi kuwa kikundi, vinginevyo tungetawanyika. 1 Kor. 3:11 - hakuna msingi mwingine isipokuwa Kristo. Yesu atakuwa na kundi lake mwenyewe, na atakuwa ndiye anayetuunganisha kuwa pamoja.

**WALA MILANGO YA KUZIMU HAITALISHINDA**.

**Kuzimu** = nguvu ya kifo au chini ya ardhi. Milango inahatimisha picha yenyewe. Mtu anapokufa anapita "milango" ya mauti, hawezi kamwe kurejea. Anachokwenda kufanya Yesu hakuna cha kuzuia. Kuna tafsiri aina tatu zinazorejea maana ya "haita-li-shinda" - (it).

1. Anahusu kanisa. Kama hivyo ndiyo maana yake, basiu kanisa haliwezi kutoweka kamwe. Linga. Dan.2:44. Tatizo la tafsiri hii ni kwamba Yesu anatumia neno la Kiyunani la kati (neuter) "it." Ikiwa alikuwa alikuwa anarejea kanisa angelitumia jinsia ya kike (her) kwa kuwa kanisa (ekklesia) ni neno la jinsia ya kike na ni "bibi arusi wa Kristo" (Efe.5:23ff).

2. Anajihusisha mwenyewe. Ikiwa inamaanisah hivi, hivyo Yesu anamaanisha kwamba ingawa atakufa, milango y kuzimu haitaweza kumzuia. Ataishi tena. Tatizo la hili ni kwamba Yesu anatumia neno la Kiyunani la kati (neuter) "haita-li-shinda" (it), baadala ya kiwakilishi cha mtu "haita-ni-shinda" (me) - milango ya kuzimu haitanishinda mimi.

3. Anarejea katika mpango wake. Yesu mara kwa mara ameyataja mahubiri yake juu ya ufalme kama kitu (it) (Kiyunani - neuter. Linga. Math.12:6,41,42). Hakuna kitu cha kuzuia kuanzishwa kwa ufalme wake.

**16:19 Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, liatakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.**

Kwa Petro, na pekee kwa Petro, Yesu anasema atampa "ufunguo wa ufalme." Ufunguo umetumika kufungulia mlango wa kitu fulani. Atakuwa na funguo za kufungulia mlango wa

ufalme wa mbinguni, kanisa. Petro alifanya hivi katika Mdo.2:38ff alipohubiri hotuba ya kwanza ya injili. Ilikuwa ni hotuba hiyo iliyofungua mlango kuruhusu watu kuingia ndani ya kanisa la Kristo. Kumbuka: Mungu aliwazidisha katika familia iliyookolewa, na wala si Petro (Mdo.2:47). Ufu.1:18; 3:7 Yesu ndiye mwenye funguo. Anashikila funguo tangu mwanzo. Lakini atamwachia Petro kwa kuwa Yesu anakwenda kwa Baba. (Angalia pia Math.18:18 kama fungu linalolingana na maneno ya mwisho ya mst. 19).

**Na lolote utakalolifunga**. Hapa kuna mfano wa faida ya kufahamu lugha ya Kiyunani ngawa kidogo kunaweza kuwa msaada sana. Katoliki inadai kwamba Yesu alimpatia Petro mamlaka yote. Ndiyo mahali wanapata mawazo ya "upapa." Lakini matumizi ya wakati wa maneno hayo, ni kwamba Petro anakwenda kufanya jambo fulani ambalo *tayari limeshatendeka*. "Litakuwa limefungwa." Wakati uliotumika katika Kiyunani ni "wakati timilifu." Petro angelifunua yale ambayo tayari yalifunuliwa mbinguni. Anafungua yale ambayo Mungu amekwisha kuamuru, na wala si kuanzisha jambo jipya. Kulingana na Efe.3 na 1 Pettro haya yalitendeka tangu kuumbwa misingi ya ulimwengu. Hili linaonyesha kwamba katika mpango wa Mungu kuna mambo yaliyofungwa kwa ajili ya wanadamu. Ikiwa walitaka kumpendeza Mungu hivyo ingewalazimu kupatana na mambo hayo. Pia, kungelikuwa na mambo ambayo "yafunguliwa" (mambo ambayo watu hawaruhusiwi kutenda: kutoa dhabihu, kufukiza uvumba, kusafiri kwenda Yerusalem, kutunza Sheria za Sabato, n.k. - Sheria ya Musa). Yesu anarudia maneno haya katika Math.18:18, akiwapa mamlaka kwa mitume wote. 1 Yoh.4 Yohana anazungumzia mamlaka ya mitume. Tunawajibika kwa kutii yale waliyofundisha mitume.

**16:20 Ndipo alipowakataza sana wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote ya kwamba yeye ndiye Kristo**.

Kufikia hapa, watu wangekuwa na fikra potofu. Anataka kuwaeleza kwa wakati wake binafsi. Wanafunzi wanatakiwa wakue katika ufahamu wao binafsi wenyewe juu ya Yesu kuwa ni Kristo. Linga. Mdo.1:6 "Je! Bwana, wakati huu ndipo unawarudishia Israeli ufalme ?" Walikuwa bado wangali hawaelewi kikamilifu, kwa wakati huu, kwamba yeye ni Kristo isingelikuwa wazo nzuri.

**16:21 Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalem, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, siku ya tatu kufufuka**.

**Tangu wakati huo**. Baada ya kukiri kwake Petro, Yesu anasisitiza mateso yajayo. Kama wanafunzi wanaamini Yesu kuwa ni Kristo, ndipo wanatakiwa wamwachie awafundishe juu ya mpango wa milele wa Mungu. Mpango huo ulikuwa mateso na kifo cha Kristo. Hivyo tunaona kuongezeka kwa "mateso" katika mafungu haya. Kuna angalau mafungu ya mateso kumi na mbili maalumu kutoka hapa hadi kusulibiwa.

**Na kuuawa**. Walikuwa na maoni juu ya "mateso ya Masihi." Walifikiria katika mtazamo wa kiongozi mwenye nguvu, Masihi mwenye jeshi hodari. Kama wangeelewa vema Isa.53, wangeelewa maana hasa ya kiongozi mwenye mateso.

**16:22 Petro akamchukua, akaanza kukumkemea, akisema, Hasha, Bwana, hayo hayatakupata**.

Tena Petro mwenye harara anasimama mbele. Inaonekana anafikiri anachosema Yesu ni kama maneno ya kuvunja moyo na akionyesha uwezekano wa kushindwa. Petro anasema, "Hasha, Bwana, hayo hayatakupata!" Petro anataka Yesu atambue kwamba yeye na wengine watapambana kwa ajili yake. Hawataki Yesu auawe!

**16:23 Akageuka, akamwambia Petro, Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawaazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.**

Petro alikuwa amejitoa wakfu, Myahudi kitaifa na anayenuia kupingana kwa ajili ya kiongozi wake. Katika kumwita "Shetani" Yesu anamaanisha ni adui wa Mungu, akipinga mpango mtakatifu wa Mungu kwa ajili ya kanisa.

**U kikwazo kwangu** = utanizuia nisifanye kilichonileta nifanye. Yesu anajua kusudi lake. Yeye ni Mwana kondoo wa Mungu, na ni lazima afe.

**16:24 Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate**.

Msitari huu ni kati ya mistari ambayo watu wanashindwa kuelewa. Yesu anafundisha somo muhimu sana. Ikiwa yeye ni Kristo, na watu wanaamini kweli kuwa ndiye, ndipo wanapaswa kujifunza kwamba yeye ni lazima atawale. Ndiye mwenye kuongoza na kulinda. Huu ni ufunguo wa "sehemu inayofuata" katika kitabu cha Mathayo. (Hii ni sehemu ya pili inayofuata. Sehemu ya kwanza ilikuwa katika Math.8:18-22).

*Kuna hatua nne ili ufanyike mwanafunzi*:

1. "**Mtu ye yote akitaka kunifuata**" - Hili linamaanisha nia, matakwa. Ni mambo ya kudhamiria, kuamua kwamba hili ndilo nitakalofanya.

2. **Ajikane mwenyewe** hufuata nia. Ni kujifunza kusema hapana kwa ushawishi mkubwa kwa mambo ya dunia. Kujikana "mwenyewe." Ikiwa unataka kumfuata Yesu ni lazima uishinde nafsi yako. Hili ni jambo gumu kulifanya, wakati wowote ule katika jamii yoyote ile. Kwa nini? Kwa sababu mara nyingi tunapenda kujitumikia wenyewe. Gal.2:20 - "Nimesulibiwa na Kristo...bali Kristo yu hai ndani yangu." Paulo anasema kwamba anatakiwa afanyike upya, au ajiumbe upya katika Kristo katika mwili wake. Kila kitu alitaka, au angependa kufanya kama Yesu asingependa afanye, alikuwa aliondoe katika maishani yake - kujikana mwenyewe. Hicho ndicho Yesu anachosema, ujikane mwenyewe. Katika sura 8 tumejadili kuweka vipaumbele na kuhesabu gharama katika kumfuata Yesu. Hii ndiyo hatua ya kwanza - kujikana mwenyewe na kumweka Yesu namba moja katika maisha yetu.

3. Chukua msalaba wako = ukihesabu gharama. Msalaba ni adhabu yenye maumivu, mateso, na kifo. Kitenzi "jitwike." Unabeba msalaba wako. Ni jambo la kunuia; kwa kukusudia kuuchukua msalaba, ukiamua binafsi, na kuuchukua mzigo ambao unatambua kwamba utasababisha kuteswa. 2 Tim.3:12 panasema tutaudhiwa. Tunapoamua kumfuata Yesu tunapaswa kuhesabu gharama, na gharama hiyo inaweza kuwa mateso, maumivu na pengine, hata kifo. Lk.9:23 anaongeza neno "kila siku." Ajitwike msalaba wake mwenyewe kila siku; ni kitu cha kila siku. Paulo anasema katika Rum.12:1,2 tunapaswa kuwa dhabihu iliyo hai. Ajitwike msalaba WAKE. Kila mtu anao wake mwenyewe. Hatubebi msalaba kwa pamoja. Kila mwanafunzi ana msalaba wake wa kubeba, na tunatakiwa kujitwika (linga. Gal.6:5).

4. **Nifuate**. Kuna wanaoudhiwa kwa ajili ya Yesu, lakini si katika njia ile ambayo Yesu anataka. Ni sharti watu wamfuate Yesu kulingana na maagizo yake katika injili. Mtu amfuate yeyey katika njia zake, na katika maelekezo yake. "Kufuata" ni neno la ufunguo katika injili ya Mathayo. Watu wanaweza kumfuata Yesu kimwili kutoka mahali fulani hadi nyingine, lakini mfuasi haswa wa Yesu ni yule anayekwenda sawasawa na Yesu anavyomwongoza. Siku hizi Yesu anatuongoza tuwe sehemu ya kanisa lake, kuwa waaminifu, na kuwaleta wengine kwake.

**16:25 Kwa kuwa mtu atakayeiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona**.

Ikiwa mtu anataka kuwa maisha "bora" - ya faraja, salama, rahisi - hivyo atapoteza nafsi yake ... maisha hayo yote ni *mazuri* (linga. 10:39). Mtu akifanya kazi ngumu kutafuta vitu anaweza kufanikiwa. Lakini Yesu anasema kwamba vitu vya dunia siyo ndiyo maisha hasa. Wafuasi wa Yesu na wanao tanguliza yeye na kuona mbingu kuwa matazamio yao watapata maisha haswa na yale yajayo.

**Kwa ajili yangu**. Hili ni ufunguo. Watu wengi wamejitoa maisha yao kwa ajili ya mambo ya dunia, lakini hakuna sababu kubwa zaidi ya ile ya Mungu. Hakuna sababu nyingine yoyote inayotoa thawabu iliyo bora kuliko hii. Faida zitokazo kwa Mungu "ziko nje na za ulimwengu huu!"

**16:26 Kwani atamfaidia nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake**?

Hapa tunapata msaada wa kueleza mst.25. Anazungumzia kuhusu mtu anayejitahidi kuokoa maisha yake kwa ajili ya mali. Je, mtu itamfaidia nini ikiwa amefanikiwa mali nyingi hata ulimwengu mzima kuwa wake? Ebu fikiria kwamba mtu ana kila kitu. Kuna thamani gani ya vitu vyote badala ya nafsi yake? Hii ni swali la kushangaza, hasa kwa Myahudi ambaye anatarajia ufalme wa duniani. Na pia ni maoni ya nguvu kwetu sisi kwa sababu ya "tamaa ya fedha" jamii tunayoishi ndani. Nafsi ina thamani zaidi kuliko kitu kingine chochote alichonacho mwanadamu (na amepata hiyo bure kutoka kwa Mungu). Wanadamu wanafanya vitu vingi vya upuuzi kulinda mali zao, lakini hawafanyi lolote juu ya nafsi zao zilizo na thamani kubwa zaidi.

**Mtu atatoa nini badala ya nafsi yake**? Jibu ni, kwa karaha, kidogo sana, katika vitu vya ulimwengu tunamosishi. Watu wengine wanapoteza nafsi zao kwa vitu vyenye thamani yoyote ile. Musa alikuwa ni mmoja ambaye hakupenda kujifurahisha kwa dhambi za kitambo. Lakini alikuwa mtu alivumilia mateso ya taifa lake kwa maana alitazamia thawabu iliyokuwa mbele - Ebr.11:24-26. Tunapaswa kuwa na tabia kama ya Musa. Ikiwa mtu anaamini kuwa dhambi huleta hukumu, na kwamba mtu atakwenda jehanamu kwa yale katika Ufu.20:8 yametajwa, hivyo basi kwa kusema uongo anapoteza nafsi yake. Kutoa nafsi yako kwa ajili ya vitu kama hivyo??? Ni jambo la upumbavu kufanya hivyo! Tunapaswa kuelewa ni nini kilicho na thamani zaidi!

**16:27 Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake**.

Hakuna shaka kabisa kuhusu hili, atarudi tena! Na, akisha rudi, atakuja na utukufu wa Baba yake. Wakati huo ni wa kuona kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi wake. Baba atamtukuza wakati huo kuliko wakati mwingine wowote ule! Waliona shaka wote, wasioamini, na wasiotii watamwona kama Paulo alivyosema katika Fili.2:10 - "Kila goti lipigwe, na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba."

**Malaika** = wavunaji katika mfano wa magugu. Angalia pia 25:31; 1 Thes.4:13-18; 2 Thes.1:7-9. Malaika watawajibika ipasavyo siku ya hukumu.

**Kwa kadiri ya matendo yake**. Huu ndio msingi wa hukumu. Wazo la kulipiza kisasi lina maana ya "kufidia." (Linga. Rum.2:6; 2 Kor.5:10; Ufu.20:12; Yoh.5:28, 29). Mtu anachofanya ndicho kitakuwa kipimo cha kuhukumiwa. Ikiwa alijaribu kuupata ulimwengu wote hivyo atalipwa na hicho alichotenda.

**16:28 Amin, nawaambieni, Pana watu wasimamao hapa, ambao hawataoja mauti kabisa, hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake**,

Yesu anazungumzia kuja kwake kuhukumu, siku ya hukumu, mwisho wa dunia. Wangali bado wakifikiria kuhusu ufalme wa ulimwenguni wa Masihi. Hivyo basi atawapatia maelezo fulani kuhusu ufalme. Anasema wengine watakuwa wakiishi wakati ufalme utakapowasili (Mk.9:1). Wengine hawataonja mauti hata watakapouona ufalme ukija **kwa nguvu**. Linganisha hili na Mdo.1:8 mitume wakipokea nguvu kutoka kwa Roho Mtakatifu. Maelezo haya yametolewa kujibu swali, "Je! Bwana, wakati huu ndipo unawarudishia Israeli ufalme?" Tafadhali zingatia:
1. Wengine hawatakufa hata wauone ufalme ukija, na ufalme utashuka na nguvu, Mk.9:1.

2. Nguvu zilishuka wakati Roho Mtakatifu alishuka, Mdo.1:8.

3. Roho Mtakatifu alishuka siku ya Pentekoste, Mdo.2:4.

4. Kwa hiyo, ufalme uliwadia siku ya Pentekoste. Wale Yesu alikuwa akizungumza nao walikuwa wangali, kwa hakika, bado wanaishi siku ya Pentekoste ilipowadia (wanafunzi, kwa mfano).

Haya yanarejea nyuma katika ukweli wa mst. 18 kwamba Petro alikuwa na ufunguo wa ufalme. Wanafunzi hawakuelewa kamwe maana hasa ya hili hata baadaye walipopokea nguvu toka kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste.

## SURA 17

**17:1 Na baada ya siku sita Yesu akawatwa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu mlima mrefu faraghani**;

Aliwachukua wavuvi watatu pamoja naye. Hawa watatu walikuwa viongozi kwa mitume, haswa uhusiano wa karibu zaidi baina ya wanafunzi, marafiki wa karibu wa Yesu.

**17:2 Akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru**.

Neno "akageuka sura" ni neno tunalopata kutoka kwa "metamorphosis." Yesu "akabadilika" umbo. Tunapata mabadiliko tunapofanyika kuwa Wakristo - Rum.12:1, 2. Akili zetu zinapitia mabadiliko.

1. Sura yake ikang'aa kama jua, na
2. Mavazi yake yakawa meupe kama nuru.

Nuru ya ajabu iliangaza toka kwa Yesu. Dan.7:13, 14 inaonyesha maana ya hili linaloongelewa hapa. Yesu ni kiumbe wa mbinguni amejitokeza katika utukufu katika Dan.7.

**17:3 Na tazama, wakatokea Musa na Eliya, wakizungumza naye.**
**17:4 Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa; ukitaka, nitafanya hapa vibanda vitatu, kimoja chako wewe , na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya**.

Katika nia yake ya kujenga mahema matatu matakatifu (maskani), anataka kuwalinganisha wote watatu. Tayari alikuwa amekiri Yesu kuwa ni Kristo, lakini sasa anataka kumweka yeye sawasawa na Musa na Eliya. Anakosa ufahamu wa kutosha wa maana ya Yesu.

**17:5 Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.**

Mungu anaingilia kati kabla ya Petro hajamaaliza kusema. Katika Math.3:17, Yesu alipobatizwa, Mungu akanena maneno kama haya - "ninapendezwa naye." Wala si Musa au Eliya aliye Mwana wa Mungu mpendwa. Mungu anasema, "Msikilizeni yeye" - Yesu.

Agano la Kale limegawanyika katika makundi makuu mawili:

1. Sheria - Musa, na

2. Manabii - Eliya.

Wawili hawa wamejitokeza kwa Yesu, lakini tunapaswa kumsikiliza yeye - Yesu, na siyo Musa au Eliya. Yoh.1:1 Yesu ni Neno, Logos. Ebr.1:1,2 - Mungu sasa anazungumza nasi kupitia Mwanawe. Yesu ndiye tunapaswa kumsikiliza, "Mwanangu mpendwa wangu." Jambo hili ni la kufurahisha kwa wanafunzi, kama Petro anavyolizungumza katika 2Pet.1:16, 17. Walikuwa mashahidi wa tukio hili la kustaajabisha la kugeuka sura (linga. 1 Yoh.1-3). Petro anatumia hilo kuthibitisha kwamba injili haikutungwa kwa werevu kama hadithi.

Mungu mara tatu amezungumza kutoka mbinguni:

1. Math.3:17 katika ubatizo,
2. Math.17:5 wakati alipojigeuka sura, na
3. Yoh.12:28 ulitukuze jina lake, nami nitalitukuza tena.

Angalia katika Zab.2:7, tumejadili haya katika Math.3:17. Alipakwa mafuta ndiye aliye Mwana mpendwa. Hili ni fungu la Masihi la wazi. Petro alimkiri Yesu kuwa Mwana wa Mungu, na Mungu akathibitisha kwa kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu."

**17:6 Na wale wanafunzi waliposikia, wakaanguka kifulifuli, wakaongopa sana**.

Jambo hili linafanana sana na mtu akiwa na maono ya mbinguni au anakabiliana na tukio la kimuujiza. Danieli , Ezekieli, na Yohana (Ufu. 1) walifanya vivyo hivyo walipoona utukufu wa Mungu.

**17:7 Yesu akaja, akawagusa, akasema, Inukeni, wla msiogope**.

Katika Math.14:27 aliwaeleza wasiogope. Yesu hataki mtu awe mwoga. Yesu hataki mtu awe mwonga, bali kujifunza kumtumaini yeye.

**17:8 Wakainua macho yao, wasione mtu ila Yesu peke yake**.

Hawaonekani tena Musa na Eliya. Pana mmoja tu anayetazamwa sasa na mtu huyo ni Yesu. Yeye ndiye pekee walipaswa (tunapaswa) kumtazama. Fungu linatia mkazo kusema kwamba pale alibakia yeye tu. Kumb.18:15 ni unabii kuhusu "nabii kwa mfano wa Musa." Ni jinsi gani walitambua kwamba hao walikuwa Musa na Eliya? Fungu hili halionyeshi jinsi.

**17:9 Na walipokuwa wakishuka kutoka mlimani, Yesu aliwaagiza, akasema, msimwambie mtu ye yote habari ya maono hayo, hata Mwana wa Adamu atakafufuka katika wafu**.

Mwana wa Adamu ni neno analolitumia Yesu mwenyewe - Dan.7:13. Inathibitisha kwamba atakufa na kufufuka. Hili ni fungu la mateso # mbili.

**17:10 Wanafunzi wake wanamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza**?

Kwa nini wanamwuliza swali hili? Walikuwa wamekwisha kumwona Eliya! Waandishi walionukuu maandiko ya Agano la Kale, hasa Mal.4:5, wangeelewa kwamba Eliya angekuja. Pengine walidhania kuwa kutokea kwa Eliya kulitimiza unabii huu.

**17:11 Naye akajibu, akawaambia, Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote**,

Yesu anamaanisha nini anaposema, "Atatengeneza yote?" Yohana Mbatizaji alimtengenezea mapito Yesu, akiwaandaa watu, na akirejeza haki ili kwamba watu wawe tayari kumpokea Masihi. Yesu haonyeshi "atatengeneza yote" kuwa anahusisha nini, bali kila jambo alilofanya Yohana, alirejeza "mambo yote."

**17:12 Ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtabue, lakini wakamtenda yote waliyotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye yuaenda kuteswa kwao.**

Anasema Eliya amekwisha kuja - wakati uliopita. Yohana alikuwa akiwa na roho na uwezo wa Eliya, na watu wakamtendea wanavyotaka na kisha kumwua.

Hili ni fungu la mateso # la tatu. Mwana wa Adamu atateseka pia mikononi mwao, na kisha kuuawa.

**17:13 Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji**.

Math.11:14 panadai kuwa Yohana alikuwa Eliya.

**17:14 Nao walipoufikia mkutano, mtu mmoja akamjia, akampigia magoti, akisema,**
**17:15 Bwana, umrehemu mwanangu, kwa kuwa anakifafa, na kuteswa vibaya; maana mara nyingi huanguka motoni, na mara nyingi majini**.

Neno rehema kwa mara nyingine tena. Kuna fungu linalolingana katika Mk.9:14-28. Hii ni moja ya hali ambapo mioyo ya wazazi wote huwatoka kama mzazi huyu. Mwanawe ni mgonjwa, isitoshe hilo, lakini ukweli wa kwamba mtoto ameendelea kupata mateso katika maisha kufikia hali ngumu. Mk.9 panaonyesha bayana kwamba ni kupagawa na pepo. Imetokea (mara kwa mara) akitupwa motoni na hata majini.

**17:16 Nikamleta kwa wanafunzi wako, wasiweze kumponya**.

Katika sura 10 wanafunzi wana uweza kuponya na kukemea pepo. Walikuwa na mamlaka juu ya pepo wabaya. Walifanikiwa hapo awali kukemea pepo, lakini sasa hawawezi kufanya hivyo. Yesu amekasirishwa kwa namna fulani.

**17:17 Yesu akajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoja nanyi hata lini? Nitachukulina nanyi hata lini? Mleteni huku kwangu**.

Yesu ana muda mchache na anatambua hilo. Ni jambo la maana kuona kwamba watu wakue na kuwa na nguvu katika imani zao. Anawataka wawe na imani kuu kabla hajawaacha. Wanafunzi

hawakuwa na imani ya kutosha kufanikiwa kumtoa pepo huyo hapo mwanzo, kama alivyoelezea katika mst.20.

**17:18 Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile.**

Hapo awali Mathayo hakutaja kuwa mtoto alipagawa na pepo, lakini sasa anathibitisha hilo. Lisilowezekana kwa wanafunzi kufanya ni rahisi kwa Yesu.

**17:19 Kisha wale wanafunzi wakamwendea Yesu kwa faragha wakasema, Mbona sisi hatukuweza kumtoa**?
**17:20 Yesu akawaambia, Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauwambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka; wala halitakuwepo neno lisilowezekana kwenu**.

Angalia tena "uhaba" wa imani yao inapingana na "imani kubwa" katika injili. Imani kuu ilikuwa ndani ya watu waliomwamini Yesu iliweza kuponya hata umbali mrefu (kama akida katika sura 8). Wanafunzi wanaamini kuwa Yesu alikuwa ni Kristo, na akakua katika imani hiyo.

**Mbegu ya haridali...ondoka hapa uende kule;...wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu**. Imani yao haikufikia kiwango kinacho hitajika. Linatofautiana hili na Mdo.16:16. Paulo alimtambua Mwana wa Adamu. Hakuwa na mashaka kabisa. Wanafunzi walipaswa kuzidi katika imani. Yesu anazungumza katika kutia mkazo, ya kwamba hakuna muujiza ambao ungetendwa bila kutimiza lengo lake. Hivyo kungekuwa na kusudi gani la kuhamisha mlima katika kumthibitisha mtu na ujumbe wake? Uwezo waliokuwa nao ni mkubwa - hivyo kikubwa i wangeuambia mlima "ung'oke" na ingetokea. Lakini si nia ya Yesu kuwa wahamishe milima. Isingetekeleza kusudi lake. Kutakuwa na watu watakao hubiri injili, na wakati pekee Mungu ataruhusu miujiza kuingilia kati katika utendaji wake mwanadamu ni kuthibitisha ujumbe. Hatuhusiki sisi siku za leo, kwa sababu kipindi hicho kilipita.

**17:21 [Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga.**]

Maandishi mengi ya kale hayana msitari huu. Inawezekana haikuwepo katika sehemu ya injili ya Mathayo.

**17:22 Nao walipokuwa wakikaa Galilaya, Yesu akawaambia, Mwana wa Adamu anakwenda kutiwa katika mikono ya watu, nao watamwua, na siku ya tatu atafufuka.**
**17:23 Wakasikitika sana**.

Hii ni fungu la mateso # nne. Pia, msitari 22 ni mwanzo wa mahubiri ya sehemu ya nne ambayo inaendelea hadi sura 18. Jinsi walivyojibu sasa si kama walivyojibu katika sura 16. Wamehuzunishwa na jinsi walivyoambiwa.

Huzuni yao inawezekana kuwa ilitokana na:
1. Upendo wa kumpenda Yesu uliongezeka
2. Kifo chake kingeliwaondolea matumaini yao ya ufalme wa duniani. Iwapo angeuawa asingewaongoza kushinda mapambano baina ya waliodharauliwa Warumi. Ingawa anasema angefufuka siku ya tatu, bado walihuzunika. Hawakuelewa maana hasa ya mpango wa Mungu.

**17:24 Hata walipofika Kapernaumu, wale watozao nusu-shekeli walimwendea Petro, wakasema, je! Mwalimu wenu hatoi nusu-shekeli? Akasema hutoa**.

Sheria ya Musa ilimtaka kila mwanamume wa umri wa miaka ishirini na zaidi kusaidia hekalu kwa kutoa kodi hiyo ya mwaka (Kuto.30:13; 38:26).

**17:25 Naye alipoingia nyumbani, Yesu alitangulia kumwuliza, akisema, Waonaje, Simoni? Wafalme wa dunia hutwaa kodi au ushuru kwa watu gani? Kwa wana wao au kwa wageni**?

Yesu ghafla alianza kuzungumzia ushuru huu pamoja na Petro kabla hata hajapata fursa ya kuzungumza na wakusanyaji wa ushuru.

**17:26 Naye aliposema, Kwa wageni, Yesu alimwambia, Basi, kanma ni hivyo, wana ni mahuru**.

Hekalu palikuwa mahali Mungu (pa mfalme) anapokaa. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu (mfalme), kwa hiyo walikuwa hawapaswi kulipa kodi. Watu wa familia ya Mungu (mfalme) walikuwa pia wasilipe kodi. Wanafunzi hawa walikuwa wana kwa kukununuliwa, pia walikuwa pia wasitoe kodi. Lakini, kushindwa kulipa kungesababisha ahesabiwe mkaidi.

**17:27 Lakini tusije tukawakwanza, enenda baharini ukatupe ndoana, ukatwaye samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake utaona shekeli; ichukue hiyo ukawape kwa ajili yangu na kwa ajili yako**.

Tukawakwaza, k.m. kuwasabisha wajikwae. Ushuru wa hekalu ulikuwa nusu shekeli kwa mtu. Josephus, Antiquities, 18:312 anataja ushuru huu. Shekeli ilikuwa na thamani ya kama shilingi nne. "Utaona shekeli." Ni majaliwa ya jinsi gani hayo! Hicho ndicho kiwango kilichotakiwa kwa ajili ya Petro na Yesu.

Angalia: Yesu hataki kuwakwaza. Hili ni fungu zuri kwao wanaotaka kusisitiza juu ya uhuru wa "Ukristo." Wanadai kwamba katika "Katika Kristo tuna haki na uhuru." Yesu angeliweza kusimamia haki yake na kusema, "Siendi kulipa." Bali hakutaka kusimama juu ya haki yake. Alipendezwa zaidi katika kuwashawishi watu wengine. Alikuwa hapendi kusababisha makwazo. Wakristo wanapaswa waache "haki" zao (kwa mfano, kula chakula katika Rum.14) kwa ajili ya wengine.

## SURA 18

**18:1 Saa hiyo wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema,**

Wanafunzi walikuwa wakiutazamia bado ufalme wa uliwenguni. Kwa kukiri kwake Petro katika sura ya 16, na kujigeuza katika sura ya 17, ni jambo la msingi kwamba mazungumzo ya aina hii yangelijitokeza baina yao.

**18:2 Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao,**

**Mtoto** = *paidia*. Mtoto huyu ametumika kama mfano.

**18:3 Akasema, Amini, nawaambia, msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.**

Yesu anatilia mkazo roho ya unyenyekevu aliyonayo mtoto, mtoto anayeacha mapenzi yake, na kutii ya wazazi wake.

**18:4 Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni**.

**Ajinyenyekeshaye** = kutii mapenzi ya mtu mwingine. Wafuasi wa Mungu huacha mapenzi yao wakitii mamlaka ya Mungu. Huu ni ubinadamu unaopinga kiburi, na unatofautiana kabisa na tabia waliyoitafuta wanafunzi, kila mmoja akitamani kuwa mkubwa katika ufalme. 1 Pet.5:6 "Nyenyekeeni...ili awekweze kwa wakati wake."

**Aliye mkuu katika ufalme wangu**. Ni jinsi gani mtu **mkubwa** unatokana na kuwa na "tabia ya utumishi." Ufalme wa mbinguni hapa unahusu utawala wote wa Mungu na wala si kuhusu kanisa.

**18:5 Na ye yote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa jina langu, anipokea mimi**;

Mapema hili alilitumia kwa wanafunzi wake (10:40), na sasa anataja mtoto. Katika Math.25:35-40 Yesu anafafanua kwa ktumia njaa, kiu, n.k. - "...kasiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Neno "kumpokea" lina maana kwamba kuna njia nyingi za kutoa msaada, kwa kufariji, na hata kifedha.

**18:6 Bali atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari**.

Sasa Yesu anabadilisha neno mtoto (*paidia*) hata kuwa wadogo (*mikron*). Kwa kutumia neno mikron inaonyesha hazungumzii haswa watoto, bali kwa wachanga katika imani, mwongofu mpya. **Jiwe la kusagia** lilikuwa kubwa kiasi cha kuhitaji mnyama mwenye nguvu kama punda au ng'ombe kulisukuma.

**Atakayemkosesha...waniaminio**. Kama mtu atamwamini Yesu na mtu mwingine amshawishi kufanya kinyume, Yesu ndipo anasema ingelifaa mtu huyo kutoswa katika kilindi cha bahari."

**18:7 Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya mambo ya kukosesha! Maana hayana budi kuja mambo ya kukosesha; lakini ole wake mtu yule aliletalo jambo la kukosesha**!

Mfano wakati wote ni juu ya watu wa Mungu. Yesu anatoa ole kwa yeyote aletaye kitu chochote kilicho na ushawishi mbaya (linga. Rum.14:13; 1 Kor. 8:9-13). Yeyote atakayesababisha mtu mwingine kujikwaa atakabiliana na ghadhabu ya Mungu.

**18:8 Basi mkono wako au mguu wako ukikukosesha, ukate ukautupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima hali umepungukiwa na mkono au mguu, kuliko kuwa na mikono miwili au miguu miwili, na kutupwa katika moto wa milele**.

Yesu anatumia mfano mmoja kama alivyoutumia katika 5:30. Anawaambia Wakristo, kwa maana wengine wote watatupwa katika ziwa la moto kwa vyovyote vile. Hapa kuna mtu anayetembea katika njia sahihi, na anajikwaa kwa sababu ya udhaifu wa mwili (tamaa, kwa mfano). Uzima (wa milele) una thamani kubwa zaidi ya kitu chochote kile. Watu wote tunapaswa kujilinda na makwazo.

**18:9 Na jicho lako likikukosea, ling'oe, ukalitupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanam ya moto**.

Sasa Yesu anatumia jicho kufafanua lengo lake. Pia anatumia neno "Gehena" kwa ajili ya

**Jehanamu**. Gehena ndiko takataka zilikochomwa, (ni sawa na dampo za taka zetu), lilikuwa upande wa kusini-magharibi mwa Yerusalem. Moto haukuzimika kamwe. Katika kipindi cha Agano la Kale mahali hapo ndipo mungu Moleki wa wapagani aliabudiwa - 2 Nyak.28:3; 33:6. Sehemu hii mbaya inatofautishwa na uzima wa milele mbinguni.

.

**18:10 Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambieni ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote hutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni**

Hao waliowadogo = *mikron*, waaminio wachanga. Mdo.12:15 panaonyesha watu waliamini malaika wa mtu anaweza kujichanganya na mtu mwenyewe. Petro anagonga mlango. Roda anakwenda ndani kuwaeleza wale wengine, lakini wanadhani kuwa ni malaika. Kuna mafungu mengi yaliyoandikwa katikati ya maagano kuhusu malaika wanaolinda (linga. Tobit 5:6, 21; Agano la Lawi 5:6). Ebr.1:14 panaonyesha kwamba malaika huwahudumia watakatifu. Fungu hili halifundishi kwamba watoto wana malaika wakuwalinda. Mafundisho kama hayo hayalingani na ya Biblia. (Kama hivyo ni kweli, kwa kuwa watoto wengi hufa vifo vya kutisha, hivyo basi hao "malaika wa kuwalinda" wanakuwa wapi?) Fungu hili ni mfano linaloonyesha upendo wa Mungu kwa kujali na kujishughulisha kwa ajili ya watoto wake, waaminio wachanga (watoto katika imani). Mungu ana malaika wanaofanya kazi na kujishughulisha kwa ajili ya watakatifu - Ebr.1:14.

**Siku zote huutazama uso wa Baba yangu** = uhusiano wa karibu. Hii ni namna ya kuonyesha jinsi Mungu anavyowasikia, akiwa pamoja nao, akiwalinda, na akiwatumikia watoto wake.

**18:11** [**Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopote**.]
Linga. Lk.19:10.

**18:12 Mwaonaje? Mtu akiwa na kondoo mia, mmoja akapotea, je! Hawaachi wale tisini na tisa, akaenda milimani, na kumtafuta yule aliyepotea**?

**Mwaonaje?** Hili swal zuri kujiuliza sisi pia. Yesu anatia mkazo umuhimu wa mtu binafsi kuliko jamii nzima. Pengine Wakristo wanapaswa kufikiria juu ya roho moja kwa wakati mmoja. Mchungaji mwenye kujali anafikiri juu ya thamani ya kondoo mmoja aliyepotea. Mkristo anayejali anatakiwa kufikiria thamani ya kila roho iliyopotea. Ingekuwa ni makosa kwa mchungaji kufikiri kondoo kondoo inastahili chochote kitakachompata kwa sababu ametangatanga mbali na kundi. Vivyo hivyo, ni makosa kwa Mkristo kutojaribu kumrejeza ndugu aliyepotea au dada aliyepotea kwa amechagua kupotea.

**18:13 Hata akipata kumwona, amini, nawaambia, amfurahiya huyo zaidi, kuliko wale tisini na tisa wasiopotea**

Dhambi haipunguzi umuhimu wa mtu mbele ya macho ya Mungu. Alimtoa Mwanawe kwa ajili ya mtu kama huyu, na anawataka warejee kwake. Anataka watu wote watubu (2 Pet.3:9) ili waokolewe (1 Tim.2:4). Kwa kuwa Mungu hataki mtu yeyote apotee, kama tutakuwa ndiyo tulio sababisha makwazo kwa mtu, tutalipwa kwa hilo.

**18:14 Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa hawa wadogo apotee.**

"Wadogo hawa" ni *mikron* tena. Wakristo wanapaswa kutilia manani kwa kondoo aliyepotea na kutia jitihada ya kumtafuta. Mchungaji aliwacha tisini na kenda kwa sababu walikuwa salama. Alifanya kila kilicho muhimu ili aweze kwenda na kumtafuta aliyepotea. Aliwaacha wapi wale

tisini na kenda? Mlimani. Kondoo ni wajinga sana, pia wanahitaji uangalizi mwingi. Ni kweli kwamba kondoo wanapoona hatari huwasukumia wadogo katikati ya kundi, huwazunguka na migongo yao ikiwa nje, hupinga mateke kama waliopagawa!

Kundi huwa na ulinzi sana na kondoo akibaki kundini mara nyingi husalimika.. Inaonekana kwamba katika makanisa yetu siku hizi, tunataka wahubiri wetu watumie muda wao na "tisini na kenda," lakini Biblia haifundishi hivyo. Mwinjilisti anatakiwa kutumia muda wake kutafuta na kuokoa kilichopotea. Wachungaji (wazee) ni wakulilinda kundi. Mhubiri hana jukumu hilo. Kusanyiko linatakiwa kujishughulisha katika kuwatunza "tisini na tisa."

**18:15 Na ndugu yako akikukisa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo**.

Kuna misemo aina mbalimbali juu ya mstari huu wa kufurahisha, na hatujui ni msemo upi bora zaidi kwa kusoma. Katika United Bible Society inasema, "Kama ndugu akikukosea" angalia takwimu 'C', wana uhakika kwamba 70% neno "angainst" halipo katika asili. Hivyo hatujui kwamba dhambi yoyote ile au dhambi juu yako. Ikiwa mtu ametambua dhambi anapaswa kuchukua hatua. Yesu anaorodhesaha *hatua 4* jinsi ya kukabiliana na hili, kwa kuwa Mungu hapendi mtu yeyote apotee. Ukiwa na hili kama wazo kuu, fikiria mistari 15-17. Ndugu akikosa:

**1. Enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu**. Neno "kuonya" ni sawa na jinsi lilivyotumika katika 2 Tim.4:2: "Kalipia, kemea..." ukimwonyesha makosa na njia zake. Mtu mmoja anatakiwa kufanya hivi, Yesu anasema, "peke yenu." Kamwe hakuna ruhusa yoyote ya Kibiblia kumweleza mtu mwingine kuhusu dhambi ya mtu uliyosikia. Kwa kumweleza, kunazaa dahmbi - dhambi ya kusegenya. Lakini mara nyingi hivyo ndivyo inavyokuwa, kabla ya muda kupita mtu anaharibiwa jina lake na kuburi chake kuangamizwa kwa masengenyo, hivyo kanisa huwa na wakati mgumu kumrejeza mtu huyo. Yesu anafundisha kumwonya mtu huyo **peke yenu**. Akikusikia umempata nduguyo. Mara nyingi mtu atakushukuru kwa jinsi unavyolikabili tatizo, na jinsi unavyolishughulikia. Dhambi yenu peke yenu lazima ijadiliwe mkiwa peke yenu. Dhambi ya halaiki lazima ijadiliwe kwa halaiki. Ndugu alipotea kwa sababu alikuwa dhambini, na kadiri alivyokuwa dhambini, alikuwa nje na kundi.

**18:16 La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike**.

Hili linaonyesha kinyume.

**2. Chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili**. Yesu ananukuu kutoka Kumb.19:15 (pia Kumb.13:12-18). Kusudi na nia ya Sheria za Musa ilikuwa kwamba mtu asingehesabiwa hatia kwa ushahidi wa mtu mmoja tu. Kulikuwa kuwe na mashahidi wawili au watatu. Ukweli wowote lazima udhihirike. Kwa hiyo, ikiwa wewe ndiye pekee unayejua dhambi hiyo, na umemwendea mtu huyo lakini hayuko tayari kutubu, hivyo unachukua mashahidi wawili wengine (hata kama hawakuona dhambi hiyo). Wanakwenda pamoja nawe ili kumkabili mtu huyo kumwuliza kama alifanya (au hakufanya) madai unayosema. Pengine atayakubali. Itakuwaje iwapo anakataa? Kufuatana na Sheria ya Musa, ikiwa ukweli haukudhihirika wazi, basi madai yalikuwa yafikie mwisho yasiweze kutolewa nidhamu ya halaiki. 1 Tim.5:24, 25 - hapo baadaye Mungu atayafunua yote, yakiwa pamoja na yale ya sirini/yasiyojulikana kwa mwanadamu (linga. Mhu.12:13, 14). Elewa hili, jambo halijafikia mwafaka baina ya mashahidi na mwenye dhambi. Ukishajua kwamba mtu fulani yuko dhambini, lakini mtu huyo amekataa mbele ya mashahidi, bado unatakiwa kumkumbusha wakati wowote mnapokuwa pamoja, ukimsaidia kuona kwamba anatakiwa kusahihisha. Kutoshirikiana na mtu kusifanyike iwapo shahidi ni mtu mmoja tu mwenye neno na ndugu na hakuna ushahidi mwingine wa kuthibitisha.

**18:17 Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.**

**3. Liambie kanisa**. Ukweli ukishadhihirika, na mtu aliye dhambini anakataa kutubu, na ujulikane hadharani. Liambie kanisa, *ekklesia*. Hii ni nguvu ya pamoja. Mtu aliye dhambini, na imethibitika kwamba yuko dhambini, hufunikwa kwa upendo wa jamii nzima ukimshauri kurejea na kugeuka maishani. Kama hilo halitasaidia,

**4. Na asipolisikia kanisa pia, "Na awe kwako kama mtu wa Mataifa na mtoza ushuru**." Haesabiwi tena kama mmoja katika kanisa. Ni mtu wa nje na wala si wa ndani ya familia. Je, kanisa linajisikiaje kuhusu jambo hili? Je, wanaachana naye kabisa? La hasha! Wanajaribu kumrejeza kwa Kristo. Kwa sababu mtu huyu hatambuliwi tena kuwa sehemu ya kanisa, angali bado anahitaji wokovu.

**18:18 Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani, yatakuwa yamefunguliwa mbinguni**.

Linga. 16:19. Mpango Yesu aliouorodheshwa kwa wanafunzi umekuwa *tayari* umepangwa mbinguni na Mungu. Wao (mitume) wanatakiwa wautendee kazi mpango wa Mungu kwa kumrejeza ndugu huyo mwenye dhambi. Hawaundi hatua za kuzifuata za nidhamu ya kanisa.

**18:19 Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni.**

Mitume wataomba mambo mengi. Nao hao watakao omba lazima kwanza wawe watoto wa Mungu (1 Pet.3:9ff; Yoh.15:9), waombe sawasawa na mapenzi ya Mungu (1 Yoh.5:13-15). Katika mazingira, hili linafafanua watoto wa Mungu wakiwaomba mitume ikiwa wanaweza kutokuwa na ushirika na mtu asiyetaka kutubu.

**18:20 Kwa kuwa walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao**.

Linarejea hili pia kwa mashahidi wawili au watatu katika mst.16. Sababu gani hawa wawili ama watatu wakusanyike? Kwa lengo la kumrejeza ndugu aliyeanguka. Wakati juhudi kama hiyo ikitendeka, Yesu anakuwa **katikati yao** - hiyo ni kwamba, anawasaidia juhudi yao. Wanafanya hivi kwa ajili ya Kristo, na yanahusu kuamua waamuzi muhimu kwa ndugu aliyekosa.

"Maamuzi ya pamoja, yakiamuliwa na watu wanaotambulika, wanaojali nini haki kwa washiriki hayo lazima yachukuliwe kuwa ni maamuzi ya mwisho. Kuna ahadi ya kukubaliwa kwake mbinguni. Mtu anayetia unajisi humtia unajisi Kristo na hujikata mwenyewe atoke katika ushirika" (Jack P. Lewis, Mathayo, vol.2, p.57).

Hapa kuna mifano ya jinsi fungu hili linavyotumiwa vibaya.

1. Familia imeamua kukasa ibada ya Jumapili asubuhi na wanakwenda safari ya siku moja milimani ambapo watapata fursa ya kuwa na ibada. Wanajifariji kwa kukosa kwao ibada na kusema, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa ajili ya jina langu, nami (Mungu) nipo papo hapo." Matumizi kama hayo hayahusiani kabisa na msitari huu! Mazingira hayazungumzii juu ya ibada hata kidogo. Siyo jambo la kimaandiko familia kuamua mahali na kuwa na ibada, wakiacha kukusanyika pamoja (Ebr.10:25). Kusudi la kukusanyika pamoja ni kuweza kuonyana pamoja kwa upendo na kwa matendo mema, na kutumia msitari huu kwa maana hiyo ni makosa.

2. Makala katika Rocky Mountain News, March 28, 19991. Katika makala hii mhubiri wa kanisa la Kristo alisema, "Kristo ni mwana sheria kwangu." Alikuwa akijitokeza mahakani kabla ya mashahidi wawili au watatu Wakristo, akidai kwamba Kristo alikuwa pale kumtetea. Yeye, pia aliutumia vibaya msitari huu.

**18:21 Kisha Petro akamwendea akamwambia ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba**?

Tungali tunazungumzia msamaha na kurejea. Msamaha ndilo wazo katika mst.15-17. Talmud ilieleza kiwango cha kusamehe mara tatu. Pengine Petro alifikiria mwenyewe kuwa na huruma nyingi kwa kuzidisha zaidi ya mara mbili hilo; hata kwa kufanya namba kamili saba.

**18:22 Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara sabini, bali hata saba mara sabini**.

Huu ni utani wa maneno kuonyesha hakuna kikomo cha *kiwango*. Hatuhesabu idadi ya msamaha kwa mtu fulani hata mara 490 na kisha akifikia 491, "Samahani, siwezi kukusamehe tena." Tunasamehe, na kusamehe, na kusamehe tena na tena. Hivyo ndivyo ilivyo. Lk.17:4 - samehe kila siku.

**18:23 Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake**.

Mfano wa mtumishi asiye na huruma ni wa pekee katika Mathayo.

**18:24 Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi**.

Tafsiri ya New American Standard maelezo ya chini ya ukurasa (footnote) hii ni fedha $ 10 milioni, lakini zaidi katika kununua haki. Kiuchumi siku hizi ingelikuwa zaidi ya $ 16 milioni. Kulingana na Math.20:2 malipo ya kutwa yalikuwa "dinari" ambayo ilikuwa sawa na senti 18 kwa siku. Deni la $ 16,000,000 lingemchukua miaka 200,000 kulilipa. Yaani, mtu huyu maskini ana deni kubwa ambalo hawezi kulilipa kamwe.

**18:25 Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyonavyo, ikalipwe ile deni**.

Kuuzwa kwa mke na watoto iliruhusiwa katika Sheria ya Musa (Kut.21:2; Law.25:39; linga. 2Fal.4:1).

**18:26 Basi yule mtumwa akaanguka akasujudia akisema, Bwana, nivumilie nami nitalipa yote pia.**

Hakuna njia ya kuliapa kila kitu, na anatambua hilo, na mfalme analitambua hilo. Basi, mfalme aliguswa na nia yake mtu huyo ya kutaka kulipa deni ingawa alitabua tayari kwamba asingeliweza kamwe kufanya hivyo.

**18:27 Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe lile deni**.

**Akamhurumia** inadhihirisha jinsi Yesu alivyo katika kitabu hiki kizima. Bwana akamsamehe deni. Tendo hili ni la huruma ya ajabu!

**18:28 Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia; akamkamata, akamshika koo, akisema, Nilipe uwiwacho**.

**Mmoja wa wajoli wake** = mwenzake, aliye sawa na yeye anayemwia karibu dolla 18. Hasa jambo hili linaonyesha utofauti mkubwa; $ 16,000,000 mbali na $ 18.00.

**18:29 Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia**.

Maneno yake yalikuwa sawa kabisa na yale ambayo yeye mwenyewe alisema masaa machache yaliyopita. Pengine ungefikiria kwamba angeguswa dhamiri yake na kukumbuka kwamba alipokea rehema hapo mwanzo.

**18:30 Lakini, hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni**.

Watoa fafanuzi mara nyingi wanasema kuwa lingekuwa jambo gumu sana kwa mtu aliye gerezani kulipa kitu chochote. Ingawa hivyo angetiwa gerazani angejitahidi kumpata mtu wa kumlipia deni. Kama kusingelikuwa na mtu kama huyo, angelikaa hakika gerezani!

**18:31 Basi wajoli wake walipoona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka**.

Walihuzunika kwa ajili ya yule mwenye kuteseka kadhalika kwa ajili ya dhambi ya mtesi. Ni jambo la kusikitisha mateso kama haya na kutokujali kunapotokea baina ya watu.

**18:32 Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi;**

Angalia: deni lake lilisamehewa kwa sababu **alimsihi** bwana wake. Hili linadhihirisha: (1) Umuhimu wa kuomba msamaha, na (2) Nia yake Bwana ya kutusamehe sisi (linga. 1 Yoh.1:8-10).

**18:33 Nawe, je! Haikupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?**

Rehema (eleeos) kwa wengine imefundishwa sehemu nyingi katika maandiko, kwa sababu hiyo, ni sharti tuzingatie. Mara ngapi Biblia inasema tunapaswa kusamehe kabla ya Mungu naye hajatusamehe? Je, tunaweza kutegemea msamaha kwa Mungu nasi tusiwatendee wengine vivyo hivyo?

Mungu amesimama kama mfalme nasi tu watumishi. Sisi wenyewe tusingeweza kulipa deni la dhambi zetu. Mungu alilipa hilo kwa ajili yetu katika kifo cha Mwanawe wa pekee. Hii ni neema yake Mungu iliyokuja chini kwa ajili ya mwanadamu.

**18:34 Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoimaliza deni ile yote.**

"Hata" hatatoka kamwe. Hana tumaini la kulipa deni. Yesu sasa anaonyesha matumizi ya fungu.

**18:35 Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msipowasamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake**.

Angalia maneno **kwa mioyo yenu**. Mtu anaweza kusema kwamba amesamehe na akawa bado ana chuki. Huo siyo msamaha ambao Mungu anautaka kwa watoto wake. Anatutaka tusamehe kama vile anavyotusamehe sisi, msamaha wa kunuia toka moyoni - kusamehe toka moyoni. - kusamehe kutoka moyoni... samehe...na usahau! Jambo hili ni gumu kulifanya, lakini Mungu

ametujalia uwezo wa kusamehe na ndivyo tunatakiwa kufanya. Ikiwa sisi si watu wa kutoa misamaha, hivyo tutakabilina na Mungu asiyesamehe. Basi, ni muhimu kiasi gani kuwa watu wa msamaha!

## SURA 19

**19:1 Ikawa Yesu alipomaliza maneno hayo, akatoka Galilaya akafika mipaka ya Uyahudi, ng'ambo ya Yordani**.

Hili ni hatimisho la sehemu # 4 (angalia "alipomaliza maneno haya").

**19:2 Makutano wengi wakamfuata, akawaponya huko.**

Hii ni sehemu # 8 ya uponyaji.

**19:3 Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, Je1 ni hala mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?**

****Angalia maelezo ya nyongeza katika sehemu hii.*

Mafarisayo walimjaribu Yesu kama matokea ya watu wengi wakimfuata yeye, na miujiza mingi aliyotenda. Ni ugumu kiasi gani wa mioyo Mafarisayo walikuwa nayo! Hapa tunaona mtu akitenda miujiza mingi ya ajabu na wanachoweza kufikiti ni juu ya kumwua. Yebamoth 14:1 anafundisha mwanamume anaweza kumwacha mkewe, lakini mwanamke asingeweza kumtaliki mumewe. Ingawa Mk.10:12 anadhihirisha mwanamke angeweza kumtaliki mume, Paulo anadhihirisha hili katika 1 Kor.7:10-13. Kwa kuwa Kumb.24:1 talaka iliruhusiwa katika Sheria ya Musa, hivyo basi swali lingebakia kuhusu *msingi* wa kutaliki. Hawaulizi kuwa ni halali kumtaliki, lakini ingekuwa ni halali kutaliki **kwa kila sababu**.

Gitin 9:10 imeandika mafundisho ya waalimu (Rabbis): Shammai, Hillel, na Akiba vinavyotafsiri Kumb.24:1 katika njia tofauti, vikitilia mkazo katika maneno "kwa kuwa ameona neno ovu kwake."

*Shammai* - kinasema "neno ovu" ni uasherati.

*Hillel* - "baadhi" ("abar" katika Kiebrania) "neno ovu" katika vitu visivyo na maana hata kama kuunguza vipande vya mikate.

*Akiba* - "hajapata kibali" Ikiwa angemwona mzuri zaidi, angeweza kumtaliki mke wake...

Yesu amejibu kwa hoja tatu.

**19:4 Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke**,

1. Yesu anarejea Mwa.1:27; 5:2. Anaipitia Sheria ya Musa katika maelezo ya mwanzo ya Mungu (na hii inalingana na ile ya mwanzo, kwa sababu yalikuwa ni maelezo ya awali kabisa ya Mungu kuhusu ndoa). Mungu alimwuumba mume mmoja kwa ajili ya mke mmoja maisha. Kwa kuwa alimwuumba mume mmoja na mke mmoja, walikuwa waishi wawili daima.

**19:5 Akasema, kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja**.

Linga. Mwa.2:24 - wazo hili ni lile lile. Mume mmoja na mke mmoja wawaache wazazi wao na kuungana katika ndoa daima.

2. Hao wawili watakuwa mwili mmoja, hawatakuwa tena wawili bali mwili mmoja. Kifungo cha "u-moja" kilianza kwa Adamu na Hawa na kinaendelea hata vizazi vyote. Wawili waliooana wamekuwa na lengo moja, wamoja katika kushirikiana, wenye mwili mmoja. (Linga. 1 Kor.6:16 - "mwili mmoja" katika mausiano ya kujamiana). Talaka huvunja umoja huo.

**19:6 Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliyewaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe**.

3. Alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asitenganishe. Watu hawa walikuwa wakitafuta sababu za kutaliki. Josephus anazungumzia visa vingi ambavyo watu walijaribu kutafuta njia za kutaliki, ama kuelezia nia zao za kutaliki. Antiquities 4.8.23 (253).

1 Kor.7:10 mke asimwache mumewe, iwapo kama ataondoka, na apatane. Ni wapi Bwana anasema haya? Anaporejea Paulo ni katika Math.19:6. Neno hapo **aondoke** ni neno sawasawa na (*choridzo*) hapa. Hapa hazungumzii kuachana kama ilivyo kawaida siku hizi (kama vile "matengano kwa majaribio" ambapo hati ya talaka haitolewi bado, lakini huishi mbalimbali kwa kipindi). Hili linarejea talaka. Ni talaka inayozungumziwa pia katika 1 Kor.7:10. Mtu asitafute njia ya kutaliki, ama kutenganisha alichokiunganisha Mungu.

**19:7 Waamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha**?

Ni wazi kwamba walielewa kabisa maana ya Mwa.2:24, lakini pia walimwelewa Yesu kuwa yu kinyume na suala la talaka hivyo, wakaliendea neno la Musa.

**19:8 Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi**.

Yesu anakubali kuwa talaka iliruhusiwa, lakini anasema haikuwa katika mpango wa asili wa Mungu kwa ajili ya ndoa. Ilikuwa kwa muda kitambo tu na lisiwe jambo la daima. Mafarisayo wanataja kwamba ikiwa Musa aliruhusu talaka (Kumb.24:1) hivyo basi haiwezekani kutokuwa halali. (Walipaswa kujali zaidi Mwa.1:27; 2:24!) Mtu hatakiwi kuunda maelezo kuhusu tofauti ya neno "amri" kwa Mafarisayo (mst.7) na neno la Yesu "ruhusa" katika (mst.8) kwa kuwa katika habari hiyo hiyo katika Mk.10:3,4 maneno yamerejezwa. Agano la Kale linaandika mambo ambayo Mungu aliruhusu kwa kipindi mambo ambayo hakupenda. Hakupenda watu wawe na mfalme, lakini aliwaruhusu wawe naye kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao (1 Sam. 8:6). Anachukia talaka (Mal.2:16), walakini akaruhusu talaka. Kwa hiyo nia ya Mungu imeonekana kwa namna aliianzisha ndoa hapo mwanzo: mume mmoja, mke mmoja, maisha.

**19:9 Nanyi nawaambia ninyi, kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa ni kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini.**

****Angalia "Bulleting" na Jack Lewis*.

Uasherati = pornea ni neno pana ambalo linajumuisha zinaa kama uzinzi, ufilaji, machukizo, na kuoa ndugu. Neno **uzinzi** ni neno *moicheia* kutoka moikao likiwa na maana "kujamiana na mke au mume wa mtu." Inahusisha mtu mmoja au wawili walioolewa. Kimsingi linamaanisha kujamiana nje na ndoa kwa wanadoa. Huo ndio uzinzi. Yesu anaonekana kukubaliana na maoni ya shule ya waalimu (Rabbi) ya Shammai: uzinzi hutendwa mtu anapooa au kuolewa na mtu mwingine. Biblia haitangui ndoa, bali Paulo anasema wabakie bila kuoa au kuolewa. Ikiwa ataoa

au kuolewa na mtu mwingine, Yesu anasema hapa wanazini. Ikiwa umemtaliki mkeo na kuoa mke mwingine, unazini.

Je, Yesu anasema unaweza kumtaliki kwa sababu yoyote? La hasha! Wala si kwa kila sababu, lakini kwa sababu moja. Sababu hiyo moja, kufuatana na Yesu, ambayo mtu anaweza kumwacha mke wake ni uasherati. Je, hiyo inampatia haki ya kuoa tena? Kama mtu anamtaliki mke wake kwa sababu mke amefanya uasherati na mtu miwingine, mume anakuwa na haki ya kuoa tena. Anamtaliki kwa sababu moja: ambayo ni uasherati. Mk.10:11, 12 anakataza kumwoa mwanamke aliyemwacha mumewe. Lk.16:18 anazungumzia ndoa kwa mke aliyeachwa. "Yeyote" lazima iwe inataja kwa watu wote, na wala si kwa watu wamaagano tu (watoto wa Mungu). Angalia mafungu katika maelezo.

**19:10 Wanafunzi wake wakamwambia, mambo mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa**.

Fungu hili ambalo wale wote wanaoeleza tofauti juu ya mst.9 hawaugusi. Wanafunzi wamestaajabia msimamo wa Yesu. Wamefadhaishwa kwa uthabiti wa mafundisho yake, kwa uwazi basi walielewa. Hatua yoyote ya mafundisho ya Kibliblia kuhusu ndoa na talaka lazima ichukuliwe kutoka katika mstari huu. Je, mafundisho haya ni thabiti sana hata kusababisha mtu kuuliza, "Mambo ya mtu na mke yakiwa hivyo, haifai kuoa."?

**19:11 Lakini yeye akawaambia, Si wote wawezalo kulipokea neno hili, ila wale waliojaliwa**.

Yesu anajibu kufuatia kustajaabia kwa wanafunzi. Neno **kulipokea** maana yake kuelewa, kulishika, kufahamu. Kupokea huko uthabiti wa mafundisho yake katika mst.9.

**Ila wale waliojaliwa**. Linawahusu tu wale ambao hujikuta wenyewe katika hali ambao anaielezea. Kuwa wale ambao pengine wasingependa kuoa au kuolewa, na kuna wale ambao wanafuraha kuwa na wenzi wao. Jambo hili halilingani na hali zao.

**19:12 Maana kuna matowashi waliozaliwa hali hiyo toka matumboni mwa mama zao; tena wako matowashi waliofanywa na watu kuwa matowashi; tena wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee**.

Mstari huu unaanza kwa neno la Kiyunani *gar*, ambalo ndilo neno **maana** (for). Kwa hiyo mst.12 unaendeleza mazungumzo kuhusu ndoa na talaka na kuoa tena. Kuna namna mbili ya kuendea mst.12.

1. Anazungumzia matowashi halisi. Yesu anasema kuna aina tatu za matoashi. Maelezo ya mtazamo huu haulingani na mazungumzo yake yaliyopita kuhusu ndoa na talaka. Kwa hiyo, msimao huu unatakiwa kukataliwa.

2. Kuelewa "towashi" kuwa ni mfano. Neno "maana" (for) linapelekea kutoa ushahidi wa majadiliano haya. Yesu anatumia mfano wa matoashi kuonyesha uthabiti wa maelezo yake. Hajawahi hapo mwanzo zungumzia juu ya matoashi, na kufanya hivyo sasa hazungumzii suala la talaka.

Kuna aina tatu za matoashi:

**1. Waliozaliwa hali hiyo**. Huyu ni yule asiye na uwezo wa kuzaa toka tumboni, mtu anayejikuta kwamba yuko katika hali ambayo haiwezi kuibadilika. Maana yake: kuna watu ambao hawataoa au kuolewa kamwe. Hao, pengine kama mtume Paulo, aliachagua kuishi maisha ya useja.

**2. Tena kuna matoashi waliofanywa na watu**. Halikuwa jambao la ajabu kipindi cha Biblia kwa serikali za Mataifa kuwachukua vijana hodari waliovutia watu kwa lengo la kuwaasi na kuwaweka katika kumtumikia malkia. Waliasiwa ili wasiweze kuwa na tamaa ya kutaka kujamina na malkia. Watu hawa hawakuchagua kuwa matowashi, walifanywa kuwa matowashi na watu weingine. Maana yake: towashi ni mtu asiye na uwezo wa kufanya tendo la kujamiana. Ikiwa mtu ameamua kumwacha mke wake (na si kwa sababu ya uasherati), amefanywa kuwa towashi (kwa mfano, siyo halisi). Siyo kwa hiari yake, lakini na mtu mwingine. Yesu alisema: "na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini" (Math.5:32). Kwa hiyo, amelazimishwa kuingia katika hali ya useja. Hali hii ni ngumu sana. Lakini hiyo haitoi ruhusa ya kuwa na mahusiano ya kujamiana na mtu mwingine, njia nyingine yoyote ile zaidi ya kuwa towashi iliyoundwa na mwanadamu ingekuwa uasherati.

3. **Waliojifanya wenyewe kwa ajili ya ufalme wa mbinguni**. Walichagua kuwa waseja kwa ajili ya ufalme. Maana yake: hapa kuna mtu ambaye, pengine kwa sababu ya kukosa uaminifu, aliachwa. Hivyo, kwa sababu ya nia yake ya kuokolewa, hataki aoe au kuolewa tena. Kwa nini? Kwa sababu alitumia vibaya haki yake ya ndoa kwa kuchagua kutokuwa mwaminifu. Kwa hiyo, anajifanya mwenyewe kuwa towashi (siyo halisi, bali kwa mfano) kwa ajili ya ufalme.

Mstari 12 unapaswa utengwe kutoka katika mazingira ya 1-11. Wazo juu ya matowashi ni fafanuzi ya mistari ya 3-11. Tafsiri ya Biblia (New English Bible) ya sasa inatafsiri mstari kama ifuatavyo: "Maana wengine hawawezi kuoa kwa sababu walizaliwa hivyo, au walifanywa kuwa hivyo na wanadamu, na kuna wengine walijifanya wao wenyewe kutokuoa kwa ajili ya Ufalme wa mbinguni."

Tunatakiwa kuelewa sababu inayomfanya Yesu kufundisha anayofundisha. Hatuambii mambo ambayo yatakuwa na madhara kwetu, bali haya yamekuwepo kwa sababu ya faida ambazo tungenufaika maishani mwetu. Kama maisha yetu ni safi hivyo basi kanisa nalo litakuwa safi na litakuwa likitenda kazi barabara. Kuna mafunzo ambayo tunaweza kuyaona katika Ezra 10. Mungu aliwatenganisha kutoka kwa wanawake na watoto ambao walikuwa si wao. Yalitendeka hayo kwa ajili ya faida yao. Kwa kufikiria juu ya majibu ya wanafunzi, tunatakiwa kujifunza kuichukulia ndoa kwa makini sana. Hatutakiwi kuingia katika ndoa bila kujali au bila kufikiri. Ni suala la kujitoa maisha. Tunatakiwa kuwafundisha watoto wetu zaidi kuhusu ndoa kuwa ni ya kujitoa maisha na kusudi la ndoa.

*Ni mambo gani huunda ndoa mbele ya macho ya Mungu*?

1. Mwa.2:24 - kumwacha baba na mama, hivyo basi kunuia kuvunja uhusiano huo mgumu.
2. Mwa.2:24 - mtu kuambatana na mkewe, yaani kuanzisha uhusiano mpya, wenye kukufunga.
3. Kwa kutii sheria za nchi - hivyo basi kutekeleza kila kitu ambacho sheria inasema kuhusu ndoa (linga. Rum.13:1-7).
4. Wakati wengine wanasema kwamba kukutana kimwili ndiko kunakounda ndoa, hakuna mstari unaunga mkono hili. Hata Math.19:6 isieleweke kusema kwamba tendo la kujamiana ndilo linafunga ndoa. Kama ingekuwa hivyo, basi ingekuwaje kwa mtu aliye hanithi? Asingeweza kuoa au kuolewa? Ingekuwaje kwa mtu alijeruhiwa vitani na kwamba hawezi kutenda tendo la ndoa? Je, hatatambuliwa kamwe kuwa ameoa? Tena, iwapo ataoa kufuatana na sheria ya nchi na akamgusa mkewe (kwa njia ya kujamiana), atakuwa ametenda dhambi?

**19:13 Ndipo akaletewa watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea; wanafunzi wake wakawakemea**.

Kuwaleta watoto mbele ya viongozi wa dini lilikuwa jambo la kawaida zamani zile, kwa sababu watu waliamini kuwa viongozi hao walibarikiwa na kwamba sala zao zilikuwa maalum. Pia,

kumgusa mtoto kungeleta baraka toka kwa Mungu. Hii inaonyesha jinsi watu walivyomsahi Yesu. Wanafunzi waliliona hilo kama kuvuruga muda wa Yesu.

**19:14 Lakini Yesu akasema, Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio kama hao, ufalme wa mbinguni ni wao**

Pengine walidhania kuwa watoto wangekuwa usumbufu, lakini lakini anasema ufalme wa mbinguni ni wao watu alio kama hawa, hivyo ni kwamba, kwa kujali tabia walizonazo watoto zinawafanya kuwa wa ufalme. Yesu hasemi kwamba watoto wako kanisani. Bali anasema ni sehemu ya ufalme wa Mungu.

Fungu hili, pamoja na mengine, linadhihirisha kwa nini watoto hawahitaji kubatizwa. Walio katika ufalme hawana dhambi. Linga. Eze.18:18ff. Mwana hatauchukua uovu wa baba. Kama utajinyenyekeza mwenyewe na kuwa kama watoto hawa, hivyo basi utakuwa katika ufalme wa Mungu.

**19:15 Akaweka mikono yake juu yao, akatoka huko**.

Yesu hakuwavunja moyo wazazi. Akaweka mikono juu yao.

**19:16 Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele**?

Hili linafanana na Mk.10:17-30; Lk.18:18ff. Lakini mtu huyu anayemjia na kumwuliza ni katika umoja (singula). Kitu gani, tendo gani moja nifanye ili nipate kuurithi uzima wa mbinguni?

**19:17 Akamwambia, kwani kuniuliza habari za wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri**.

Katika habari ya Mark, anasema, "mwalimu mwema" - akimwita Yesu kuwa ni mwalimu mwema. Mtu huyu hakuelewa haswa maana ya "mwema," lakini alikiri bila kufikiri. Hakutambua nguvu ya ukiri wake. Yesu anasema usitumie neno **mwema** bila ya kufikiria na kuelewa maana yake. Kwa nini Yesu aseme hivyo? Kwa sababu alihitajika - na tunahitajika - kuelewa mambo yote yanayohusiana na "mwema."Yeye siyo tu mwema. Hana dhambi. Yeye ni Mungu. Yesu anamweleza kuwa akitaka kuingia, ashike amri. Kushika, na *kudumu kuzishika*, amri.

**19:18 Akamwambia zipi? Yesu akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo,**
**19:19 Waheshimu baba yako na mama yako, na mpende jirani yako kama nafsi yako.**

Amri katika mst.18, na ya kwanza katika mst. 19, zinatoka katika Amri Kumi. Lakini ile ya "jirani yako" inatoka kutoka Law.19:18. Yesu alitaka watu watii sheria zote. Hatoi kibali cha kuzitii baadhi na kuzidharau zingine. Katika Lk.5:14 mwenye ukoma aliamuriwa kwenda kwa kuhani (Math.23:23 Yesu anasema, "Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira ... hayo ... wala yale mengine msiyaache." Kuna mambo muhimu zaidi kuliko mengine, lakini hatupaswi kuyapuuza mengine. Sheria yote ni lazima tuishike.

**19:20 Yule kijana akamwambia, haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena?**

Kijana yule alikuwa ametenda mambo mengine mema, na alikuwa amejitahidi kutii Sheria. Je, kulikuwa na chochote alichoacha?

**19:21 Yesu akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate**.

Kuna mambo matatu alitakiwa kuyafanya.

1. Nenda ukauze mali yote uliyonayo.
2. Chukua mali hizo ulizouza na kuwapa maskini. (Ndipo utakapokuwa na hazina mbinguni - linga. Math.6:19-21).
3. Kisha njoo unifuata. Kuweka kipaumbele, hesabu gharama, kisha fuata. Kwa mtu huyu kulikuwa na gharama kubwa. Angalia mstari unaofuata.

**19:22 Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.**

Kijana huyu alikuwa mdogo lakini alikuwa na mali nyingi, maisha yote yalikuwa mbele yake. Ebu angalia katika Marko habari huii:

Marko 10:21 - "Yesu akampenda." Hapa tunaelezwa jambo ambalo Mathayo haelezi. Swali hili analouliza linaonekana kuwa swali la msingi sana. Haonekani kuwa anatafuta sababu za kumshitaki Yesu. Anaonekana anajitahidi kuifuata Sheria ya Musa, lakini moyo wa Yesu unampenda kwa sababu anatambua kwamba ni vigumu kwa kijana kutoa mali zake kwa ajili ya kumfuata yeye. Anapungukiwa na "kuachilia na kumkubali Mungu." Je, tungependa, ikiwa hayo ndiyo Bwana anataka tuyafanye, kuuza kila tulichonacho? Yesu hajatutaka sisi kuuza mali zetu na kumfuata yeye kule milimani Palestina. Ametutaka tujikane sisi wenyewe. Math.6:33 - "Lakini tafuteni kwanza ufalme wake na haki yake." Ametutaka kuhesabu gharama.

**19:23 Yesu akawaambia wanafunzi wake, Amin, nawaambieni, ya kwamba itakuwa shida tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni**.

Hazungumzii kanisa hapa. Kuingia katika ufalme wa milele wa Mugu ni vigumu kwa sababu ya kujitoa sadaka kote na kuweka kipaumbele impasavyo tajiri afanye. Siyo kwamba haiwezekani, bali hilo ni jambo gumu. Hata hivyo, wanafunzi wameshangazwa haswa na maneno hayo na yale anasema katika mst.24.

**19:24** Nawaambia tena, Ni rahisi zaidi kwa ngamia kupenya tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.

Fungu hili ni zuri kuthibitisha kwamba ufalme wa mbinguni na ufalme wa Mungu ni sawa. (Linga. Lk.15:18, 21).

Wengine wanasema kwamba tundu la sindano ulikuwa mlango mdogo katika mlango wa mji mkubwa. Mtu aliweza kutembea kiurahisi kupita hapo, lakini ingempasa ngamia kupita kwa kutumia magoti yake. Mlango kama katika kuta za Yerusalemu, lakini ilijulikana kama "Tundu la Sindano" wakati wa kipindi cha Yesu. Yesu hazungumzii mlango, bali sindano ya kushonea. Ngamia kupita katika tundu hilo isingewezekana...au ingewezekanaje?

**19:25 Wanafunzi waliposikia, walishangaa mno, wakisema, Ni nani basi awezaye kuokoka**?

Je, ngamia anaweza kupita katika tundu la sindano? Hapana, haiwezekani isipokuwa kwa msaada wa Mungu. Wafuasi hawa walitazamia kuwa matajiri siku moja kwa kuwemo katika ufalme wa Masihi wa ulimwenguni, na sasa Yesu anawambia tajiri ni vigumu kwake kuingia katika ufalme.

Hili pia linaelezea mawazo mengine waliyokuwa nayo watu zamani za kale. Iwapo ulikuwa tajiri basi ulihesabiwa kuwa umebarikiwa na Mungu, na ikiwa ulikuwa maskini basi ulilaaniwa na Mungu. Mtazamo wenye makosa huo upo hata siku hizi.

Isa.53:8 "...Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai..." Pia katika mst.4 "...Tulimdhania ya kuwa amepegwa, amepigwa na Mungu, na kuteswa." Ni nani angefikiria kwamba Yesu angechukua mateso ambayo walistahili? Je, walitambua kwamba Mungu alimpinga bila kuwa na hatia? Wao walistahili kupigwa, lakini Yesu alifanya hivyo kwa ajili yao.

Marafiki wa Ayubu pia walikuwa na mawazo potofu kuhusu utajiri na jinsi ya kukubaliwa na Mungu. Ayubu alipoteza mali zake, hivyo wakaamini kwamba Mungu alikuwa akimwadhibu. Angalia Zab.73. Asafu anazumgumzia juu ya waovu wanavyofanikiwa...lakini si hivyo kwa wenye haki, wana dhiki. Hakuelewa hadi mst. 17, "Hata nilipoingia katika patakatifu pa Mungu, nikautafakari mwisho wao."

Ni nani basi atakayeokoka? Ikiwa watu waliopata kibali machoni pa Mungu hawataokoka, ni nani basi anaweza? Watatakiwa kubalisha kabisa mtazamo wa kufikiri kwao.

**19:26 Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana**.

Nyogeza hii ya maelezo Yesu haungumzii kuhusu mlango Yerusalemu. Isingewezekana kwa mtu kupanda ngamia na kupita katika mlango. Anazungumzia kitu ambacho mwanadamu asingeliweza kukifanya. Mungu anatuokoa, hatuwezi kujiokoa wenyewe. Hakuna tunachoweza kutenda kustahili wokovu wetu wenyewe.

Akisha kusema kwamba tajiri alikuwa na wakati mgumu kuingia katika ufalme wa mbinguni, akazua maswali kwa Petro na mitume wengine.

**19:27 Ndipo Petro akajibu, akamwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata tutapata nini basi?**

Wanafunzi walikuwa na mawazo ya kuwa matajiri katika ufalme wa Masihi. Kutokana na mafundisho yaliyopita muda si mrefu, tumaini lao hilo lilikuwa limekufa.

Hatuna sababu za kulijadili swali hili. Ni swali la msingi. Sisi nasi tunafanya vivyo hivyo. Kwa nini tunajitahidi kuishi maisha ya Ukristo? Tunataka kupata hazina, tunatazamia kupata thawabu. Rum.8:18 - tunaona yale yatakayofunuliwa. Mungu anatambua kwamba tunatamani kupata thawabu. Ndiyo sababu katika Ufunuo tunaona kwa uchache yaliyokuweko huko. Tunaweza kuona yale yaliyoko kule kwa ajili yetu ikiwa tunapenda kulipia gharama ya sasa.

**19:28 Yesu akawaambia, Amin, nawaambia, ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu makabila kumi na mbili ya Israeli**.

Angalia maana aina tatu Yesu anazungumzia hapa:

1. "Mwana wa Adamu" atakuja siku ya hukumu, Math.25:31,
2. Atakuwa juu ya kiti chake cha hukumu, na
3. Ninyi (mitume) mtakaa katika viti kumi na mbili vya enzi. Mitume walitarajia utawala wa duniani; Yesu anawaahidi viti vya enzi mbinguni. (Linga. Ufu.3:21; 4:4; 20:4). Tutatawala

pamoja naye - 2 Tim.2:12a.

**Katika ulimwengu mpya** = *palingenesia*. Neno hili limetumika mara nyingine tena katika Agano Jipya (Tito 3:5 ambapo linazungumzia ubatizo). Neno hili lilipendwa na Wanostiki (Gnostics). Waliamini katika ulimwengu mpya, kuzaliwa mara ya pili, kwa ulimwengu: uumbaji, kisha maangamizi, tena ulimwengu mpya, maangamizi, na kadhalika. Yesu anafundisha kwamba kutakuwa ulimwengu mpya - kuumbwa upya - kwa ufalme wa Mungu wenye utukufu.

**19:29 Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kurithi uzima wa milele.**

Hapa kuna ahadi bora (linganisha na Mk.10:30). Yesu anazungumzia kuhusu ahadi ya kujitoa sadaka. Kijana huyo alikuwa hayuko tayari kuacha mali yake, lakini Yesu anasema kwamba yeyote ambaye atakuwa tayari kufanya hivyo atapokea mara nyingi sana, na kisha uzima wa milele. Tafsiri ya Marko imefafanua zaidi - atapewa mara mia sasa katika ulimwengu huu...na katika ulimwengu ujayo, uzima wa milele." Ikiwa wafuasi wa Yesu watajitoa sadaka kwa ajili yake basi mambo haya tutapokea katika ulimwengu huu na ule ujayo.

Hakuna ahadi wala masharti ya kupata mali, lakini kuwa ahadi kwamba tunapojitoa sadaka kubwa Mungu anapenda na yuko tayari kutujalia na thawabu zipitazo thawabu kubwa. Ikiwa kijana tajiri angeuza kila kitu alichokuwa nacho, basi angelijazwa na kufurikizwa na baraka zipitazo ujira. Alishindwa kuelewa hilo, kama ilivyo kwa watu wengi siku hizi wanashindwa kuyaona hayo.

**19:30 Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza**.

Katika 20:16 maneno haya yamerudiwa tena. Katika 20:27 tunaona maneno yanayolingana na haya. Kulingana na tukio lile lililomhusu tajiri, na majadiliano na Petro, Yesu anaenda kuzungumzia kuhusu ujira. Atakapozungumzia ujira, kuna uwezekano wa mambo mawili ambayo mtu angejiuliza:

1. "Je nitafanya kazi tu kwa ajili ya kupata ujira?" Kazi isingefanywa kutokana na upendo, na wala si kwa kujitoa sadaka, bali kwa ajili ya nia ya kutaka kupata ujira. Hivi sivyo haswa Yesu anavyowahamasisha.
2. "Kwa nini basi usisubiri dakika ya mwisho kutii iwapo thawabu iko mbinguni?" Majibu yote haya mawili yanajimbiwa katika mfano ulio katika sura ya ishirini.

## SURA YA ISHIRINI

**20:1**

Yesu anafafanua yale aliyosema katika 19:30.

**20:2**

Dinari, kutokana na Tobit 5:4, ni ujira wa kutwa, karibu senti 18 kwa kutwa. Kazi ya kawaida ilitofautiana ikitegemea majira. Kazi kwa kawaida ilianza saa 12 kamili asubuhi (linga. bBaba Mezia 83b katika Talmud ya Babeli).

**20:3**

Saa tatu kamili anawaona watu wengine wakisimama sokoni bila kazi mahali ambapo watu waliotafuta kazi wangekusanyika.

**20:4**

Angalia kwamba hakuna kiwango cha ujira kilichotajwa, “na iliyo haki” nitawapa.

**20:5**

Mchana, tena saa tisa kamili alasili.

**20:6**

Hii ingekuwa karibu saa kumi na moja kamili jioni.

**20:7**

Ufunguo ni kiwango cha muda wa kazi ya kutwa. Watu walikuwa hawapo kazini - si kwa sababu *hawakutaka* kufanya hivyo, bali ni kwa sababu hawakupata *wito* wowote. Mstari huu umetumiwa na watu wanaoamini katika “toba ya kitanda cha mauti.” Iwapo mtu anaacha sasa kumtii Mungu akingojea kumtii karibu na kifo chake, anajahatarisha maisha yake mwenyewe. Mungu anataka tumwendee pale anapotuita.

**20:8**

Law.19:13; Kumb.24:15 - chini ya Sheria ya Kale wafanya kazi walilipwa mara tu walipomaliza kazi mwisho wa siku.

**20:9**

Katika mst.2 mwenye shamba alikubali kuwalipa ujira huu. Wate walikwenda kufanya kazi walikubaliana na kiasi hicho.

**20:10**
**20:11**
**20:12**
**20:13**
**20:14**
**20:15**

Inaonekana kuwa siyo haki kutokana na kazi na ujira waliolipwa. Si sawa ikizungumzia kuhusu mambo ya neema. Bwana aliwalipa wale wote waliofanya kazi kwa masaa mengi na wale wote waliofanya kazi masaa machache. Hatuwezi kustahili kamwe kulipwa kile Mungu anachotupatia, basi tunabahatika kupata tunachotenda kutoka kwa Bwana - thawabu toka kwa Mungu ni uzima wa milele (Rum.6:23). Hauwezi kustahili huo, bali utazama kwamba mshahara wa dhambi ni mauti.

**20:16**

Siyo kutaka kuwa wa kwanza bali kupenda kuwa mtumishi, na kupokea thawabu ambayo Bwana wetu anatupatia.

**20:17**
**20:18**

Hii ni mara ya tano Yesu anasema juu ya mateso tangu kukiri kwake Petro katika sura 16.

**20:19**

Yesu anatambua unyanyasaji, mateso, na kifo cha kikatili angepata. Anawaeleza sasa (kama mara nyingine) angefufuka siku ya tatu (12:40; 16:21; 17:23).

**20:20**

Yakobo na Yohana ni wana wa Zebedayo. Fungu linalolingana na hili ni Marko 10:35 - 40 anasema Yakobo na Yohana ndio wanaomwomba, wala si mama yao. Je, hapa kuna kupingana? Pengine watatu wote wapo, lakini ni Yakobo na Yohana wanaoomba kupitia mama yao, pengine kukwepa majibu yoyote yale yaliyo kinyume ambayo Yesu angewajibu.

**20:21**

Mapema Yesu aliongelea viti vikiwa vimekaliwa na mitume, Yakobo na Yohana walipewa hapo nyuma heshima na Yesu (Math.17 alipobadilika sura). Kwa nini wanaomba kitu cha juu kabla hata ya Petro hajapata fursa hiyo?

**20:22**

"WAKAMWAMBIA," (they) wala si akamwambia (she), tunaweza. Wanafunzi hawakupenda kuona Yesu kama mfalme atakayeteseka, hivyo hawakuweza kuelewa sala kwa maana ya fahari lazima ziwe sala kwa maana ya mateso kama yeye alivyopenda. Wanafunzi hawakuweza kuamini kwamba Yesu angekalia kiti cha enzi cha Daudi cha mbinguni. Wanamwona yeye akiwa katika kiti cha enzi cha Yerusalemu.

**Kikombe** = mateso na mauti.

**20:23**

**Mtakinywea**. Yakobo alikuwa mtume wa kwanza kuuawa. (Mdo.12:2 kwa mkono wa Herode).

**Na Baba yangu**. Mungu anaandaa thawabu na atawapatia wao awapendao. Yesu hayupo hapa katika shughuli za "kutoa thawabu." Hilo amewekwa mikononi mwa Baba.

**20:24**

Mitume waliosalia wasingelichukia kama na wao, pia, walikuwa hawana roho na ufahamu wa jinsi hiyo (kushindwa kuelewa) kama vile Yakobo na Yohana.

**20:25**
**20:26**
**20:27**

Hii ni mara ya tatu tunapata maneno "wa kwanza atakuwa wa mwisho." Yesu anawafundisha kwamba ukuu duniani huo si ukuu wa kweli. Ukuu wa kweli hupatikana katika kutumika, nao wanaotumika watakuwa wakuu.

**20:28**

Yesu anatumia mfano wake mwenyewe kama ulio kamili. Neno “ukombozi” (lautron) limetumika hapa kwa mara ya kwanza na linamaanisha kulipia fidia kununulia kitu fulani au mtu fulani. Fungu linatueleza fidia hiyo ya ukombozi kuwa ni kitu gani. Uhai wake. Hakuna gharama nyingine ingetosha. Kila kitu ambacho Yesu alipaswa kutoa alipenda kutoa, na atatoa maisha yake kwa ajili ya wengi. Haya ni maelezo ya kwanza juu ya kusudi la kifo cha Yesu. Alisema mara tano hapo awali kwamba angekwenda kufa. Hili ni fungu la sita juu ya mateso. Anaeleza sasa kwa nini itampasa kufa.

Math.26:28 - damu ilimwagika kwa ajili ya “wengi” kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Matumizi haya hayaelezei juu ya kupatanishwa watu wachache. 2 Kor.5:14; Ebr.2:9 anafundisha kwamb Kristo alikufa kwa ajili ya watu wote. Walakini, watu wote hatabarikiwa na kumwaga kwa damu kwake. Wale tu wanaotii injili wapata faida. Wanafunzi wa Kristo wanapaswa kujitahidi kutumika, na wala si kutafuta fahari na utukufu.

**20:29**
**20:30**

Watu hawa walimwita Mwana wa Daudi, Masihi. Hawakuona shaka kusema hivyo! Kadhalika walisema, “Uturehemu!” (eleeos).

**20:31**
**20:32**

“Mnataka niwafanyie nini?” Swali la maana sana! Vipofu waliomba macho yao yapate kuona tena. Unataka Yesu aakufanyie nini? Je, unataka msamaha na uzima wa milele? Yesu anaweza kukupatia. Kila unachotaka, anaweza Yesu kukupatia. Baraka zote za rohoni zinapatikana katika Kristo (Efe.1:3).

**20:33**
**20:34**

Watu wanaweza kumfuata haswa Yesu. Ingawa hawakuweza kuona, watu hawa waliweza kumkiri Yesu kuwa Bwana. Msitari huu unatumika kama fafanuzi ya yale Yesu anasema katika Yoh. 9. Mafarisayo waliweza kuona, lakini walikuwa vipofu kiroho.

SURA YA ISHIRINI NA MOJA

Katika sura hii yameandikwa mambo matano ambayo yaliwakalishisha sana viongozi wa dini Yerusalem.

1. Kuingia kwa shangwe kwa Yesu - 1-11.
2. Kuwafukuza wafanya biashara hekaluni - 12,13.
3. Kutenda kwake zaidi uponyaji - 14.
4. Kukabiliana na viongozi wa dini kwa mara ya kwanza na viongozi wa dini - 15-17. Kibwagizo kifupi: Anatumia fafanuzi za uweza wake kujibu maswali yao kuhusu mamlaka - 18-22; mtini uliolaaniwa.
5. Kukabiliana kwake na viongozi wa dini mara ya pili - 23-27.

**21:1**
**21:2**

**21:3**

Yesu anajiandaa kuingia kwa shangwe. Lakini, cha muhimu zaidi, ni ukweli wa kwamba hili lilitimiza unabii.

**21:4**
**21:5**

Mathayo anatumia maandishi ya Zakaria kwa kuongeza katika sura hizi chache (linga. Math.21:5; Zak.9:9; Math.24:30, 31, Zak.13:7; Math.27:9; Zak.11:12, 13). Mafungu haya yanalengi moja kwa moja, bali yana uhusiano fulani.

"**Tazama, mfalme wako anakuja kwako**" = unabii wa Kimasihi.

**Mwana punda** alitambuliwa kama mnyama wa amani; farasi mnyama wa vita. Kulikuwa hakuna kudharaulika ukipanda mnyama kama huyo, kama wanavyodai watu wengine. Punda walikuwa moja ya rasilimali kubwa ya matajiri (angalia Waam.5:10; 2Sam.16:2; Ezra 2:67; Ayu.1:3). Yesu atampanda mnyama mwenye alama ya amani. Yeye siyo Masihi mwenye jeshi hodari.

**21:6**

Hili ni somo bora kwa kila mtu. Kutenda sawasawa na jinsi Yesu alivyoagiza.

**21:7**
**21:8**

2Fal.9:13 - watu walifanya hivi kumtambua Yehu kama mfalme. Hili ni tendo la kumtangaza Yesu kuwa mfalme (Law.23:40; Ufu.7:9; 1 Makabayo 13:51; 2 Makabayo 10:7).

**21:9**

**Hosana** linatoka katika neno la Kiebrania "Joshua" na "Hosea" (lenye maana "wokovu"). Katika mstari huu neno limetumika kama amri katika lugha ya Kiyunani na linamaanisha, "Okoa, nakusihi." Tafsiri zingine zinasomeka kama "okoa sasa." Wanamtangaza Yesu kuwa Masihi, yeye ajaye kwa jina la Bwana.

**Juu mbinguni** = ikimwakilisha Mungu aliye juu sana. Wananukuu Zab.118:12ff, fungu la Kimasihi la wazi.

**21:10**

Hili ni swali zuri. Kuna mabadiliko gani, iwapo yapo ya aina yoyote ile, kutoka Math.16 alipouliza, "Watu hunena kuwa mimi ni nani?" Ni majibu gani sasa wanampatia?

**21:11**

Wanadai kuwa YEYE ni nabii, Yesu, wa Nazareti ya Galilaya, atakayekuja kwa mfano wa Musa - Kumb.18:15. Inawezekana akilini mwao walielewa kikamilifu mashaka haya, lakini walitokea mbali.

**21:12**

Hekalu palikuwa mahali pa kuu kwa ajili ya Wayahudi, wahali walipokaa waandishi na Mafarisayo. Yesu akakasirika kwa sababu watu walipoteza malengo yao: wakitumia hekalu kama mahali pa kutengeneza fedha badala ya kuwa mahali pa ibada.

**21:13**

Inatoka Isa.56:7. Mathayo hataki tupoteze lengo la kwamba Yesu anatimiza unabii wa Kimasihi. Hekalu la Mungu lilipaswa kuwa mahali pa kunyenyekea, kubudia, na kusalia. Badala yake pakawa mahali ambapo watu walinyang'anya kwa wizi. Wevi mara nyingi wangefichama katika mapango na ikitokea mtu kupita hapo pangoni, angekabiliana na shida. Ndivyo inavyotokea kwa watu wasio na hatia wanapokwenda hekaluni. Viongozi hawa wangechukua kila walichokuwa nacho. Ilikuwa kama walitembea katika mapango ya wevi.

**21:14**

Viongozi wa Kiyahudi walichukia kwa sababu:

1. Miujiza ya kweli ilitendeka.
2. Miujiza inatendeka katika nchi "yao" - Yerusalem.

**21:15**

1. Maajabu aliyoyafanya.
2. Watoto wakilia hekaluni.

Walichukizwa na ukweli kwamba Yesu aliweza kufanya miujiza, na walichukizwa na jinsi alivyokubalika na watu; hasa kutoka katika vinywa vya watoto wakirudia kupinga kelele zile zilizopigwa na wazazi wao. Hasira zikapanda. Wanatakiwa wamshughulikie mtu huyu. Jambo fulani ni lazima lifanyike!

**21:16**

Ni jambo gani linahusishwa na swali lao? "Wasikia...?" Kwamba aweze kunyamaza kutofanya anachofanya, kisha kuwanyamazisha watoto wasifanye wanachofanya.

**Hamkupata kusoma** tena akiwaonyesha ujinga juu ya neno la Mungu miongoni mwa viongozi wa kiyahudi). Ananukuu kutoka Zab.8:2. "Vinywani mwa watoto wachanga...nawe." Wakati mwingine watu wazima hawawezi kuona ukweli, kuna baadhi ya ukweli watoto pekee wanaweza kuona. Watoto hawa walipiga kelele, wakisema ukweli mtupu, "Hosana mwana wa Daudi!" (Hili ni moja kati ya makabiliano mawili baina ya viongozi wa Kiyahudi).

**21:17**

Aliutumia muda wake hapo, kisha akarudi Yerusalem asubuhi yake.

**21:18**
**21:19**

Wanafunzi wakaliona hili na kustaabia. Yesu alikuwa ametenda, machoni mwao, mijiza mingi ya ajabu, lakini hili liliwashangaza kwa namna ya pekee.

**21:20**

Tini zilipatikana tu wakati majani yalipokuwepo. Mk.11:12-14 anatueleza kuwa haukuwa msimu wa tini. Lakini, kwa kuwa mti na majani, ahadi ilitolewa ya matunda, lakini hayakuwemo. Hivyo, Yesu anafikisha mwisho wa ahadi ya mti ya uongo. Maana yake ni kwamba Mafarisayo ni kama mti huu wa tini. Wanatoa ahadi nyingi, lakini hakuna cha kutoa, hivyo wanakwenda kuhukumiwa.

Wanafunzi walistaajabu! "Jinsi gani mtini umenyauka mara?" Wameshangazwa na nguvu alizonazo mtu huyu!

**21:21**

Linga. 17:20 kwa maelezo zaidi juu ya nguvu ya imani.

**21:22**

Ukiomba lolote ingekuwa sawa na 1 Yoh.5:14, 15, sawasawa na mapenzi ya Mungu. Yesu anatumia tukio la mtini kudhihirisha nguvu ya imani. Mungu asingetenda muujiza kama ingekuwa kinyume na mapenzi yake. Tunatambua kwamba miujiza ilikoma 1 Kor.13:8, 9). Miujiza si moja ya mpango wake siku hizi. Kwa kuwa Mungu hatendi tena miujiza, ikiwa tutaomba kwake kufanya hivyo, basi ni kuomba kinyume na mapenzi yake, na maombi hayo hayawezi kujibiwa. Uweza utokanao na sala ni ule ambao Yakobo anautaja (5;18ff). Tunatakiwa kuwa watu wa imani na kuomba siku hizi.

**21:23**

Yesu anaonyesha mamlaka, na wanamjia kumwuliza yanakotoka.

Ni kwa amri gani unatenda haya? "Mamlaka" ni neno la ufunguo katika kitabu cha Mathayo. Yesu hakuwahi kuhudhuria shule zao, na siyo "mmoja wao," wala si kiongozi, au Rabi anayejulikana. Kwao, "ana lolote." Viongozi wa kidini hawatambui nguvu alizonazo Yesu, na mema yote anayotenda. Wanachopendezwa nacho ni, "Nani amekupatia haki ya kufanya haya?"

**21:24**

Mmeniuliza swali mimi, nami nitawauliza swali. Mkisha nijibu swali langu, nitawajibu swali lenu.

**12:25**
**12:26**

Wamewekwa katikati ya "mwamba na mahali pagumu", katikati ya mashaka ya kuchagua moja. Yohana alimshuhudia Yesu, akimsema kuwa yeye kuwa ni mkuu kuliko yeye mwenyewe. Ikiwa walimtambua Yohana, basi ni lazima pia wamtambue yeye ambaye Yohana alimtambua kuwa ni mwana kondoo wa Mungu. Wakati fulani watu huuliza maswali ya kujiangamiza wenyewe.

**21:27**

Kwa kusema, "Hatujui" wamejishutumu wao wenyewe kwamba hawakuwa mahakimu wanaostahili. Anayesimama mbele yao ni mmoja aliye wa maana sana katika historia, na hata hawamtambui kuwa yeye ni nani! Ni uhakika gani watu wawe nao kwa ajili ya kuamua lolote lile watu hawa wangeliamua?

Unafikiria nini watu hawa walifikiria akilini mwao kwa swali lao? Waliamini angekufuru iwapo angedai kwamba mamlaka yake yalitoka kwa Mungu. Yesu akasimama kinyume na mambo yote waliyokuwa kinyume nayo. Kama angedai kuwa na mamlaka ya Mungu, wangemshitaki kwa kukufuru na wangemwondoa.

**21:28**

Anaanza hapa mfululizo wa mifano kuwashawishi viongozi wa Kiyahudi. Wa kwanza ni mfano wa wana wawili. Kwa kuwa hawakufahamu majibu ya swali la kwanza, alitaka waweze kuamua.

**21:29**
**21:30**
**21:31**
**21:32**

Mtu aliye na wana wawili alitarajia kwamba wangefanya kazi. Maana yake imetolewa katika mst.31, 32. Wakaulizwa, ni yupi aliyefanya mapenzi ya babaye? Walijibu hili. "Yule wa pili." Yule aliyesema kwamba hataki kwenda, lakini baadaye alikwenda. Waandishi na Mafarisayo wanasimamia mwana wa kwanza. **Watoza ushuru na makahaba** wanawakilishwa na mwana wa pili aliyetubu na kwenda. Katika mst.25, 26 Yesu aliuliza juu ya ubatizo wa Yohana. Yohana alikuja kwa njia ya haki. Ubatizo wa Yohana ulitoka kwa Mungu.

****Angalia somo juu ya "Mfano wa wana wawili."*

**21:33**

Mfano huu pia umetolewa kuwashawishi viongozi. Shimo la shinikizo ndani yake inahusisha mashimo mawili yaliyotengenezwa chini ya ardhi yaliyounganishwa na tundu au mrija. Mizabibu huwekwa katika moja lililo juu, na mizabibu inapodondoka majimaji yanatiririka kupitia katika tundu kungia katika pipa kubwa. Mwenye shamba hujenga ugo kuzunguka shimo la shinikizo kwa ajili ya kulinda shughuli yake. Mnara umejengwa kwa ajili ya ya kuonyesha walinzi mahali pa kulinda hatima ya uzalishaji. Maana ya mfano huu ni kwamba mwenye mali amechukua tahadhari kubwa katika kuhakikisha kwamba mizabibu inazalisha kadiri iwezekanavyo.

**12:34**

Katika Palestina msimu wa kuvuna mizabibu ungeanza mwaka wa tano (linga. Law.19:25).

**21:35**

Watumwa wanasimamia manabii wa Agano la Kale. Yerumia alipigwa na kutiwa gerezani. Zakaria alipigwa mawe (2Nyak.24:20f).

**21:36**
**21:37**

Hapa mwana anakuja kwa mfano wa watumwa (linga. 20:28; Fil.2:5ff) na anafanya kazi ambayo watumwa walipaswa kuifanya.

**2 1:38**
**21:39**

**21:40**
**21:41**

Yesu sasa anatoa maana.

**21:42**

Ananukuu Zab.118:82. Huu ni mmoja ya mistari ya kuvutia waandishi wa Agano Jipya (linga. Mdo.4:11; 1 Pet.2:7; Rum.9:33). Kukataliwa kwa jiwe inaonyesha wajenzi hawakuona mahali pa hilo jiwe. Mjenzi alikuwa apate mawe yaliyochongwa mbali na kuyaleta eneo la ujenzi. Hapa wajenzi wamepokea, tena wakalikataa. Kutoka Zab.118, kukataliwa kwa jiwe hakutalizuia lisitumike kuwa jiwe kuu la pembeni. Sababu gani? Kwa sababu Mungu alitambua tangu mwanzo kwambaYesu angekuwa jiwe kuu la pembeni kwa ajili ya imani ya Wakristo, hata ingawa viongozi walimkatalia, lakini hawakumzuia Mungu kutekeleza alichopanga.
**21:43**

Yesu anachukua maamuzi ya viongozi wa dini waliyafikia katika mst.41 na kuyalenga kwao. Ufalme utachukuliwa kwao na litapewa taifa lizaalo matunda.

**21:44**

Kuna madhara makubwa ya kutojenga juu ya Yesu. Ama utajikwaa juu yake, au kuangukiwa na hilo (hukumu zake kukwangukia).

**21:45**

Yesu alizungumza nao kwa uwazi! Ingawa ulikuwa mfano, hata hivyo waliweza kumwelewa maana halisi.

**21:46**

Walipokwisha kuelewa, walitafuta kumkamata, lakini waliogopa makutano. Kuna jambo la mzaha katika hili. Yesu katika mfano alikwisha waeleza kwamba mwenye shamba alimtuma mwanawe, na sasa wanaelewa kwamba anazungumza kuhusu wao, wanajaribu kumkamata Mwana. Amewahubiria "walio viziwi."

****Angalia karatasi juu ya "Mfano ya wafanya kazi shamba la mizabibu.*"

**SURA YA ISHIRINI NA MBILI**

**22:1**

Mfano wa tatu unaowashawishi viongozi wa Kiyahudi.

**22:2**

Sherehe za arusi zilizofanywa na mfalme, kwa heshima ya mwanawe! Ni furaha ilioje!! Tukio hili ni kubwa ajabu!

**22:3**

Siyo kwamba wasingeweza kufika, bali hawakutaka. Mfano huu umesimulia ukimlenga hasa

mfalme. Tumepewa hivyo ili tuweze kujisikia jinsi mfalme anavyojisikia. Amewatuma watumwa wake wawalike watu kuja katika sherehe ya mwanawe na hawataki kuja. Jambo hili lingemkasirisha sana mfalme.

**22:4**

Pengine walishindwa kuelewa jinsi ya ukubwa wa sherehe hii ulivyo. Kwa nini waliamua kutokuhudhuria? Walipewa nafasi nyingine kuitika wito wa mfalme - kama vile Yesu alivyomfuata Yohana watu walipewa fursa nyingine kumwendea Mungu.

**22:5**

Kwa kukusudia, bila kujali, kudharau jinsi mfalme anavyotaka - kuwepo watu walioalikwa.

**22:6**

Wamechoshwa na mwaliko wa mara kwa mara, wamechoshwa na watumwa wa mfalme wakiwasumbua. Wanamambo ambayo wanataka kuyafanya katika njia zao wenyewe. Lakini:

**22:7**

Kwanza alidhalilishwa. Lakini sasa, baada ya kuwatendea vibaya na kisha kuwaua watumwa wake, amefukizwa na ghadhabu.

**22:8**
**22:9**

Mwaliko sasa umekwenda jumla kwa yeyote yule. “Na wote mwaonao waiteni arusini...” hakuna upendeleo, waalike wote. (Pengine hii inarejea kwa watoza ushuru na wenye dhambi, na kisha watajumuishwa Mataifa).

**22:10**

Walitii amri. Waovu walialikwa vile vile na wema, na ukumbi wa sherehe ukajaa waalikwa.

**22:11**
**22:12**

**Vazi la arusi** = mavazi ya sherehe, na mtu mwenye uwezo alipoalika watu wengine mavazi yaligawiwa kutoka kwa mwenyeji wao. Anayekuja ndani anaonyesha kutokuheshimiwa kwa mwenyeji kwa kutokuvaa mavazi yaliyotolewa kwa ajili yake. Mtu hana cha kusema kwa sababu ya mavazi hana udhuru kwa maana hajavalia ipasavyo. Jambo hilo lilichukuliwa kama kumdhalilisha mfalme na kwa mwana aliyepewa heshima.

**22:13**

Linga. 8:12; 13:42, 50. Mtu aliye thubutu kuingia katika shereha za mfalme bila kuvalia vema alitupwa mahali pa adhabu. Wanadamu leo wamevalia haki wanapotii injili ya Kristo. Kushindwa kutii injili kutasababisha kuhukumiwa (Ufu.3:4,5,18).

**22:14**

Wito kwanza ulikuwa kwa ajili ya wageni waalikwa (Wayahudi) lakini waliamua kutokuhudhuria. Baadaye wakaalikwa watu katika njia kuu. Waliochaguliwa ni wale waliotenda masharti ya mfalme anayotaka.

****Angalia maelezo ya nyongeza katika "Mfano wa Sherehe za Arusi*."

**22:15**

Hawakuweza kumtenga katika mambo aliyofanya, kwa sababu kila anachofanya ni chema. Walifikiri pengine kuweza kumnasa katika maneno anayosema.

**22:16**

Je, waliamini haswa kuwa Yesu angekamatwa na wafuasi wake wachanga? Kwamba angesema jambo pasipo kuwajali wao?

**Maherodi**. Watu wa chama cha kisiasa waliounga mkono utawala wa kifalme wa Herode. (Angalia maelezo zaidi). Uadui ulijenga mahusiano ya kushangaza baina yao. Makundi haya mawili kwa kawaida hayakupatana.

**Wala hujali cheo cha mtu ye yote yule**. "Tunaamini una uwezo hata kusema uovu wa serikali. Hautamwogopa mtu awaye yeyote yule."

**22:17**

Kodi ilikuwa ni ushuru uiotakiwa kwa watu wote na serikali ya Rumi. Kama Yesu akisema ni halali angekosana na makutano walipinga utozaji wa kodi.

**22:18**

Kuna mtego gani katika swali hili? Mtu hawezi kujibu bila ya kuonyesha upendeleo. Kama Yesu atajibu ndiyo Yesu atakuwa kinyume na Wayahudi na sheria zao. Ikiwa atajibu hapana, wangempeleka kwa Warumi.

**22:19**

Kodi ilikuwa kama malipo ya kutwa nzima ikalipwa kwa serikali iliyochukiwa ya Rumi (angalia maelezo katika dinari, 20:2).

**22:20**
**22:21**
**22:22**

Yesu alitoa jibu ambalo pande zote mbili zisingejikwaa. Kwa Mafarisayo alisema, "Cha Mungu mpatie Mungu;" na kwa Maherodi, "Mpeni Kaisari kilicho chake." "Sarafu iliyokuwa na picha ya Kaisari ni mali ya Kaisari na ilitakiwa irudishwe kwake. Mtu katika sura ya Mungu (Mwa.1:27) ni mali ya Mungu na anatakiwa amwendee yeye." (Jack Lewis.)

**22:23**

Masadukayo wakajiunga na wengine katika kumhoji Yesu. Swali lao ni la kipekee kutokana na

mtazamo wao juu ya ufufuo (kama Mathayo anavyoeleza).

**22:24**

Hii ni kweli, Kumb.25:5. Hii imetambulikana kama Sheria ya ndoa ya Walawi. Mtu anapokuwa amekufa na kumwacha mkewe bila watoto, nduguye humtwaa mke na kumzalia watoto kwa ajili ya urithi, kumjali na kumtuza anapokuwa mzee.

**22:25**
**22:26**
**22:27**
**22:28**

Hoja ikithibitishwa zaidi, hupoteza maana na huwa haina faida tena. Masadukayo walifundisha kwamba roho hufa pamoja na mwili, na kutumia amri kama ya Musa kujaribu kuonyesha kwamba ufufuo ni jambo la upuuzi. Ikiwa ndoa itaendelea baada ya maisha haya (maisha yajayo, ufufuo) matatizo mengi yangezaliwa kwa sababu ya hali hii (halisi au dhana tu) wali leta. Mke angekuwa na mume mmoja tu. Mke wa yupi kati ya wale saba?

**22:29**

Mwapotea = "mnakosa" (err) tafsiri ya King James. Kushindwa kuelewa kwao maandiko kumepelekea kufikia hatimisho potofu, imani potofu, na hivyo basi mazoea mabaya. Hakika, somo zuri ni, ikiwa tumeshindwa kuelewa maandiko na uweza wake Mungu hivyo tunakosea; "unatenda dhambi." Tunawajibika kufahamu na kutii neno la Mungu (Yoh.12:48; Ufu.20:11-15).

**22:30**

Hawakuelewa kwamba ndoa haikuwepo katika kiama. Hakutakuwa kuoa au kuolewa mbinguni. Yesu hasemi kwamba tutakuwa malaika, bali uhusiano wetu utakuwa kama ule wa malaika.

**22:31**

Mara nyingine tena, Bwana wetu alitarajia watu hawa kuwa wanafunzi wa neno. Angalia tena, **hamjalisoma neno**. Agano la Kale liliandikwa kwa ajili yao ingawa liliandikwa miaka mingi iliyopita kabla **na Mungu**. Hapa tunaona uvuvio.

**22:32**

Ananukuu Kut.3:6 - tukio la kuwaka kwa kichaka, Mungu alipozungumza na Musa na kujitambulisha kuwa yeye ni Mungu wa Ibrahim, Isaka, na Yakobo. Ikiwa ni Mungu wa hao watatu, na kuwa Mungu wa walio hai, hivyo wangali wanaishi. Lakini Agano la Kale linaandika vifo vyao.

Tunawajibika kufahamu na kutii maandiko. Wanaotutaka tukubali "tafsiri ya kisasa" wanafundisha kwamba amri tu ndizo tuzifuate, na si kuhusisha, au mifano. Mafarisayo na Masadukayo walipotea kwa sababu hawakujua mambo yahusuyo ufufuo. Hapakuwa na fungu lolote ambale lilitaja moja kwa moja "kuna ufufuo." Maadiko *yalihusisha* ukweli juu ya fufuo. Walipaswa waelewe hayo kutokana na maelezo ya maandiko yanayohusisha jambo hilo. 2 Tim.1:10 - Yesu alileta uhai na uzima kupitia nuru ya injili. Mpaka Yesu alipofika kulikuwa na mafundisho yasiyoeleka mengi. Haukuwa mpango wa Mungu kuzungumzia jambo hilo katika Agano la Kale, lakini alitaka Yesu afundishe haya katika Agano la Jipya.

**22:33**
**22:34**
**22:35**
**22:36**

Nipe amri moja ambayo itazizidi zingine zote - na kuziondoa - sheria zingine katika Torati. Mwangalie mwana-sheria huyu, mtu mwenye ujuzi, anauliza swali.

**22:37**

Inatoka Kumb.6:5 na amri iliyokuu kwa sababu ni msingi wa sheria zote. Kila kitu tufanyacho, tunakitenda kwa sababu ya upendo. Tunampenda Mungu kwa:

1. *Moyo wako wote* - kujitoa sadaka kwa Mungu. Siyo tu misisimko ya mwili, au kutumika "kwa midomo," bali tunatii kwa sababu tumeguswa dhamiri na Bwana.

2. *Nafsi zetu zote* - eneo la kiroho la mtu, tukimpatia kila tulichonacho yeye. Hakuna yeyote anashirikiana naye kiti cha enzi cha kiroho. Yeye ndiye pekee tunayemtumikia.

3. *Kwa akili zetu zote* - "chombo tunachotumia kufikiri" - chunguza, utambuzi. Tunafikia kumtambua yeye, na tunampenda.

Upendo huleta utiifu wa dhati. Ndiyo maana hiyo ni amri iliyo kuu. Kulikuwa na sheria mamia na mamia katika Sheria za Musa, lakini upendo ukikaa moyoni basi sheria zote zitakuwa zimetimizwa.

**22:38**

Anampatia mwana-sheria zaidi ya alichoomba.

**22:39**

Ananukuu Law.19:18. Yesu anatambua kwamba mtu anapaswa kujipenda mwenyewe, akisha elewa kuwa upendo ndio msingi kwa yote tufanyacho, anatueleza ni jinsi gani ya kuwapenda majirani zetu - kama nafsi zetu. Katika Kiebrania neno "rafiki" na neno "jirani" ni mamoja na yanamaanisha jambo moja. Kwa habari za Luka mwana-sheria, akitaka kujiona mwenye haki, akauliza, "Na jirani yangu ni nani?" -(Lk.10:29). Yesu alijibu kwa kutoa mfano wa Msamaria mwema.

**22:40**

Yesu aliligawa Agano la Kale katika makundi mawili: Torati, na Manabii. Maelezo haya yanachukua viatabu vyote thelathini na tisa vilivyokubaliwa katika Agano la Kale. Bila ya amri hizi mbili, hakuna sheria za Mungu ambazo tutazitii kwa njia ile Mungu anataka sisi tutii. Yohana anasema katika 1Yoh.4:19-20, tunapenda kwa sababu yeye ametupenda kwanza, na ikiwa utasema kwamba unampenda Mungu na kumchukia ndugu yako wewe ni mwongo. Upendo ni ufunguo wa kutii yale yote Mungu ameagiza.

**22:41**
**22:42**

Yesu ametajwa mara nyingi kama mwana wa Daudi. Maelezo haya ni ya muhimu sana kwa

Mathayo. Yesu anataka aulize swali ambalo litapima kuelewa kwao juu ya Masihi, na kupitia yeye Masihi angekuja. Swali limejibiwa kwa usahihi. Ni mwana wa Daudi, lakini...yeye ni zaidi ya huyo!

**22:43**

**Katika roho** = Yesu ni njia ya kusema "kwa uvuvio."

**22:44**

Akinukuu kutoka Zab.110:1. "Bwana" wa pili ni mfalme. Ikiwa Yesu ni mwana wa Daudi, jinsi gani Daudi amwite mwanawe, "bwana?"

**22:45**

Je, Daudi anaweza kumwita mwanawe, "Adoni" (Bwana)? Hapana! Hakika haiwezekani! Haya ni maelezo juu ya ukuu. Ni nani aliye mkuu, Daudi au Masihi ambaye atakuja kutoka kwa Daudi? Katika mawazo ya Wayahudi mwandamu halisi, na Masihi ni mmoja atakayewarejeza kule ambako Daudi alikuwa. Ingawa tena, kupitia *kuhusisha* katika Agano la Kale, ukweli unafunuliwa na kuwa rahisi! Masihi ni mkuu kuliko Daudi. Ndiyo maana Daudi anamwita yeye "Bwana."

**22:46**

Kulikuwa na kuelewa vibaya juu ya jinsi Masihi atakavyokuwa, atakakotoka. Mathayo amekwenda kwa mapana kuelezea Yesu kuwa ni mwana wa Daudi, na ananukuu matukio mbalimbali ya watu kumwita hivyo. Ameitwa mwana wa Daudi kwa sababu ametoka katika ukoo wa Yese na kupitia ukoo wa Daudi. Lakini Wayahudi walishindwa kuelewa, wakidhania *ukoo wa duniani*. Yesu anataka wafahamu kwamba ni zaidi ya ukoo wa kimwili wa Daudi. Anataka wafahamu kuwa yeye ni Mungu na ni wa milele!

**SURA 23**

**23:1**

Mafarisayo wako katika kukabiliana na moja na maneno makali mno ya maandiko! Yesu anawaita "wanafiki" kwa maana wanasema kwamba wana mamlaka ya Musa, lakini wakikana mamlaka ya Mungu kwa kujitia katika haki yao wenyewe.

Huu ni mwanzo wa *sehemu ya tano ya mahubiri*, na inaendelea hadi sura 25. Hapa Yesu anazungumza na makutano na wanafunzi juu ya waandishi na Mafarisayo.

**23:2**

Waliketi wao wenyewe mahali pa nafsi ya Musa (ofisi) ya kufafanua Sheria.

**23:3**

Walichofundishwa na Mafarisayo kufanya toka katika Sheria za Musa, walitakiwa kutenda. Lakini, hawakustahili kuwafuata mifano yao ambayo ilikuwa kinyume na Sheria. Mafarisayo "hawakufanya yale waliyohubiri."

**23:4**

Math.11:28 - “Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo...” Mizigo hiyo mizito ndiyo Yesu alikuwa akiizungumzia hapa - siyo mizigo ya kimwili, lakini mizigo ya kiroho. Ni mizigo gani ya kiroho Mafarisayo walikuwa wakiwatwisha watu? Mapokeo yao wenyewe; toka kuvunja masuke, hata kuosha mikono, n.k. Waliwatwisha watu, lakini wao wenyewe hawakuibeba.

**23:5**

Angalia sura 6:1, 5, 16 - mambo yaliyofanywa ili kutazamwa na watu kama vile, kutoa zaka, kusali, na kufunga. Anataja mambo sita ambayo yanawaelezea, au vitu wanavyofanya.

**1. Hupanua hirizi zao**. Tafsiri ya New American Standard ina maelezo chini ya ukurasa yanayofafanua vikasha vilivyokuwa na mafungu ya maandiko, vilivyovalia kwa kusudi la dini. Utepe ulioshikilia vikasha hivi ulipitia katikati ya paji la uso, au ulivaliwa katika mkono wa kushoto, au mikono yote. Kusudi ilikuwa kuwakumbusha maneno ya Mungu. Kufuatana na Arndt - Gingrich yalitumika kuzuia madhara na/au kutoka katika nguvu ya mapepo (uk.876). Linga. Kumb.6:8 - “Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.” Mafarisayo na waandishi walitanua kuwa kubwa zaidi kuliko mtu mwingine yeyote ili watu wadhanie kuwa ni wanaheshimu zaidi sheria kuliko hasa walivyokuwa.

**2. Huongeza matamvua yao**. Katika Math.9:20 tunaona kwamba Yesu alikuwa na upinde katika vazi lake, lakini kamwe hakuiongeza.

**23:6**

**3. Hupenda viti vya mbele katika karamu**. Walitaka “vitu vya kuchagua”, nafasi ya ukubwa, katika mkusanyiko wowote wa watu.

**4. Na kuketi mbele katika katika masinagogi**. Walipenda kuketi katika “mabenchi ya mbele.” Linga. Lk.11:43.

**23:7**

**5. Na kusalimia masokoni.** Walipenda kutambulikana kwa kuheshimiwa sana.

**6. Na kuitwa na watu, “Rabi**.” Neno la Kiebrania “Rab” (“mkuu”, “nguvu”, “mwenye mamlaka”, limeundwa katika neno-miliki likimaaanisha “mkuu wangu” au “mwenye uwezo wangu” kimiliki Likawa neno lililohusiana na walimu waliokuwa na mvuto mkubwa katika Israeli.

**23:8**

**Mmoja** = Yesu au Mungu. Ndugu wa Kiyahudi walikuwa wawe na mamlaka sawa, wasijiunue juu ya wengine. Katika Math.20:25 Yesu aliwashutumu watu wa Mataifa kwa kutumia vibaya mamlaka - “huwatawala kwa nguvu” watu wengine. Walio “wakubwa” ndiyo wanapaswa kuwatumika, na wala si kuwa mabwana.

**23:9**

Rabi walikuwa na namna ya vyeo na **baba** walikuwa wamepanda viwango vya vyeo katika shule

za Rabi. Yesu hazungumzii baba wa familia za duniani, anazungumzia kuwa *vyeo katika dini*. Wakatoliki mapadri wanaitwa “Baba”, ni kufundisha kinyume na Yesu anavyofundusha.

**23:10**

Katika sura 15:14 Yesu alisema “kipofu akimwongoza kipofu”, wakijiona kuwa na mamlaka na kuongoza wengine, wao wenyewe, walitakiwa kuwa wafuasi.

**23:11**

Je, hii ni amri au ahadi? Pengine, yote. Mtu wa kweli haswa ni yule anafanya kazi kuwahudumia watu wengine. Linga.20:26, 27.

**23:12**

Kukweza huku kunatoka kwa Mungu, 1Pet.5;6, na wala si kutoka kwa mwanadamu. Mstari 13 ni mmoja wa ole saba.

****Angalia orodha za ole hizi*.

**23:13**

MAONYO YA YESU KATIKA MATHAYO 23.
YESU ANAWASHUTUMU WAANDISHI NA MAFARISAYO KWA MAANA WANATUMIA MAMLAKA WASIYOKUWA NAYO.

Mungu ndiye mwenye mamlaka, na wala si Mafarisayo.

1. MAMLAKA YA KUTAWALA NANI ANAINGIA UFALME (23:13).
Walifunga ufalme kwa kufundisha mafundisho ya uongo, wakiongeza mapokeo yao wenyewe, na kujaribu kuthibitisha kwamba Yesu hakuwa Masihi aliyeahidiwa. Kwa kufanya mambo haya, viongozi wenyewe hawakuwa tayari kuingia.

**23:14**

Linga. Mk.12:40; Lk.20:47.
**23:15**

2. MAMLAKA KUAMUA SIFA ZIFAAZO KUINGIA UFALME (23:15).

**Mwana wa** ni njia ya kuonyesha asili. Kuwa wana mara mbili maana yake wamekuwa na sifa na tabia za Mafarisayo na tena wamekwenda mbali ya hivyo. Wana tabia ya Jehanamu, uovu na ubaya, wametengana na Mungu, wako gizani. Mafarisayo walikuwa waijilisti, wakijaribu kuwaongoa watu kuingia katika Uyahudi. Walipofanikiwa waliwafanya wale waliongolewa, kuwa wasiompendeza Mungu kuliko hata awali.

**23:16**

3. MAMLAKA JUU YA ULIMI (23:16-22).

**23:17**

Angalia maelezo katika 5:33-35, njia hii ilikuwa ni moja ya kuondoa majukumu na ahad. Ikasababisha ungumu wa kutumaini maneno ya mtu. Katika jamii ikiwa yoyote iwapo hakuna kuaminiana, kazi na maana ya jamii hiyo ni mbaya.

**23:18**
**23:19**

Kuna mifano miwili, dhahabu na hekalu, madhahabu na sadaka.

**23:20**
**23:21**
**23:22**

(Linga. 5:34). Ninyi mgepaswa kuwa watu wa neno. Hakukupaswa kuwa watu wa kuapa ili watu wapate kuwaamini. Jamii iliporomoka sana hata hapakuwepo na kuaminiana. Ni nani alifanya jamii ianguke kufikia hatua hiyo? Viongozi! Waandishi na Mafarisayo!

**23:23**

4. MAMLAKA YA KUAMUA NINI NI MUHIMU NA NINI SI MUHIMU KATIKA SHERIA YA MUNGU (23:23-24).

Mafarisayo walishindwa kuthamini umuhimu wa hekalu na vitu vilivyokuwemo hekaluni, pia hawakuelewa vyema na kuthamini Sheria za Mungu. Waliketi wao wenyewe katika kiti cha Musa, wakizifanya baadhi ya sheria kuwa ni muhimu zaidi ya zingine. Wanadamu wanapojitia mahali hapo, wanakuwa wanachukua nafasi ya Mungu. Katika neno lake, Mungu ameweka thamani kubwa katika mambo kama **adili**, **rehema** na **imani**. Lakini, mtazamo mwingine wa Sheria zake, mambo kama zaka, nayo hata hivyo ni lazima tutii.

**23:24**

Kwa hiyo, tatizo lilionekana kwamba waliacha mambo fulani ambayo yalikuwa muhimu kwa Mungu.

1. Adili ilipotea. Waliamua wao ni nini haki na bora, badala ya kumruhusu Mungu aamue mambo hayo.

2. Rehema haikuwepo. Hawakuwa na rehema kwa (k.m. sadaka) zao. Mara mbili Yesu alisema, “Nataka rehema (huruma), wala si sadaka” (Math.9:13; 12:7).

3. Walidharau imani, katika mambo ya kufanya kila siku kama Mungu alivyosema. Walijipangia wenyewe kuamua kilicho chema na kilicho kibaya mbele za macho ya Mungu. Hawakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo.

Wenye kuchuja mbu. Walikuwa na tatizo la kushika mambo madogo na kuondoa na kudharau mambo makubwa. Walikuwa watu “walijishughulisha na vioo.”

**23:25**

5. MAMLKA YA KUAMUA KILICHO SAFI NA KILICHO KICHAFU (23:25-26).

**23:26**

Je, ilikuwa sahihi kuwa na uchafu kidogo katika vikombe na bakuli zao, maisha yao? La hasha? Hapana, haikuwa sahihi! Linga. Math.5:8 - heri walio wasafi wa moyo. Mafarisayo walitaka watu wawaamini kuwa walikuwa watu wenye haki, hivyo wakafika hatua ya kujionyesha wenye haki kwa nje, lakini kwa ndani walikuwa kinyume. Walijaa uharibifu kwa ndani. Yesu anasema ni bora kusafisha kwanza ndani - moyo - kisha matendo yatakuwa matakatifu na safi. 1 Tim.1:5 - lengo ni kuwa waaminifu, imani isiyo na unafiki. 2Tim.2:21 -"Basi ikiwa mtu amejitakasa mwenyewe kwa kujitenga na hayo, atakuwa chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kazi iliyo njema." Tunawajibu wa kulinda ndani ya "vikombe" na "vyombo" maisha yetu - safi!

6. MAMLAKA KUAMUA JAMBO GANI NI HAKI (23:27-28).

**23:27**

Mafarisayo walivaa nguo zilizosimamia kiroho na utakatifu (kama vikundi vingi vya dini leo). Walakini, nguo hivyo haziamuriwa na Mungu. Hataki watu wake wajitenge kutoka "wenye vyeo" kuja "watu wa chini." Sisi sote ni sawa - ndugu na dada. Mtazamo hivyo, badala ya utakatifu kuonekana kwa nje ni usafi wa moyo.

**23:28**

Watu ni wajinga wa kuhukumu kiroho. Ni rahisi kuwadanganya watu. Lakini Mungu, anajua na kuona yote, hawezi kudanganywa (linga. Gal.6:8f).

**23:29**
**23:30**

Mafarishayo walidhihirisha ujinga wao juu ya kushindwa kuelewa kiwango cha haki zao na za baba zao. Waliwashutumu haraka baba zao kwa kushindwa kuwaelewa manabii wa Mungu. Lakini, ukweli, hawakuwa na tofauti yeyote. Wao, kama baba zao, walikuwa wabinafsi mno, wenye kijiangalia wenyewe hata kushindwa kuwaona watu wa Mungu wa kweli. Ndiyo sababu hawakumtambua Yohana Mbatizaji, au Yesu. Ndiyo sababu hasa hawakuwatambua mitume na manabii wa Agano Jipya.

**23:31**

Walisema wasingefanya makosa ambayo Baba zao walifanya. Walakini, wanafanya makosa yale yale. Hivyo basi wamejishuhudia wao wenyewe, wakikiri makosa yao.

**23:32**

Watakwenda kuhatimisha hukumu yao wenyewe kwa kumsulubisha Yesu msalabani.

**23:33**

Mungu ameamua kuwahukumu hukumu ya milele kwa wanao mkataa yeye na wafanya kazi wake. Mafarisayo walikuwa wakiongoza katika kumkana. Yesu alizungumzia mapema hasira ya Mungu kwa wale wote wanaowapotosha watu wengine (Math.18:6,7).

**23:34**

Yesu anatabiri yatakayowapata mitume na manabii. Hakika mateso yote ambayo mwanadamu

anaweza kufikiri, yaliwapata wanafunzi wa Yesu!

**23:35**

Makosa ya kizazi cha kwanza yatakuwa juu yao, kwa sababu ya kiburi chao cha kusema wasingefanya kamwe mambo hayo baba zao walifanya. Ingawa wanafanya makosa hayo hayo. Tena, kinachofanya adhabu yao kuwa nzito zaidi ni kwamba wao walipokea baraka zaidi ya kizazi kilichopita! Kwa hiyo, kwake yeye aliyepewa zaidi itatakiwa zaidi. Nguvu zaidi za ghadhabu ya Mungu itakuwa imemwagwa kizazi hiki kikaidi. Yesu, katika msitari huu, anatia muhuri kuthibitisha Agano la Kale. Kwa kumtaja Habili, anarejea kitabu cha kwanza cha Agano la Kale kwa Kiebrania (Mwa.4:8ff). Kunukuu kwake Zakaria kunatokana katika Biblia ya Kiebrania (2Nyak.24:21). Haya hivyo, ni misemo inayolingana kutoka "Mwanzo hadi Malaki" tulivyonavyo. Misemo kama hiyo imeeleweka tukijumuisha vitabu vyote vinavyo katikati ya viwili hivi. Kwa hiyo, Yesu anatambua vitabu vyote thelathin na tisa vya Agano la Kale - na wala si Apokrafa au vinginevyo "vilivyopotea."

**23:36**

Msemo "kizazi hiki" kinahusu waliokuwa wanaishi wakati huo - anaozungumza nao Yesu. Angalia maelezo 24:34.

**23:37**

Yesu haonyeshi furaha katika sentensi hii ya hukumu. Upendo wake kwa Yerusalemu ni wa kweli. Alifanya kazi kwa ajili ya mji huu (yaani, watu waliutengeneza mji) kwa vizazi na vizazi. Angalia Eze.16 kwa mfano mrefu. Bahati mbaya, ukweli ni: haukuwa tayari kumrudia Mungu. Hata leo sisi, tunaweza kufafanuliwa sawa kwa kutokutaka kurejea kwa Mungu.

**23:38**

Kila kitu walitarajia Mafarisayo wao wenyewe (kwa mfano viti vya mbele katika ufalme wa Masihi) vitakuwa vimepotea. Kibaya zaidi, nyumba ya Israeli itaachwa ukiwa - pengine anarejea maangamizi ya Yerusalem (yamejadiliwa sura inayofuata).

**23:39**

Yesu hakabiliani na viongozi hawa wa Kiyahudi moja kwa kama alivyofanya hapo nyuma. Nafasi yao ilikuwepo kisha ikatoweka.

**SURA 24**

MASOMO KATIKA UNABII WA KIBIBLIA (****Angalia maelezo ya nyongeza*).

SURA HII IMETUMIKA KUUNGA MKONO MAFUNDISHO YAFUATAYO:

1. Kuja kwake Yesu kulikuwa kuanguka halisi kwa Yerusalemu na hatakuwa tena.

2. Kila jambo katika Agano Jipya (pamoja na Ufunuo) linalozungumzia kuja kwake Kristo linazungumzia kuanguka kwa Yerusalem 70 B.K. halisi. Haya ni "Maoni ya Max King 70 B.K."

3. Kuja kwake Kristo kutaambatana na ishara nyingi zilizotajwa katika sura hii. Haya ni

mawazo ya utawala wa Yesu duniani wa miaka elfu moja unafafanuliwa katika sura hii.
a. Vita na matetesi ya vita (mst.6),
b. Taifa na taifa kupigana (mst.7),
c. Njaa (mst.7),
d. Tetemeko la ardhi (mst.7),
e. Wengi watajikwaa (mst.10)
f. Manabii wa uongo watainuka (mst.11),
g. Uasi utazidi (mst.12)
h. Upendo wa wengi utapoa (mst.12).

**MSINGI WA HISTORIA**

Wanafunzi walikuwa wakimwonyesha majengo mazuri Yesu (mst.1). Josephus anasema hekali lilikuwa: "Jumba la ajabu ambalo hatukuwahi kuliona ama kulisikia, tunapotafakari muundo wake, ubora wake, uzuri wa kila mahali pake, au sifa za mahali pake pa Juu" (Wars, 6,4.8 [267]).

"Umbo la nje la jengo hakuna ambacho kisingeliweza kustaajabisha ama akili au macho. Kwa maana, ikisha funikwa kila upande na vipande vikubwa vya dhahabu, jua halikuwa tena angani bali kueneza nuru kwa nguvu kama mwanga ambao uliwapashinda watu kuangalia na macho yao, kama miari ya jua. Kwa wageni kukabiliana nalo ilitokea kutoka umbali kama mlima ulifunikwa barafu; kwa sehemu ambayo haikufunikwa na dhahabu ilisafishwa kwa kung'arishwa na weupe safi (Wars, 5:5.6. [222fff).

**24:1**

Kazi ya hekalu ilianza **<u>20 K.K. na ikamalizika katika 64 K.K.</u>** - ujenzi wa kipindi cha miaka arobaini na sita (Yoh.2:20). Lilivunjwa mwaka 70 B.K., ambapo watu walifurahia kwa miaka sita tu.

**24:2**

Yesu alijibu akisema majengo haya yangebomolewa. Katika Wars, 6.4.6ff. [254.] Josephus anaelezea kubomolewa na kuchomwa kwa hekalu na askari wa Rumi katika 70 B.K..

**24:3**

Wanafunzi waliunganisha maneno ya Yesu ya mambo yajayo na ufalme wa Masihi,

1. **Mambo haya yatakuwa lini**? - Swali haswa linahusiana na maneno ya Yesu katika mst.2. "Mambo haya" yanahusu kubomolewa kwa hekalu - Lini yatakuwa mambo haya?

**Nayo ni nini dalili ya kuja kwako**? - "Dalili ya kuja kwako" iko katika tukio linalohusiana na swali #1, na linatendeka wakati huo huo.

3. (**Dalili itakuwa nini**) **ya mwisho wa dunia**? - Swali hili linahusu kuja kwa Kristo mara ya pili na mwisho wa dunia. Yesu ataonyesha kwamba hakuna dalili za mwisho wa dunia.

Yesu mara moja anaanza kujibu swali la kwanza na la pili, yote yakiwa yanalenga tukio la aina moja - kuanguka kwa Yerusalem. Anasema mambo mawili kuhusiana na tukio hili.

1. Wakati utakuwa mgumu sana.
2. Itakuwa rahisi "kupotoshwa." Ametaja hili mara nne (mst.4,5,11,24) - kudanganywa kwamba

huo ni mwisho wa dunia. Inaweza kuonekana kama ndio wenyewe, lakini siyo wenyewe. Msije mkamruhusu mtu kuwadanganya kufikiri kwamba ndio mwisho.

**24:4**

Ni wajibu wenu kujua ili kwamba msidanganywe.

**24:5**

Watu lazima wajiandae kwa ajili ya tukia hili! Josephus katika (Antiquities, 18, anadai kwamba wengi walijitokeza kuwa ndiyo wenyewe. Katika Mdo.5:36, 37 Yuda na Thadeo kila mmoja alidai kuwa ni Masihi (linga. pia 24:24).

**24:6**

Wataona nyakati kama hizo za taabu, na pengine kufikiri walikuwa katika maandalizi ya ufalme ujao wa Masihi. Ni makosa kufikiri kwa namna hiyo. Nyakati hizo hazikuwa ni za mwisho wa dunia, au kuja kwa ufalme wa kipindi cha Masihi.

**24:7**

Maangamizi ya kawaida yatatokea, lakini mambo haya ni ya mwanzo tu.

**24:8**

Wangefikiri ni mwisho wa dunia, lakini haukuwa bado. Mateso hayakufikia mwisho 70 B.K. baada ya Yesu kufa. Katika Ufu.7:14 alipouliza watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? “Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu.” Hata katika 96 B.K. watu waliuawa. Mambo hayo yatatokea lakini yasiwafanye mpotee. Siyo dalili za mwisho wa dunia.

**24:9**

Math.10:16-23 Yesu aliwaonya, lakini katika Yoh.15:18-27 ni fungu linalofahamika zaidi. Dhiki? Mauti? Kuchukiwa? Hawakuwahi kufikiria hivi akilini mwao; siyo katika ufalme ujao wenye utukufu! Haya hayaonekana kama kuketi na kula chakula katika ufalme wa Kimasihi na saa waliyoitarajia.

**24:10**

Mateso yanadhihirisha ni nani aliye upande wa Mungu, na nani aliye upande wa Shetani. Ni hatua dhahiri la “kung’oa magugu!”

**24:11**

Aliwaonyo juu ya manabii wa uongo watakao kuja (mst.5), na katika mst.23, 24 atawaonya tena. Kuna watu daima wanaotafsiri wao wenyewe dalili hizi. Walikuwepo kipindi cha Vita vya Ghuba ya Uajemi ambao walisema vita vile vilikuwa dalili za mwisho wa dunia. Matukio kama hayo yanaleta “wauzao unabii.” Jambo baya katika hili ni kwamba watawapotosha watu kwa sababu kuna watu daima wanaoamini wanachosema.

**24:12**

Mstari huu unafunganisa pamoja sababu ya kuanguka kwa Yerusalemu. Upendo wa watu

utapungua, hivyo uasi utazidi. Hii ndiyo sababu Mungu anakuja katika kuhukumu.

**24:13**

**Uvumilivu** ni ufunguo wa wokovu (Math.10:22). Uanafunzi ni kuunga pamoja, kuunganana, mashindano ya mbio ndefu, na unathamani kuliko kitu chochote. Mstari huu kimazingira hauzungumzii mwisho wa dunia, bali kustahimili manabii wa uongo, ishara za uongo, upendo kupoa, uasi, n.k. Watakao vumilia haya yote wataokoka.

**24:14**

Kuna mambo mengi ya kuyaangalia katika fungu hili. Yesu anafundisha kwamba vita, matetesi ya vita, n.k. mwisho bado (mst.6) bali mwanzo (mst.8). Mstari 14 unafunua "mwisho" utakuja haswa, lakini ni pale tu injili itakapokuwa imehubiriwa ulimwenguni kote. Mwisho huu si wa dunia kwa sababu:

1. Anaendelea kuelezea maangamizi ya Yerusalemu na watu wengi wa kutembelea mji. Kuna watu wanaosema kuwa hapakuwa na Wakristo waliouawa katika maangamizi ya Yerusalemu kwa sababu walimwamini Yesu, na kufanya alichowaamuru kufanya. Josephus anaelezea haya kama mauaji mabaya ambayo hayakuwahi au hayatawahi kutokea, ambayo Yesu aliyaongelea katika mst.21. Ni hakika haswa kwamba ilikuwa dhiki kubwa, lakini Mungu alifupisha muda huo kwa ajili ya wateule wake.

**24:23**

Hata baada ya haya yote kutokea, wengine watadai "yule kule" au huyu huku" ni Kristo. "Msisadiki."

**24:24**

"Watatoa ishara kuwbwa na maajabu" ni maneno hayo hayo yametumika kuonyesha miujiza aliyokuwa akifanya Yesu. Hizi ni nguvu kuvunja asili, lakini zilizofanywa na manabii ya uongo (linga. Math.7:22). Angalia tena sisitizo liko katika **kuwapoteza** (linga. Efe.5;6; 1Yoh.2:26; Kol.2:8; Gal.6:7; Ufu.12:9).

**24:25**

"Kuonywa mbele ni kuvalia silaha mapema" ni msemo uliozoeleka. Baadaye watatazama nyuma na kukumbuka haya kwamba yalifundishwa na Bwana wao.

**24:26**

Mara nyingine tena maneno ya kupotezwa. Wanafunzi lazima wao watambua vyema, na kuwatambua manabii wa uongo.

**24:27**

Linarejea hili katika maangamizi ya Yerusalemu. (Angalia sababu itakayotolea hapo baadaye). Mambo kufikia mst. 35 yanahusu kuanguka kwa Yerusalemu.

**24:28**

Mzoga unasimamia kufa kwa Yerusalemu, na tai wanawakilisha manabii wa uongo mst.26.

**24:29**
**24:30**
**24:31**

Sehemu hii ngumu zaidi. Wengine wanaitaja kama "Ufunuo mdogo wa Yesu." Ufunguo wa kuelewa haya ni kuona kama ufunuo - lugha ya picha.

Katika mst.29 Yesu anaelezea kwamba **mara baada ya dhiki ya siku zile** akitumia lugha ya ufunuo kufanya wazingatie umuhimu wa matukio haya. Siyo kuyachukulia kama mambo halisi, bali anafafanua maana. Biblia inajaa maelezo ya jinsi hii, na vitabu kama Ezekieli, Zakaria, Isaya, Danieli, na Ufunuo (ambacho kimeitwa "Kitabu cha Picha") ambacho kimejaa alama na picha.

**Mara**. Katika lugha ya ufunuo haina maana kwamba yatatokea ghafla. Maandiko hayo hayana maana kulingana na nyakati, kwa hiyo lugha hii haitakiwi kuchukuliwa kwa kufuata nyakati. Lakini inalenga nini, hivyo, katika kipindi hicho hicho? **Siku zile**. Siku zipi? Siku za kuanguka kwa mji wa Yerusalemu.

**Jua litatiwa giza**. Misemo katika lugha ya ufunuo.Angalia: lugha ya ufunuo Kibiblia:

1. **Jua kutiwa giza** inarejea matukio yafuatayo katika Biblia:
    a. Kuanguka kwa Babeli - Isa.13:10,
    b. Dhiki ya Misri - Eze.32:7, na
    c. Siku ya Pentekoste - Yoeli 2:28-31; Mdo.2:20. Matendo ni mfano bora kwa sababu Petro anasema, "Hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli." Hili ni pamoja na "jua litatiwa giza." Je, haya yalitokea halisi siku ya Pentekoste? Hapana, hakuna Myahudi angesema ilitokea hivyo. Inajulika kuwa kubwa, siku iliyo kuu, lakini hayakutendeka halisi.

2. **Nyota kuanguka** inarejea:
    a. Kuanguka kwa Babeli - Isa.13:10, na
    b. Kuanguka kwa Edomu - Isa.34:4.

3. **Akija juu ya mawingu**: mfano wa lugha ya ufunuo yanayohusu kuja Bwana kuhukuhu - Isa.19:1; Maomb.2;1; Eze.30:18. Yesu ananukuu Dan.7:13, "...pamoja na mawingu...Mwana wa Adamu akija..." "Kuja katika mawingu" yanahusu utawala wa kifalme na uongozi wake. Kuanguka kwa Yerusalemu halikuwa jambo la ugaidi la Warumi, bali lilikuwa Yesu akija katika hukumu, "akija mawinguni." Mungu anatawala mataifa. Kwa sababu ya maneno haya hatuhitajiki kutilia mkazo kwamba sehemu hii (29-31) inahusu kuja kwake Kristo mara ya pili, bali kwamba hilo linadhihirisha Bwana kuja katika kuhukumu na kutamka hukumu juu ya Yerusalemu.

Mathayo alitumia neno **akija** mara kwa mara katika njia mbalimbali:
1. Kuja kwake katika Roho siku ya Pentekoste (Math.10:23),
2. Kuja katika maangamizi ya Yerusalemu (Math.24:3), na
3. Kuja kwake siku ya hukumu (Math.25:31ff).

Hivyo basi sura nzima inaweza kugawanywa kulingana na ilivyo.
1. Mistari 1 - 35 kunguka kwa Yerusalemu.
2. Mistari 36 - 51 - kuja Kristo mara ya pili.

**24:32**
**24:33**
Kama vile anaweza kutambua majira ya mtini vile vile, mtu anapoona dalili anazozungumzia (chukizo la ukiwa, n.k.), hivyo anapaswa kutambua hukumu i karibu. Mateso na dhiki hizi haina maana Yesu amewaacha.

**24:34**

**Kizazi** = *genea*, neno lililo muhimu sana. Yesu anatumia maneno haya mara kumi na moja katika Mathayo (11:16; 12:34,39,41,42,45; 16:4; 17:17; 23:33, 36; 24:34). Inahusu kundi la watu ambao walikuwa wanaishi kipindi hicho, na hasa kipindi hicho ambacho Yesu anazungumza. Kizazi hiki, *watu wote ninyi mnaishi sasa*, hamtakufa hata mtakapoona matukio haya ninayoeleza sasa kutukia. Wanaoshikila utawala wa Yesu duniani wa miaka elfu wanasema neno lilipaswa kutafsiriwa "kabila" (pia imefafanuliwa katika maelezo ya chini katika 'New American Standard Version). Kufuatana na fundisho hilo, Yesu anasema, "taifa la Wayahudi" halitatoweka hata hata haya yote yatimie. Taifa la Kiyahudi bado halijatoweka, hivyo kuna mambo ambayo yangali bado kutokea, utawala wa miaka elfu, n.k.). Hapa basi patakuwa ni mahali pekee panapomaanisha taifa katika kitabu kizima.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya msingi kuwa haya yanamaanisha mambo mengine zaidi ya kwamba watu hawa wangeshuhudia unabii wa Yesu wao wenyewe. Kama mtu akitafakari haya kwa kuzingatia wakati, yataleta maana zaidi. Yesu alinena maneno haya karibu 33 B.K., na kuanguka kwa Yerusalemu kulitokea 70 B.K. - miaka 37 tu baadaye. Hakika kuna watu wengi waliosikia unabii wa Yesu na kuishi kushuhudia utimilifu wake.

**24:35**

Wakati mengine yanasimama imara, mengine siyo hivyo. Maneno ya Yesu yatadumu! Tena, yatadumu milele!

**24:36**

Tafadhali angalia mabadiliko ya tofuati - "Lakini kuhusu siku na saa ile." Kuna sababu nne za kuigawa sura hii kama ifuatavyo: Mistari 1-35 - kuanguka kwa Yerusalemu, na mistari 36-51 - kuja kwake Kristo mara ya pili.

1. Kila kitu hadi mst. 36 kimetanguliwa na dalili (mst.15,27,30) wakati kuja kwake mara ya pili hakuna dalili (mst.36,42,44,50). Kabla ya kuona chukizo la uharibifu, radi, na Mwana wa Adamu akija, n.k. Lakini Yesu ajapo tena hapatakuwa na dalili. Kwa nini zisiwepo? Wakati Warumi wakija watu watapaswa kufanya jambo fulani (kukimbia). Lakini Yesu atakaporudi tena, hakuna mtu ataweza kufanya jambo lolote. Kurudi kwake Kristo ni mwisho wa mambo yote. Tutakutwa ama tumejiandaa ama la.

2. Yesu anazungumzia mambo ambayo yatatokea kabla ya "kizazi hiki" kupita (mst.34). Basi, mistari 34 na 35 inajumuisha na kuhatimisha mgawanyo wa awali: kuangamia kwa Yerusalem, mistari 1-34.

3. Matumizi ya viwakilishi vya kuonyesha - "Mambo haya" baina ya "Siku ile." Haya pia yanapinga maoni ya 70 B.K. yanayodai kwamba sura 24 inahusu kuanguka kwa Yerusalem.

4. Mabadiliko kutoka uwingi "**siku hizo**" kuwa "**siku ile**." Kabla ya (mst.1-35) Yesu

anazungumzia matukia ambayo yatatendeka muda wa siku kadhaa. Anapojibu swali la tatu la wanafunzi (lini utakuwa mwisho wa dunia?) Anasema itatokea siku moja tu. Maandiko mengi sana yanataja kuja kwake Yesu kama "siku moja" ya Bwana (Yoh.6:39,40,44,54; 1 Thes.5:1ff; 2 Pet.3:10-13).

Kuanzia mst.36 ni sehemu ya mwisho wa mahubiri. Sehemu hii ni maonyo muhimu zaidi ya kujiandaa.

**JIANDAE**
**SABABU YA MATHAYO 24 & 25**

******24:36-44
*Hatari ya kutojiandaa*. Watu katika siku za Nuhu walionya, lakini hawakufanya chochote kujiandaa kwa ajili ya gharika (Linga. 1Pet.3:20).

******25:45-51
*Hatari ya kuchelewa kujiandaa*. Mtumwa alikuwa na kazi aliyokabidhiwa, lakini anafikiria kwamba bwana wake angesafiri muda mrefu. Kwa sababu hiyo anaacha asifanye lolote na anapata adhabu mbaya sana.

******25:1-13
*Hatari ya maandalizi nusu*. Wanawali watano walijiandaa - kifikia kiwango hicho, lakini haikutosha.

******25:14-30
*Mifano ya maandalizi sahihi na yasiyo sahihi*. Watu watatu walipewa talanta kuzitunza. Wawili walifanya matayarisho na mmoja hakufanya yoyote.

******25:31-41
*Matokea ya maandalizi ya mtu*. Thawabu au adhabu itakuwa ndiyo matokeo kutokana na maandalizi ya mtu.

**Habari ya siku na saa ile hakuna ajuaye**. Mungu ana siku akilini mwake. Ingawa malaika wanaokizunguka kiti cha enzi, hawatambui siri ya mpango wa Mungu. Wala mwana hajui. Tafsiri zote mbili (King James Version na New King James Version) vimeondoa neno "Mwana." Ushahidi wa kuingiza maneno haya ni bayani. (United Bible Society) inatoa kiwango cha 'C,' ikimaanisha kwamba 75% uhakika wa kwamba hayapo katika fungu hili. Kama mtu akijua kila jambo(ana hekima zote), hivyo hawezi kukua katika hekima. Luka anatueleza katika 2:52 kwamba Yesu "akazidi kuendelea katika hekima." Kwa hiyo, hakujua kila kitu kwa sababu, alipokuwa katika mwili, Yesu "alijifanya kuwa hana utukufu" akawa ana mfano wa wanadamu. Hivyo sasa Yesu ameungana na Baba yake, anatambua siku na saa.

Swali kuzingatia Fundisho la 70 B.K.: Je, Yesu alikuwa anazungumzia kuhusu kuangauka kwa Yerusalem katika fungu hili? Maana ya msingi iliyojadiliwa mapema (mstari 1-35) yalikuwa yakiwatayarisha kwa ajili ya maangamizi. Anawapa mawazo jinsi maangamizi yatakavyokuwa. Sasa, basi, (mstari 36-51) Yesu anawaeleza kwamba fungu hili litawajia kama jambo la ghafla. Pia, haileti maana kabisa kwamba Yesu asingejua "siku ile" ya maangamizi ya Yerusalem. Ikiwa hajui, hivyo maana ya awali (kama vile chukizo la ukiwa) haileti maana kabisa.

Ilikuwa mpango wa Mungu kwa malaika na mwanawe wasijue wakati, basi ni ujinga watu kudai kwamba wanajua! Kuna sababu za msingi kwetu kutokujua, na kwamba Mungu alitaka tuishi *tukijiweka tayari wakati wote*. Ikiwa watu wangejua kurudi kwake Yesu mara ya pili, wangeishi

maisha wapendayo, kisha “kutubu” karibia kabisa na kurudi kwake Bwana.

**24:37 Kwa maana kama vile ilivuokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.** Siku zote watu wamejiamulia mambo ya kufanya, bila kujali vile Mungu alivyoamuru.

**24:38**

Yesu hasemi kwamba walikuwa wakijishughulisha na matendo maovu. Hakuna kosa kula na kunywa, na kuoa na kuolewa, n.k. maana yake, matendo haya ndiyo yalikuwa mtazamo wao mkuu. Hawakuwa wakijiandaa kwa ajili ya uzima wao wa milele, bali waliishi kwa ajili ya “sasa.”

**24:39**

Nuhu, mtu mwenye haki, alihubiri kwa miaka 120 akidumu kuwahamashisha wajiandae, lakini hawakuelewa hadi gharika ilipowafika. Kwa kipindi kifupi hicho cha kufa kwao walielewa, lakini walikuwa wamechelewa sana. Iliwafika ghafla bila kutarajia na hivyo ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Yesu mara ya pili.

**24:40**

Kwa maelezo zaidi, Yesu anasema kwamba marafiki wawili (wenzi au wanao shiriki pamoja kazi) watachukuliwa wakati huo huo; mmoja atachukuliwa (kwenda mbinguni) na mwingine kwenda hukumuni). Angalia 1 Thes.4:13-18.

**24:41**

**Aachwa** kwa maana ya kwenda hukumuni, kuachwa kuielekea ghadhabu kubwa ya Mungu. Hapa kuna watu wawili wanaofanya kazi ya aina moja, lakini mmoja anaishi maisha akiwa amejiandaa kwa kuja kwake Bwana, wakati mtu mwingine hajajiandaa. Yesu anasema kwamba “saa iyo hiyo” wote walio makabulini (waovu na wema) watasimama mbele za Bwana katika hukumu (Yoh.5:28-29).

**24:42**

**Kesheni basi**. Iweni tayari kwa sababu...inawezekana ikawa leo!

**24:43**

Zamani za kale nyumba zilijengwa kwa udongo-mfinyazi ambo ulikuwa rahisi kubomolewa. Kama kichwa cha nyumba kingejua kwamba kulikuwa na mwizi kuingia ndani, angemweka mtu wa kumlinda - jirani, ndugu, au polisi. Lakini, kwa kuwa hajui, hivyo lazima achukue tahadhari wakati *wote*. Watu leo wanafanya mambo kama hayo, kufunga milango na madirisha kabla ya kwenda kitandani. Wanafanya hivyo kwa mambo ya mwili.

Tunatakiwa kiroho kufanya vivyo hivyo - kuwa makini daima kwamba maisha yetu yanakubalika mbele ya macho ya Mungu. Kwa njia hiyo hatuhofu Bwana akirudi. Tunatambua kwamba anarudi, kwa hiyo tunaishi tukiwa daima tayari.

**24:44**

**Kwa sababu hiyo**. Kwa kuwa anakuja, uwe tayari pia, kwa sababu Mwana anakuja katika saa tusiyodhani “kuwa anakuja.” Mnaweza “kudhania”, au “kuwazia” lini atarudi tena, lakini hatarudi kipindi hicho. Maneno “mwivi usiku” yanatokea tu katika 1 Thes.5:2. 2 Pet.3:10 anasema Bwana atarudi kama mwivi, lakini haongezi neno “usiku.”

**24:45**

Hapa ni mwanzo wa sehemu ya pili ya *hatari ya kuchelewa kujiandaa*. Kazi ya mtumwa huyu ni kuangalia maandalizi na kuandaa chakula kwa wakati wake. Mtumishi huyu ni:

1. Mwaminifu kutimiza wajibu wake, na
2. Ana akili kwamba amepangili kila kitu vyema.

Hatuwezi kujianda dakika ya mwisho kumlaki Bwana wetu. Maisha yetu lazima tuwe daima tumejiandaa.

**24:46**

Bwana anarejea nyumbani kumwona mtumwa kama amefanya kama alivyoamuriwa kufanya, na mtumwa ni “*makarios*,” (linga. Math.5:3ff). Hivi ndivyo ilivyo hata kwetu. Tutabarikiwa ikiwa tutatekeleza wajibu wetu atakaporudi Bwana.

**24:47**

Mtumishi aliyepewa majukumu, na anatimiza wajukumu hayo, atapewa thawabu - katika hali yake kimwili **na** kadhalika katika hali yake kiroho.

**24:48**

**Anakawia**. Neno lingetafsiriwa “kaa muda mrefu.” (Linga. 25:5,19). Yesu amelitumia neno katika mifano mitatu, akizungumzia maandalizi katika mtazamo wa *kukawia* au bwana aliyechukua muda mrefu.

**24:49**

Mtumwa huyu, aliyekabidhiwa mali nyingi, anatenda kwa ubinafsi na bila kuwajibika. Anaonyesha pia kwamba hajali kuwa ni sawa, na watumwa wengine. Anatumia muda wake na watu ambao kimaadili ni wabaya.

**24:50**

Baadhi ya watu wanaosadiki utawala wa Yesu miaka elfu duniani wanasema hawawezi kutabiri siku na saa, lakini tunaweza kutabiri juma. Lakini kama mtumwa alimtarajia bwana wake kurudi juma hilo, je asingejiandaa? Hakika angejiandaa! Bali anafikiri atachukua **muda mrefu**. Hakika hakutarajia kurudi mara moja.

**24:51**

**Atamkata vipande** = atapigwa na kupatilizwa. Kulia na kusaga meno inaonyesha maumivu makali. Mtumwa huyu amepewa mamlaka makubwa juu ya nyumba ya bwana wake, lakini anaitumia fursa hiyo vibaya hata anakuwa hajali, hauzuniki, na mlevi. Mwangalie sasa...katika maangamizi, amedharaulika na kukataliwa.

## SURA 25

**25:1**

Anaendeleza wazo la kuja kwa Kristo mara ya pili. Sasa tunaendea hatari ya tatu, ya *maandalizi nusu*. Mfano huu ni wa kipekee katika namna mbili.

1. Ni wa pekee kwa Mathayo, na
2. Ni wa pekee kwamba somo lake kuu ni wanawake.

"Wanawali" ni neno "parathanos" likimaanisha wasichana umri wa kuolewa, vijana wa kike.

Walitwaa taa zao. Taa katika kipindi cha karne ya kwanza zilikuwa inchi mbili tatu ukubwa na hazikuchukua kiasi kikubwa cha mafuta. Ikiwa watu walitarajia kuchukua muda mrefu gizani basi walibeba mafuta ya ziada.

**25:2**

Wanawali hawa wanawakilisha walio kanisani, ambao huwa watu waovu na wema. Kuna watu kanisani waliojiandaa kwa ajili ya kurudi kwake Bwana, na wale ambao hawajajiandaa.

**25:3**

Hawalikuwa wapumbavu kwa sababu hawakujiandaa kuchukua mafuta ya ziada kutosheleza urefu wa muda.

**25:4**

Wakati hawakutarajia pengine kuchelewa kurudi kwa bwana arusi, walifikiria mbele na kujiandaa kwa uwezekano huo.

**25:5**

Neno **alipokawia** ni sawa kama katika 24:48; 25:19.

**Wakasinzia wakalala usingizi**. Hakuna kosa lolote kuhusu ukweli wa kulala usingizi. Hawakulaumiwa kwa sababu hiyo.

**25:6**
**25:7**
**25:8**
**25:9**

Kila mtu anawajibu wa kufanya maandalizi yake. Katika mifano yote kulikuwa na maduka yalikuwepo wazi kwa wakati huu.

**25:10**

Wale wote waliokuwa tayari, waliokuwa wamejiandaa, waliingia katika sherehe. Angalia - mlango ulifungwa.

**25:11**

Bwana - linga. Math.7:21

**25:12**

Maana yake ni...

**25:13**

Kwa sababu hatujui siku wala saa, tunatakiwa kujiandaa (linga.24:36,42,44,50).

****Angalia katika "Wanawali Kumi.*"

**25:14**

Sasa anajadili *mifano ya maandalizi sahihi na yasiyo sahihi*. Mfano huu unasisitiza kusudi la kufanya kazi wakati tukikesha. Wenye busara ni wale wote wanaotumia muda wao kwa busara wakimsubiri Bwana. Wanatumika wakimsubiri

**25:15**

Talanta ni sawa na dinari 6,000. Dinari moja yalikuwa ndio malipo ya kutwa, hivyo hii 6,000 ni malipo ya kutwa. Talanta tano ziligawiwa kwa mmoja, mbili kwa mwingine, na moja kwa wa tatu. Talanta siyo vipaji, bali ni mali ambayo Mungu amembarikiwa mtu kuwa nayo. Mtu ni lazima atumie uwezo Mungu aliomgawia! Mali (talanta) aligawiwa mtu kulingana na uwezo wa mtu kutumia talanta hizo. Mtumishi mmoja alionyesha uwezo kuzitumia talanta tano, basi walipewa zaidi kuliko wengine. Kila mwanadamu anaonekana kustahili kupokea baadhi ya talanta (na kutumainiwa na Bwana). Kibaya zaidi watu wengine husumbukia walichogawiwa watu wengine; hata wanashindwa kushukuru kile walichogawiwa.

**25:16**
Hakupoteza muda, akaenda mara moja.

**25:17**

Akimaanisha mara moja, vile vile.

**25:18**

Mfano wa hii ni kama hazina iliyositirika katika shamba - 13:44. Angalia kwamba wakati wengine "mara" wakaenda kazini, mtumwa yule mwovu alionekana "mara" akaifukia ya kwake. Tabia yake inaonekana kwamba alishindwa kabla ya kuanza. Kamwe hakuwahi kujaribu kuifanyia chochote talanta!

**25:19**

Kwa mara tatu, **siku nyingi**. Alikawia. Walitambua kwamba angekuja baadaye. Pia walitambua kwamba atakapokuja angeona jinsi gani wametumia walivyokabidhiwa. Ingawa alichukua muda mrefu, siku ya kurudi kwake imefika.

**25:20**

Alionyesha thamani yake kwa bwana. Alidhihirisha alistahili kupokea talanta tano.

**25:21**

Bwana anasema mambo mawili kuhusu mtumwa huyu.

1. Ni **mwema**. Alifanyia kazi mali aliyopewa, na hakufanyia kwa matumizi mabaya.

2. Ni **mwaminifu**. Alikuwa mwaminifu katika kuwajibika katika kazi aliyodhaminiwa.

**25:22**
**25:23**

Amefanya vile vile, akisha pata faida ya mbili zaidi. Alitumia aliyopewa na, kama matokeo ya uaminifu wake wa kuwajibika katika kazi yake, Bwana atamzawadia zaidi ya alivyotarajia. Angalia - kila mtu alihukumiwa kulingana na jinsi alivyofanya na alichopewa; pasipo kulinganishwa na wengine, au na walichopewa wengine.

**25:24**

Gal.6:7 - "Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Kutokana na mtazamo wa mtumwa huyu Bwana ni mtu mgumu, huvuna asipopanda, hutaka zaidi ya matarajio halali. Maana yake si kwamba Bwana hapandi wala kuvuna, bali kwamba *anamwezesha* mtumwa wake kufanya hivyo kwa ajili yake. Hakutaka chochote toka kwa mtumwa ambacho, binafsi, asingeweza au hawezi kufanya. Mungu ametukabidhi sisi, anatuwezesha sisi, kufanya kazi. Tunauwezo, na Mungu anafahamu wajibu wetu. Kwa maana ya uwezo huo anatuwezesha na kutupatia vitu ili tuweze kutumia uwezo huo kwa ajili ya utukufu wake. Jambo la huzuni hapa si kwamba mtumwa alikabidhiwa talanta moja. Jambo baya zaidi ilikuwa alishindwa kutumia talanta yake moja.

**25:25**

Ikiwa hayo tu ndiyo Bwana yalimhusu, angeweza kuitunza. Mtumwa huyu alipewa wajukumu mepesi kuliko wale watatu, lakini hakupata zaidi ya uwezo wake iwapo *angejaribu*. Alikuwa anaogopa kukosea, lakini makosa yake makubwa yalikuwa kutokutumia uwezo aliopewa.

**25:26**

Aliwaita watumwa wengine "wema na waaminifu." Huyu anamwita kama "mbaya na mlegevu."

1. **Mbaya**. Kwa sababu ya tabia yake, na mawazo yake juu ya, bwana wake.
2. **Mvivu**. Kwa sababu alikuwa hataki kuifanya lolote talanta.

Mungu anatarajia kwetu kumzalia matunda katika ufalme wake, siyo tu kurejeza kwake kile alichotupatia (linga. 24:14). Atatuhukumu siyo tu kwa yale tunayofanya, bali pia kwa yale ambayo hatukufanya.

**25:27**

Sheria ilimkataza Mwebrania kumtoza riba ndugu yake. Kumb.23:19; Kut.22:25; Zab.15:5 inaonyesha kwamba iliruhusu kutoza riba kwa wasio Waebrania. Edmond Burk alisema, "Hakuna makosa makubwa kuliko mtu asiyefanya lolote kwa sababu tu asingeweza kufanya lolote." Mfano ni wa mtumwa huyu haswa!

Katika kanisa kila mtu ana uwezo tofauti na vitu mbalimbali alivyokirimia. Kuna wengine wanaweza kufanya kazi kubwa kuliko wengine, na ni bora kuliko wengine. Lakini hilo halitoi udhuru wa mtu kutokufanya *chochote*!

**25:28**

Kisichotumika, kimepotea! Yesu anaonya juu ya kuwa wavivu, walegevu .

**25:29**

Ebu fikiria binafsi kitu gani Mungu amekugawia. Ni kutu gani unamzalishia? Tunapaswa kuwa watu kumzalia matunda! Mungu ametujalia na vitu ambavyo vinaweza kuletea utukufu na kuuzidisha ufalme wake. Basi na tutumie kile alichotujalia!

**25:30**

2 Kor.5:10 - "Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya."

**Asiyefaa** = asiyezalisha. (Linga. 24:51; 13:42,50; 22:13. Mifano hii inaleta matokeo ya kupata thawabu na hukumu. Kuwajibika kumetarajiwa).

**25:31**

Huu ni mwanzo wa sehemu ya mwisho ya kujiandaa: *matokea ya mtu kujiandaa*. "Atakuja pamoja na malaika wa uweza wake, wakilipiza kisasi." 2 Thes.1:7.

Kiti cha utukufu. Atakuja na kuketi katika kiti chake cha enzi kwa kusudi la hukumu. Katika Yoh.19:13 Pilato alipokuwa akiamua juu ya Yesu, aliketi chini. Watasimama kusikia ushahidi, na kisha kuketi kutoa hukumu. Jambo hili ni wazi katika mst.32.

**25:32**

Mataifa yamekusanyika kwa ajili ya hukumu yao wakibaguliwa (linga. juya Math.13:47, 48; ngano na magugu - Math.13:30).

Katika Palestina kondoo na mbuzi huchungwa pamoja, lakini wakati maalum (kulingana na matakwa ya mchungaji) hubaguliwa hutendeka. Kwa hiyo tunaona tena mfano wa watu wabaya na wema wakiwa pamoja hadi hukumu.

**25:33**

**Kulia** ni mahali sahihi. Yesu ameketi upande wa kulia wa Mungu - Ebr.12:2. Kushoto ni mahali kusikofaa.

**25:34**

Ana jambo la kusema kwao walio kulia: Njooni - hapa tunaona mwaliko. Wanakaribia kupokea thawabu. Wako mahali pazuri kwa sababu Baba ameyashuhudia maisha yao, ibada, kujitoa kwao.

**Urithini**. Wazo la kitu kupata kutoka kwa mwingine kwenda kwa mtu mwingine. 1 Pet.1:4 urithi wetu imetajwa kuwa usioharibiki, usio na uchafu, usionyauka." Watarithi "ufalme." Je, fungu hili linazungumzia kanisa? Je, watarithi kanisa? Hapana. Hapa ni mfano mwingine ambapo ufalme umetajwa lakini hauhusu kanisa. Lazima kila fungu lijadiliwe kwa kujitegemea na kuruhusu mazingira kuamua ikiwa neno "ufalme" linahusu kanisa au utawala wa Mungu wote.

**Msingi wa ulimwengu**. Katika 1 Yoh.14:1-3 tunaona kwamba mbinguni ni mahali palipoandaliwa kwa ajili ya watu waliojiandaa. Hili linaonyesha kusudi la Mungu la kuwapa thawabu wenye haki hata kabla hajachukua hatua za uumbaji. Sababu ya kurithi, imetolewa mst. 35ff.

**25:35**

Yesu anataja aina 6 ya mambo ya kumtumikia. Wengine ni wagonjwa kimwili. Wengine wamepungukiwa na chakula na kinywaji. Watu hawa waliyashughulikia mahitaji ya Bwana, lakini hawakudhamiria huduma waliyoifanya. Hawakutambua kwamba walikuwa wakimhudumia Yesu. Yesu anajibu katika mst. 40, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Hawakufikiria kwamba walimhudumia Yesu. Nikimsaidia mtu mwenye njaa chakula, ni sawa na kumsaidia Yesu chakula.

Kuna watu wanaodai kuwa ni wenye haki, watu wa kiroho lakini hawasaidii watu wengine. Lakini ikiwa Yesu angekuwa hapa wangeliweza kumsaidia. Wengi wetu hatuna vitu au mali nyingi, lakini tulichonacho kichache tungeligawa pengine kwa ukarimu kwa Yesu ikiwa angelikuja kuishi pamoja nasi. Yesu anasema kwamba kuwatumikia wengine ni sawa na kumtumikia yeye. Yohana anatueleza kwamba hatuwezi kumpenda Mungu ikiwa hatuwapendi watu wengine (1 Yoh.4:19-20).

**25:36**
**25:37**
**25:38**
**25:39**
**25:40**
**25:41**

Mungu ameandaa mahali kwa ajili ya Bwana na malaika wake (linga. Ufu.12:9; 19:20). Yesu sasa anatoa mfano kwa watu wasio wasaidia watu wengine. Moto wa milele umewekwa kwa ajili yao. Adhabu ya milele itakayotolewa ambayo Mungu ameiweka tangu awali imefundishwa hapa wazi wazi. Walimtumikia shetani katika maisha haya, na watakuwa pamoja naye milele katika maisha yajayo. Sababu ya kupokea hukumu hii imetolewa katika mistari inayofuata:

**25:42**

Waliacha kuwatendea watu na, kwa kufanya hivyo, waliacha kumtendea Yesu.

**25:43**

Katika Mdo. 9:4 Sauli alishutumiwa kuwa alimwudhi Yesu, ingawa haswa, alikuwa akiwatesa wanafunzi wake Yesu. Mstari huu unatusaidia kama mfano wa kile Yesu anachofundisha hapa. Hawakumtambua Bwana katika mahitaji ya watu. Wanakana dai hili alilowashutumu, kwa kuwa hawakuwahi kumwona Yesu akiwa ana njaa au na kiu au mgeni, au uchi, au mgonjwa, n.k. Kustaajabu kwao kunalingana na 7:22. Wanajaribu kujitetea kama katika 7:23 walivyofanya. Pia walimwita yeye kuwa **Bwana**.

**25:44**

Walitambua uweza na mamlaka yake - sasa - na siku ile ya hukumu. Hawakuwahi kumfanya yeye kuwa Bwana wao, kiongozi wao, mwenye mamlaka katika maisha yao.

**25:45**
**25:46**

Wakati uzima wa milele ni kwa wenye haki, adhabu ya milele itakuwa kwa ajili ya waovu. Kubaguliwa na hukumu ni hatua ya mwisho! Juu ya mambo yote mtu anayoweza kutarajia kuwa katika habari za mbinguni kujifunza kinachookoa na kinachohukumu mtu, si jambo la ajabu kujifunza kwamba ni...kutumika tu? Hata hivyo, hatutakiwi kuweka mkazo katika fungu hili na kuacha mengine juu ya jinsi kufanya ili tupate kuokoka.

Kila mmoja atayesimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu siku ya hukumu watakuwa na wajibu muhimu na mali alizopewa kutekeleza mambo haya sita; wengine kiwango kidogo kuliko wengine, walakini hata maskini kabisa wanaweza kutoa kikombe cha maji, au kutembelea walio wagonjwa. Yesu haombi kwa mtu yeyote kitu asicho na uwezo nacho. Matendo ya Mkristo siyo ndiyo yanastahili wokovu. Hukumu yetu itakuwa sawasawa na jinsi tulivyofanya na hivyo, kwa urahisi, ndio wajibu wetu kwa yale Mungu aliyotutaka tufanye. Kama tunampenda, hivyo tutashika amri zake. Ikiwa tutahukumiwa itakuwa ni kwa sababu hatukumpenda yeye. Siku hizi Amerika, serikali hutoa wanachohitaji watu maskini; chakula, nguo, nyumba, madawa, n.k. Utaratibu huo hauondoi wajibu wa Wakristo kutii maagizo ya Kristo kutafuta, na kuona njia za kumtumikia mwanadamu mwingine - hasa walio nyumbani mwa Mungu. (Linga. Gal.6:10).

SURA 26

**26:1**
**26:2**

Pasaka iliangukia siku ya 14 ya Nisani (March/April).

Sehemu ya mateso hii ya #7.

**26:3**

Kayafa alikuwa mkwewe na mrithi wa Anasi. Aliteuliwa kuwa kuhani mkuu na Gratiani, ambaye alikuwa liwali aliyemtangulia Pilato. Alikuwa na nafasi kama aliyokuwa nayo Pilato. Kayafa alishika nafasi kutoka 18-36 B.K.

Katika Agano Kale mtu mmoja alitumika wakati mmoja; na ofisi ilirithiwa, na ilikuwa kwa uhai wake wote. Hata hivyo katika Agano la Jipya viongozi wa Kirumi walijitwalia madaraka ya kumteua kuhani mkuu kwa akili zao. Kati ya 37 K.K. na 67 B.K. kulikuwa na watu ishirini na nane waliokalia ofisi ya kuhani mkuu. Kayafa ni mmoja wao. Watu hawa walitaka kumpatia Kayafa wajibu wake, lakini pia hawakutaka aache wa Anasi. Ndio maana wote wamehusika katika kuhukumu. Kayafa alitambuliwa kama kuhani mkuu na Warumi.

**26:4**

Hakuna shaka walikuwa na jambo moja tu akilini. Hata hivyo, waliogopa makutano. Basi walitaka mambo yao yawe ya siri, bila watu kufahamu.

**26:5**

Walitambua kwamba wasingemkamata siku ya Pasaka kwa sababu ya namna watu walivyo mtazamia Yesu. Sherehe zilikwisha kwa siku nane na watu wengi wakiwa wamekusanyika, wakati huo ulikuwa mbaya.

**26:6**

Mkoma, kulingana na sheria, alikatazwa kuungana na watu (Law.13:45). Mawazo hapa ni kwamba Simoni alikuwa ameponywa, lakini alikuwa amejulikana bado kama “mkomo.”

**26:7**

Marko, katika sura 14, anatueleza gharama yake zaidi dinari 300, ambazo zilikuwa kipato cha mwaka mzima. Yohana anatueleza kuwa jina lake alikuwa akiitwa Mariam, na kwamba Yuda alijaribu kuzuia kutafuta sifa (Yoh.12:3-5).

**Akaimimina...chakulani**. Hili lilikuwa tendo la kuwakarimu wageni. Zab.23:5 -”Umenitia mafuta kichwani pangu.” Lk.7:46 ni fungu linalolingana.

**26:8**
**26:9**

Yuda hakuwa hasa akitaka kuwapa maskini fesha hizi.

**26:10**

Anazungumzia kwao waliofikiri ni kupoteza fedha. Alionyesha upendo, imani, kutokuwa mchoyo. Yesu alistahili kupewa heshima, na mwanamke huyu ni kati ya wachache wenye kuelewa hilo. Hata wanafunzi hawaelewi hili.

**26:11**

Kumb.15:11 anazungumzia maskini, wamekuwepo daima katika jamii, na fursa ya kuwasaidia. Anajibu mst. 9. “Kwa maana maskini mnao siku zote pamoja nanyi; lakini mimi hamko pamoja nami.” Fursa hii ilikuwa kwake ya kipekee kufanyia Bwana, na akaitumia. Yesu akamsifia kwa ajili ya hilo.

**26:12**

Kama vile mwili mfu unavyoandaliwa kwa ajili ya mazishi - hupakwa na kuviringishwa nguo - Yesu anatumia jambo alilolifanya kama tendo la kumfanyia maandalizi. (Linga. Yoh.19:39-42).

Sehemu hii ya mateso ni ya #8 (tangu kukiri kwake Petro katika sura 16).

**26:13**

Atasifiwa kwa ajili ya mfano wake bora wa kutoa sadaka na kutokuwa na uchoyo. Hakika injili imehusisha alichofanya mwanamke huyu.

**26:14**

Angalia hila za Yuda katika kulinganisha na kutoa, bila choyo, kitendo cha Mariamu. Moja ya jambo baya katika huduma yake Yesu ni kwamba alikuwa na miongoni mwake na atakaye msaliti.

**26:15**

Haya yalikuwa malipo kwa ajili ya mtumwa aliyejeruhiwa (Kut.21:32; linga. Zaka.11:12). Maelezo ya Yuda yalikuwa sawa kabisa na jinsi wakuu hawa waliyohitaji. Yuda angelijua njia na tabia za Yesu, na angeliweza kuwaongoza kufika sehemu mbalimbali za siri ambazo Yesu alikwenda pamoja na wanafunzi wake - Yoh.18:2.

**26:16**
**26:17**

Pasaka ilisherehekewa usiku mmoja, na siku saba zilizofuata zilikuwa za mikate isiyotiwa chachu.

**26:18**

"Muda wangu umekaribia" ni fungu la msingi sana katika Yohana. Inadhihirisha kwamba Yesu anajua kwamba alikuja duniani kufa, na sasa kifo chake kimekaribia.

Nitaifanya...pamoja na wanafunzi wake. Mtu asiyetajwa jina lake ana vitu (vifaa alivyokuwa navyo) vya kutoa, na anapenda kutoa kwa Yesu kutumia nyumba yake kwa ajili ya chakula cha Pasaka.

**26:19**

Yale Yesu aliyowaambia kufanya, wanafunzi walifanya! (Je, sisi tunaitika haraka?) Maandalizi ya Pasaka yanaweza kuonekana katika Mishnah, Pesachim 1:1; 4:1; 10:1ff.

**26:20**

Kusanyiko hili lilikuwa tu kwa Yesu na mitume wake kumi na wawili.

**26:21**

Pasaka ilisherehekewa kukumbuka Mungu alivyoruka nyumba zilizokuwa na damu katika miimo ya milango yao. Wakati mitume na Yesu wanafikiria kuhusu wokovu wa Mungu toka katika utumwa, Yuda anafikiria kumpeleka Yesu utumwani.

**26:22**

Wanafikiri mioyoni mwao kwamba hawakusudii kamwe kufanya jambo ovu kama hilo.

**26:23**

"**Aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe**" sawa na neno "aliyebatiza." Kuchovya, kutia mkono ndani ya bakuli. Katika ulimwengu wa Mashariki watu walichovya mkate katika bakuri, na kumsaliti mtu unayekula naye inadhihirisha ugumu wa moyo, kwa sababu chakula kinaonyesha ushirikiano wa pamoja, upendo, na undugu katika kushirikiana bakuli moja.

**26:24**

Hata ingawa Agano la Kale lilitabiri kwamba mtu mmoja angemsaliti Yesu, halikumaanisha kwamba msaliti huyo hatawajibika kwa kitendo chake.

**26:25**

Yesu anajibu kwa kukubali. Wanafunzi wengine wanaonekana kutoelewa yale yanayotendeka. Yuda anashangaa kweli kwa yanayoendelea kwa sababu haamini anayokwenda kufanya kuwa mabaya. Yesu anapotumia neno "kunisaliti" katika mst. 24, Yuda hata hakufikiria kwamba alikuwa akisemwa yeye. Alitambua kwamba kuna jambo alikuwa akifanya, lakini hakufikiria kwamba hilo lilikuwa ni kumsaliti.

**26:26**

Mwana wa Mungu alitambua wapi baraka zilikuwa zikitoka. Kama yalivyokuwa maisha yake, alitioa shukurani.

Neno lililotumika hapa ni "metonymy", lugha ya picha akisema kitu fulani kinachosimama kitu kingine. Mkate si mwili halisi wa Kristo, bali ni *badala* yake.

**26:27**

Aliwaita wote washiriki. Je, ni pamoja na Yuda? Hatujui kwa uhakika. Pengine alikuwa amendoka tayari (linga. Yoh.13:26-30).

Mathayo anaandika kwamba Yesu alichukua **kikombe**. Hakuna jambo la maana kuhusiana na chombo hiki. Kwa kudhania tu kilikuwa moja ya vikombe vinne vilivyotumika kipindi cha chakula cha Pasaka.

**26:28**

Damu ya Yesu ilimwagwa kwa kusudi mbalimbali - "msamaha wa dhambi" (linga. Efe.1:7; Mdo.2:38; 22:16). Damu hii ilimwagwa kwa ajili ya wengi - msemo unaoweza kumaanisha:

1. Watu wengi wanaoishi,
2. Wengi ambao watachukua fursa ya kutii injili,
3. Wote - kwa kuwa Biblia haiungi mkono fundisho la upatanisho kwa wachache. Yesu alimwaga damu kwa watu wote (20:28; Ebra.2:9; 2 Kor.5:14,15).

Damu ya agano. "Agano" ni neno la Kibiblia lenye maana sana. Agano ni mapatano au mkataba baina ya watu wawili au zaidi. Damu hutia muhuri, au huakiki, agano tulilonalo na Bwana. Bila ya damu agano haliweza kuwepo. Hakuna njia ya sisi kuwa na uhusiano na Mungu bila ya kumwaga damu yake Yesu (Ebr.9:15-22).

**26:29**

Anarejea katika meza ya chakula ya Masihi (Isa.25). Anawapa moyo kwamba siku moja watafurahia mahusiano yasiingiliwa kati. Ni ufalme wa nani watakunywa huu? **Ufalme wa Baba yake**. Hapa hapahusu kanisa, bali mbinguni. Mara nyingi mtu atatoa sala katika meza ya Bwana na kusema kwamba mzao wa mzabibu "unasimama, au ni badala ya," damu ya Yesu. Wazo la Katoliki la kuwa mzao wa mzabibu unageuka kuwa damu halisi ya Kristo (baada ya kuibariki).

Lakini Yesu anasema “hii ni damu yangu” na pia anataja kuwa “mzao wa mzabibu.” Mzao wa mzabibu haukugeuka kuwa damu yake. Siyo damu halisi ya Yesu, bali inawakilisha damu ile.

***Angalia makala: “*Kusudi la Chakula cha Bwana*.”

**26:30**

Kuimba nyimbo ilikuwa desturi ya wakishakunywa kikombe cha nne na chakula cha Pasaka.

**26:31**

Linga. Zaka.13:7. Yesu amehuzunika kwa sababu baadhi yao watachukizwa kwa ajili yake, lakini hilo halina maana kwamba walikata tamaa juu yao. Alikuwa na imani kubwa katika mitume ambao walikuwa pamoja naye kwa miaka mitatu, na ingawa walichukizwa - na watachukizwa tena, anapenda kuwasamehe.

**26:32**

Hili ni fungu #11 la mateso.

**26:33**

Petro kwa ujasiri anadai angekuwa tofauti na wengine.

**26:34**

Kabla ya usiku, Petro atakuwa amemkana Yesu mara tatu.

**26:35**

Petro hakuwa kamwe mwoga, wala hakuwa mtu mwenye wasiwasi. Petro alijiandaa kwa vita, kufia katika mapambano makali; akifa wakati akipambana kwa ajili ya Bwana, akisaidia kuutwaa ufalme.

**26:36**

“*Geth*” ni neno la Kiyunani “kinu cha kusindika”, na “*semane*” ni neno lenye maana “shamba la mizeituni.” Yesu anakwenda hapo kusali.

**26:37**

Wana wa Zebedayo ni Yakobo na Yohana. Yesu hakika ni mwanadamu, na ni mtu wa huzuni.

Kuhuzunika maana yake alifikiri mno na alifadhaishwa moyoni.

**26:38**

Alitaka wajihadhari, wawe makini, kuwa macho. “Mkeshe pamoja nami”, kama ni si kwa sababu nyingine isipokuwa kupata msaada wa uadilifu. Hawatambui hata ni kitu gani wanatakiwa wakeshe kwacho, pengine Petro alikuwa akifikiri kuhusu jeshi.

**Huzuni...kufa** hayatokei haya msalabani, bali huzuni iliyokuwa mst.37. Lk.22:41-44

panazungumzia kuhusu jambo hili.

**26:39**

Kufikia hapa Yesu anafikiria kama kungekuwa na njia nyingine ya mpango wa Mungu kutekelezwa.

**Ikiwezekana...lakini mapenzi yako**. Hazungumzii kuwa Mungu anaweza au hana uwezo, bali inawezekanaje, katika kutimiza mpango wako, kuniepuka kikombe hiki? Katika Math.20:21,22 Yakobo na Yohana walimwendea wakitaka kuketi mmoja kulia na mwingine kushoto katika ufalme. Yesu aliwauliza kama wanaweza kunywa "kikombe" chake. hiki ndicho kikombe Yesu alikuwa akizungumzia; mateso. Yesu alipendelea asingekunywa kikombe, walakini alitaka ayafanye mapenzi ya Baba yake, na kupitia kifo ambacho kulikuwa mbele zake. Tabia zetu zingelikuwa kama ile ya Yesu. Anachotaka Mungu ni muhimu sana kuliko tunachotaka (linga.Gal.2:20; Efe.2:1; Fil.2:5-8, 13; Ebr.5:8-9).

Ebr.12:1-13 Yesu alistahimili msalaba. Sasa ni wakati wetu kukimbia mbio, na kuweka kando kila dhambi ituzingayo kwa upesi.

Hili ni fungu la #12 la mateso.

**26:40**

Petro ambaye muda si mrefu alijisifia kuwa mwaminifu kwa Yesu, hakuweza hata kukaa macho kwa saa moja tu! Inawezekana hili lilimletea Yesu ajisikie "upweke" Yesu lazima anajisikia kama inavyoonekana katika usemi wake, "Mbona Umeniacha?" Alihitaji faraja haswa kutoka kwa marafiki zake, na hatabaki hata macho wamfariji.

Rum.7:14ff. Wakati mwingine tunatumia neno "mwili" kama udhuru wa kutofanya mapenzi ya Mungu. Yesu aliushinda mwili, na akautawala. Hakuruhusu umtawale.

**26:42**

Yesu yu karibu na kukata tamaa muda huu, akishatambua kifo chake kuwa ni lazima. Tunatakiwa kutambua uweza wa Yesu anaoudhihirisha. Angesema, "Inatosha maana yake inatosha!" akawaita jeshi la malaika. Upendo kwa wanadamu ndio uliomfanya aende msalabani. Hakika hili **halitaweza** kupita - hakuna njia nyingine.

**26:43**

Amedhoofu kimwili na kiakili. Ni jambo gumu kwao kubakia macho.

**26:44**

Aliuliza Yesu mara tatu. Mara tatu alikanwa. Kama Mungu hawezi kubadilisha mpango wake kwa ajili ya mwanawe mpendwa wa pekee, je kwangu mimi na wewe.

**26:45**

Wakati umefika. Kusalitiwa kumekaribia. Kutimia kwa maandiko kama Isa.52-53 u karibu kutimia.

**26:46**

Yuda amekamilisha kazi yake. Yesu ametambua kwamba wanamfuata yeye.

**26:47**

Tunatambua kwamba Yuda alikuwa mmoja kati ya mitume kumi na mbili, lakini Roho Mtakatifu amemvuvia Mathayo kutukumbusha mara nyingine. Ni jambo muhimu kuona kwamba mmoja kati ya marafiki wa karibu wa Yesu kuwa msaliti. Yuda ni mfano mzuri kuona kwamba mtu kuwa karibu zaidi na ukweli lakini ashindwe kuona ukweli. Pia, ukweli kwamba Yuda na usaliti wake umetajwa katika vitabu vya injili vyote, ikionyesha kuwa lilikuwa zito na lenye wazo la kipekee kwa waandishi kama Roho Mtakatifu alivyoona vyema kulirudia, tena na tena.

**26:48**

Wanataka kuhakiki kwamba hawamkamati mtu mwingine tofauti. Wanamtaka Yesu tu. Busu nzito ya Yuda (*katephilesen* kama kinyume cha *phileso*, kama busu rahisi) ndio ushahidi ambao wakuu walihitaji kumtambua.

**26:49**

Kuna njia mbili kuangalia haya:

1. Kama unafiki mkubwa. Yuda hakujisikia upendo kwa Yesu, au
2. Amemtambua Yesu kuwa mwalimu mkuu na anamshawishi ajitangaze kuwa mfalme wa (duniani) Kimasihi.

**26:50**

Ndipo walipomwendea, wakaweka mikono yao juu yake, na kumkamata. Akishakuwa ametambua yale yote ambayo Yuda aliyofanya, na anayofanya, Yesu bado anamwita "rafiki,"akikabiliana na Yuda kwa upendo. (Angalia: kila mara, katika Mathayo, Yesu anapomwita mtu fulani "rafiki", yuko katika kutenda makosa.)

**26:51**

Tunatambua kutoka katika kitabu cha Yohana kwamba mtumishi aliyekatwa sikio lake la kuume alikuwa Marko - Yoh.18:10. Luka pia anatueleza kwamba lilikuwa sikio la kuume (Lk.22:50).

**26:52**

Kuzuia ni jambo bure. Kutumia nguvu kunaleta kulipiza kisasi na kutumia nguvu zaidi. Yesu anataka kutawala hali hiyo. Anaeleza hivyo kwa Pilato katika Yoh.18:36 sababu ya watumishi wake kutokupigana ni kwa kuwa ufalme wake si wa ulimwenguni hapa; si ufalme wa kidunia.

**26:53**

Majeshi ya malaika kumi na wawili ni malaika 72,000. (Jeshi moja lina watu 6,000). Pamoja na uweza ambao malaika wanao, majeshi ya Yesu hasingeshindwa kamwe.

**26:54**

Yesu alikuwa akitambua kusudi lake kuwa ni kutimiza unabii wa Agano la Kale. Alikuja autoe uhai wke kwa ajili ya ukombozi wa watu wengi - Math.20:28.

**26:55**

Yesu anawakemea kwa kumjia kama mtu mwenye hatia, giza lilipotanda. Kwa nini walimwendea namna hii? (Angalia wafuasi wa Shetani wanafanya kazi usiku, pia). Hawakuweza kumkamata wakati wa mchana. (Hapo awali walisema kwamba waliongopa makutano.)

**26:56**

Siyo tu unabii kuhusu kusulibiwa umetimia, bali unabii wote toka Musa hadi Malaki. Wote umekutana msalabani. Hayo ndiyo malaika walitamani kuyaona, 1 Pet.1:10-12; (linga. Efe.3:10-11; Kol.1:16). Yote yale ambayo Mungu alitaka kumtendea mwanadamu yaliyokuwa mema yameonekana katika Yesu. Angalia pia Lk.24:44-46.

**26:57**

Kufuatana na Mishnah (Sanhedrin 4:1) isipokuwa hukumu imetendeka mchana, ndipo hukumu ya kifo haiwezi kutolewa. Je, hii ni kumsikiliza kwa mwanzo kuona kama kuna ushahidi wa kutosha, au ni jambo lililo kinyume na sheria?

Sanhedrin ilikuwa na watu sabini na moja ikingozwa na kuhani mkuu, lakini baraza ya watu ishirini na tatu ndilo lililo hitajika kusikiliza kesi. Hawa ishirini na tatu walichaguliwa kwa makini sana! Kulikuwa na wengine miongoni mwao, kama vile Nikodem, ambao wasingeunga mkono wa jambo hili.

**26:58**

Akimfuata. Petro alikuwa akimfuata Bwana kutoka mji hadi mji, kutoka nchi uande wa Palestina, bali sasa anafuata **kwa umbali**. (Je, tunafuata kwa umbali?") Katika kitabu cha Yohana tunaona kwamba Yohana binafsi alifahamika na kuhani, aligeuka na kumpitisha Petro mlangoni - Yoh.18:15,16.

**26:59**

Wanajiandaa kutoa ushahidi wa uongo. Moja ya Amri Kumi ni "Usishuhudie uongo..."

**26:60**

Ushahidi waliokuwa nao hakutosha kuleta matokeo ambayo waliyataka. Kumb.19:15. Sheria ilifundisha mashahidi wawili au watatu wathibitishe jambo na kumshitaki mtu kuwa ana hatia.

**26:61**

Linga. Yoh.2:19. Marko 14:58 anaonyesha kulikuwa na kutokukubaliana na maelezo ambayo ushahidi wa mashahidi hawa wawili, na ikathibitika kwamba ni mashahidi waongo. Mashahidi wa uongo walitakiw wauawe, hivyo basi Sanhedrin inawezekana ilifanya jambo fulani kuwashawishi washuhudie uongo (kuhatarisha maisha yao wenyewe).

**26:62**

Kwa kuchagua kwake kufanya mapenzi ya Mungu, ameamua kutojitetea mwenyewe.

**26:63**

Mathayo ameeleza tayari kwamba Yesu angemshida kila mtu. Angeweza kujibu yeye binafsi kuhusu hayo. Kunyamaza kwake ni kwa sababu alikusudia kwenda msalabani. Tunatambua kwamba Yesu aliomba ili aweze kuokolewa na hilo, na aliweza kujilinda mwenyewe, lakini hakuweza kufanya hivyo. Huo ndio upendo kwa vitendo. "Wala hakufunua kinywa chake...kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni...kondoo anyamazavyo mbele ya yao wakatao manyoya..." Isa.53:7.

**26:64**

Anamwapisha Yesu atoe jibu moja kwa moja kutokana na swali. Yesu hajitambulishi mwenyewe kutokana na mawazo yao ya kutomjua Masihi, lakini kama Mwana wa Adamu katika Danieli; ambaye ndiye atakaye hukumu baadaye watu wote.

**Mwana wa Adamu akiketi mkono wa kuume wa nguvu**. Yesu ametajwa kuwa wa mbinguni katika mafungu mawili ya Agano la Kale:

Zab.110:1 Akiketi mkono wa kuume wa nguvu.
Dan.7:13 Akija pamoja na mawingu kutoka mbinguni. Mawingu pia yakitumika katika mazingira ya hukumu.

**26:65**

Kusingelikuwa na hitaji la mashahidi wengine. Chini ya Sheria ya Musa kukufuru mshahara wake ni kifo (Law.24:10-16; linga. Sanhedrin 7:4-5).

**26:66**

Ujinga wa mahakama hii umeonekana hapa. Hakuna jambo lolote lililofanywa linalostahili kifo. Ni wazi kwamba haya yalikuwa yamepagwa mapema.

**26:67**

Haya yalikuwa kudhalilisha haswa. Kumebaki hata leo. Angalia Hes.12:14; Kumb.25:9; Isa.50:6.

**26:68**

Walijumuisha madhalilisho yao pamoja na dhihaka na kumpinga.

**26:69**

Wakati Yesu amekwisha kupigwa na kutendewa mabaya. Petro ameketi nje, asijue kilichokuwa kikiendelea ndani ya kuta mahali pa kuhani mkuu.

**26:70**

Alikana mbele ya watu "wote." Kundi zima la watu lilishuhudia alichosema Petro.

**26:71**

**26:72**

Katika hali ya kukata tamaa Petro anajisikia kuzidisha kukana kwake. Basi anakana kwa kuapa, au ahadi nzito - kwamba hamjui Yesu.

**26:73**

Tafsiri ya (Revised Standard Version) inasomeka, "Usemi wako unakushuhudia." Lugha ya Kaskazini (Galilaya) ilikuwa tofauti na lugha ya kawaida Judea.

**26:74**

Kwa nini Petro alifanya hivi? Je, alikuwa mwonga? Hapana. Pengine alikarihishwa, fadhaishwa, vunjwa moyo, changanyikiwa. Alitenda dhambi kwa namna mbalimbali:

1. Kukana kwake,
2. Alilaani na kuapa, na kisha kudanganya,
3. Lugha yake katika mst. 74. Kulaani, kuapa (kutangaza laani juu yake kama anasema uongo).

**26:75**

Alikumbuka jinsi Yesu alivyosema. Mara tatu alipata fursa ya kukiri, lakini kila wakati alimdhalilisha Bwana wake.

## SURA 27

**27:1**
Sasa kundi zima la Sanhedrin, watu sabini na moja, wamejikusanya pamoja ili kufanya shauri la kumwua Yesu.

**27:2**

Pilato, maliwali wao, wana nguvu za mwisho kufanya wanachotaka kufanyika. Angalia kundi lililofanya mashauri pamoja: **wakuu wa makuhani** (Sanhedrin), na **wazee** (watu wazima, viongozi walioheshimika miongoni mwa jamii). Wote wanatafuta njia ya kumwua Bwana, lakini wanataka Pilato afanye "kazi" yao yote "chafu."

**27:3**

Yuda anaona mpango wake hajafanikiwa. Hili linatoa mawazo kwamba Yuda hakutaka Yesu ahukumiwe.

**27:4**

Pengine anafikiri kwamba mambo haya mawili yatamwacha huru Yesu:

1. Kurejeza fedha, na
2. Usahahidi. Ni nani aliye bora kuliko yeye binafsi (mtu ambaye alikuwa jirani naye) kukiri kwamba Yesu ni mtu asiye na **hatia**?

Hawa ni viongozi wa dini ya watu ambao wanatakiwa wajali ukweli. Lakini wanajali zaidi kuhusu mamlaka.

**27:5**

Ilikuwa hakuna njia yoyote ya Yuda "kuzitunza fedha zenye damu hizi." aliweza kuona kwamba hapakuwa na njia ya kumwachilia Yesu kufikia hapa, hivyo Yuda anajiua mwenyewe.

Usiruhusu dhambi ikuangamize! (Somo zuri kutokana na maisha ya Yuda.) Maandiko yanatueleza kwamba Yuda alikuwa mwivi. Alishindwa kuishinda dhambi maishani mwake. Dhambi yake kubwa, hata hivyo, ndiyo haswa iliyomwangamiza yeye.

**27:6**

Ni unafiki ulioje!! Wako tayari kumwua mtu asiye na hatia, lakini wanajali kuzitumia vibaya fedha chache kwa ujanja! Wanaogopa kwamba wanaweza kulinajisi hazina ya hekalu na fedha hizo ambazo wao walimlipa Yuda. Wanachuja mbu na wakati huo huo kumeza ngamia (Math.23:24).

**27:7**
**27:8**

Kihistoria eneo hili linapatikana upande wa kusini mtelemko bonde la Hinoni, karibu na kiunga cha Mto Kidroni.

**27:9**
**27:10**

Mathayo anachangia fungu hili "konde la mfinyazi" kwa Yeremia (18:23), wala si yeye ama Zakaria (11:12, 13) anayetumia maneno haya. Kutokana na waandishi wa Kiyahudi, kitabu cha Yeremia kiliwekwa cha kwanza katika sehemu iliyojulikana "Kitabu cha Manabii." Pengine Mathayo hanukuu kutoka kwa mwandishi mwenyewe, bali kutoka sehemu hii ya gombo.

**27:11**

Katika Yoh.18:36 Yesu anamwambia Pilato kwamba ufalme wake si wa ulimwengu huu, lakini yeye ni Mfalme.

**17:12**

Viongozi wanashitaki kwa nguvu. Angalia 1Pet.2:23. Kwa namna yoyote ile mashitaka haya yote hayakuwa na uhakika na ukweli, lakini yalipangwa haswa yakimchokoza Yesu aseme jambo fulani ili wamshitaki.

**27:13**

Hakika hiki ni kitu ambacho Pilato hajawahi kushuhudia kabla; mtu anayeshutumiwa makosa yapasayo adhabu ya kifo, lakini hajaribu hata kujitetea mwenyewe.

**27:14**

Yesu anatimiza unabii wa Isa.53:7. Hakujibu lolote. Mtu mwingine yeyote angejitahidi kuokoa maisha yake. Tumeona jinsi Yesu hapo awali alivyoweza kumjibu mtu yeyote. Hili linaendelea kuthibitisha kujitoa kwake kwenda msalabani.

**27:15**

Lilifanyika hili ili liwali kutafuta umarufu.

**27:16**

Baraba alifungwa kwa ajili ya unyang'anyi (Yoh.18:40), uasi, na mauaji (Mk.15:7).

**27:17**

Maandiko mengine ya Kiyunani yana jina kama "Yesu Baraba." Pilato anawauliza wachague kati ya watu wawili wanaoitwa "Yesu." Ni kweli pia anauliza mnamtaka **Yesu aitwaye Kristo**. Ni nani alimwita hivyo, isipokuwa ni Petro katika Math.16:16? Hivyo, kuna watu wengine waliomwona kwa njia hiyo. Neno "Kristo" kwa Kiebrania ni "Masihi." Je, walitaka Pilato amwachilie Yesu?

**27:18**

Hapakuwa na shitaka la kweli aliloshhitakiwa Yesu. Pilato alitambua kwamba alishutumiwa kwa ajili ya **husuda**.

**27:19**

Alipowaza juu ya uamuzi, mkewe akamtumia ujumbe. Tukio hili ni la pekee kwa Mathayo. Watu wa kale waliheshimu mno ndoto. Ndiyo maana aliona ni jambo la dharura kwake kumpelekea Pilato ujumbe.

**27:20**

Makuhani wakuu na wazee waliwashawishi watu wengine kufanya hivi. Watu wanaweza kushawishika kuchagua kufanya mambo mabaya. Watu hawa walishawishiwa kutomchagua Yesu. Tunaweza kufanya kama hao. Lazima tuwe makini!

**27:21**
**27:22**

Walitamani Yesu auawe! Jambo hili lazima lilimshangaza Pilato, kwa maana alitambua kwa uhakika jinsi Yesu alivyofahamika na makutano.

**27:23**

Makutano hawakujibu lolote kutokana na swali lake. Waliendelea kupiga kelele wakitaka damu ya Yesu.

**27:24**

Hali inazidi kuwa mbaya. Kupitia kitendo hicho cha kufananisha kwa kuosha mikono yake, anatangaza kwamba haoni lolote la kufanya mtu huyu.

**27:25**

Watu wamekubali wajibu Yesu kuuawa. Bila kujali hili, walipewa fursa ya kutubu (Mdo.2:37-

39; 3:17). (Mdo.5:28 hawataki damu yake mikononi mwao).

**27:26**

Kupiga mijeledi ilikuwa kawaida kabla ya kusulubiwa. Kupigwa mijeledi, kwenyewe, kungeliweza kumwua mtu. Mjeledi wa ngozi aliocharazwa mtu mgongoni wenye vipande vya mifupa na vyuma mwishoni. Mtu aliinamia katika mhimili wa kupigia mjeledi akiwa mikono yake amefungwa, wakiitandaza ngozi kwa kadiri iwezekanavyo, na kisha kuchanwa-chanwa wakati kupigwa kulipoanza. Inawezekana hili likafafanua sababu ya Yesu kutokuchuka muda mrefu msalabani kama ilivyokuwa kwa wengine aliosulubiwa nao.

**27:27**

Praitorio ni jumba la kifalme la serikali ambamo Pilato aliishi.

**27:28**

Walimvika mavazi ya kifalme, vazi jekundu; alivikwa, haswa, kwa kudhihakiwa.

**27:29**

Mwanzi unasimamia fimbo, fimbo ya kiongozi. Taji iliundwa kutoka katika miiba yenye ncha ndefu na kali sana. Ndipo walipomdhihaki na kudharau.

**27:30**
**27:31**

Linga. Mk.15:16-20. Wayahudi walitoa kazi yao chafu kwa Warumi, na wakafanya kama Wayahudi walivyotaka. Jinsi gani jambo hili lilikuwa gumu kwa Mungu kushuhudia! Mijeledi, kudhalilishwa, kudhihaki, kumchoma na kadhalika. Mungu aliruhusu dhihaka hii itendeke yote kwa ajili ya upendo (linga. Yoh.3:16).

**27:32**

Yohana 19:17 pekee ndiye anaandika kwamba Yesu alibeba msalaba wake, na hakuna maandiko yanayosema kwamba alianguka kwa sababu kulemewa na uzito. Marko 15:21 anaandika majina ya wana wa Simoni. Inaonekana kuleta maana kwamba alifanya hivi kwa sababu walifahamika na wasomaji kuwa Wakristo. Hivyo, kwa namna yoyote ile, mtu aliyebeba msalaba wa Yesu baadaye "aliubeba msalaba wake mwenyewe" kumfanyika mwanafunzi wa Yesu, kama walivyofanya watoto wake.

**27:33**

Neno "Golgota" ni la Kiarami, hivyo Kiyunani kinalitafsiri "Mahali pa Fuvu." Maana ya Kilatini ni "calvus" ("Calvary") ikimaanisha "upara" au "sehemu ya kichwa." Neno la Kilatini cranium sawa na neno la Kiyunani kranion.

**27:34**

Yohana anaelezea kwa maelezo mengi katika 19:28-32. Zab.69:21 ilitabiriwa hili.

**27:35**

Tena utimilifu wa unabii wa Agano la Kale - Zab.22:18. Nguo toka mwilini pengine ndiyo yalikuwa moja ya vitu vichache ambavyo askari wangelipwa kutokana na "kazi ya msalaba." Chochote ambacho mtu alikuwa nacho chenye thamani, wangechukua, kupiga kula kwa masharti fulani.

**27:36**

Lazima wabakie hata Yesu amekufa. Waliweza pengine kujisikia kufarijika, hivyo wakaketi. "Mlindeni" ni maneno ya aina moja kama 26:40 wanafunzi walipoombwa kukesha na Bwana.

27:37

Ashara hii inaonyesha madai waliyomshitaki kinyume. Madai yake hayakuwa kufanya ghasia au kukufuru. Ilikuwa tu yeye kuwa ni mfalme wa Wayahudi. Pilato ndiye aliyeandika maandishi haya, ingawa Wayahudi hawakupendezwa nayo. Pilato aliyaandika na hapajatokea hata mtu mmoja mwenye kupewa cheo kama hicho tangu wakati huo. Yesu amesimama ulimwenguni sasa kwa miaka 2,000 akiwa pekee na mfalme wa mwisho wa Wayahudi.

**27:38**

Yesu alisulubishwa pamoja na wevi; waliokuwa wamevunja Sheria ya Mungu na sheria ya mwanadamu (linga. Isa.53:9). Katika siku zetu, mwizi anapata "kipigo kidogo tu cha kiwiko" au huonywa kutorudia kufanya tena, lakini karne ya kwanza, mwizi alipigiliwa msalabani.

**27:39**

Watu mambo ya upumbavu bila kujua.

**27:40**

Linga. 26:61.

**Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani**. Watu hawa wamekuwa vipofu mno kwa miujiza aliyotenda hapo awali, hata kama Yesu angeshuka mbele ya watu wote hao, je wangeamini? Hapana. Mioyo yao ni migumu mno. Ikiwa walishidwa kuamini miujiza ya kwanza, wasingeliamini hata angeshuka chini.

**27:41**
**27:42**

Wanakosea! Siyo kwamba **hawezi kujiokoa**, bali kwamba *hatajiokoa*. Alichagua asijiokoe mwenyewe ili aokoe wengine.

**27:43**

Mwana wa Mungu. Kama katika mst. 40 walimtukana. Lakini, wanavyomwita na kusema kuhusu yeye, hakika, ni kweli kabisa, ingawa wanafanya kwa kudhihaki.

Angalia sisitizo katika Zab.22 juu ya sehemu hii nzima.

**27:44**

Mwanzoni wevi wote walimdhalilisha Yesu, lakini mmoja alitambua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, akatubu (Lk.23:39-43).

27:45

Kuanzia saa 6 mchana hadi saa 9 kamili mchana ilikuwa giza; jambo la ajabu lisilo la kawaida. Hicho hakika ni kipindi cha giza sana katika historia ya mwanadamu. Marko anaandika kwamba walimsulubisha saa ya tatu (3:00 kamili mchana).

**27:46**

Yesu anazungumza katika Kiarami, na Mathayo anatafsiri. Haya ni maneno pekee ambayo Mathayo na Marko wanayaandika kutoka kwa Yesu anasema akiwa msalabani. Kuma maneno saba Yesu anayasema akiwa msalabani. Luka na Yohana kila mmoja anayaandika matatu ya hayo.

**27:47**

"Eliya" na "Eli" yanasikika karibu sawa. Eliya maana yake "Mungu wangu ni Jehovah." Eli maana yake tu ni "Mungu wangu."

**27:48**

Yohana 19:29 anazungumzia pia kuhusu hili. Hili ni tendo moja la wema alilotendewa alipokuwa msalabani saa za mwisho za uhai wake.

**27:49**

Mathayo amesema mengi kuhusu Eliya. Ni kitabu gani cha Agano la Kale kilitabiri kuhusu kuja kwa Eliaya? Malaki. Wanafikiria kuja kwa Eliya, na pengine wanafikiria kwamba wangemwona akija kwa macho yao.

**27:50**

Yesu anatamani kufa. Akajikabidhi mwenyewe kwa Mungu.

**27:51**

Pazia ilitenganisha kati ya Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu. Kupasuka kwake kuna maanisha mambo mengi:

1. Unajisi wa mahali,
2. Kuondoka kwa Mungu kutoka mahali hapo,
3. Mwisho wa Sheria ya Kale kwa sababu hekalu na patakatifu pa patakatifu palikuwa ndio mtazamo mkuu wa Sheria ya Kale, na
4. Tunaye Yesu ambaye amepita pazia (Ebr.10:19-22). Damu yake unatufanyia hivyo sisi.

Tetemeko la ardhi lilikuwa la nguvu kubwa hata kufunua makaburi na miamba ikapasuka.

**27:52**
**27:53**

Hapa kuna moja ya ishara kubwa iliyofuatia kusulubiwa. Haya yote yanathibitisha kwamba Yesu ni Mungu. Biblia inayaandika ili kuonyesha umuhimu wa yaliyotokea. Baada ya kufufuka kwake Yesu, waliofufuka waliwatokea watu wengi. Isingelikuwa, kwa hiyo, kutia shaka kwamba jambo la ajabu limetukia.

Tukio la ufufuo huu ni la pekee kwa Mathayo. Kuna maswali mengi yanajitokeza kutokana na mistari hii, (Waliishi muda gani tena? Je, walimshuhudia Yesu?), haya tuliyonayo ndiyo yaliyoandikwa.

**27:54**

Wakimlinda = wakimwangalia Yesu. Watu hawa wameona jinsi Yesu alivyokuwa kupitia mambo mabaya haya yaliyompata. Sasa wanaona hata vitu vya asili vinajibu yanayomtokea Yesu. Huyu si mtu wa kawaida tofauti na watu waliokuwa wamezoea kuwasulubisha misalabani siku zilizopita. Mtu huu alikuwa wa ajabu!

**27:55**
**27:56**

Waliomfuata (tena) ni wazo analolitilia mkazo Mathayo. Kulikuwa na idadi kubwa ya wanawake ambao walimsaidia (**mhudumia** au mtumikia) Yesu, na waandishi wote wa injili wanasisitiza kazi zao. Hakuna mwanamke hata mmoja aliyeandikwa katika Biblia aliyempinga Yesu. Wote waliompinga walikuwa wanaume.

**27:57**

Angalia Lk.23:50-53; Yoh.19:38ff. Mtu huyu hasa (pamoja na Nikodemu) ni wa pekee. Yusufu ni mtu mwenye mamlaka na mwenye uwezo.

**27:58**

Yusufu pia ni mtu jasiri kwa sababu amekwenda akiomba mwili wa Yesu. Kuzikwa kabla ya giza ilikuwa ndivyo Sheria ya Musa ilivyoamuru (Kum.21:23).

**27:59**
**27:60**

Ni upendo wa jinsi gani alioudhihirisha! Waandishi wote wa injili wanaeleza **kaburi** hili kuwa **jipya**. Pengine hii ndiyo sababu ya kufufuka kwa mtu aliyegusa mifupa ya Elisha 2 Falm.13:20-21. Hakuna mtu atakayeweza kubishana kwamba Yesu alifufuka kutokana na kugusa mifupa ya Elisha katika kaburi la zamani.

**27:61**

Wanawake walikuwa kukamilisha matayarisho ya mazishi ya mwili wa Yesu. Mathayo anatueleza kwamba Yusufu alileta kitani safi. Yesu anatueleza kwamba Nikodemu alitoa manemane na uudi, vyenye uzito wa pauni mia-moja. Havikufaa kutumika kimoja pasipo kingine. Kifo cha Yesu kilisababisha “siri ya uanafunzi” kufunuliwa bayana, na utimilifu wa Isa.53:9, “...na pamoja na matajiri katika kufa kwake...”

**27:62**

***Angalia makala: “Reckoning of the Passover”

**27:63**

Viongozi wa Kiyahudi walikumbuka vyema unabii wa Yesu kuhusu ufufuo - ingawa hata alisema kwamba angefufuka siku ya tatu. (Kwa nini mitume hawakukumbuka???) Hata hivyo, wanataka Pilato afahamu kwamba hawaamini kabisa madai hayo; kwa haswa, yaliyonenwa na **mjanja** huyo. (Linga.Yoh.7:12) Walakini...

**27:64**

Wanafikiria kwamba huenda mwili wake ukaibwa na mitume wake, hivyo basi wanachukua hatua ya kuulinda wao wenyewe. Katika kufanya hivi, hata hivyi, wanapunguza uzito wa madai yao wenyewe (baada ya kufufuka) kuwa mwili uliibiwa (Math.28:13).

Udanganyifu wa “kwanza” ulikuwa madai ya kwamba alikuwa Mwana wa Mungu. Dai la kwamba amefufuka toka kwa wafu litazidi hata ile “kazi ya udanganyifu” ya Yesu.

**27:65**

Pilato amecha ulinzi wa kaburi katika ungalizi wao. Angalia, ingawa, Pilato hayuko tayari kutuma askari wake hata mmoja. Kufikia hapa hawezi kulaumiwa kwa jambo lolote lile baya linaloweza kutukia.

**27:66**

Kwa kuwa askari waliwekwa, na jiwe lilifunika, watatambua iwapo kuna kilichoharibika. Katika Mathayo 16 Yesu alisema milango ya kuzimu (kaburi) visingeweza kushinda madai aliyokiri Petro kwamba ni Kristo, Mwana wa Mungu. Lolote mtu au shetani analojaribu kufanya kumzuia kaburini, kamwe hawatafanikiwa.

## SURA 28

**28:1**

Linganisha na Marko 16. Wakati huu walifika kaburini ni siku ya kwanza ya juma. Salome (Mk.16:1) na Yoana (Lk.24:10) wote walikwenda kaburini.

**28:2**

Tetemeko la nchi ilikuwa ni kazi ya Mungu. Warumi 1:4 anasema alilifufua kutoka kwa wafu.

**28:3**

Picha hii ni ya kuvutia sana! Hakika alikuwa na uwezo mkubwa sana, akisha liondoa jiwe kiurahisi.

**28:4**

Walinzi walitetemeka kwa hofu, na kwa sababu nzuri hasa! Ambapo 27:66 ametajwa mlinzi mmoja aliyewekwa kulinda (katika tafsiri za kiingereza), mtari huu unaonyesha kwamba Wayahudi wazi waliongeza angalau walinzi wengine kwa usalama zaidi. Tena, ingawa, hili lilitendeka kinyume nao, kwa maana sasa kuna watu zaidi ya wawili (na si wanafunzi wake)

ambao wangeweza kushuhudia picha hiyo ya mbinguni.

**28:5**

Malaika anawaambia wanawake kutokuona hofu; hakuna kibaya kilichotokea katika mwili wa Yesu. Walikuja "wakimtafuta." (Je, siku hizi wangali wanamtafuta Yesu?)

**28:6**

Hili ni tangazo la ushindi! Mara ngapi Yesu alisema kwamba angefufuka? Malaika wanahakiki kwamba Yesu amefufuka, hakika, wanathibitisha unabii wa ufufuo wake.

Wanawake wameombwa wapaone mahali mwili wake ulipolazwa. Walipata fursa ya kuwa wa kwanza kushuhudia kaburi wazi.

**28:7**

Wanawake wanakazi ya kufanya: "nendeni mkawaambie wanafunzi." Ni kiasi gani ujumbe huu ulileta furaha walivyoupokea? Tunafahamu kutoka katika waandishi wengine wa injili kwamba wanafunzi hawakuamini, hivyo basi Yesu alijitokeza kwao. Malaika anasema, "Mtakakomwona."

**28:8**

Ni jambo la kufurahisha, na hivyo la ajabu! Walichoshuhudia ni jambo kubwa na la kushangaza! Ebu fikiria jinsi walikuwa wakififikiri akilini mwao; hofu, huzuni, kuchanganyikiwa, furaha, n.k. Ni lazima walifurahi pamoja na kutetemeka - Zab.2:11b.

**28:9**

Hili ni *proskeneo* (abudu). Ebu fikiria juu ya kukua kwa imani yao katika Yesu! Wana ufahamu mpya wa jinsi Yesu alivyo. Walikwenda kaburini wakitarajia kuukuta mwili wake, lakini kaburi wazi limekamilisha kuelezea yale ambayo walitarajia katika Yesu. Sasa wanamwabudu! Wao (pamoja nasi) tunatakiwa kumwabudu Mungu na kumtumikia yeye peke yake (Math.4:10). Wanamwabudu Yesu kwa sababu ni Mungu.

**28:10**

Waliambiwa hivi katika mst. 5 lakini, mst. 8, bado walikuwa na hofu. Yesu aliwambia hivyo, na malaika aliwaambia hivi.

Mdo. 1:3 - Yesu aliwatokea kwa muda wa siku arobaini. Paulo anajadili kutokea kwake mara kwa mara katika 1 Kor.15:3-8 kuondoa ubishi kwamba ufufuo ulikuwa umeundwa tu na mitume. Watu hawa waaminifu waliuawa wakiamini na kuhubiri kuwa Bwana alifufuka. Walikuwa na imani isiyokufa kwamba Yesu yu-hai! Alikuwa Bwana wao!

**28:11**

Maskari hawa wanahofia maisha yao. Kumpoteza mfungwa na mtu fulani waliyekuwa wanamlinda adhabu yake ilikuwa kifo. Hii ndiyo aina ya ushahidi bila utata ambao utamhawishi mtu yeyote aliye na moyo mkunjufu. Labda hili linaeleza Mdo.6:7; ambapo makuhani walikuwa wakitii imani.

**28:12**

Baada ya kwa hila kupatana na kushauriana, mipango yao yote imeoneka bure. Badala ya kuwauwa maskari kwa kutokuzingatia majukumu yao, wanahonga (na pesa nyingi) kusema uongo juu ya wanafunzi wa Yesu.

**28:13**

Huu ni mfano bora wa jinsi Yesu walivyowaambia watu hawa katika Math.23:3, "...lakini mfano wa matendo yao msitende;..." Watu hao walikuwa waovu sana. Ni wazi kuona kwamba mioyo yao ni migumu na hawana nia ya kujua ukweli (2 Thes.2:10).

**28:14**

Hili linaonyesha kwamba maskari hawa walikuwa Warumi. Pilato alikuwa liwali, na walikuwa rahisi kupokea rushwa.

**28:15**

Hili linaonyesha jinsi ya uundaji na hila walizokuwa nazo kubuni maneno. Siku aliyoanza Mathayo kuandika injili, miaka thelathini baada ya kufufuka, kulikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi walioamini habari hizi. Kuna wengi, hata siku zetu hizi, wanaoamini haya. Hugh Scofield katika kitabu chake (The Passover Plot - analijadili imani hii.

**28:16**

Wanaenda kuonana mahali maalum. Wengine wanafikiri kwamba hapo mahali ndipo alipoonana na ndugu mia-tano walimshuhudia Yesu aliyefufuka wakati mmoja - 1 Kor.15:6. Yesu alijitokeza kwa siku arobaini kabla ya kupaa kwake - Mdo.1:3.

**28:17**

Baadhi mara moja waliitikia kwa namna fulani. Yohana amemtaja Tomaso, ambaye, katika Yoh.20:24-29, alitia mashaka, na anasema mpaka atakapoona alama za misumari mikononi mwake, na kugusa umbavuni mwake asingesadiki. Mashaka yake yaliondolewa alipomgusa Yesu. Wakamsujudia, wakimtambua kuwa ni Mungu, kama Tomaso alivyosema, "Bwana wangu na Mungu wangu!"

**28:18**

Huu ni utimilifu wa injili ya Mathayo; maana aliyokuwa akiifanya. Anawaandikia jamii ya Wayahudi, akiwasihi wakubali ufalme wa Yesu, ndiye Masihi. Mathayo alianza akionyesha kuwa Yesu ni wa Daudi; akidhihirisha nguvu zake kwa miujiza mingi. Alikuwa ni mwalimu mkuu. Alitimiza unabii wa Agano la Kale mwingi na mwisho - kupitia habari za mashahidi waliomwona tunafahamu kwamba Bwana amefufuka!

Mamlaka - neno la ufunguo! Nguvu *alipewa* Yesu. Yesu hakujifanya binafsi kuwa na mamlaka, bali alipewa. Ni mamlaka izidiyo mamlaka yoyote ile, mbinguni na duniani. Tunatambua kutoka Fil.2:9-11 kwamba kila ulimi utakiri na kila goti litapigwa mbinguni, na duniani. Hapa tuna Yesu akiungana na Mungu wakati ufalme wake (kanisa) utatawaliwa duniani. Yesu atakaa mkono wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu.

**28:19**

Ukizingatia mamlaka ambayo Yesu amepewa, anaagiza kwenda. Hii ni lazima! Anawaagiza kwenda na **kufanya wanafunzi**. Lazima mtu awe mwanafunzi ili afanye wanafunzi. Ni jinsi gani tunaweza kuwafanya wengine wamfuate Yesu isipokuwa sisi wenyewe tunamfuata? Katika 1Kor.11:1 Paulo anasema, "Mnifute mimi..." Ndiyo njia pekee ya uanafunzi ilivyo...kwa kuiga. Jambo la kwanza Yesu aliwaeleza kufanya ni kwenda na kufanya wanafunzi. Walijifunza maana ya hilo kwa kuhesabu gharama na kuweka kipaumbele - Math.8:18-22. Mwanafunzi hujifunza - na kamwe hasahau - huyo ni mfuasi na wala si kiongozi, Math.10:24. Neno "mwanafunzi" linamaanisha "mfuasi." Ndipo katika Math.16:24 Yesu anasema mambo haya manne: ni lazima *utake* kufuata, *unajikana* mwenyewe, *unachukua msalaba*, na kisha *unafuata*. Ni lazima uwe tayari kujitoe sadaka.

Ni jinsi gani tunafanya wanafunzi? Katika Kiyunani kuna aina mbili za nyakati timilifu ambazo zinatueleza jinsi ya kufanya hivi. Zote mbili ziko katika "wakati uliopita shurutisho" (aorist imperative."

Mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Katika Mk.16:16 Yesu aliamuru wanafunzi kubatiza wengine. Tunatambua kutoka Yohana 3 kwamba Yohana alibatiza. Yametolewa mamlaka kwa ajili ya ubatizo huu - katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Wanafunzi hawana zaidi ya kuwa wanafunzi, hawabatizi kwa mamlaka yao wenyewe, bali kwa mamlaka ya Yesu. Yesu hatoi "kanuni ya kubatizia," bali kuonyesha kuwa mamlaka ya kubatiza ni yale yanafungwa na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Ubatizo ni tendo la utiifu, na watatu hawa wamehusika katika tendo hili. Ubatizo pia ni tendo la kuabudu.

**28:20**

**Na kuwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi**. Yesu aliwafundisha, na sasa anawaamuru waende na kuwafundisha wengine. Hatupaswi kuwa kama wanafunzi katika Math.26:56, "Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia." Tunatakiwa kuwa wanafunzi ambao Bwana atawakuta wakifanya kazi. Mara mbili Mathayo anazungumzia wanafunzi wakiwa wanatenda kama walivyoamuriwa - 21:6; 26:19. Je, Yesu atatukuta tukitenda kama alivyoamuru sisi kutenda?

**Na kuwafundisha kushika**. Ni kazi ngumu kuuza bidhaa usiyoitumia, au dini usiyoishi kwayo. Angalia kwamba mafundisho yanafuata ubatizo. Kuwafanya wanafunzi inakupasa kufundisha, na ndipo kubatiza, na kisha kufundisha zaidi kile kinachotakiwa kufanya sasa kuwa wamekuwa wanafunzi. Neno kufundisha limekuwa katika wakati timilifu. Kufundisha - na kujifunza - haviishi kamwe! Maana ya kufundisha ni kuleta utiifu. Tunajaribu kuleta aina fulani ya kuishi.

Pamoja nanyi...hata mwisho wa dunia. Wanafunzi hawatakiwi kufikiria kuwa Yesu hayupo pamoja nao. Alikuwa ametabiriwa Imanueli (Math.1:21, 23) - "Mungu pamoja nasi."

Aliwahakikishia kwa uweza wake, aliwapatia agizo; kuwepo kwake kutakuwa pamoja nao!